

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Ishirini na Tano – Tarehe 9 Mei, 2018**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

#### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu.

**NDG. LINA KITOSI – KATIBU MEZANI:**

#### HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. LINA KITOSI - KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 207

**Hospitali za Wilaya**

**MHE. ESTHER L. MIDIMU** aliuliza:-

Wilaya ya Itilima na Busega ni Wilaya mpya na hazina Hospitali za Wilaya.

Je, ni lini Serikali itajenga Hospitali za Wilaya kwenye Wilaya hizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri za Wilaya ya Itilima na Busega zilianzishwa mwaka 2015 na zina idadi ya watu 346,170 kwa Itilima na 224,527 kwa Busega. Ni kweli kwamba Halmashauri hizi bado hazina Hospitali za Wilaya na wananchi wanapata huduma kupitia zahanati 45 na vituo vya afya saba ambapo kati ya hivyo zahanati 27 na vituo vya afya vitatu vipo Halmashauri ya Wilaya ya Itilima na zahanati 18 na vituo vya afya vinne vipo Halmashauri ya Wilaya ya Busega.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mpango wa maboresho na uimarishaji wa huduma za afya kwa kushirikiana na wadau (Canada na UNFPA), Serikali imepeleka kiasi cha shilingi bilioni 1.215 kwa ajili ya uboreshaji

wa miundombinu ya vituo vya afya. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 525 ni kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu katika Kituo cha Afya Ikilindo klichopo Halmashauri ya Wilaya ya Itilima na shilingi milioni 450 ni kwa ajili ya Kituo cha Afya Nasa katika Halmashauri ya Wilaya Busega. Shilingi milioni 240 ni kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya zahanati nane ambapo kila zahanati imepatiwa shilingi milioni 30; zahanati hizo ni Gaswa, Mahembe, Migato na Nangale zilizopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Itilima na Badugu, Nayamikoma, Ngasamo na Kikoleni zilizopo Halmashauri ya Wilaya za Busega.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri za Wilaya ya Itilima na Busega zimetengewa shilingi bilioni 1.5 kila moja kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali za Wilaya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwanza kabisa, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri yaliyojitosheleza. Pia naishukuru Serikali yangu kwa kutenga hizo shilingi bilioni tatu kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali za Wilaya za Itilima na Busega. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize swali la nyongeza; kwa kuwa Hospitali ya Mkoa wa Simiyu jengo la *OPD* lipo tayari na maeleo ya mkandarasi ambaye ni *TBA* amesema jengo hilo litakabidhiwa tarehe 28 Mei, 2018 kwa Katibu Tawala wa Mkoa. Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuweza kutujengea wodi ya wazazi, watoto, wanawake na wanaume ili hospitali hiyo ianze kazi haraka? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Hospitali Teule ya Mkoa haina kabisa gari la kubebeta wagonjwa kupeleka Hospitali ya Rufaa Bugando, gari liliopo wanatumia *hardtop* almaarufu chai maharage; je, ni lini

Serikali itatuletea gari la kubebbea wagonjwa kupeleka katika Hospitali ya Rufaa. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya naona umesimama, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya Wizara ya Afya ambayo tumeipitisha hivi karibuni, Serikali imetenga zaidi ya shilingi bilioni 30 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali za Rufaa za Mikao ya Katavi, Njombe, Simiyu, Songwe na Mara. Kwa hiyo, Hospitali ya Simiyu ni sehemu ya hospitali ambazo zitaendelezwa kujengwa katika mwaka huu wa fedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba ya hilo, Serikali imeagiza *ambulances* na zitakapofika Mkoa wa Simiyu utakuwa ni mmoja ya mkoa ambao tutaufikiria kupata *ambulance*. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mary Chatanda swali la nyongeza.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Korogwe hususan Korogwe Mjini tuna Hospitali ya Magunga, lakini tuna kata mbili ambazo zipo mbali nje ya mji kabisa, Kata ya Kwamsisi na Kata ya Mgombezi ambazo zina vijiji kama sita sita. Je, Serikali itakuwa tayari kutusaidia kupata fedha kwa ajili ya kuwajengea vituo vya afya? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo imeelekezwa kwenye Ilani ya CCM kwamba Serikali ina wajibu wa kuhakikisha kwamba

tunajenga vituo vya afya kila kata, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni suala tu la bajeti na safari ni hatua. Yeye mwenyewe ni shuhuda jinsi ambavyo tumeanza ujenzi wa vituo vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini kabisa wakati mwiningine hatua nydingine itafika mahali ambapo hizo kata ambazo zipo mbali zitafikiwa kwa sababu ndiyo azma ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa Sera ya Afya inazungumzia zahanati kwa kila kijiji, vituo vya afya kila kata na hospitali za wilaya katika wilaya, jambo ambalo sera hii hajakamilika hasa katika Mkoa wetu wa Rukwa ambao hauna Hospitali ya Wilaya hata moja, ni lini sera hii itakamilika kikamilifu hasa katika Mkoa wetu wa Rukwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimetoka kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mary Chatanda na Mheshimiwa Khenani ni shuhuda kwamba mionganoni mwa Wilaya 67 ambazo zinaenda kujengewa Hospitali za Wilaya, ni pamoja na Wilaya ya Kalambo, Sumbawanga Vijijini pamoja na Wilaya ya Nkasi. Sasa siyo rahisi kusema lini *exactly* kwa sababu na ujenzi nao ni *process*, lakini na yeye mwenyewe ni shuhuda jinsi ambavyo Serikali imeazimia na inatekeleza.

Na. 208

## **Kupandisha Hadhi Hospitali ya Wilaya ya Vwawa**

**MHE. RISALA S. KABONGO** aliuliza:-

Hospitali ya Wilaya ya Vwawa ambayo inatoa huduma kwa Halmashauri nne za Mbozi, Ileje, Songwe na Mombia inakabiliwa na upungufu wa vifaatiba, wodi, watumishi pamoja na Madaktari Bingwa.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupandisha hadhi Hospitali ya Vwawa kuwa Hospitali ya Mkoa ili iweze kutengewa bajeti ya kutosha kukabiliana na changamoto zilizopo sasa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Risala Said Kabongo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilituma timu ya wataalam kutoka Idara mbalimbali na Hospitali ya Taifa Muhimbili ambayo ilifanya ukaguzi wa siku kumi kuanzia tarehe 25 Agosti, 2017 hadi 5 Septemba, 2017 katika Hospitali ya Vwawa iliyopo Wilaya ya Mbozi Mkoa wa Songwe ili kufanya tathmini kuona kama hospitali hiyo inaweza kutumika kama Hospitali ya Mkoa na hatimaye kuwasilisha matokeo ya tathmini hiyo kwa Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri aliridhia Hospitali ya Wilaya ya Mbozi yaani Vwawa itumike kwa muda kama Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe wakati Mkoa unaendelea na taratibu za kujenga Hospitali ya Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha huduma katika hospitali hii, Serikali ilipeleka watumishi tisa akiwemo Daktari Bingwa wa Magonjwa ya akina mama pamoja na kufunguliwa akaunti Bohari ya Dawa (*MSD*) yenye namba MB 310004 yenye kutoa mgao wa dawa ngazi ya mkoa ili kuweza kutoa huduma kama Hospitali ya Rufaa ya Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeshatoa kiasi cha shilingi milioni 767 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe ambapo eneo lenye ukubwa wa hekari 23 lilitopo Hasamba katika Mji Mdogo wa Vwawa limeshatengwa na taratibu za kuanza ujenzi wa Hospitali hiyo kwa awamu ya kwanza zimeshaanza ikiwemo uandaaji wa michoro ya usanifu inayofanywa na Wakala wa Majengo Tanzania. Inatarajiwा Wakala wa Majengo ndiye atasimamia ujenzi wa hospitali hiyo. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Risala Kabongo, swalı la nyongeza.

**MHE. RISALA S. KABONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nimesikia majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa idadi ya wagonjwa wanaotibiwa katika Hospitali ya Vwawa ni kubwa, *out patient* tu wanaotibiwa pale ni 150 mpaka 200 kwa siku. Je, Serikali kwa nini isijenge jengo kubwa la *OPD* ili kuweza kukidhi mahitaji ya wagonjwa wanaopata huduma kwa sasa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya wanawake wanaojifungua katika Hospitali ya Vwawa ni kuanzia 15 mpaka 20 kwa siku, huku vifo vya watoto kuanzia sifuri mpaka miezi 28 ni 180 kwa takwimu za2015. Je, Serikali ina mkakati gani wa haraka wa kuongeza Madaktari, Wauguzi na vifaa tiba ili kupunguza vifo vya akina mama na watoto katika Hospitali ya Vwawa na pia kupunguza vifo vya wananchi katika Mkoa wetu wa Songwe? Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la msingi la Mheshimiwa Risala aliongelea suala zima la kuwa na Hospitali ya Rufaa na katika majibu ambayo tumetoa tunamhakikishia na taratibu za ujenzi zimeshaanza na pesa imeshapelekwa. Sasa katika swali lake la nyongeza anarudi tena katika ile hospitali ambayo tumesema kwamba itaendelea kuwa Hospitali ya Wilaya na kwa sasa hivi inatumika *temporarily* kama Hospitali ya Rufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge, ni vizuri tuchague njia moja ya kupita, hatuwezi kuwa na mawili kwa wakati mmoja. Jitihada ambazo zinafanyika na Serikali za kuhakikisha kwamba inajengwa Hospitali ya Rufaa ikizingatia ramani ya Hospitali ya Rufaa ni vizuri tukaiheshimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili anaongelea juu ya suala zima la vifo vya watoto na akina mama kutohana na upungufu wa madaktari. Naomba nimhakikishie na yeye alikuwepo wakati Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Utumishi akiwa anatoa takwimu juu ya tarajio la Serikali la kupata vibali kwa ajili ya kuajiri watumishi wa sekta ya afya na elimu, ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba tunaajiri watumishi wa kutosha ili kupunguza vifo vya mama na mtoto. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kahigi swali la nyongeza.

**MHE. ALFREDINA A. KAHIGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wilaya ya Bukoba Vijijini tuna tatizo la ma-engineer wa ujenzi na tulitengewa fedha za *force account* shillingi milioni 900 kwa ajili ya kutujengea Kituo cha Afya katika kata mbili, kata za Kishanje na Rubafu, lakin hatuna ma-engineer wa ujenzi. Tunajenga chumba cha mama na mtoto, *mortuary* na chumba cha Mganga katika kata hizo mbili.

Je, ni lini Serikali itatusaidia ma-engineer wa ujenzi? Ahsante. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nikupongeze kwa *Tulia Marathon* mmeefanya vizuri sana. Hongera sana. (*Makofî*)

Pia nampongeza sana Mheshimiwa Mama Kahigi kwa sababu amekuwa mfuatiliaji mzuri sana tokea alipokuwa Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesikia kilio hiki kwa sababu tunajua kwa Mkoa wa Kagera tulikuwa hatuna hospitali zile za Wilaya na ninyi mmeleta *concern* hizo kubwa na ndiyo maana mwaka huu wa fedha tunaenda kujenga hospitali tatu mpya kule Karagwe, Kyerwa pamoja na Bukoba Vijijini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunapeleka *infrastructure* nydingi sana katika eneo hilo na suala zima la kupata wataalam tutaweka kipaumbele chetu, lengo kubwa ni kwamba vile vituo vya afya na hospitali ambazo tunaenda kuzijenga tuwe na wataalam wa kutosha kwa ajili ya kuweza kusimamia. Kwa hiyo, tunalichukua kwa ajili ya kwenda kulifanya kazi. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Catherine Magige, swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa uongozi wa Mkoa wa Arusha chini ya Mkoo wa Mkoa Ndugu Mrisho Gambo, anafanya jithada mbalimbali za ujenzi wa vituo

vya afya na zahanati katika Mkoa wetu wa Arusha. Mfano tu katika Jiji la Arusha kuna ujenzi wa Kituo kikubwa cha Afya cha Murieth pamoja na Hospitali ya Wilaya ya Arusha Mjini unaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kufahamu, Serikali imejipanga vipi kutuletea watumishi mara tu vituo hivi vitakapokamilika? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba uniruhusu nichukue fursa hii kuupongeza Mkoa wa Arusha kwa kazi nzuri ambayo wanafanya katika suala zima la ujenzi wa vituo vya afya na hasa hicho Kituo cha Afya cha Murieth maana na mimi nimeenda kukitembelea, ni mionganoni mwa Vituo vya Afya ambavyo vimejengwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba Vituo vya Afya vinapokamilika huduma ziweze kutolewa na hakuna Kituo cha Afya hata kimoja ambacho kitakamilika Serikali ikakosa kupeleka watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie, *immediately* baada ya kwamba Vituo vya Afya vyote vya Arusha na maeneo mengine vikishakamilika, Serikali itapeleka watumishi pamoja na vifaa ili huduma za afya ziweze kutolewa kama ambavyo Serikali imekusudia. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagula, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalii lake.

Na. 209

## **Ukosefu wa Maji Safi na Salama Mkoa wa Geita**

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA** aliuliza:-

Kumekuwepo na tatizo kubwa la ukosefu wa maji safi na salama katika Mkoa wa Geita pamoja na Wilaya zake kama Bukombe, Chato, Mbogwe na Nyang'hwale.

Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza tatizo hilo la maji kwa wananchi wa Mkoa wa Geita na Wilaya zake?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagula, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuboresha huduma ya maji katika Mkoa wa Geita kwa kutekeleza miradi mbalimbali. Kwa upande wa maji vijijini Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya maji kuitia Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*WSDP II*) kwa Halmashauri zote za Mkoa wa Geita kama ilivyo katika Halmashauri zote hapa nchini. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2018 Serikali imetekeliza miradi 66 katika vijiji 217 vilivyopo katika wilaya za Mkoa wa Geita zikiwemo Wilaya za Bukombe, Chato, Mbogwe na Nang'hwale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa maji mijini, Serikali imeendelea na juhudhi mbalimbali za kuboresha huduma ya maji ambapo imekamilisha upanuzi wa mtandao wa usambazaji maji na jumla ya kilometra 101.3 za mabomba zimelazwa. Mradi huo umewanufaisha wakazi 14,300 wa Mji wa Geita. Kwa upande wa Mji wa Ushirombo katika Wilaya ya Bukombe, Serikali imekamilisha usanifu wa uboreshaji wa huduma ya maji ambapo mradi huo unawanufaisha wakazi

10,722. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2018, taratibu za kumpata mkandarasi wa mradi huo zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuitia Awamu ya Pili ya Utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, itaendelea kutekeleza miradi mbalimbali kwa lengo la kuwapatia wananchi wengi zaidi huduma ya maji safi na salama.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Chagula, swalii nyongeza.

**MHE. JOSEPHINA T. CHAGULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na ya kujitosheleza. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la kwanza, kwa kuwa mahitaji ya maji katika Mji wa Geita na vitongoji vyake ni makubwa mno ukilinganisha na maji tunayopata; mahitaji halisi ni lita milioni 15 kwa siku, lakini maji tunayopata ni lita milioni nne kwa siku. Kwa hiyo, tuna upungufu wa lita milioni 11 ambayo ni sawa na asilimia 29 kwa siku. Je, Serikali haionti kuna haja sasa ya kuongezea nguvu na uwezo Mradi wa Ziwa Victoria ili tuweze kupata maji ya kutosha kulingana na mahitaji yetu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili; kuna mradi wa maji katika Wilaya ya Nang'hwale. Mradi huu ni wa siku nydingi sana, hivi sasa ni miaka sita tangu uanzishwe, bado wananchi wanateseka wanahangaika kwa kupata maji. Naishukuru Serikali kwa kuweza kutenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya maji katika Wilaya ya Nang'hwale, je, Naibu Waziri yuko tayari sasa kwenda Nang'hwale ili akajionee hali halisi ya mradi ule ambao sasa hivi ni miaka sita haujakkamili na wananchi wanaendelea kuteseka mpaka sasa? Ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, nadhani hayo ndiyo maswali pekee yaliyopigiwa makofii sana humu ndani.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Chagula, ye ye ni mama na anadhihirisha kwamba mama wajibu wake ni kuhakikisha familia inapata maji. Nimkumbushe kwamba Serikali tayari imeshatekeleza awamu mbili za Programu ya Kulinda Ziwa Victoria, awamu ya kwanza ilikamilika na awamu ya pili imekamilika Desemba, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tumeanza awamu ya tatu na katika awamu hii Mheshimiwa Chagula, tayari tumepanga kutekeleza miradi kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka Ilemela, Buchosa, pale Geita, Katoro Buseresere. Pia tunatarajia haya maji tutapeleka hadi Mbogwe. Hili eneo la Mbogwe linaweza likapata maji kutoka eneo la Katoro, Buseresere au kutoka Msalala.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, mradi huu utahusisha pia kupeleka maji Buhongwa, Sumve na Usagara. Majadiliano na wafadhili wakiwemo *European Investment Bank*, Benki ya Maendeleo ya Afrika, yanaendelea vizuri na pia tutahakikisha kwamba hili eneo la Geita Mjini ambao ni mkoa mpya nalo limeingizwa ili tuweze kuongeza kiwango cha maji katika hilo eneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusu Nyang'hwale, kwa bahati nzuri nimetembelea Nyang'hwale nikakuta ule mradi umekaa muda mrefu sana. Nilitoa maelekezo na kila siku tatu naongea na Mbunge wa Nyang'hwale ili awe ananipa *progress* nini kinaendelea. Ameniridhisha kwamba mkandarasi sasa yuko *site*. Na mimi sasa kwa sababu ameomba kwenda na Mheshimiwa Naibu Waziri, nampa kibali hapa hapa Mheshimiwa Mbunge aende naye. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa matatizo ya Geita yanafanana kabisa na yale ya Wilaya ya Kigamboni na Mbagala katika Wilaya ya Temeke, pamoja na juhudzi za Serikali za kuchimba visima virefu katika Kata ya Kisarawe II Wilaya ya Kigamboni, lakini wananchi wale hawana kabisa mtandao wa maji safi na salama.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuweka mtandao wa maji safi na salama katika Wilaya ya Kigamboni na maeneo ya Mbagala? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza sana mama yangu, Mheshimiwa Mariam kwa namna ya kipekee anavyowapigania wananchi wake, lakini kubwa mimi kama Naibu Waziri nilipata kibali cha kufanya ziara katika Mkoa wa Dar es Salaam na moja ya maeneo ambayo nilifanya ziara ni eneo la Kigamboni, Temeke na maeneo mengine. Ni kweli zipo changamoto katika suala zima la maji, hususan pembezoni mwa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wizara ya Maji tumechimba visima 20 pale Mpera na Kimbiji katika kuhakikisha tunatatua tatizo hili la maji, lakini visima vile bado havijafanyiwa utandazaji. Sisi kama Wizara tumeona haja sasa ya kufanya *phase one* ili kuhakikisha wananchi wale wanapata maji safi, salama na yenye kuwatoshleza.

Kwa hiyo, Mheshimiwa mama yangu Mheshimiwa Mariam, sisi kama Wizara ya Maji na kwa kuwa siyo Wizara ya ukame, tupo tayari kuhakikisha wananchi wa Kigamboni wanapata maji safi, salama na yenye kuwatoshleza. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Mpanda Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 210

### **Usambazaji wa Pembejeo**

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itahakikisha inasambaza pembejeo kwa wakati na kwa kuzingatia msimu na jiografia ya maeneo husika?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Mpanda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, blashara ya pembejeo hufanywa na sekta binafsi, hususan makampuni na wafanyabiashara wadogo wa pembejeo za kilimo huhakikisha kuwa husambaza na kuuza pembejeo za kilimo kwa wakulima kulingana na mahitaji. Jukumu la Serikali katika kuhakikisha pembejeo zinawafikia wakulima kwa wakati ni kuratibu mahitaji, upatikanaji na matumizi yake na kuelekeza aina za pembejeo zinazofaa kwa kuzingatia msimu wa kilimo katika maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuandaa mifumo ya kuhakikisha kwamba pembejeo za kilimo zinasambazwa na kuwafikia wakulima wengi kwa wakati na kwa bei nafuu. Ili kutekeleza azma hiyo, kuanzia mwaka 2017/2018 Serikali imanzisha na kutumia Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja (*Fertilizer Bulk Procurement System*) ili kuhakikisha mbolea inapatikana na kusambazwa kwa wakulima kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo wa *BPS* umeleta faida nyingi zikiwemo kuongezeka upatikanaji kutoka tani 277,935 mwaka 2016/2017 hadi tani 310,673.7 mwezi Aprili, 2018 na kupungua kwa bei za mbolea kwa kati ya asilimia

11 hadi 39.5 ikilinganishwa na bei ya mbolea kabla ya Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari mbolea tani 109,000 ikiwemo mbolea ya kupandia (*DAP*) tani 55,000 na mbolea ya kukuza (*Urea*) tani 54,000 zimeingizwa na kusambazwa katika mikoa mbalimbali hapa nchini. Mbolea hizo hutumika kwa zaidi ya asilimia 62 kwa mwaka.

Aidha, siku ya Jumapili, tarehe 13 Mei, 2018, tutawapitisha Waheshimiwa Wabunge wote humu ndani katika semina ambayo inahusu Mfumo wa Uagizaji wa Mbolea kwa Pamoja ili tujenge ufahamu kwa wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mbegu bora, kuanzia mwaka 2017/2018 Serikali imefuta tozo saba kwenye mbegu. Mpango huu umelenga kupunguza gharama za uzalishaji, kuongeza upatikanaji na kupunguza bei ya mbegu bora kwa mkulima. Kwa kufuta tozo hizo, Serikali inategemea bei ya mbegu bora itapungua na wakulima wengi wataweza kununua na kutumia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sebastian Kapufi, swali la nyongeza.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFİ:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kuathiri wajibu wa Serikali wa kuratibu, ni kwa nini kusiwe na soko huria la mbolea kwa sababu haipatikani kwa wakati?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, wakati watu wanaongezeka, ardhi hususan inayofaa kwa kilimo haiongezeki. Nini mkakati wa Serikali wa kuja na mkakati mpya wa kuratibu kilimo chenye tija katika eneo dogo? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa sababu ameuliza swali ambalo pia linaendana na Wabunge wote hususan wale wanaotoka katika majimbo ya mijini, naye ni Mbunge wa mjini, hususan kuhusu kwamba watu wanaongezeka lakini ardhi haiongezeki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilieleze Bunge lako tukufu kwamba sisi kama Serikali tumejipanga kuongeza uzalishaji na teknolojia ya hali ya juu. Vilevile lengo letu kubwa ni kuhakikisha kwamba wakulima hawa siyo tu kwamba wanalima kilimo cha kujikimu lakini vilevile kiwe ni kilimo cha kibiasara. Naasa kila Halmashauri zote nchini ziweze kuwa na zile *green houses*. Kilimo kile kinalimwa katika sehemu ndogo lakini uzalishaji wake unakuwa ni mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza ni kwamba soko huria Serikali kazi yetu ni kuratibu, *ku-control* na *ku-regualte*, kwa maana hiyo, kwenye mbolea soko huria lipo, isipokuwa katika zile mbolea za *DAP* pamoja na *Urea* kwa maana ya kupandia na kukuzia, hiyo sisi kama Serikali kama tulivyosema ni kwamba Jumapili tutatoa semina kwa Waheshimiwa Wabunge ili waweze kuwa na uelewa mpana na wa pamoja kuhusu nini maana ya bei elekezi. Vilevile mbolea kuanzia sasa ziweze kufika kwa wakati na ziweze kuenea kwenye maeneo yote ya vijiji ili iwe kama soda na sukari. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Selemani Kakoso swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Mkoa wa Katavi unazalisha mazao ya kilimo ya biashara na chakula, nini mkakati wa Serikali wa kuwasaidia wakulima hawa ambao wamejitolea, wanafanya kazi kwa bidii lakini tatizo kubwa ni ukosefu wa masoko kwa mazao wanayozalisha? Nataka kupata...

**NAIBU SPIKA:** Umeshauliza Mheshimiwa Kakoso. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mazao ya chakula na mazao yale ya kimkakati ya biashara sisi tumesema kama Serikali hatufanyi biashara, kazi yetu ni ku-regulate na ku-control. Isipokuwa kama Serikali, sisi kuanzia sasa tunatoa vibali ili wakulima wote wawe na uhuru wa kuweza kuza bidhaa zao zote au mazao yao yote nje ya nchi lakini kwa kuhakikisha kwamba pia kama Serikali tuna chakula cha kutosha ndani ya nchi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda sasa aulize swalı lake.

Na. 211

#### **Wananchi Kutelekeza Wito wa Serikali Kulima Pamba**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE** aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha pamba yote iliyopo katika Jimbo la Bunda inanunuliwa kwa bei nzuri na kwa wakati muafaka?

(b) Katika Jimbo la Bunda kuna kilimo cha mkataba kwa kampuni moja na wakulima wana hofu kuwa huenda kampuni hiyo isifanye vizuri kwa wingi wa pamba iliyopo, je, Serikali inatoa kauli gani juu ya hali hiyo?

#### **NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swalı la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Jimbo la Bunda Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Bunda katika msimu huu imelima ekari 71,668 na inatarajia kuvuna pamba tani 21,000 za pamba mbegu. Kampuni mbili za *Olam Tanzania Ltd.* na *S&C Ginning Company Ltd.* ndizo zitakazonunua pamba katika Wilaya ya Bunda. Kutokana na uchunguzi uliofanywa na Bodi ya Pamba, kampuni hizi zina uwezo mkubwa wa kifedha na kwamba tayari zimekwishapata fedha kutoka vyombo vyta fedha tayari kwa ajili ya kuanza kununua pamba baada ya msimu kuzinduliwa tarehe 1 Mei, 2018. Aidha, nichukue fursa hii kipekee kabisa kuwahakikisha wakulima wa pamba wa Wilaya ya Bunda na maeneo yote yanayolima pamba kwamba pamba yao yote itanunuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika msimu wa kilimo wa 2017/2018 Wilaya ya Bunda na Wilaya nyingine 38 zimetekeleza kilimo cha mkataba baada ya kupewa idhini na Serikali ya kuingia mikataba na makampuni ya pamba. Katika Wilaya ya Bunda makampuni mawili ya *Olam Tanzania Ltd.* na *S&C Ginning Company Ltd.* ndiyo yaliyoingia mkataba na Halmashauri ya Wilaya ya Bunda na Bunda Mji kwa ajili ya kutekeleza kilimo cha mkataba. Makampuni hayo yamekopesha pembejeo wakulima ambapo fedha hizo inabidi zirejeshwe wakati wa kipindi cha mauzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya wakulima 42,000 wamenufaika na mfumo huu wa kilimo katika Wilaya ya Bunda. Kwa kuwa makampuni haya yamewezesha wakulima kulima kwa tija na kwa ubora unaotakiwa na soko ni muhimu, mkataba katika maeneo haya lazima uheshimiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejiridhisha na uwezo wa makampuni haya na kwamba pamba yote katika Wilaya ya Bunda itanunuliwa kwa wakati na bei ya kuanzia itakuwa bei elekezi ya shilingi 1,100 kwa kilo na bei inaweza kupanda kulingana na hali ya soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kampuni ya *Olam Tanzania Ltd.* ambayo itanunua pamba katika Jimbo la Mheshimiwa Boniphace Getere ni kampuni kubwa na

imejipanga vizuri kuhakikisha itawahudumia wakulima wa pamba ipasavyo kama ilivyofanya katika ule msimu wa ununuzi wa 2017/2018. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Getere, swalil la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini pia nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na watendaji wote wa Kilimo, wanajitahidi sana kuokoa zao la pamba. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Kabla sijauliza, nisahihishe tu kwenye Hansard kwamba hakuna Jimbo linaitwa Bunda Vijijini. Kuna Jimbo linaitwa Bunda. Kwa hiyo kwenye *Hansard* kusomeke kuna Jimbo linaitwa Bunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalil la kwanza, kwa kuwa wakulima wa pamba na kwa kuwa katika jibu la msingi Naibu Waziri amesema kuna watu walikopa pamba na kuna vikundi vilifanya mkataba na wana makampuni kukopa pamba, sasa hili tamko la Serikali la kukata shilingi moja kwa kila mkulima ili kulipia pembejeo na hata yule ambaye hakukopa, ni la nini? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalil la pili, Serikali imejiandaa vipi sasa kukabiliana na changamoto zitakazojitokeza kutokana na miongozo yake ya mara kwa mara ambayo haijawa na maandalizi? Kwa mfano, kuna suala la wakulima kufungua akaunti, kuna suala la pamba kununuliwa na ushirika au na watu binafsi kwa maana ya ushirika kununua pamba, kuna suala la kwamba ushirika hauna fedha ya kununulia pamba, sijui ni watu binafsi watatoa kwenye ushirika; Serikali imejiandaa vipi sasa kukabiliana na matatizo haya ambayo watu watayapata kutokana na miongozo yake hii mifupi? (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya swali la msingi. Pia nampongeza Mheshimiwa Getere kwa maswali haya ya muhimu sana katika tasnia ya pamba. Nianze na swali lake la nyongeza la kwanza kuhusu fedha; shilingi moja moja alioisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pembejeo waliyopata wakulima wengi walio katika mkataba ni lazima ilejeshwe na utaratibu wa kuirejesha ile pesa ni kwa makato kutokana na mauzo yao. Hiyo fedha inayokatwa siyo tu kwamba itafanya kazi ya kurejesha pembejeo waliyopata, lakini ili twende vizuri katika msimu ujao tunapaswa kuwa na fedha ya kuanzia kwa ajili ya kupata pembejeo hizo hizo ambazo wakulima watapata. Ndiyo maana Serikali imeshatamka kwamba msimu ujao wakulima wa pamba kote nchini hawatakopeshwa au pembejeo kwa maana ya dawa au mbegu za pamba. Watapata bure na hii inatokana na hii fedha ambayo wanakatwa sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili la nyongeza, siyo kwamba Serikali imesema ushirika utanunua pamba ya wakulima, kwa sababu wakulima wenyewe ndiyo ushirika. Kwa hiyo, kitakachofanya sasa hivi na kinachofanyika ni ushirika unakusanya pamba ya wanachama wake halafu wanunuzi wanaenda kununua kwenye ushirika huo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona.

Kati ya wakulima wanaopata taabu kwa kulaliwa bei na watu ambao hawana soko la uhakika ni wakulima wa pamba. Kwa sababu wanunuzi wengi wanalangua na wanapanga bei wanayoitaka wao na mwisho wa siku wakulima wanapata hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni kwamba, ni lini Serikali itawatafutia wakulima wa pamba soko la uhakika ili na wenyewe waweze kunufaika na kilimo cha pamba? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, majibu kwa swali hilo.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nitofautiane kidogo sana na Mheshimiwa Bulaya kuhusu uhakika wa soko. Soko la pamba ni la uhakika na hatujawahi kuwa na tatizo la kuuza pamba nchini. Pamba ni bidhaa inayouzwa na nchi nydingi duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, soko la Tanzania haliwezi kuwa tofauti na Soko la Dunia la Pamba. Majadiliano yanapofanyika kati ya wadau na wauzaji, ni zao pekee ambalo kwa msingi wadau wanajadiliana na wanunuzi, wanafikia muafaka wa bei. Hii inakuwa *pegged* kwenye bei ya pamba katika Soko la Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, bei inayopatikana siyo kwamba inawalalia wakulima, lakini pia inawapa faida wafanyakibashara na wakulima wanapata haki yao kutegemea na soko la dunia liliyvo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mashimba Ndaki swali la nyongeza.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Suala hili ni nyeti sana na sjui kwa muda tulionao kama unatosha kulizungumzia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Waziri anasema pamba itauzwa kwa kukusanya na Vyama vya Ushirika vilivyoko kwenye maeneo yetu, makampuni wataenda wanunue pamba hapo. Tunajua wote ushirika kwenye nchi yetu hali yake ilivyokuwa na sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kuuliza swali, nisirefushe maneno, je, Serikali imejiaandaa kwa namna gani

kuhakikisha kwamba huu ushirika tunaouzungumza uko imara na kwamba utahakikisha mkulima hapotezi pamba yake na bei ya pamba inapanda kulingana na mahitaji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo majibu kwa swali hilo.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ni kweli ushirika kwa miaka ya nyuma hapa umekuwa na tatizo sana hasa ushirika wa zao la pamba. Siyo siri kwamba wakulima wengi wa pamba walipoteza pesa zao kutokana na viongozi wa Ushirika ambao hawakuwa waaminifu na hivyo kupelekea Serikali wakati ule kuruhusu watu binafsi kuingia katika kununua pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Ndaki na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba tumefanya jitihada kubwa sana kwanza za kuhakikisha kwamba viongozi waliochaguliwa katika Vyama vya Msingi vya Wakulima wa Pamba safari hii ni wale viongozi waadilifu ambao hawatachezea pesa za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetoa rai kwa Viongozi wa Ushirika katika Vyama vya Msingi nchini kote kwamba yule anayetaka kuonja sumu kwa kuiba pesa ya wakulima wa pamba afanye hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na matatizo ya ushirika yaliyokuwapo, lakini lengo la Serikali ni kuhakisha kwamba ushirika utaimarika, wizi katika ushirika utakoma na wakulima wapate sauti ya pamoja kupitia ushirika. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Mheshimiwa Othman Omar Haji, Mbunge wa Gando sasa aulize swali lake.

Na. 212

### **Mafanikio ya AICC**

**MHE. OTHMAN OMAR HAJI** aliuliza:-

Madhumuni makubwa ya Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC) kilichoanza shughuli zake Julai, 1978 kufuatia kuvunjika kwa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977 ilikuwa ni kuendesha biashara ya mikutano na upangishaji wa nyumba.

Je, ni mafanikio gani ambayo Serikali imeyapata kutokana na kuanzishwa kwa taasisi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Othman Omar Haji, Mbunge wa Gando, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu kuanzishwa kwa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC) mwaka 1978, Serikali imeweza kupata mafanikio mbalimbali. Baadhi ya mafanikio hayo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo huchangia katika pato la Taifa kwa kulipa kodi stahiki kwa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa kwa wakati, kwa mfano, kwa miaka mitatu mfululizo kuanzia mwaka 2014/2015 hadi 2016/2017 kituo kimelipa kodi ya jumla ya shilingi bilioni 6.05.

Pili, kituo huchangia katika bajeti ya Serikali kwa mfano kwa mwaka 2014/2015 hadi 2015/2016 kituo kimechangia jumla ya shilingi milioni 586. Aidha, kwa mwaka 2016/2017 kituo kimetoa gawio kwa Serikali la shilingi milioni 400.

Tatu, kituo kimewezesha Taasisi za Kimataifa nchini kwa kuwakodishia Ofisi na makazi yanayokidhi mahitaji yao. Kwa mfano, AICC ilikuwa ni Makao Makuu ya Mahakama ya Kimataifa inayoshughulikia Mauaji ya Kimbari ya Rwanda. Pia ni Makao Makuu ya Bodi ya Ushauri ya Umoja wa Afrika kuhusu masuala la rushwa. Vilevile baadhi za Ofisi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zipo katika eneo la AICC.

Nne, kituo kimeweza kuleta mikutano ya Kimataifa ambayo imechangia kuvutia wageni kutumia fursa ya kutembelea vivutio vya utalii nchini na kutembelewa na viongozi wakubwa na maarufu duniani na kufanya vyombo vya habari vya Kimataifa kuimulika Tanzania na hivyo kuifanya nchi yetu kutambulika zaidi ulimwenguni.

Tano, kituo kimeweza kutoa ajira kwa Watanzania wapatao 132 hadi kufikia mwezi Mei, 2018.

Sita, kituo kimeweza kujenga majengo matatu ya ghorofa ya makazi kwa familia 48 Jijini Arusha, hivyo kuwawezesha wakazi wa Arusha kuishi katika makazi bora.

Saba, kituo kinahudumia zaidi ya wageni 30,000 kwa mwaka, hivyo kuchangia katika kukua kwa sekta za hoteli, usafirishaji, utalii na wajasiriamali wadogo na wakubwa katika jiji la Arusha.

Nane, kupitia hospitali ya kituo, huduma ya afya kwa jamii imeweza kutolewa kwa wafanyakazi wa Jumuiya za Kimataifa, wageni wanaokuja kwa ajili ya mikutano mbalimbali na watalii wanaofika Arusha kutembelea vituo vya utalii.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Othman Omar Haji, swali la nyongeza.

**MHE. OTHMAN OMAR. HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu aliyoyatoa. Nina maswali mawili ya nyongeza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar ni mshirika wa A/CC na ina haki ya kupata gawio, lakini kauli za Mawaziri zinazohusu gawio la A/CC zinakinzana. Mfano, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anasema kwamba A/CCinapeleka gawio Serikali Kuu, lakini Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati akijibu swalii la Na. 110 katika Kikao cha Sita, Mkutano wa Kumi alisema kwamba A/CC bado haijawahi kupata gawio na kwamba *Joint Finance Commission* wakishirikiana na Msajili wa Hazina wameunda kikosi kazi ili kuiwezesha A/CC kutengeneza faida na kuleta gawio Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, Mheshimiwa Waziri kauli ya Waziri wa Fedha inakinzana na kauli ya Waziri mwenye dhamana. Kwa maana hiyo, gawio linalotoka A/CC haliendi Serikali Kuu. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba Zanzibar sasa hivi inakosa gawio kutoka A/CC toka ilipoanzishwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, A/CC imekuwa ikifanya uwekezaji mkubwa sana kule Arusha kama alivyozungumza Mheshimiwa Waziri, lakini imeshindwa kuwekeza katika mazingira ya Zanzibar pamoja na kuwa mazingira yake yanaruhusu.

Mheshimiwa Naibu Waziri, anaweza kutueleza kwa sababu gani A/CC imeshindwa kufanya uwekezaji katika Visiwa vya Zanzibar?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swalii lake la kwanza kwamba Mheshimiwa Waziri wa Fedha alidanganya, naomba niseme siyo sahihi. Mheshimiwa Waziri wa Fedha hakudanganya, alisema Msajili wa Hazina wameunda mkakati kwa kushirikiana na kituo husika ili kuona kituo kinatoa gawio.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama amesikiliza vizuri katika jibu langu la msingi, nimesema kituo kimeanza kutoa gawio mwaka 2016/2017 na katika gawio hili Serikali ya Zanzibar inapata mgao wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swalii lake la pili kwamba kituo hakiwekezi Zanzibar. Napenda kuliharifu Bunge lako tukufu kwamba kituo kinatekeleza mpango mkakati wa miaka mitano ambao umeanza kutekelezwa mwaka 2017/2018 hadi 2021/2022 na ambao katika mambo yanayotakiwa kutekelezwa ndani ya mpango mkakati huo ni kujenga vituo vingine kwa uwekezaji na katika maeneo ambayo vituo vitajengwa mojawapo ni Zanzibar na kituo kwa sasa kinaanza kujenga Dodoma na baada ya Dodoma kinakwenda kujenga Zanzibar. Kwa hiyo, uwekezaji huu unakwenda katika pande zote mbili za Muungano.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Mheshimiwa Injinia Ramo Mataala Makani, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, sasa aulize swalii lake.

Na. 213

**Utekelezaji wa Sera ya Huduma za Afya ya  
Mama na Mtoto**

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI** aliuliza:-

Serikali inatekeleza sera inayohusisha huduma bora za afya ya mama na mtoto.

Je, utekelezaji huo umenufaishaje Jimbo la Tunduru Kaskazini?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA  
WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba

kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer Ramo Mataala Makani*, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, afya ya mama na mtoto ni moja ya maeneo yaliyopewa kipaumbele katika Sera ya Afya mwaka 2007. Hivi sasa Serikali inatekeleza mpango mkakati wa miaka mitano wa mwaka 2016 hadi 2020, ambao unajulikana kama *National Road Map Strategic Plan to Improve Reproductive Maternal, New Born, Child and Adolescent Health in Tanzania*, unaolenga kuboresha afya ya uzazi ya mama mtoto na vijana. Katika kutekeleza mkakati huu, Wizara imezingatia maeneo makuu matatu ambayo ni huduma ya uzazi wa mpango, huduma wakati wa uzazi na huduma wakati wa kujifungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Wilaya ya Tunduru, Serikali imehakikisha upatikanaji wa bidhaa muhimu za uzazi na mtoto ikiwemo dawa ya uzazi wa mpango kwa maana ya (sindano ya *depoprovera*, vipandikizi na vitanzi) dawa za watoto (*ORS zinc*) kwa ajili ya kutibu kuharisha na dawa za *antibiotics* za watoto ya *amoxyllin* kwa ajili ya kutibu nimonia) dawa za uzazi salama ikiwepo dawa ya kuongeza uwingi wa damu kwa maana ya *Fefol*, dawa ya kuzuia mama mjamzito kupoteza damu baada ya kujifungua kwa maana ya *oxytocin* na dawa ya kuzuia kifafa cha mimba kwa maana ya *magnesium sulfate*.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI inatekeleza mpango wa kukarabati na kupanua vituo vya afya 208 nchini ili viweze kutoa huduma za uzazi wa dharura, ambapo Kituo cha Afya cha Mkasale kilichopo katika Wilaya ya Tunduru kimepewa fedha shilingi milioni 400 kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa miundombinu ikiwemo chumba cha upasuaji, jengo la huduma za mama na mtoto, maabara na nyumba ya mtumishi. Kituo cha Afya cha Matemanga kimetengewa fedha katika awamu inayofuata.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer Ramo Makani*, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa umahiri wake wa kijibu swali, siyo hili tu, hata mengine ambayo nimeshuhudia akiwa anayajibu. Naipongeza pia Wizara kwa ujumla kwa jinsi na namna ambavyo inachapa kazi kwa ufasaha na ufanisi. Pia kwa Serikali nzima ya Awamu ya Tano katika Sekta ya Afya nikipita kwenye mitandao huko kote kwa kweli nataka kuipigia chapuo Serikali kwa *performance* hiyo. Hongera sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maswali mawili ya nyongeza; swali la kwanza, kwa kuwa Serikali inatekeleza mpango mkakati iliyoutaja kwa mwaka 2016 mpaka 2020 na kwa kuwa katika utekelezaji wa mpango huo Serikali imizingatia maeneo matatu na moja ya maeneo hayo ni huduma wakati wa kujifungua na kwa kuwa katika huduma za wakati wa kujifungua mojawapo ya mahitaji muhimu ni chumba cha upasuaji na kwa kuwa ndani ya chumba cha upasuaji mojawapo ya vitu muhimu ni vitanda vya upasuaji ambavyo vinaitwa *operation beds au operation tables*; na kwa kuwa katika Hospitali ya Wilaya ya Tunduru hospitali pekee katika Wilaya ambayo ina vijiji karibu 160 hali ya chumba hicho ni mbaya kwa maana ya miundombinu ya jengo lenyewe lakini pia na vifaa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweza kurekebisha chumba hiki cha upasuaji ili kiweze kuwa bora kabisa cha kuweza kutoa huduma kama sera inavyoelekeza? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwanza naipongeza Serikali kwa kuboresha vituo vya afya hivi vichache ambavyo tunavyo. Isipokuwa vituo vyetu vya afya viko mbali sana kutoka kwenye Hospitali ya Wilaya na kwa hiyo, ili uweze kutoa huduma bora zaidi ya uzazi wa mpango au kutoa huduma vizuri zaidi kwa mpango wa uzazi na mtoto unahitaji kufikisha wagonjwa kwa wakati kwenye Hospitali ya Wilaya, lakini hatuna magari ya wagonjwa hata moja. Kwa muda mrefu tumekuwa tukiomba Serikalini tuweze kupatiwa angalau...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa naomba uulize swali tafadhali.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali sasa. Ni lini Serikali itaweza kuipatia Wilaya ya Tunduru gari la wagonjwa kwa ajili ya kuwahudumia akina mama wajawazito pamoja watoto kwa ajili ya huduma za afya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE, NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa kwa kufuatilia sana masuala ya afya na hususan afya ya uzazi katika Wilaya yake ya Tunduru. Takwimu zinaonyesha kwamba akina mama wa Tunduru wanafanya vizuri sana kwa kujifungulia katika Vituo vya Afya kwa zaidi ya asilimia 81 lakini vilevile katika matumizi ya uzazi wa mpango. Nawapongeza sana kwa kazi kubwa na nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na maswali yake ya msingi ambapo ameuliza kwamba, jengo pamoja na chumba cha upasuaji na upatikanaji wa kitanda cha upasuaji ni changamoto katika hospitali ya Wilaya, naomba niseme kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hospitali zetu hizi pamoja na hii hospitali ya Tunduru ambayo ni hospitali ya Wilaya zina vyanzo mbalimbali. Kwanza, kupitia Serikali Kuu tumekuwa tunapeleka fedha za dawa. Naomba Waheshimiwa Wabunge, tunaposema fedha ni za dawa, haimaanishi ni dawa peke yake. Ni fedha za dawa, vitendanishi na vifaatiba. Meza ya upasuaji ni moja ya kifaatiba. Kwa hiyo, kuna vyanzo viwili ambavyo hospitali hii inaweza ikatumia ili kuweza kupata ile *operating table* na moja ya chanzo ni fedha zile tunazozipelekea katika hospitali yetu na katika mgao huu wa fedha mpaka sasa hivi Wilaya ya Tunduru tumeshapeleka shilingi milioni 268.

Mheshimiwa Naibu Spika, chanzo kingine ambacho wanaweza wakakitumia ni makusanyo yao ya ndani pamoja na makusanyo kupitia mfuko wa *NHF*. Kwa hiyo, niendelee kumshauri Mheshimiwa Mbunge wakae katika ngazi yao ya Halmashauri na kupanga matumizi mazuri ya fedha ambazo wanazipata na wanazozizalisha katika hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swalı lake la pili, ameulizia kwamba ni lini Serikali itaipatia huduma ya *Ambulance Hospitali* ya Tunduru. Mimi niseme tu kwamba Serikali imeagiza magari na yatakapofika, tutaangalia vigezo vyta uhitaji kulingaa na umbali na idadi ya vifo vyta akina mama na watoto na Wilaya ya Tunduru itakuwa ni moja ya Wilaya ambazo tutazifirkiria. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa Lupembe, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalı lake. (*Makofi*)

Na. 214

### **Hitaji la Kituo cha Polisi Wilaya ya Mlele**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi Wilaya ya Mlele?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swalı la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua uhitaji wa vituo vyta polisi pamoja na nyumba za kuishi askari kote nchini ikiwemo Wilaya ya Mlele. Ili kutatua changamoto hii, Serikali kupitia Jeshi la Polisi inashirikisha wananchi pamoja

na wadau mbalimbali wengine wa maendeleo ili kufanikisha azma ya Serikali ya kujenga vituo vyta polisi vya kisasa nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ufinyu wa bajeti na uhitaji wa vituo vya polisi katika maeneo mbalimbali nchini kuwa mkubwa, namwomba Mheshimiwa Mbunge kushiriki katika jitihada hizi kwa kuhamasisha wananchi wake kushiriki katika mpango huu ili kuhakikisha huduma za Kipolisi zinaimarika karika eneo hilo. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, swali la nyongeza.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza naomba nimpongeze Mkuu wa Wilaya ya Mlele, tayari ameshaanza kufanya hamasa kwa ajili ya Kituo cha Polisi Wilaya ya Mlele, lakini kwa kuwa jengo hili la polisi ambalo wanalitumia sasa hivi ni jengo ambalo walijenga wananchi wakati ikiwa Kata ya Inyonga kwa ajili ya usalama wao, sasa hivi imekuwa Wilaya na matukio yamekuwa mengi zaidi kupita nyuma na uhitaji wa usalama unahitajika zaidi kwa sababu sasa hivi ni Wilaya siyo Kata na wananchi wale walivyojenga hili jengo ambalo walilikabidhi Polisi, walijenga Kituo kidogo na chumba cha mahabusu kidogo...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naomba uulize swali tafadhalii.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama wananchi walijenga, Serikali inatakiwa ifanye maboresho. Je ni lini Serikali itafanya maboresho ili sasa kile kituo kionekane kama kituo cha Wilaya?

Swali langu la pili, kutokana na chumba kidogo cha mahabusu, kwa sababu sasa hivi mahabusu wale wanachukuliwa wanapelekwa Mpanda Mjini, halafu

wanarudishwa Inyonga, ghamama kila siku gari limekwenda Mpanda linaludi Inyonga, Serikali haioni ni vyema zile ghamama ambazo zitumika kila siku kupeleka gari Mpanda Mjini na kurudisha Inyonga zikatumika kujenga Kituo cha Polisi katika Wilaya ya Mlele?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge na wananchi wake wa eneo hilo na Mbunge wa Jimbo husika kwa jinsi ambavyo wameweza kufanikiwa kuanza ujenzi wa kituo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimekuwa nikijibu mara kadhaa hapa, siyo kwamba Serikali haina mpango wa kujenga vituo vya polisi hususan katika ngazi za Wilaya, mpango huo upo. Nilizungumza jana kwamba tuna mpango wa kujenga vituo takribani 95 nchi nzima, lakini kwa sasa hivi bado hali ya kibajeti haijakaa sawa. Pale ambapo hali ya kibajeti itakapokaa vizuri, eneo hili ni moja katika vipaumbele vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kabisa tutakapo jenga kituo katika eneo hilo, litatatua vilevile changamoto ya udogo ya chumba cha mahabusu. (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 215

#### **Hitaji la Kituo cha Polisi Wilaya ya Itilima**

**MHE. GIMBI D. MASABA** aliuliza:-

Wilaya ya Itilima haina Kituo cha Polisi cha Wilaya.

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Itilima?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi lina jumla ya Wilaya za Kipolisi 168 nchi nzima ambapo kati ya hizo, Wilaya 127 zina majengo kwa ajili ya Ofisi na Vituo vya Polisi vya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhaba wa vituo vya polisi pamoja na nyumba za kuishi askari nchini umesababishwa na kukosekana kwa rasilimali za kutosha kukidhi mahitaji ambayo ni makubwa. Hata hivyo, Serikali kuititia Jeshi la Polisi linafanya jitihada mbalimbali kama vile kutumia rasilimali zilizopo katika eneo husika pamoja na kushirikisha wadau mbalimbali wa maendeleo ili kukabiliana na tatizo la uhaba wa vituo vya polisi nchini. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba, swali la nyongeza.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; Wilaya ya Itilima Makao Makuu yake yako Kata ya Lagangabiliti na Kituo cha Polisi kipo Kata ya Luguru. Je, Serikali ina mpango gani kuhamishia Kituo cha Polisi katika Makao Makuu ya Wilaya ya Itilima? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa kituo kinachotumika kwa sasa kilitolewa kwa hisani ya Ndugu Paulo Ng'hwani kwa muda mrefu na kituo hicho kwa maana

ya hilo jengo limeharibika, je, mna mkakati gani sasa wa kupeleka fedha angalau kukarabati jengo hilo ambalo lilitolewa kwa hisani ya Ndugu Paulo Ng'hwani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kwanza kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mbunge wa Itilima, Mheshimiwa Njalu ambaye wakati wa ziara yangu nilipofanya kule nilliona jitihada zake kubwa sana ambazo amekuwa akizitoa katika kufanikisha kutatua changamoto kwenye eneo la Polisi kwa ujumla wake. Moja kati ya jitihada hizo ni kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa Kituo cha Polisi ambacho sasa hivi kinaendelea na ujenzi wake. Vile vile Mheshimiwa Mbunge aliniahidi kwamba kazi hiyo ataendelea nayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge Dotto naye namshukuru vilevile kwa kuona changamnoto hizo. Naomba tu aendelee kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo na Serikali kwa pamoja tutashirikiana kufanikisha ujenzi ukamilike kwa haraka ili kituo hiki kiweze kutumika. Ukarabati wa kituo kingine utategemea na hali ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutamalizia swali la mwisho la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Edwin Mgante Sannda, sasa aulize swali lake.

Na. 216

**Elimu Bure kwa Kidato cha Tano na Sita**

**MHE. EDWIN M. SANNDA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza Sera ya Elimu Bure kwa kidato cha tano na sita ambalo ndilo kundi pekee liliobaki kugharamiwa na Serikali?

## **NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Edwin Mgante Sannda, Mbunge wa Kondoa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka kipuambele cha kuhakikisha fursa sawa ya kupata elimu kwa ngazi ya elimu ya awali, msingi na sekondari, kidato cha kwanza hadi cha nne kwa sababu hii ndiyo ngazo ya elimu ambayo humpatia mhusika *study* za msingi za kuweza kukabiliana na mazingira yake. Dhana ya elimu bila malipo inazingatia uendeshaji wa shule bila ada wala michango ya aina yoyote ya lazima kutoka kwa wazazi au walezi wa wanafunzi na hivyo kuondoa vikwazo vya uandikishaji na mahudhurio ya watoto shulenii.

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya mpango huu, Serikali inafidia ghamraza za uendeshaji wa shule ambapo hupeleka fedha moja kwa moja shulenii kama fidia ya ada, chakula cha wanafunzi na fedha za ruzuku ya uendeshaji wa shule (*capitation grants*). Jumla ya fedha ya kugharamia elimu bila malipo inayotolewa na Serikali kila mwezi kwa ajili ya shule za msingi na sekondari ni shilingi 20,805,414,286.14. Katika hizo, shilingi 5,459,265,929 ni kwa ajili ya shule za msingi na shilingi 10,054,298,857 ni kwa ajili ya shule za sekondari; na shilingi 5,091,850,000 ni posho ya madaraka ya Maafisa Elimu Kata, Walimu Wakuu na Wakuu wa Shule. Serikali pia hupeleka fedha kiasi cha shilingi 6,005,374,781 kwa ajili ya chakula cha wanafunzi wa bweni wa shule za sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Elimu Bila Malipo umeonesha mafanikio makubwa tangu ulipoanza mwaka 2016. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na uandikishaji na uimarishaji wa mahudhurio ya wanafunzi darasani, kwa mfano, watoto wa darasa la awali walioandikishwa wameongezeka kutoka wanafunzi 1,015,030 mwaka mwaka 2015 hadi wanafunzi 1,320,574 mwaka 2017

sawa na ongezeko la watoto 300,544, yaani ongezeko la asilimia 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya wanafunzi wa darasa la kwanza walioandikishwa imeongezeka kutoa wanafunzi 1,028,021 mwaka 2015 hadi wanafunzi 1,896,584 mwaka 2017 sawa na ongezeko la wanafunzi 868,563 ambalo ni ongezeko la asilimia 84.48.

Aidha, udahili wa wanafunzi wa kidato cha kwanza umeongezeka kutoka wanafunzi 451,392 mwaka 2015 hadi wanafunzi 554,400 mwaka 2017. Hili ni ongezeko la wanafunzi 103,000 ambalo ni sawa na asilimia 22.82. Hali hii imetokana na mwitikio chanya wa wazazi na jamii kuhusu elimu bila malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mafanikio ya Mpango wa Elimu Bila Malipo, Serikali inafanya jitihada za kukabiliana na changamoto zilizojitekeza kama vile mahitaji makubwa ya vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo, maabara, madawati, walimu, vifaa vya kufundishia na kujifunzia pamoja na TEHAMA. Aidha, Serikali inaendelea kufanya ukarabati wa majengo ya shule yaliyochakaa. Lengo ni kuhakikisha kuwa elimu inatolewa kwa ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba kwa sasa Serikali haijaandaa Mpango wa Elimu Bila Malipo kwa ngazi ya elimu ya kidato cha tano na sita bali inaelekeza jitihada zake za kuboresha miundombinu na ubora wa elimu kwa ngazi zote za elimu ikiwemo elimu ya kidato cha tano na sita.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Edwin Sannda, swalii la nyongeza.

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza; kama alivyoeleza Naibu Waziri mpaka sekondari elimu bure, lakini pia ukienda Chuo Kikuu kwa elimu ya juu tunayo mikopo ya wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kundi lililobaki ni kidato cha tano na cha sita. Kwa kuwa changamoto ya uwezo wa kugharamia elimu iko pia kwa wananchi hasa ambao nao wanakwenda kidato cha tano na cha sita ambapo imapelekeea baadhi yetu nikiwemo mimi kuweka mpango mahsus i kwenye Majimbo yetu ya kuwalipia wanafunzi wanaofaulu kwenda kidato cha tano na cha sita; pamoja na changamoto ya uwezo wa Serikali; je, Serikali sasa haioni umuhimu wa kulijumuisha kundi hili la kidato cha tano na cha sita kwenye Mpango wa Elimu Bure? Hilo ni swali la kwanza. (*Makofi*)

Swali la pili. Ili mpango wowote ufanikiwe, ni lazima kuwe na lengo na dhamira ya dhati ya kuhakikisha jambo hili linafanikiwa na kuwekewa mikakati. Kama tunavyozungumzia kwenye upande wa maji, tunasema mpaka 2020/2021 tuwe tumefikia asilimia 85 ya Watanzania wawe wanapata maji safi na salama; je, Serikali haioni umuhimu sasa kuweka muda mahususi kwa maana ya *time frame* na malengo lini tutaanza kutoa elimu bure kwa kidato cha tano na cha sita kama ilivyo kwenye maeneo mengine? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaingia kwenye maswali, naomba nikiri kwamba Mheshimiwa Sannda ni mmoja kati ya Wabunge wanaofuatilia sana masuala ya elimu. Pale Wizarani amezoeleka sana kiasi kwamba haulizwi tena kwamba anataka kuonana na nani? Kila siku utamkuta yupo mlangoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kama Serikali ina nia ya kuhakikisha kwamba hata kidato cha tano na sita nao wanapata mpango ule wa elimu bure, kwa sasa Serikali imeweka nguvu nyingi katika kukabiliana na changamoto ambazo zimejitokeza baada ya elimu bila malipo kuanza kutekelezwa, lakini baadae kadri fedha na uwezo

utakapoimarika tutafikiria hata kwa elimu ya kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, kwamba kwa nini angalau tusiweke basi mpango wa muda mrefu; nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba pamoja na kwamba haionekani kwenye mipango yetu kuhusu muda, lakini nia yetu kama Serikali ni kuhakikisha kwamba kadri uwezo unavyoongezeka kuendelea kutoa changamoto zinazowakabili wananchi kwenye Sekta ya Elimu na ikiwezekana huko mbele kadri uchumi wetu utakapoimarika kama nchi, hakuna shida hata mpaka Chuo Kikuu inaweza ikawa elimu bure kama ilivyo kwenye baadhi ya mataifa ya Ulaya.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwenda, kwa hiyo, tunaendelea. Kwanza nilete matangazo tuliyonayo siku ya leo na nitaanza na matangazo ya wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Wageni watatu wa Mheshimiwa January Makamba ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ambao ni wadau wa Mazingira kutoka *World Wide Funds For Nature (WWF)*, karibuni sana.

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Jumaa Aweso ambaye ni Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, ambao ni familia yake kutoka Pangani Mkoani Tanga wakiongozwa na Bi. Fatma Masanga ambaye ni mama yake mzazi, karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni 105 wa Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira kutoka UWT Kata ya Msalato na wageni wake wengine ambao ni Wanachuo wa *Dodoma Secretarial College (DOSCO)*, karibuni sana. (*Makofii*)

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Willy Qambalo ambaye ni Mbunge na huyu mgeni wake anatoka Karatu Mkoani Arusha anaitwa Joseph Amsi, karibu sana. (*Makofii*)

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Mwantumu Haji, ambaye ni mtoto wake Zanzibar naye anaitwa Rukia Haji Ussi, karibu sana. (*Makofi*)

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Martin Msuha ambaao ni ndugu zake, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Maria Kangoye ambaao ni wanafunzi kutoka Chuo cha Serikali za Mtaa Hombolo Dodoma, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Aida Khenani ambaye ni ndugu yake kutoka Zanzibar naye ni Ndugu Zuhura Mohamed Mwinyi, karibu sana. (*Makofi*)

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambaye ni Dkt. Frank Manase ambaye ni daktari wa binadamu kutoka Dar es Salaam, karibu sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni 20 wa Mheshimiwa Eng. Ramo Makani ambaao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotoka Tunduru Mkoani Ruvuma, karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tunao wageni waliotembelea Bungeni kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wanafunzi 80 na walimu watatu, kutoka Chuo cha Afya ya Maendeleo ya Jamii kilichopo Jijini Dodoma. Nadhani watakuwa bado hawajaingia.

Tangazo lingine linatoka kwa Mkurugenzi wa Shughuli za Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa leo siku ya Jumatano tarehe 9 Mei, 2018 kutakuwa na warsha itakayohusu Uhamasishaji wa Afya Bora na Jinsi ya Kujikinga na Magonjwa Yasiyoambukiza (*Non Communicable Diseases*).

Waheshimiwa Wabunge, warsha hii itaratibiwa na Taasisi ya Magonjwa yasiyo ya ambukiza nchini inayoongwa na Dkt. Kaushik Ramaiya ambayo imekuwa mstari wa mbele

katika kuhamasisha jamii kujikinga na kupambana na magonjwa yanayohusiana na kisukari, kiharusi, shinikizo la damu na kansa. Waheshimiwa Wabunge wote, mnaombwa kuhudhuria warsha hiyo muhimu itakayoanza saa 7.00 mchana mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge katika Ukumbi wa Pius Msekwa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Jasson Rweikiza ambaye ni Katibu wa Wabunge wa CCM, naye anawatangazia Wabunge wa CCM kuwa kutakuwa na *caucus* kwa Wabunge wote wa CCM leo Jumatano tarehe 9 Mei, 2018 saa 8.00 mchana Ukumbi wa *White House*. Mnasisitizwa wote kuhudhuria bila kukosa.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea, niwakumbushe mwongozo aliowahi kuutoa Mheshimiwa Spika kuhusu maswali. Maswali ya msingi kuwa marefu na pia majibu ya msingi kuwa marefu. Kwa sababu watalaam wa Wizara wako hapa, Mheshimiwa Spika alishatoa mwongozo. Swali limeuliza lini? Majibu yake yanajaa ukurasa mzima.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani wote tunajua, hata sisi maswali ya nyongeza, mtu anauliza dakika tatu swalii la nyongeza. Majibu kwa sababu tunapewa mapema, tutayariske hayo maswali kabisa, kuliko unaenda unasema je, unaanza kwa sababu, unasema je, unasema kwa nia, unasema tena je? Sasa uelewe hayo ni maswali matatu au ni swalii moja?

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, naomba tuzingatie huo mwongozo aliota Mheshimiwa Spika, lakini pia Wizara zizingatie mwongozo huo wa kuleta majibu mafupi. Nadhani wanaoongoza kwa mfano mzuri ni Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, wanaleta majibu mafupi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

## MWONGOZO WA SPIKA

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jaku, Mheshimiwa Bobali, Mheshimiwa Maftaha, Mheshimiwa Gimbi Masaba, mwingine nani?

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI:** Nipo hapa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa LijuaLikali.

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI:** Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jaku.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza na mimi niungane na Mheshimiwa Selemani Jafo kwa jinsi ulivyoendesha mashindano yale ya *Tulia Marathon* na vilevile ni mtu wa mazoezi. Jana niliona Mawaziri wawili wakifanya mazoezi, wakati wa maswali na majibu ya Naibu Waziri mmoja kupanda ngazi na kushuka, alikuwa Mheshimiwa Mwaijage na nguo zake nzuri, Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Ashatu Kijaji na Mheshimiwa Jenista Mhagama wakipanda ngazi na kushuka wakati wa maswali na majibu. Niwafahamishe tu kwamba wakati wa mazoezi unakuwa asubuhi au jioni. Niliiwaonea huruma sana jana mimi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu, imesimama kwenye Kanuni 68(7) nafikiri nisipoteze muda wako kuusoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pana kadhia ya muda mrefu imetokea na Serikali naona imekaa kimya na hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa muda huu kuhusu Benki ya FBME. Kuna wafanyakazi mpaka muda huu hawajalipwa, kuna watu tayari wameshakwenda mbele ya haki, kuna watu wanadaiwa Mahakamani wanataka kulipa na dhamana wa benki na *Bureau de Change* ni Benki Kuu. Nao kwenye vyombo vyaa habari utasikia pesa hizo ziko salama. Usalama uko wapi? Mpaka leo wateja hawajalipwa wanateseka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tuelezeni sababu gani? Serikali ndio hii. Jana tumeshuhudia mwongozo wa mafuta hapa, leo tunategemea jawabu litapatikana. Naiomba Serikali kuna wapiga kura wetu huko wanateseka, wakati ni mgumu. Kwa hiyo, naiomba Serikali ije itufahamishe suala hili kwa umakini wa hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo mafupi, naomba mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Nasimama kwa Kanuni ya 47, ikikupendeza angalau Bunge lako lipate dakika 30 tujadili suala ambalo ni mahsusni na ni la dharura kutokana na muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Waheshimiwa Wabunge wanachangia Ofisi ya Rais, lilizungumzwa suala la tende kuingizwa kwa kodi na nyngine zile ambazo zinaletwa kwa misaada kushindikana kurudi na nyngine kwenda kushushwa Kenya. Mheshimiwa Kubenea aliomba mwongozo humu ndani ya Bunge wiki iliypita. Siyo hivyo tu, Mheshimiwa Bashe naye akaomba mwongozo humu ndani ya Bunge. Jambo hili Serikali limekaa kimya, hakuna majibu yanayotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mwezi wa ramadhani unaanza wiki iiao, lakini hapa tunapozungumza, kuna makontena yapo kwenye meli yametolewa kwa msaada wa mali za wakfu. Watu wanajichangisha mali zile za wakfu, zinaletwa katika nchi zetu hizi na wao wanatafuta thawabu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naliomba Bunge lako kwa ridhaa yako, angalau nusu saa, kwa sababu jambo hili pia linaiaibisha Serikali hii kuona kwamba kwa nini Kenya tende zinaingia bure, Zanzibar bure, Rwanda bure, Msumbiji bure; ni Tanzania peke yake katika ukanda wetu ambako

tende zinatozwa kodi na ikijulikana kabisa kwamba tende ni bidhaa muhimu kwenye mwezi wa Ramadhani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wote bila itikadi tuunge mkono, tulijadili jambo hili. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bobali, hiyo Kanuni ukiisoma vizuri huwezi kutoa hoja sasa. Kwa hiyo, umeshaeleweka, wewe kaa. Ili uweze kutoa hoja, lazima nikuruhusu baadae.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maftaha.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mapema jana na leo, viwanja hivi vya Bunge, tunao wageni wa Wizara ya TAMISEMI ambaao ni watendaji wa Wizara ya Ardhi wanaotoka Manispaa ya Dodoma ambaao wanafanya kazi ya kuhakikisha kwamba sisi Wabunge tulipo hapa tunapewa viwanja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maftaha ili nielewe, unasi mama kwa kanuni ipi?

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kwa Kanuni ya 68(7) na nilichojaribu kusema ni kwamba Bunge hivi sasa, sisi kama Wabunge, japokuwa kanuni hazikatazi kufanyika Vikao vya Kamati za Bunge maeneo mengine zaidi ya Dodoma, lakini hivi sasa Serikali imeamua kwamba vikao vyote vya Kamati za Bunge tunafanya Dodoma lakini pia Vikao vya Bunge tunafanya Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa mwaka takribani Waheshimiwa Wabunge tunaishi Dodoma miezi saba, ukipiga mahesabu katika siku zile za Kamati na siku zile za Mabunge madogo na Bunge hili kubwa la Bajeti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mwongozo wangu, nilikuwa naomba kwako kwamba jana na leo katika viwanja hivi nya Bunge tumekuwa na wageni wanaotoka TAMISEMI (Halmashauri ya Jiji la Dodoma) ambao wanagawa viwanja kwa Wabunge na viwanja hivi vimepewa *limit* ya malipo yake yaani ndani siku 30 uwe tayari umeshalipa kiwango kile chote.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba mwongozo wako; kwa kuwa Wabunge tunapokuwa Dodoma kwenye Vikao nya Bunge na Vikao nya Kamati za Bunge lazima tuishi mazingira ambayo ni *comfortable*, tuwe na majumba hapa Dodoma kwa sababu tunakaa muda mrefu, kwa nini Wizara ya TAMISEMI isione umuhimu wa kushirikiana na Bunge kwamba vile viwanja viweze kulipwa hata kwa miezi sita hata saba taratibu taratibu badala ya kulipa kwa siku 30? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako kwamba Bunge liweke utaratibu, kwa sababu nchi ina mihimili mitatu; ina Bunge, *Executive* na Mahakama. Sisi wote tunafanya kazi kwa kushirikiana. TAMISEMI ni Serikali pia. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba uwekwe utaratibu tuweze kulipa hata kidogo kidogo ndani ya miezi kadhaa ili tuweze kuwa na viwanja wote hapa Dodoma kwa sababu tunaishi kwa muda mrefu hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako Mheshimiwa Naibu Spika. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Naona kama Mheshimiwa Bilago ana majibu tayari alitaka kukupa hapo. Mheshimiwa Gimbi Masaba.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) na kutokana na muda, naomba nisiisome.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nauliza swali langu la msingi namba 215, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, hajanijibu swali langu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati anajibu amesema kwamba hata Mbunge wa Jimbo la Itilima wakati yeye alifanya ziara kule alimwambia kwamba atajenga Kituo cha Polisi. Sasa nataka kujua kwa nini amelidanganya Bunge kwamba kuna kituo kule Wilaya ya Itilima kinajengwa ilhali hakuna kituo kinachojengwa? Hali kadhalika, niliyeuliza swali ni mimi kwa misingi ya kwamba ni moja ya uwajibikaji nami kama Mbunge. Kwa nini aje kujibu majibu ya Mbunge wa Jimbo la Itilima? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako, ni halali kwa Naibu Waziri kujibu majibu ya Waheshimiwa Wabunge? (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lijualikali.

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kwa Kanuni ya 68(7). Humu Bungeni tunaongozwa kwa Kanuni na Mbunge anapozungumza, anazungumza kwa kufuata Kanuni. Kama ameongea jambo ambalo limeenda kinyume na utaratibu, aidha, kiti chako kinamwambia afute kauli, ama *Chief Whip* anasema futa kauli na Mbunge anapaswa kutekeleza hiyo amri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ambacho nashangaa ni kwamba tukiwa tunazungumza humu Bungeni unakuta hujapewa amri yoyote ya kufuta kauli, unaongea mpaka mwisho, unapewa *Hansard* iliyokamilika kwa asilimia mia moja kila ambacho ulikizungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha ajabu watu hawa wa *Hansard* tunapoenda kuomba *clips* zetu kwa ambacho tumeongea humu Bungeni, kinakuwa kimekatwa kwa asilimia karibu 90. Wakati kiti hakijianiambia nifute kauli yoyote watu wa *Hansard* kwenye *clips* za *video* zile wanakata kwa asilimia 90.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nifahamu, hawa wanaokata hizi *clips*, wanakata hotuba zetu kwa amri ya nani? Nani anatoa hii amri wakati Mbunge nimeongea

Bungeni, kiti kimeruhusu niongee mpaka nimemaliza. Huyu anayekata haya maneno yetu, anakata kwa Kanuni ipi? Kwa nguvu ipi? Kwa maelekezo ya nani? Ili iweje? Kwa faida ya nani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipate Mwongozo. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa miongozo kadhaa hapa. Nimeombwa Mwongozo na Mheshimiwa Jaku akitumia Kanuni ya 68(7) na ametoa maelezo marefu kuhusu kadhia ambayo waliokuwa wateja wa *Federal Bank of Middle East* wamepata kwa upande wa Zanzibar. Anasema kwa muda wa miaka mitatu wateja hawajalipwa mpaka wengine wamepoteza maisha.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 68(7) inanitaka nitoe Mwongozo kwa jambo lilitotokea mapema Bungeni siku hiyo, lakini hata hivyo kwa sababu amelizungumza hapa na ni wananchi wanaopata taabu, Wizara ya Fedha imesikia impatie Mheshimiwa Jaku ufanuzi kuhusu jambo hili ili naye aweze kuwafafanulia wapiga kura wake.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijajibu Mwongozo wa Mheshimiwa Bobali, nimeombwa Mwongozo na Mheshimiwa Maftaha kuhusu viwanja ambavyo sasa vinagawiwa hapa, lakini Wabunge kutakiwa kulipa katika siku 28 au mwezi mmoja. Mheshimiwa Maftaha ametoa maelezo marefu ambayo sina haja ya kuyarudia na katika maelezo yake akataka pengine mwongozo utolewe ili Waheshimiwa Wabunge walipe ndani ya miezi sita.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyozungumza, Mwongozo wa Kiti unatoka kwenye jambo lilitotokea mapema humu ndani na swali ni kama hili jambo linaruhusiwa ama haliruhusiwi. Utaratibu wa kuomba muda wa ziada kwenye kulipia viwanja ambavyo vinatelewa chini ya Wizara ya Ardhi, ni utaratibu nje ya kikao hiki cha Bunge.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ambao wana shida hiyo, kwa sababu nimeona makofi yamepigwa mengi, wafuate huo utaratibu wa kuijulisha Wizara kwamba wanahitaji muda zaidi, lakini kitu hakina mwongozo kwenye jambo hilo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa pia Mwongozo na Mheshimiwa Gimbi Masaba akitumia Kanuni ya 68(7) kuhusu majibu yaliyotolewa wakati Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi akijibu swali namba 215 ambalo limeulizwa na Mheshimiwa Gimbi Masaba.

Mheshimiwa Gimbi Masaba anasema, Mheshimiwa Naibu Waziri amedanganya kwamba kituo kinajengwa wakati hakuna. Kwa maelezo ya Mheshimiwa Gimbi Masaba, ni kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri wakati akijibu swali la msingi alisema, Mbunge wa Itilima Mheshimiwa Njalu Silanga alipotembelewa wakati Naibu Waziri ameenda huko alimwambia anajenga hicho kituo. Kwa hiyo, hicho kituo hakipo wala hakijengwi, kwa hiyo, swali la Mheshimiwa Masaba halijajibiwa na pia ametoa maeleze kwamba, kwa kuwa yeye ndiye aliyeuliza anataka kujua kama inaruhusiwa Mheshimiwa Naibu Waziri kuja kujibu akizungumzia Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo hilo wakati aliyeuliza na yeye ana uwezo wa kuuliza swali kwa kuwasemea watu wa Simiyu na Itilima.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ameuliza mambo mawili hapa, moja ni la kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri amedanganya katika majibu yake na pili ni kuhusu yeye ndiye aliyeuliza yote haya mawili nitayatolea mwongozo hapo baadaye baada ya kujua kama Mheshimiwa Naibu Waziri alichokisema kwa swali ambalo Mheshimiwa aliuliza kina makosa kwa hiyo mwongozo huu nitautoa baadae leo.

Waheshimiwa Wabunge, pia nimeomba mwongozo na Mheshimiwa Peter Lijualikali ametumia Kanuni ya 68(7) akitoa maelezo kwamba Bunge hili linaongozwa kwa mujibu wa Kanuni tulizojiwekea na ametoa maelezo kwa kirefu

ambayo sina haja ya kuyarudia nae amezungumzia hasa kuhusu *Hansard* kwamba inapoletwa Taarifa Rasmi za Bunge zinakuwa ziko kamili kwenye kila jambo allolizungumza Mbunge kwa asilimia mia moja, lakini Waheshimiwa Wabunge wanapokwenda kuomba maelezo hayo ambayo yapo kwenye *clips* za *video* anasema yanakuwa yamekatwa kwa asilimia 90, anauliza hapo maswali mengi kwamba nani anayewatuma kukata hiyo asilimia 90 wakati katika hali ya kawaida Taarifa Rasmi za Bunge zinaweka mambo yote isipokuwa yale ambayo yamekatazwa humu ndani Kikanuni au kama mtu alisimama na kusema maneno hayo yafutwe kwa utaratibu tulionao.

Waheshimiwa Wabunge, Taarifa Rasmi za Bunge huchapwa na Mbunge hukabidhiwa, lakini utaratibu wa Bunge kutoa *clips* za Waheshimiwa Wabunge huo ni utashi wao watoaji, kwa hiyo hata kuna wakati wanaweza wasikupe na wala hawalazimiki kufanya hivyo. Kwa hiyo, kama kuna jambo lolote ambalo umeenda kuomba na wao hawajajikamilisha wewe waambie unaomba muda wako wa dakika 10, labda wamekupa dakika mbili badala ya 10. Kwa hiyo, waambie unahitaji zote inategemea ninyi mmetumia utaratibu upi kuzipata hizo taarifa. Lakini Taarifa Rasmi za Bunge ni zile zilizoandikwa na si hizi tunazozungumza. Kwa hiyo, ndiyo utaratibu tulionao Waheshimiwa Wabunge. Hii habari ya kukata na kutokukata yale ambayo unayoyaletewa kimaandishi ndiyo Taarifa Rasmi za Bunge na siyo hii ambayo inakuwa imerekodiwa wakati tukizungumza. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, kuna jambo amelieleza Mheshimiwa Hamidu Bobali akitumia Kanuni ya 47 kwamba kuna hoja kuhusu tende ambazo huletwa na wahisani tuseme wa maeneo mbalimbali na wakati mwingine Serikali inashindwa kuingiza hizo tende bila ya kudai kodi wakati zimekuja kwa msaada, na ametoa maelezo kwamba Mheshimiwa Saed Kubenea na Mheshimiwa Hussein Bashe walishawahi kuomba juu ya jambo hili na bado Serikali iko kimya.

Mheshimiwa Bobali ametoa maelezokwamba kuna makontena ambayo mengine yapo njiani na mengine yapo bandarini na bado Serikali hajasema lolote kuhusu jambo hili. Ametumia Kanuni ya 47 akitaka jambo hili tulijadili na ametaja na muda hapo wa dakika 30, hizi dakika 30 ni pale ukitumia Kanuni ya 69, kwahiylo Kanuni ya 47 siyo lazima utaje muda. Ila kwa jambo hili anatoa maelezo kwamba limeshazungumzwa humo ndani, na utaratibu wake upo kisheria Serikali imeshakusikia nadhani ilifanyie kazi jambo hili ione namna bora ya kulishughulikia. Kama mbavyo Mheshimiwa Hamidu Bobali ametaja mifano ya huko kwengine mimi sijasisoma sheria zao na kujua zinasemaje lakini sheria tunatunga kama Bunge watekelezaji Serikali, upande wa watekelezaji muangalie namna ya kulishughulikia jambo hili lili mwezi wa Ramadhani basi wenzetu wa imani ya dini ya Kiislam waweze kupata hizo huduma ambazo zipo klutaratibu. Baada ya kusema hayo tutaendelea. Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji na  
Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. JAKU HASHIMAYOUB:** Mheshimiwa Naibu Spika ungeagiza Wizara ya Fedha inijibu ndani Bunge hili.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeletewa orodha hapa...

Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub naona umesimama Wizara imekwisha kusikia hilo jambo Kiti hakiwezi kutolewa mwongozo kwa sababu halijatokea hapa ndani. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha yupo pale na amekusikia.

Waheshimiwa Wabunge, imeletewa orodha za

vyama vyote vilivyoko Bungeni ambavyo vinataka kuchangia, tutaanza na wachangiaji wa CCM Mheshimiwa Emmanuel Papian John, Mheshimiwa Mussa Sima atafuatia, Mheshimiwa Oran Njeza ajiandae.

**MHE. EMMANUEL P. JOHN:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Waziri kwa hotuba na kwa bajeti yake ambayo ameweza kutuwasilishia. Niombe kumshukuru kwa Bwawa la Dongo ambalo limewekwa kwenye mpango ambapo hili bwawa sasa kwa pesa zilizotengwa japo ni kidogo, lakini naomba hizo pesa zitoke na usanifu uendelee ili wale wananchi wa vijiji vya Dondo na Laiseri viweze kupata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kiteto ina tatizo kubwa sana la maji kwa kipindi kirefu na kwa maeneo mengi ambayo tumekuwa na tatizo na maji ni kwamba tuliahidiwa kupata mabwawa kwa sababu yale maeneo ni kame. Ninaomba Waziri na Wizara yake waweze kutusaida kukarabati mabwawa yetu upande wa Makame, bwawa ambalo lilichimbwa na wananchi lakini halijakamiliaka katikati ya Lukiushi na Makame.

Ninaomba pia kukarabatiwa Bwawa la Matui ambalo Mheshimiwa Waziri ulilionia, ulilikagua na ukaona kwamba linastahili kukarabatiwa na ni bwawa kubwa ambalo linastahili kukarabatiwa na lipate pesa kwa ajili ya maji ya binadamu, pia umwagiliaji kwa ile kanda ambayo kuna wananchi zaidi ya 20,000 ulijionea mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna bwawa la umwagiliaji la Enguselo, hili bwawa limefanyiwa upembuzi yakinifu wananchi walishaachia yale maeneo yao kwa hiari yao na maeneo mengi yameshaachwa kwa muda mrefu na mashamba wameyaacha. Sasa ni lini Wizara itatenga pesa muda wa kufanya uhuishaji kwa kukarabati lile bwawa na kuliujenga tayari kwa wanachi kuweza kulitumia kwa ajili ya kilimo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo mabwawa mengi kwa sababu Kiteto ni eneo kame, na jambo la kutusaidia ni mabwawa, kwa mazingira yetu ya wafugaji na wakulima ni lini Serikali itatusadia kupata mabwawa upande wa Makame, Ndido, Rorela, maeneo ambayo ni kame lakini wafugaji wengi hawana mabwawa na mifugo inalazimika kwenda upande wa Simanjiro, upande wa Kilindi na kwenda upande ambako mifugo yetu inalazimika kutafuta maji ikihangaika huku na kule na wafugaji wanapata shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo miradi mingi ya vijiji ambayo haijakamilika, tunaomba Serikali itsaide ni namna gani tunaweza kupata pesa ili hii miradi ya vijiji vya Dosidosi, Ndughu, Nguselo, Lergu, Ndido, Songambele na vijiji vyetu vingi ambavyo sasa viro kwenye mpango vingine nimevitaja kwenye maandishi baada ya kuwa nimekuandikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba kwa mpango wetu bajeti tuliyotengewa ni ndogo, karibu shilingi bilioni 1.329, sasa Mheshimiwa Waziri kwa pesa hii umepunguza bajeti yetu kwa bajeti ya mwaka jana, kwa bajeti hii miradi yetu ya maji na shida tulizonazo hebu niambie Waziri tunakwenda wapi? Nikuombe Waziri *review* bajeti yako, fika mahali sasa Kiteto uionee huruma, kwa jinsi ambavyo tuna shida ya maji muda mrefu, katika ilani yetu ya utekelezaji 2015 - 2020 ni mikoa mitano ambayo ipo kwenye *plan* na ni mikoa kame ambayo ilikuwa na *priority*. Mkoa wa kwanza ni Simiyu, Mkoa wa pili ni Dodoma, Mkoa wa tatu ni Singida, Mkoa wa nne Shinyanga na Mkoa wa tano ni Manyara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Manyara leo kwenye bajeti ukiangalia mkoa mzima sisi ni karibu bilioni 7.9 ambayo ni pesa tuliyotengewa. Ukiilinganisha na mikoa ambayo bado ina maji na vyanzo vingi vya maji, sasa Mheshimiwa Waziri nikujombe hili nenda nalo, angalia ni namna gani ya kufanya uweze ku-rescue mkoa mzima wa Manyara kwa sababu ya hali nzima kubwa ya upungufu wa maji tulionao kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nmshuruku Mheshimiwa

Waziri kwa kututengea pesa kwa ajili ya Mji wa Kibaya, Mji huu ulikuwa ni kame kwa muda mrefu, lakini tuna visima vingi ambavyo vimechimbwa kwa msaada wa jitihada zetu za pesa na ndani kwa maana ya Halmashauri yetu na Mkurugenzi na Baraza letu la Madiwani tumekaa tukapanga tukachimba visima, sasa tunaomba pesa kwa ajili ya ukamilishaji, tunamalizia ili yale maji na zile tenki tulizojenga pale ulipokagua wewe mwenyewe ulivyofika *site* tuweze kupata namna pesa zinaweza kutusaidia kuhakikisha kwamba zile tanki zinakamlilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, visima vinafungwa pampu maji yanapandishwa pale ulipoona kwenye tanki ili Mji wote wa Kibaya uweze kusambaa maji kwa ajili ya matumizi ya watu wetu kulingana na jinsi ambavyo unaona yale maeneo yetu watu wanaongezeka, ujenzi unaongezeka, lakini na matumizi ya maji yanatakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo shida kubwa muda mrefu sana ambayo imetukabili kwa mazingira yetu ya maji, lakini kumekuwa na miradi mingi ambayo imekuwa inahujumiwa na miradi mingi unakuta tunao mradi wa Matui ambo ulijengwa pale Chapakazi zaidi ya milioni 600 zimetumika lakini wananchi hawapati maji, mradi upo nikuombe Mheshimiwa Waziri utakapopata nafasi baada ya maswali na majibu tuongozane, twende Chapakazi uone mradi uliogharimu shilingi milioni 600, kodi za Watanzania na wananchi hawapati maji ili uweze kujiridhisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuomba kwamba lile eneo la Matuhi unalifahamu, kuna zaidi ya watu 20,000 tumekubaliana kwamba kisima cha Nchimila kifungwe *pump*, kifungwe umeme ili kiweze kusambaza maji. Tumeshakuletea ile *planned feasibility design* nzima imeshakuja, Wizarani tunaomba *approval* ile *design* iweze kwenda na tupate pesa ili kuhakikisha kwamba tunatandika mabomba wale wananchi zaidi ya 20,000, ikiwemo vituo vya afya makanisa, misikiti na maeneo yote ya makazi na vituo vidogo zaidi ya 40 zimeshakuwa *designed* waweze kupata maji kwa sababu kunaweza kutokea mlipuko wa magonjwa kipindi

kijacho kwa sababu ya upungufu wa maji na shida kubwa ya maji ya watu ambayo wanapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, ahsanta sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Musa Sima atafuatiwa na Mheshimiwa Oran Njeza na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko ajiandae.

**MHE. MUSA R. SIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru na nikupongeze sana kwa *Tulia Marathon*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri wanayoiendelea kuifanya kwenye Wizara yao ya Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue hii kuwashukuru kwenye taarifa yake ya kwenye kitabu hiki Singida Mjini walau tumeonekana, ninamshukuru sana. Eneo langu la Irau pale Kisaki limetengewa fedha kama shilingi milioni 900 na kama haitoshi kuna fedha zingine za upanuzi wa miundombinu ya maji kama shilingi bilioni moja, kwa ujumla yake tumepata kama shilingi bilioni tatu. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuieleza hofu yangu ya upatikanaji wa fedha hizi, inanitia mashaka kidogo kama fedha hizi zitakuja, kwa sababu bajeti ya mwaka 2016/2017 nilitengewa shilingi bilioni 2.4 fedha hizi hazikuwahi kuonekana mpaka leo. Mheshimiwa Waziri alifika Singida akasema tumetengewa fedha, lakini akiwa bado anachangia Mpango wa Maendeleo hapa Bungeni alitolea mfano wa Singida kwamba tulitengewa fedha na hatukuziomba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kulisema hili kwa sababu katika mazingira ambayo ninayaona Wizara inatenga fedha zinazokwenda Halmashauri na mimi

nakwenda kuongea na wananchi wangu kuwaambia tumetengewa fedha za maji zinakuja, lakini fedha haziji na Mkurugenzi anaulizwa anasema hana taarifa ya fedha zinazoletwa na Wizara. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto hii imekuwa kubwa sana ndiyo maana hofu hii naileleza wazi. Lakini nimeendelea kuifuatilia na katika kufuatilia kwangu nimegundua uzembe mkubwa sana unaofanywa na Halmashauri zetu hizi, ukiangalia malalamiko makubwa ya miradi ambayo haitekelezwi kwenye Halmashauri ni miradi ambayo inasimamiwa na TAMISEMI. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tuliweke jambo hili wazi, Wizara ya Maji inatenga fedha, lakini fedha zinazokwenda Halmashauri zinasimamiwa na TAMISEMI na TAMISEMI tumekwishamaliza bajeti yao hapa, sasa niombe Serikali iangalie jambo hili na ninaiomba Idara ya Maji kwenye Halmashauri isibaki kwenye Halmashauri, isimamiwe na Wizara ya Maji na Umwagilaji. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeweza kutofautisha leo Wizara ya Afya, hospitali za Rufaa za Mikoa zinasimamiwa na Wizara ya Afya, kwa nini Idara za Maji za Halmashauri zisisimamiwe na Wizara ya Maji ili kuweka utaratibu mzuri wa kuweza kulisimamia jambo hili. Eneo hili linatupa mkanganyiko mkubwa sana na TAMISEMI imeshakuwa kubwa, hebu tuipunguzie mzigo yenye ibaki kufanya *monitoring*, suala la maji libaki kwenye eneo la Wizara ya Maji, niuombe Mheshimiwa Waziri akija alione eneo hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi naungana na wenzangu kuomba kuundwe tume ili kuweza kufatilia miradi ya maji ambayo imeshindwa kutekelezeka na mikataba mibovu iliyotengenezwa huko nyuma imefanya wananchi wetu wasipate maji, niombe sana Bunge lako liweze kuliangalia hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo fidia ya maji kwenye maeneo yetu, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri alitupatia

fedha kwenye Kata yangu ya Mwankoko shilingi 1,500,000,000 lakini bado kuna fedha zingine wananchi wanadai nimuombe ili aweze kutupa hizo fedha. Lakini tunalo eneo la Irao ambalo lipo Kisaki wananchi wanadai fedha ya fidia shilingi bilioni 2.1, bado kule Misaki Mandeo wanadai shilingi milioni 200, jumla ni takribaki shilingi bilioni 2.5 nimuombe Mheshimiwa Waziri hili nalo aliangalie wananchi hao wanahitaji kulipwa fidia ya maji ili iweze kuwasaidia kwa sababu wananchi walikuwa waungwana kupisha vyanzo vya maji tuweze kupata maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Singida unakua kwa kasi sana, tunataka tuendane na kasi ya ujenzi wa viwanda. Viwanda haviwezi kujengwa kama hatuna maji ya kutosha, kuendelea kutegemea visima maji yanayochimbwa maana yake hatutafikia malengo. Ninamuomba Mheshimiwa Waziri, ule mkakati wa maji ya kutoka Ziwa Victoria unaokwenda mpaka Simiyu usiishie Simiyu, utoke Simiyu uingie Mkalama, utoke Mkalama uende Kiomboi, uingie *Singida DC*, uje Singida Mjini, Ikungi, Manyoni na Itigi, Mkoa mzima utakuwa umeweza kuingia kwenye mtandao wa maji wa Ziwa Victoria. Ninamuomba sana Mheshimiwa Waziri eneo hili ni muhimu mno hatuwezi kuendelea kutegemea visima peke yake tukawa na viwanda vya kutosha, watusaidie wasiishie Simiyu waje moja kwa moja mpaka Mkoa wa Singida na wote tutaweza kuendana na kasi hi ya ujenzi wa viwanda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Manispaa ya Singida inakua kwa kasi mnoo, kumekuwa na ongezeko kubwa la watu lakini kama haitoshi watu wanajenga kwa kasi kubwa lakini miundombinu ya maji taka haiwezi kutosheleza mazingira tuliyonayo. Wameshafanya *feasibility study* kwenye eneo la Manispaa, tunahitaji fedha ili kuweza kuweka miundombinu rafiki kwa ajili ya maji taka. Eneo hili litatusadia sana, tukiacha hivi ilivyo tutakuwa na mazingira magumu sana ya kesho kuendelea ku-solve tatizo hili kwa kutumia magari ya maji taka. Pale Singida hatuhitaji magari ya maji taka, tunahitaji kuhakikisha kwamba kuna miundombinu rafiki kwa ajili ya kuondoa majitaka yale na kwenda kwenye

Maziwa yetu tunayo mabwawa mawili pale ya Singidani na Kindai. Ni lazima Serikali ije na mkakati wa uvunaji wa maji, hatuwezi kuendelea kutegemea visima kama nilivyo sema awali na Singida tunalo eneo ambao tulikwisha lipanga kwenye *master plan* yetu, eneo hili linamiliikiwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe Mheshimiwa Waziri atusaidie kushirikiana na Wizara hii, lile eneo tulilolitenga maalum eneo lile tuweze kupewa kwa ajili ya kuchimba bwawa ili tuweze kuyavuna maji haya. Itatusaidiasana kupunguza tatizo la maji katika Jimbo la Singida Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamesema wenzangu kwamba lazima kuwe na Wakala wa Maji Mjini na Vijijini, lakini walio wengi wanazungumza Wakala wa Maji Vijijini, hapana! Tuzungumze Wakala wa Maji Mjini na Vijijini. Tumefanya kosa kwenye REA, tumezungumza Wakala wa Umeme Vijijini peke yake na leo wa Mjini tunahangaika na suala la umeme. Sasa tuzungumzie Wakala wa Maji Mjini na Vijijini, tukiliweka hivi maana yake tutaondoa shaka tunaoishi Mjini. Ninamuombe Mheshimiwa Waziri aliweke kwenye mazingira hayo, litatusaidia sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wamezungumza wenzangu kuhusu nyongeza ya shilingi 50 kwenye lita ya mafuta ya petroli na dizeli nami nataka niwaunge mkono, ukifanya hesabu ya haraka unaongeza kwenye bajeti hiyo isiyopungua bilioni 160, siyo fedha ndogo. Niwaombe sana Wabunge wenzangu na niiombe Serikali ione umuhimu huu wa kuweza kuweka nyongeza hii. Tutaondokana na tatizo la maji kwenye mazingira haya ambayo yanatukabili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nichukue fursa hii kuunga mkono bajeti na nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri, ama hakika kitabu hiki walimu tuliozoea kusoma kitabu hiki kina mikakati ya kutosha na kitabu hiki kinajitosheleza. Tukiweza kukisoma vizuri nadhani tutatumia muda wetu mzuri kuweza kutatua matatizo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Oran Njeza, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma ajiandae.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nianze kwa kumpongeza kwanza Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na timu yake ya wataalam ikiongozwa na Katibu Mkuu, wamefanya kazi nzuri sana. Ukiangalia katika hii ripoti utaona ni kiasi gani wamefanya mageuzi katika hii Wizara. Mwaka uliopita utendaji ulikuwa ni asilimia 25 lakini kwa mwaka huu tulionao wa 2017/2018 Wizara hii imetekeleza kwa asilimia zaidi ya 56. Hiyo ni mara mbili ya ule utekelezaji wa mwaka jana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninapenda kumpongeza Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa ziara walizozifanya kwenye Jimbo langu, zimeleta mageuzi makubwa. Naibu Waziri alikuja, alishuhudia mwenyewe miradi ya mabilioni ya pesa ambayo ripoti zake zinaonesha kuwa imetekelezwa na amekwenda *site* kwenye tenki akaambiwa hilo tenki lina maji, akapanda kwenye tenki kuangalia badala ya maji akakutana na mazalia ya popo. Kwa hiyo, inasaidia sana hizi ziara za Mawaziri wanapokwenda wenyewe *site* na kujionea ni nini kinachofanyika huko. Utekelezaji kwenye miradi mingi hasa ya vijijini ni kwa kiasi kidogo sana. Ni hela nyngi sana nchi hii zimeliwa, nakubaliana na wenzangu ambao wamependekeza kuundwe Tume ichunguze miradi ya maji ili tujue ni kiasi gani cha pesa zilizoliwa kwa vile tutaongeza tozo tutamlalamikia Waziri wa Fedha lakini kusipokuwa na usimamizi, hali huko vijijini ni mbaya sana, pesa zimeliwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni shahidi wa kilichotokea kwa Mheshimiwa Waziri kuchukua miradi ya Mbeya Vijijini, tulikuwa na asilimia mbili tu kwa mwaka

uliopita lakini alipokuja Waziri akachukua miradi yote ya Mbeya Vijiji, leo tuko na asilimia zaidi ya 60 za utekelezaji. Miradi mingi inatekelezwa vizuri sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kuna mradi wa Iwindi, Izumbe, Mwashiawala uko katika utekelezaji mzuri sana. Mradi wa Mbalizi tulikuwa tunalalamikia Mbalizi hakuna maji, lakini Waziri amechukua *initiative* zake za kuunganisha Mamlaka ya Maji Mbalizi na Mamlaka ya Maji Jiji. Miradi yote ya vijiji kumi ambayo ilikuwa imekwama kwa miaka zaidi ya saba leo hii iko kwenye utekelezaji mzuri sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata wewe mwenyewe ni shahidi, ninaomba kukushukuru kwa juhudzi zako na jitihada zako umeweza kutusaidia mradi wa Iota ambao leo hii tuna imani tutaletewa zaidi ya shilingi milioni 250 kwa ajili ya kile kijiji ambacho killikuwa hakina maji kabisa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naisoma vizuri sana hii ripoti, tunaomba maji lakini ukiangalia ukurasa wa tano, hayo maji tunayoyaombea pesa hayapo! Mwaka 1962 uwezo wa maji tuliokuwa nao ilikuwa ni mita za ujazo 7,800, mwaka jana zimepungua mpaka mita za ujazo 1,800 kwa mtu kwa mwaka. Mwaka 2025 inaonesha tutakuwa na mita za ujazo 1,500; maana yake nchi hii itakuwa imeingia kwenye nchi ambazo hazina maji. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaongea sana hapa, tunataka bajeti za maji, maji yako wapi? Naliomba Bunge lako liunganishe nguvu za Wizara hizi mbili, Wizara ya Mazingira na Wizara ya Maji zifanye kazi kwa karibu. Wenzetu wameshachukua kwa makusudi kabisa kuvuna maji. Kuvuna maji ya mvua yamewasaidia vilevile hayo maji yanayozalishwa imekuwa ni zao ambalo linaloziletea hizo nchi pesa za kigeni kwa vile maji ukiangalia nchi zinayoizunguka Afrika Kusini wanayakusanya maji ya mvua na yale maji yanapelekwa Afrika Kusini na inazipatia pesa za kigeni hizo nchi, pesa nydingi sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoa mfano wa kule

Jimboni kwangu, tuna mvua nyingi sana lakini mito mingi sasa hivi inakauka, mto Nzovwe unakauka, Mto Songwe unakauka na ukiangalia kuna mimomonyoko ya udongo, mvua zikishanyesha udongo wote unakwenda Ziwa Rukwa, na ziwa karibu linakauka. Nafikiri Wizara iangalie bajeti kubwa, ningeomba kwanza uanzie kwenye Jimbo langu kwenye Kata ya Mjele, jenga mabwawa ya kutosha ili tuweze kuvuna maji ya kutosha tuongeze huu ujazo wa maji badala ya kufanya *projections* za maji kukauka, tufanye *projections* za maji kuongezeka, hiyo *trend* ibadililike. Tusiongelee mita za ujazo 1,500, tuongelee ni namna gani turudishe mita za ujazo 7,800 na zaidi. Hilo ni jambo muhimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika bajeti ya Waziri wengi sana wamejadili kuhusu kuanzisha Mamlaka ya Maji Vijijini. Kama nilivyosema, Halmashauri yangu iwe ni *pilot*, imefanya kazi vizuri mno. Nakuomba Waziri, hili suala litakapoanza tumia *modal*/uliyotumia Mbeya Vijijini iende kila Halmashauri, italeta mageuzi mno na hatutahitaji pesa nyingi kwa ajili ya maji. Tutahitaji bajeti ndogo, pesa ndogo sana kwa ajili ya maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naungana na wenzangu kuhusu kuongeza tozo kutoka shilingi 50 kwenda 100. Ni jambo muhimu, litatuletea neema sana, ukiangalia bajeti ya mwaka huu kwa kiasi kikubwa imetegemea tozo ya mafuta ya dizeli pamoja na petroli, bila hivyo tusingefikia hiyo asilimia 56. Kwa hiyo, tunaomba tuangalize zaidi namna ya kujitegemea badala ya kuangalia ni namna gani tutegemee misaada kutoka nje ambayo kutoptaka na halilivyo sasa siyo ajabu hatutaipata hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningeomba Wizara ya Fedha ingeangalia. Kwa ile mitambo ya kuchimba mabwawa ya maji na ile mitambo na vifaa vyote vya maji vingeondolewa kodi ili viwezeshe kupunguza gharama za uchimbaji wa maji na miradi ya maji. (*Makofii*)

Baada ya kusema hayo, naomba na mimi niunge mkono hoja. Nashukuru sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Magdalena Sakaya ajiandae.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukru. Nami niweze kuchangia Wizara hii muhimu sana, Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni uhai lakini pia maji ni uchumi. Kwanza kabisa nianze na Jimbo langu la Tarime. Ukiangalia kitabu hiki *page* namba 175 ningependa kuja kupata ufanuzi wa kina kwa sababu hizi fedha ambazo mmezi-*allocate* hapa na kusema miradi imekamilika kwa asilimia 100 ni vitu viwili tofauti. Pia *page number* 180 maji ambayo tunapata Tarime yanatokana na chanzo cha Bwawa la Nyanduruma. Bwawa hili ni tangu enzi za Mjerumani mpaka sasa hivi halijafanyika ukarabati wowote limetekelezwa, alipokuja Waziri Mkuu alielekeza na Katibu Mkuu ulikuja na timu yako, nashangaa kwenye kitabu bado mmeendelea kutenga shilingi milioni 300 ambazo mmekuwa mkizitenga miaka miwili au mitatu iliyopita bila kuzileta. Ningependa kuweza kupata ufanuzi wa kina, ile timu iliyokuja iliweza kufanya utafiti upi na imeweza kushauri vipi ili lile bwawa liweze kutengenezwa kwa muda mfupi wakati tukisubiria chanzo kikuu ambacho nimekuwa nikipigia kelele hapa cha maji kutoka Ziwa Victoria ambayo itakuwa ni suluhisho kwa Wilaya ya Rorya, Tarime kwa maana ya Jimbo la Vijiji na Jimbo la Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ya Ziwa Victoria ni sehemu fupi sana ambayo yanatolewa, Shirati Jimbo la Rorya ambayo inaweza ikaleta Rorya na Tarime lakini imekuwa ni kizungumkuti kwa Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi kuhakikisha kwamba inawaletea wananchi wa Tarime na Rorya maji ili waweze kufanya shughuli zao zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nirudi kwenye hoja ambazo ni za kitaifa zaidi. Tumeshuhudia kabisa Serikali ya Chama cha Mapinduzi ikiwaambia Watanzania kwamba Sera ya Maji tutapata maji ndani ya mita 400 lakini Awamu

hii ya Tano wakaja wakatuambia kwamba wanamtua mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ni vitu viwili tofauti, wanaahidi hawatekelezi, wanapanga hawatekelezi na hii inajidhihirisha kwa hizi bajeti ambazo tumeweza kuziainisha. Bajeti ya mwaka 2015/2016 wlileta hapa Bungeni tukawatengea shilingi bilioni 485 lakini wakaweza kupeleka kwenye fedha za maendeleo shilingi bilioni 136 tu, ambayo ni sawasawa na asilimia 28. Ikaja mwaka 2016/2017 shilingi bilioni 913 wakapeleka shilingi bilioni 230 ambazo ni asilimia 25.7 tu. Mwaka 2017/2018 wakarudi tena wakaomba shilingi bilioni 623 lakini mpaka Machi ingawa Waziri ameendelea kusema zimekuja zingine, zilikuwa zimeenda asilimia 22 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hoja hii utaona kabisa Serikali ya Chama cha Mapinduzi haina dhamira ya dhati ya kutatua tatizo la maji kwa Watanzania. Watanzania ambao, akina mama wanatembea usiku kutafuta maji, wanaliwa na mamba, wanaliwa na fisi, wanapata talaka, wanabakwa, wanapata magonjwa mbalimbali ya vichocho kwa sababu maji ni mabaya, watoto wetu chini ya miaka mitano wanafariki kwa sababu maji si safi na salama, leo Serikali ya Chama cha Mapinduzi inaendelea kuwahadaa Watanzania kwamba wana dhamira ya dhati ya kutatua tatizo la maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili niweze kuungana na Mheshimiwa Mnyika ambapo jana alipendekeza tumalize michango yetu, leo jioni Wizara isihitimishe bali waende wahakikishe kwamba bajeti tulioitenga mwaka jana ambayo inamalizika Juni, iweze kupelekewa fedha walau ifikie asilimia 80 tutatue matatizo ya maji vijijini na mijini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi niliona Katibu Mkuu ametoa takwimu na hapa wamezirudia wakisema kwamba maji kwa vijijini asilimia 59 ingawa najua hii ni *average*, kuna vijiji havina maji kabisa, hata ukibaki kwenye asilimia 59 yenye na *World Bank* wamesema ni asilimia 50 utaona

kabisa kwamba hamna ile dhamira ya dhati. Asilimia 59 hii ndiyo iliyokuwepo kwenye Awamu ya Nne mwishoni, sasa ndani ya miaka miwili na nusu, Serikali ya Chama cha Mapinduzi Awamu ya Tano haijafanya chochote bado imestuck kwenye asilimia 59. Huu ni uhalisia kwamba maji siyo kipaumbele, tunatenga *billions of money* lakini hawapeleki fedha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jana ndugu yangu Mheshimiwa Anna Gidarya alifanya *analysis* hapa kwamba kuna kijiji kimojawapo Hanang wanunua maji lita 200 kwa shilingi 7,000. Kwa shilingi 7,000 kwa mwaka unatumia shilingi milioni 2.5, pato la wastani la kila Mtanzania ni shilingi milioni 2.1. Ina maana huyu anatumia pato lake zaidi kwa asilimia 119 kununua maji tu, bado mahitaji mengine na maji ya vijijini siyo safi na salama, hayajawa *treated* kama maji ya mjini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Taifa liendelee, lazima tuboreshe huduma za maji. Maji ni uchumi, bila maji hamna viwanda ambavyo mnasema Serikali ya viwanda. Maji ni uchumi, bila maji hamuwezi kujenga hizo barabara, bila maji hata magari tunayotumia hayawezi kwenda. Kwa hiyo, maji ni kila kitu. Taifa ambalo unataka liendelee lazima tuweze kuwekeza kwenye maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ni kuhusiana na ufisadi ambao wa kweli umekithiri kwenye miradi ya maji. Tunatenga bajeti zinakwenda kidogo lakini hata hiyo kidogo na yenewe inafisadiwa na hatuoni hatua zikichukuliwa pamoja na kwamba Serikali ya Awamu ya Tano mnasema mna-*fight* ufisadi, tunataka tuone kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano tu kwenye ripoti ya CAG anasema kuna mradi ulikuwa Geita ulikuwa ni wa shilingi bilioni 6.6 ambao ulisainiwa Mei, 2015 na ulikuwa ukamiliike ndani ya mwaka mmoja, katika ya kampuni ya MSJC and Company Ltd. mpaka Novemba 2017 mradi haujakabidhiwa, fedha zilitolewa zote na zilikuwa za mfadhilli (*African Development Bank*) hatua hazijachukuliwa, kitu cha

ajabu wamefanya tu kumtoa Meneja wa Maji Geita, wamempeleka Wizarani. Kumhamisha kutoka eneo moja kumpeleka eneo lingine!

Mheshimiwa Naibu Spika, hii haikubaliki na katika mantiki hiyo tunajua kuna miradi mingi Tanzania nzima imefisadiwa, tunaomba kabisa, siyo Tume, tuunde Kamati Teule ya Bunge ambao ndiyo tunaisimamia Serikali ili tuweze kuhakikisha inapita kwenye miradi yote kuainisha ujisadi umesababishwa na akina nani ili hatua ziweze kuchukuliwa. Vinginevyo tukisema tuunde hii tume kama ambavyo wenzangu walisema awali, inaenda, inajadiliwa juu kwa juu hatujui wahusika ni akina nani, Bunge tunaisimamia Serikali tuweze kuunda Kamati Teule ya Bunge iende ipitie kama ambavyo imeshafanyika huko nyuma kwenye Nishati na Madini enzi za Jairo, tuliunda Kamati Teule ya Bunge ikaja na majibu hapa tukaweza kupata ufumbuzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye maliasili na utalii tuliunda kuhusu ile operesheni tokomeza ikaja na majibu hapa tukapata ufumbuzi. Miradi ya ujisadi ya maji ambayo tunatumia kodi za wananchi maskini imekithiri ilhali Watanzania wakiendelea kufa kwa kukosa huduma bora ya maji. Tuunde Kamati Teule ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika,...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, kuna taarifa. Mheshimiwa Mtulia.

## **T A A R I F A**

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kumheshimu sana mchangiaji na kutokuwa na shaka na kiwango chake cha uelewa wa mambo, nataka nimpe taarifa kuwa jambo analolitaka liundiwe Tume ya Kibunge ni jambo ambalo tayari Mheshimiwa Rais ameshalitolea kauli na akasema hadharani kwamba yejote anayekula hela ya maji anakula sumu na Rais amekwenda mbali zaidi kuhakikisha watu wote walioshiriki kwenye ujisadi

watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, hakuna haja ya kutengeneza tume ambazo sidhani kama zitaleta tija. Tumuachie Rais aendelee nalo. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, *at a time, we don't need to waste time!*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni Bunge, linaisimaia Serikali, unavyoniambia Rais katoa kauli wakati nimetoka kusema hapa Mtendaji wa Geita amefanya kuhamishwa kupelekwa Wizarani, tafadhali sana, tusiwe tunapenda kuingiliana kwenye kuchangia kama unajua unatoa hoja ambayo haina mantiki, tuko *serious* hapa kufanya mambo ya Watanzania. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ambayo inachukua muda mrefu bila kukamilika, ambayo inazidi kuongeza gharama kwa fedha za Watanzania walipa kodi maskini, utakuta miradi inachukua zaidi ya miaka saba haijakamilika na kuhakikisha kwamba shilingi yetu thamani yake inazidi kushuka kila siku ukillinganisha na dola, kwa hiyo gharama za mradi zinazidi kuwa kubwa zaidi na huu unakuwa ni mzigo kwa Watanzania. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wa hii ni ule mradi wa Bwawa a Kidunda, Kimbiji na hata Mpera, umechukua miaka mingi sana, kwa nini Serikali inapoteza fedha za Watanzania kwa kuacha kukamilisha hii miradi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusositiza Serikali ya Chama cha Mapinduzi jana Wabunge wenzangu waliongea hapa mkawa mnawadhihaki, Serikali ya Chama cha Mapinduzi msiwekeze kwenye maendeleo ya vitu wekezeni kwenye maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa *analysis* ile ambayo mliisimamia jana mkatoa na miongozo hivi kwa akili ya

kawaida kabisa vipaumbele vyetu ni vipi, kununua ndege ambayo *only 5% of Tanzanians* ndiyo wanatumia na kwa wengine *is not even a basic need* hiyo ni *it's a luxury need*. Ni nini ambacho tunaanza nacho kama nilivyosema awali kwamba maji ni uchumi, unasema kwa sababu ya utalii ute fedha. Hivi mtalii gani atakuja anaingia hotelini akifungua bomba linatoa maji kama chai ya rangi, wakati alipotoka unatumia *tap water* kunya maji *straight*, tujiulize mara mbili tuboreshe kwanza kuhusu maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo unawekeza kwenye ndege asilimia tano ya Watanzania wanatumia, unaacha asilimia mia moja ambayo ni maji kila Mtanzania anahitaji, viumbe hai vinahitahi hayo maji, mimea inahitaji maji *and then* mnakuja mnalihadaa Taifa kwamba tumewekeza kwanza kwenye ndege ambazo zinaleta utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizo ndege ambazo zinaleta utalii *let's start with things* ambazo tukiwawezesha Watanzania wetu hawataugua, watakuwa na afya, watafanya kazi, uchumi utapanda kuliko ilivyo sasa hivi *and then automatically* tutanunua hizo ndege tutajenga viwanda, tutafanya vitu vingine vyote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwenye maji. tumeshuhudia kwamba....

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili Mheshimiwa, ahsante sana kwa mchango.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma atachangia dakika tano atafuatiwa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya kwa dakika 10, Mheshimiwa Juma Nkamia ajiandae kwa dakika tano.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwapongeza Mawaziri, Waziri Kamwelwe ambaye ni Waziri pamoja na Naibu kwa sababu walifanya ziara kwenye Mkoa wangu wa Morogoro na walifanya ziara mpaka Malinyi, walifanya ziara Mlimba na Morogoro Mjini lakini ziara imefanyika ila bado kuna matatizo mbalimbali. Nashukuru Serikali kwa miradi ambayo tayari inatoa maji na kwa upande wa umwagiliaji ambayo tayari inafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na mradi wa maji Morogoro Mjini. Mradi wa Maji Morogoro Mjini umechukua muda mrefu na hiki kilio tumekiflikisha mpaka kwa Mheshimiwa Rais alipokuwa kwenye ziara Morogoro, naomba sana huu mradi uweze kumalizika kwa sababu unafadhiliwa na Wafaransa pamoja na Serikali ya Tanzania ambapo Serikali ya Tanzania kwenye bajeti hii imetenga shilingi bilioni nane pamoja na *Euro*. Naomba sana Waziri aione kuwa ni kazi kweli mradi huu wa maji Manispaa kukosa maji siyo vizuri sana. Kuna baadhi ya Kata ambazo hazipati maji kabisa zingine zinapata maji kwa mgao, kwa hiyo, naomba sana aifanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Maji Vijijini kama wenzangu walivyosema naomba na yenyewe ifanyiwe kazi na yenyewe iweze kuanzishwa. Miradi ya Benki ya Dunia ambayo haijamalizika iweze kumalizika. Miradi mingine ya umwagiliaji pamoja na maji viporo iweze kumalizika. Mradi wa Chalinze awamu ya tatu nao umechukua muda mrefu tatizo ni kuwa mkandarasi alisitisha mkataba, naomba ifanyiwe kazi ili kusudi uweze kuanza kwa sababu unatoa maji kwenye Mkoa wa Pwani, Kibaha pamoja na Morogoro kwenye vijiji vingine vya Morogoro kama Kidugalo.

Kwa hiyo, naomba na wenyewe ufanyiwe kazi uweze kufanya kazi, Mheshimiwa Waziri unajua kuwa umechukua muda mrefu naomba uweze kufanyiwa kazi. Bwawa la

Kidunda naomba na lenyewe lifanyiwe kazi ni kweli limekuwa la muda mrefu lakini nashukuru naipongeza Serikali kwa sababu imetenga hela, kwa hiyo, hizo hela ziweze kusimamiwa na kuangaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha umwagiliaji ndiyo muhimu kwa nchi yetu ya Tanzania kutokana na tabianchi. Ni asilimia 1.6 mpaka sasa hivi ambayo inamwagiliwa, lakini kuna mpango kabambe ambao umepangwa naomba ufuatwe na uweze kukamilika kusudi tuweze kupata kilimo cha umwagiliaji.

Pia naipongeza Serikali kwa miradi ya kilimo cha umwagiliaji ambayo inafanyika Mkoani Morogoro. Kwa mfano, kilimo cha mpunga ambacho kinafanyiwa Msolwa Stesheni, Ujamaa, *scheme* za Ludewa pamoja na Rumuma na zingine ambazo kwa bajeti hii zimetengewa shillingi billioni 7.2, naomba hizi hela ziweze kutolewa na ziweze kusimamiwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye mteremko wa fedha, mteremko wa fedha wengi wameshachangia lakini naomba hasa kwenye fedha za maendeleo ambapo lazima miradi ya maji iweze kuisha, *scheme* za umwagiliaji ziweze kukamilika. Naomba hizo hela tunazotenga kwenye Bunge kama inawezekana naiomba Serikali yangu ziweze kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uvunaji wa maji kutokana na tatizo la tabianchi naomba tuweze kufuata uvunaji wa maji na hii sera iweze kufuatwa na kuwekewa mikakati kabisa pamoja na vyanzo vyaya maji viweze kutunzwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba sana tena sana miradi ya maji iweze kukamilika. Umenipatia dakika tano na *point* zangu nimeziongea kwenye dakika tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Magdalena Sakaya kwa dakika kumi, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Nkamia kwa dakika tano na Mheshimiwa Peter Msigwa kwa dakika tano ajiandae.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa niweze kuchangia kwenye bajeti muhimu sana ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilio cha maji kwa Watanzania ni kilio kikubwa sana na ukiangalia hata siku ambayo maswali ya maji yanazungumziwa humu ndani ya Bunge hili *almost* karibu robo ya Bunge wanasmama kwa ajili ya kuuliza masuala ya maji. Hii inaonesha ni jinsi gani Taifa kwa ujumla tuna shida kubwa ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, jaribu kuangalia jinsi taratibu za kutatua changamoto ya maji na hii kampeni ya kwenda kumtua mama maji kichwani sioni kama inaenda sambamba na fedha zinazotolewa. Ukiangalia kwa kweli kwa asilimia 54 inayotengwa, tutenge shilingi bilioni karibu 623, tutoe shilingi bilioni 349 kwa *speed* hii kampeni itafanikiwa lini? Hili ni tatizo. Lazima Serikali iamue kwa uhakika kwamba tunataka sasa kuondoa tatizo la maji nchini, kama tulivyopanga kwa masuala ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunazungumzia habari ya vijiji karibu zaidi ya asilimia 80 zinaenda kupata umeme, hivyo hivyo kwenye maji lakini *speed* ni ndogo leo na kila siku tunalia hapa Bungeni ni shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa *speed* tunayoenda nayo kama hatuna mkakati maalum kuja na Wakala kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge wenzangu na naunga mkono Wabunge waliozungumza suala la wakala. Hatuwezi kuondokana na kero ya maji na akina mama wanateseka, hawaingii kwenye shughuli za maendeleo, hawaendi kulima hawaendi kwenye miradi yao midogo midogo, watoto wetu wa kike hawasomi kwa muda wanaenda kufata maji

kisimani ndio waje waingie darasani, hatuwezi kuwatoa Watanzania mahali walipo kwa *speed* hii tunayoenda nayo ni ndogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la umwagiliaji. Serikali tumekuwa na malengo, *almost* karibu miaka mitano sasa kuweza kuwa na heka milioni moja kwa ajili ya umwagiliaji. Lakini nenda kwenye vitabu, leo mmeona vitabu vyote hapa karibu vinne vya miaka minne mfululizo angalia inayotengwa yaani kwa mwaka mmoja tuna hekta 6.7, 7.2 ni aibu, kwa nchi ambayo inategemea kilimo kwa hatua kubwa. Tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda, tunafahamu tunataka kwenda kwenye umwagiliaji kwa *speed* hii tunayoenda nayo itachukua muda wa miaka karibu, nilikuwa nafanya mahesabu ya haraka hapa, kwa *speed* tunayoenda nayo, ukiangalia 2016 hekta za umwagiliaji tunaenda 7000.02; mwaka 2017 ni hekta 6,712 kwa hiyo ukiangalia *trend* hiyo ili tuweze kufika milioni moja hekta tunahitaji karibu miaka 50, hivi tutakuwepo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali lazima tuamue tunakwendaje kwenye uchumi wa viwanda wakati hatuwekezi vya kutosha kwenye umwagiliaji, bado ni tatizo kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni la upotevu wa maji, ukiangalia *speed* ya upotevu wa maji wakati tunalia hatuna maji, hata mijini watu hawana maji, vijijini watu hawana maji asilimia 33 ya maji yanapotea, hayatumiki na mengine tumeshaingia gharama za walipa kodi. Kwa hiyo, naiomba Serikali lazima ije na mpango maalum, waweke utaratibu maalum wa kuboresha miundombinu mingi imechoka, miaka 20, miaka 30, miaka 50 leo ukienda baadhi ya maeneo unakuta maji yanamwagika barabarani. Inaumiza wananchi wako wanapokuwa hawana maji unafika maeneo unakuta maji yanamwagika barabarani hayatumiki, ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima Waziri aje na mkakati, awe na utaratibu maalum, *regularly* mpango wa

kurekebisha mabomba yaliyochakaa kuhakikisha kwamba maji hayapotei yanayopatikana yakatumike kwa Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la *charge za maji*. Kwenye gharama za maji tumeweka kitu kinaitwa *service charge* kama ilivyokuwepo kwenye umeme hizi Mheshimiwa Waziri hazimsaidii Mtanzania, zinamuumiza. Hizi *service charge* kwenye maji wakati tayari bili analipa bili nzima na kama analipa maji taka yapo, leo mnaweka tena na *service charge* tunaomba iondolewe kama ilivyoondolewa kwenye umeme ili kupunguza gharama za maji kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la maji kutoka Mwanza kuja Mkoa wa Tabora. Tulifurahi sana tukajua kwamba sasa Mkoa wa Tabora japokuwa halfiki Kaliua na Urambo angalau shida kubwa ya maji inaondoka. Lakini jaribu kuangalia kwa miaka mitano tumetekeleza kwa asilimia 17 ya utekelezaji wake, ili mradi huu ukamilike utahitaji karibu miaka mingapi, karibu miaka labda kumi. Hivi kweli kama ni mpango mkakati, kama ni mradi wa kimkakati kwa *speed* hii ya asilimia 15 ya utekelezaji, nasikitika sana kwa kweli hii pengine hatutakuwepo wakati huo.

Naiomba Serikali kwa kuwa huu ni mradi ambao unaenda kulisha karibu Wilaya tano za Mkoa wa Tabora na kilometra 12 pande zote ambazo bomba linapita iwekewe fedha ya kutosha ili *speed* yake iongezeke na itengewe muda maalum, tuambiwe sasa kwamba mradi huu utakamilika lini? Lakini kwa asilimia inayokwenda nayo bado ni ndogo sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee Kaliua, mimi nasikitika na kiukweli natamani kupiga yowe hapa kwenye hili Bunge. Ninaongea kila siku habari ya Kaliua, nimesoma hiki kitabu *page by page, line by line* Kaliua huku haimo, Mheshimiwa Waziri huoni hata huruma, Kaliua haimo, hivi Kaliua hawaishi watu? Mradi pekee ambao umetoka Kaliua ambao hauonekani wanasesma kwamba Mradi wa Maji

Kaliua, kata mbili, Kaliua na Ushokora mradi unaotekelawa na Mko. Fedha haionekani, kuptoka wapi haionekani, wala ni lini hajjulikani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na mradi Waziri mwaka jana alisema kutoa maji Malagarasi kuleta Kaliua na Urambo, ukiangalia imetengewa shilingi milioni 500 na nimeongea na Waziri akasema siyo mradi wa leo wala kesho. Sasa mpango wa kupatia maji wananchi wa Kaliua uko wapi? Leo kama unazungumzia habari ya kata mbili za Kaliua na Ushokora. Kaliua ina Kata 28, ina vijiji 101, ina vitongoji karibu 460, leo unazungumzia habari ya kata mbili na hakuna mradi mwingine wowote hatuko kokote, kwenye visima hatumo, kwenye mabwawa hatumo, kwenye miradi ya *quickwins* hatumo, kwenye miradi ya mkakati hatumo, miradi mikubwa hatumo, hivi Kaliua wanaishi watu wa aina gani? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ukija unijibu kwa nini kwenye kitabu hiki Kaliua umewasahau, kuna baadhi ya Wilaya nimeangalia huku mpaka inauma. Wilaya ina miradi yote kwenye visima wamo, kwenye mabwawa wamo kila mahali wamo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana walikuja mradi wa kuchimba visima pamoja na mabwawa, wakaainisha maeneo ya kimkakati kuweka mabwawa saba, nimeshangaa huku hamna hata bwawa moja, hii kwa kweli muone aibu Serikali. Naomba Mheshimiwa Waziri uniambie kwa habari ya Kaliua kama wanawake wa Kaliua wataendelea kuteseka na maji miaka mingapi nijue, hata kama mimi siyo Mbunge lakini wana Kaliua wana haki ya kupata maji, wanalipa kodi kama Watanzania wengine, akina mama wale wanataka wafanye shughuli za maendeleo, lakini kwa *speed* hii mimi nakataa kwamba Kaliua hajatendewa haki. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri na nikuombe bajeti ikiisha twenda Kaliua ukaone mateso wanayopata wale watu, kwa kweli ni maumivu

makubwa sana, yaani hata bwawa jamani ni kweli kwamba arди yetu haina maji chini na hata visima vyā Mradi wa *World Bank* hatukunufaika navyo kabisa kwa sababu hatuna maji chini. Hata kutuwekea mabwawa ili mvua zinaponyesha tukusanye tuyatumie, inasikitisha, inaumiza sana, sijui nitumie lugha gani! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilijua kwa kilio changu miaka yote inakwenda kwa Waziri tungeangaliwa angalau mwaka huu lakini inasikitisha sana, kwa kweli inaumiza sana. Mradi wa Malagarasi haujulikani, Mheshimiwa Waziri ukija hapa Bungeni na mimi nang'ang'ania shilingi yako mpaka njue wannchi wa Kaliua wanapatiwaje maji, karekebishe bajeti, haujatutendea haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Juma Nkamia atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Msigwa na Mheshimiwa Ally Seif Ungando ajiandae.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa dakika tano kwa sisi wataalam wa habari dakika tano ni muhtasari tu wa habari. Kwa hiyo, nitaenda *straight*.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kupoteza muda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu kaka yangu Kitila kwa kazi nzuri mnayofanya. Mwaka jana kwenye Bunge hili nilitoa maombi kwamba iundwe Tume Maalum ya kuchunguza miradi ya maji. Mwaka huu wakati wa Ofisi ya Waziri Mkuu nilitoa ombi hilo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingi ya maji ni zaidi ya makinkia, naomba Bunge liunde Tume huru ya Bunge ichunguze miradi ya maji. Nimemsikia kaka yangu hapa akisema, Mheshimiwa Rais ameanza kuchukua hatua hakuna sababu, tusimwache Rais peke yake, Bunge lina nafasi yake kama muhimili, likachunguze miradi hii ya maji lakini wakati Bunge linaunda Tume hiyo na watu wa Mambo ya Ndani

wajiandae kupanua Magereza. Miradi mingi ya maji kwa Wabunge tunaotoka vijijini imekuwa ni *deal* tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikupe mfano mmoja mdogo sana, Chemba pale tuna miradi mitatu, kwa mfano Mradi wa Goima aliyepewa ukandarasi alikuwa Afisa wa TAKUKURU. Mimi nimemkuta *sitemu* Afisa wa TAKUKURU ndiye Mkandarasi aliyepewa mradi wa Maji wa Goima na sasa hivi amekimbia kabisa hata Kondoa hayupo. Kelema Kuu pale umechezewa tu, hela inachezewa tu hivi halafu tukisema humu ndani tunaonekana kama watu wa hovyo hivi, hapana! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ninaomba hata ukizunguka kukagua miradi yote Tanzania bila kuchukua hatua na ukaunda tume ya kukusaidia wewe kesho na kesho kutwa utaonekana hujafanya kazi, utapanda kwenye matenki, huwezi kupanda kwenye matenki yote Tanzania nzima. Umri wako nao unakwenda, unafanya kazi nzuri sana, lakini mwisho utakuja kuanguka kwenye matenki bila sababu. Jambo la kwanza ni kuunda Tume huru ya Bunge ifanye uchunguzi nchi nzima, miradi mikubwa na midogo inapigwa. Pili, ninakuomba Mheshimiwa Waziri mmeshafanya tathmini Bwawa la Farkwa wananchi wanasubiri fidia wako tayari kupisha ujenzi wa mradi ule wa maji. Tatu, hizi *COWSOS* mnazosema ni sera ya Taifa ya maji wananchi hawana utaalamu wowote wa kusimamia miradi ya maji, mkishatumia shilingi milioni 500 mnakabidhi kijiji mradi wa maji baada ya miezi miwili ama mitatu mradi unakufa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sera inaweza ikabadilishwa, badilisheni hii Sera ya *COWSOS* tuangalie namna gani ya kusimamia miradi hii ambayo imekamilika lakini leo unatengeneza mradi baada ya miezi miwili unakufa, unawakabidhi mradi wanakijji hawana utaalamu wowote unawaambia mtasimamia huu mradi, badilisheni hii sera. Wamewaletea wazungu ikifika wakati haifai badilisha, wananchi tunachotaka ni maji siyo sera nani asimamie mradi wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, Mheshimiwa Waziri ninakuomba kwa dhati kabisa njia sahihi ni kujenga mabwawa. Chemba kule tunaomba hela ya mabwawa mawili kati ya Kinkima na Churuku, kati ya Itolo na Mlongia hatuna matatizo yoyote na kujenga Bwawa la Kisangaji kule Kondoa, lakini Kondoa mmetugharimu sana kwenye Mradi wa Maji wa Ntomoko, na leo watu karibu zaidi ya 18 wanahojiwa kule Kondoa, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuchukua hatua hiyo, tujengeni mabwawa tumalize hilo tatizo.

Pia Mheshimiwa Waziri nikuombe hivi hawa *DCCA* wameenda kutuibia kule, wamechimba kisima cha maji pale Ovada shule ya sekondari fedha ya Serikali wamelipa milioni 32 hicho kisima hakina hata maji, tumechimba kisima kingine *what kind of this?* Mpaka *DCCA* kampuni ya Serikali nayo wezi! Nilikuwa najiluliza hivi wanalipwaje hawa watu hakuna maji? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, ninakuomba pamoja na kuunga mkono hoja...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kw amuda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mhesimiwa Nkamia muda wako umekwisha. Mheshimiwa Peter Msigwa dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Seif Ungando dakika kumi atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Bulembo dakika tano.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi, dakika tano na mimi nitakwenda *brief*, hazitoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mtaalam mmoja na mwalimu wa mambo ya kidini anasema; “*the greatest mistake in life is being busy but not effective na the greatest challenge in life is knowing what to do*”. Kwa bahati mbaya sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi hii ya Awamu ya Tano inaonekana iko *busy*sana, lakini haiko *effective*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niungane na Mheshimiwa Mnyika kama kweli tuko *serious*, kuna Wabunge hapa wanasmama kwamba kwenye Majimbo yao upatikanaji wa maji ni asilimia 16 na bado wanapiga makofi wanaunga mkono bajeti hii. Mheshimiwa Mnyika amependekeza hapa tuunde Kamati Teule kama ambavyo na Mheshimiwa Esther Matiko amesema, kama ambavyo Mabunge huko nyuma yamefanya kwa ajili ya kutatua tatizo la maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu tatizo la maji ni kubwa sana kama Serikali hii ina-*synchronise* utendaji wake kazi, mojawapo ya kikwazo kikubwa cha watalii kuja Tanzania ni pamoja na mambo ya *hygenic*. Inaonesha Tanzania kuna uchafu mkubwa hakuna maji, sasa usafi utapatikanaje bila maji? Hiyo ndiyo inatuangusha duniani kwamba kuna uchafu Tanzania, kuna kipindupindu, maana yake watu wanakula kinyesi na maji yanasaababisha watu wasiugue. Sasa tunaleta utani katika masuala ya maji, jukumu pekee ambalo tunalo Watanzania ni kuondokana na bla bla za Chama cha Mapinduzi ambazo zimefanyika muda mrefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ndugu zangu kama kweli Wabunge tunavaa na suti hapa, inaingiaje akilini kwamba matatizo ya maji kijiji mpaka Mheshimiwa Rais apige simu amuambie Katibu Mkuu wa Wizara anamuunganisha na Mtendaji wa Kijiji, tunaona ni jambo la kawaida kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Katibu wa Wizara ambaye juzi nilisema hapa wajibu wake mkubwa kusimamia hizi sera na utendaji, amekazana kwenye mitandao anagombana na maaskofu, *this is a serious business*, hajawahi kutokea katika nchi hii Katibu wa Wizara ana majukumu makubwa ya Wizara, badala ya kushughulika na matatizo ya maji, hivi akilini inaingiaje kwamba Katibu wa Wizara unamuunganishaje na Mtendaji wa Kijiji wakati hiyo shughuli iko kwenye *Local Government?* Inaonesha kwamba *system* *ime-fail*, haifanyi kazi. Tunafanya majukumu mazito

tunashindwa utekelezaji wa kazi. Hili suala la maji ni *serious business*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niaombe Wabunge...

### **KUHUSU UTARATIBU**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msigwa, *Chief Whip* amesimama, Mheshimiwa Martha Mlata naomba ukae. Mheshimiwa Jenista.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni shida sana kuendelea kumuacha Mheshimiwa Msigwa aendelee kuzungumza vitu ambavyo vinavunja utaratibu kwa mujibu wa Kanuni kama anavyoendelea kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaendelea kukumbusha sana, Kanuni ya 64(1) madaraka aliyopewa Rais ni madaraka ya Kikatiba na anaweza kusimamia jambo lolote, wakati wowote, kwa utaratibu wowote anaoona unafaa kwa muktadha wa maendeleo ya Watanzania. Kanuni zetu ndani ya Bunge zinaendelea kutukumbusha, Mbunge unapozungumzia jambo lolote hapa ndani usizungumzie mwenendo wa Rais ambaa amepewa kwa mujibu wa Katiba ambayo tunayo hapa ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuacha jambo hili liendelee na hasa kwa *style* anayoendelea nayo Mheshimiwa Msigwa ni kuvunja Kanuni za Bunge, lakini kuingilia madaraka ya Rais kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Mheshimiwa Mbunge aheshimu Kanuni ya 64(1)(e). Kama itakupendeza hayo anayoyatumia kuzungumzia mwenendo wa Rais yafutwe na vilevile anapoendelea na mchango wake aheshimu Kanuni tulizonazo. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 64(1),(e), ndicho ambacho anakisema Mheshimiwa Jenista Mhagama aktuelekeza kwenye mchango unaotolewa na Mheshimiwa Msigwa wa kuhusu jambo ambalo Mheshimiwa Rais alilifanya la kumpigia simu Katibu Mkuu ili azungumze na Mtendaji wa Kijiji kwa maelezo ya Mheshimiwa Msigwa. Wakati akizungumza jambo hilo amelisema kana kwamba, ni jambo ambalo halipaswi kufanywa na Rais kwa kumpigia simu Katibu Mkuu ili aongee na Mtendaji wa Kijiji. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, huwa nawakumbusha siku zote kwamba kikisimama Kiti mkisikilize ili twende vizuri, mnapokuwa mnazungumza mnapitwa na maelekezo halafu mnarudia makosa yale yale kila wakati. Kwa hiyo, tuwe tunasikilizana tukiombwa Utaratibu au Mwongozo ili tusirudie makosa yale yale. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Jenista ametukumbusha kwamba Katiba yetu inampa mamlaka Rais na Katibu Mkuu yeye ni mteuliwa wa Rais, anafanya kazi kwa lugha ya wenzetu ambayo imesheheni zaidi *at the pleasure of the appointing authority*. Kwa sababu hiyo, kitendo kilichofanywa hakina kosa lolote Kikatiba wala kisheria na kwa sababu hiyo, Mheshimiwa Msigwa... (*Makofii*)

Mheshimiwa Mnyika unisikilize nikiwa nazungumza, siwezi mimi kuzungumza na wewe, unazijua Kanuni sawasawa. Kwa hiyo, mimi nikiwa nimesimama hata usiniongeleshe, wala wewe usizungumze, nyamaza kimya, ndiyo Kanuni zinavyosema, nikiwa nazungumza wewe unanyamaza kimya, acha tu kuniongelesha, unanyamaza hata jirani yako usimsemeshe ndiyo Kanuni zinavyosema. Kwa hiyo, usifike mahali ukadhani nimesimama hapa wewe unawenza kuwa unazungumza hata na jirani yako huruhusiwi, kwa hiyo, nisikilize vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Msigwa kwa Utaratibu ambao umeombwa na Mheshimiwa Jenista na kwa mujibu wa hii fasili ya pili na pia kwa mujibu wa kanuni zetu, Kanuni ya 72, Mheshimiwa Msigwa hayo maneno unayochangia kwanza

ufuate kanuni, lakini pia ulichozungumzia kuhusu mwenendo wa Rais wa kuzungumza na Katibu Mkuu na kumwambia azungumze na Mtendaji, wewe nakuomba hapo uya fute hayo maneno ili tuendelee na utaratibu ulio mbele yetu. (*Makofi*)

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninachozungumza mimi hapa...

**NAIBU SPIKA:** Aahh! Kilicho semwa na mimi sicho unachozungumza wewe. Uya fute hayo maneno yanayozungumzia mwenendo wa Rais, kama huyajui yapi ufute, basi futa mchango wako wote halafu ndiyo uendelee, kama huyajui ya kufuta, futa chote ulichokisema halafu ndiyo uendelee.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumza kwa mfumo *ku-fail*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msigwa, huwezi kusema mfumo *ume-fail*, naomba ukae chini Mheshimiwa Msigwa, naomba ukae chini.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** *I know you are scared of me.*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimemuita Mheshimiwa Ally Ungando, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Bulembo, Mheshimiwa Lathifah Chande ajiandae. (*Makofi*)

**MHE. ALLY S. UNGANDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi leo nichangie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitaanza na Mradi wa Maji Kibiti, naomba nilithibitishie Bunge lako Tukufu kwamba sasa hali ya ulinzi Kibiti imeanza kuimarika, Kibiti shwari, sasa shida yetu maji, wale watu waliokuwa wanatuua tumewamaliza sasa hivi shida yetu imekuwa maji, tatizo Kibiti ni maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na mradi wa maji Kibiti. Huu mradi wa maji wa Kibiti umekamilika na unatoa huduma, lakini bado unasuasua kwa sababu huu mradi ni mkubwa na haupatiwi fedha ya aina yoyote ya ruzuku ili kuweza kuendesha mradi ule. Tuna għarama kubwa ya kulipa bili ya umeme, vibarua, hata na baadhi ya vioski, tunaomba sasa Wizara iangalie kwa jicho la huruma mradi huu wa maji Kibiti ingeweza kuwapatia fedha kidogo ili kuweza kuendesha mradi huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, iko miradi saba ambayo haifanyi kazi kutokana na miradi hii kuchakaa. Miradi hiyo ni kama Kijji cha Luaruke, Jaribu Mpakani, Mtawanya, Muyunu, Mkenda na Kibiti. Wizara iangalie jinsi gani ya kuweza kupeleka fedha za ukarabati wa miradi hii ili iweze kutoa huduma, miradi hii ipo kwa muda mrefu imekosa fedha ya kufanya ukarabati kwa hiyo, inashindwa kutoa huduma illyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kule Jimboni kwangu nimechoka kusuluhisha ndoa kwa sababu muda mwingi wanandoa wanakwenda kutafuta maji visimani na baba anashindwa kuwa na imani mkewe kweli amekwenda kisimani au amekwenda kwenye mchepuko. Kwa sababu maji yanatoka mbali na huko kisimani ukienda maji yenye we yanakuwa ya kulindia, kwa hiyo, baba anakosa imani kwa hiyo, tumekuwa na migogoro mikubwa ya wanandoa kule Jimboni kwangu Kibiti. Ningemba Mheshimiwa Waziri aangalie jinsi gani ataangalia Kibiti kwa jicho la huruma utupatie maji katika vijiji vyetu ya Kibiti vilivyobakia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia mwaka jana tulipata fedha, zile fedha tumeziona kwenye makaratasi tu, lakini uhalsia maji yenye we Kibiti hakuna. Sasa hapa Waziri hebu angalia ilionekana kama kuna mgomo baridi baina ya Wizara na Halmashauri zetu kwamba fedha zinakaa Wizarani lakini mradi unatekelezwa Wilayani, kule Wilayani hampeleki fedha kwa ajili ya ufuutiliġi, ukiangalia ni kama kuna mgomo baridi, mnasema ninyi huko Wilayani mtangaze *tenderhalafu muandae certificate* mlete huku Wizarani, kule

Wilayani kwenyewe kazi hazifanyiki kwa wakati, sasa hilo nalo mliangalie kwamba mgomo baridi huu upo wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana kwamba watu sasa wameamua kugoma kuwaangalia ninyi Wizara mtafanikiwa au hamtafanikiwa. Kwa hiyo, ningeomba ili muangalie kama mnawenza mkafanya hii miradi ya maji kwa kutumia *force account* basi fanyeni kwamba hizi fedha ingizeni kwenye kijiji husika wao wenyewe wasimamie maana ndiyo wenye uchungu na ndiyo wenye shida ya maji, tunaweza tukafanikiwa kwa jithada zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unavyoizungumzia Kibiti lazima uzungumzie maeneo ya Delta kwamba Kibiti zipi kata tano ambazo ni Delta ambayo ina vijiji 17, vitongoji 42, huko kote hatuna maji safi na salama. Unapokosa maji safi na salama hata shughuli za uzalishaji zinashindwa kufanya kwa wakati. Maeneo hayo kama ya Nyamisati, Kiomboni, Sanninga na Simbaulanga, kote huku hatuna maji ya uhakika, ningeomba Wizara angalieni jinsi gani ya kutufikishia maji katika maeneo hayo ya Delta. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hivyo hatuna watumishi wa kutosha katika Idara hii ya Maji Wilayani kwetu Kibiti. Wilaya hii inaelekea tunaweza tukakosa ufanisi wa kazi wenye tija kutokana na upungufu wa watumishi na vitendeakazi. Mpaka leo Kibiti hatuna gari idara ya maji, unapokosa vietendeakazi utashindwa kufanya kazi yao kwa ufanisi. Kwa hiyo, ningeomba sana Wizara muangalie kwa jicho la huruma Kibiti. Kwanza tumeathirika kwa yale mauaji tu Kibiti tumeathirika. Kwa hiyo, Wizara lazima uiangalie Kibiti kwa jicho la huruma mtusaidie Kibiti tumeathirika tatizo maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hiyo viko baadhi ya vijiji kama vile Makima, huu Mji unakua kwa kasi lakini pana tatizo la maji na ndiyo maana ukiangalia kila Mbunge humu akisimama analia na maji na ukiangalia mwaka 2015 katika ahadi zetu tulisema tunakabidhi maji kila kijiji, sasa leo usiku wa deni mfupi, Wandengereko kule

tunasema hakuna shughuli ndogo kwamba mwaka 2020 tukifika tutaongea nini majukwaani? Maji yenyewe mpaka leo tumeishia kuyaona kwenye makaratasi tu? Ukiangalia kwenye makaratasi kweli maji unayaona, lakini ukienda uhalisia kule vijijini maji hakuna, sasa nashindwa kujua kwamba hawa wataalam wetu wanatufanyia mawele au wanatufanyia nini? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tatizo la maji hili ni janga la kitaifa, muangalie jinsi gani ya kutusaidia katika Wilaya yangu mpya ya Kibiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunisikiliza, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Shukrani sana. Mheshimiwa Abdallah Bulembo atafuatiwa na Mheshimiwa Lathifah Chande, Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga ajiandae.

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, ingawaje dakika tano ni kidogo, ngoja nijaribu tuone.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa anayoifanya na Naibu wake. Ziara zenu zinaleta tija Mwenyezi Mungu awape afya, muendelee kufanya kazi kama mlivyoagizwa. Nimpongeze Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu kwa kazi wanazozifanya. Vumilieni tu kwa sababu lazima tuwaseme kidogo kwa sababu kwenye Idara hiyo, lakini kazi mnachapa na Mungu anajua. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianzie hapa, ndani ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwenye eneo la maji tumesema kutakuwa na wakala wa maji, ndani ya ilani, leo tunaelekea mwaka wa tatu. Mheshimiwa Waziri kitu hiki ni muhimu sana kwa sababu kila ukiangalia Wabunge wanaosema wengi siyo wa mijini waliokuwa wengi ni wa vijijini, ni wa vijijini kwa sababu pesa zile ziko kule chini ndani ya Halmashauri ndiyo wanafanya nao kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia hali ilivyo Wizara yako ni inaingiliana na TAMISEMI, *Engineer* aliyeo kwenye Halmashauri ukienda kesho kwenye ziara akiwa ameiba wewe huna *file lake*, *file lake* liko TAMISEMI. Chochote kitakachofanyika kule chini utaenda utafanya ziara, wanaoamua ni watu wengine. Wakala huu unakuja kukusaidia ninyi, kwa sababu leo ukija mijini tunazo zile taasisi kwa maana kuna bodi, kuna ile taasisi iliyoanzishwa, mjini hakuna shida, lakini wakala huu ukipatikana utakusaidieni sana ninyi Wizara. Kwa sababu unavyoenda kwenye Halmashauri Mhandisi yule unaweza kumuwajibisha, kama siyo hivyo utaenda kwa Katibu Mkuu Profesa, Profesa amwambie Mzee lyombe, hapa kama hakuna mahusiano ya karibu nayo ni shida. Kwa hiyo, neno wakala hii ni muhimu sana. Muende kwenye meza mjipange, mliandae lije huku wabariki ili mpate wepesi wa kazi zenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwa utaratibu wa Madiwani tulivyokuwa tunaishi huko Mkuu wa Idara kumshughulikia, siyo rahisi ukatoka maji ukamshughulikia aliyeo TAMISEMI ni kazi ngumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa naiomba Serikali yangu suala hili kwa sababu, liko ndani ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi muende mezani mkae nao tuanzishe wakala huo ili uwape wepesi katika kazi zenu mnazofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine niseme dogo hapa, katika Bunge lilitopita hapa katikati kabla ya bajeti ndani ya Bunge hili tulikubaliana tuunganishe DAWASCO na DAWASA, ndani ya Bunge humu, ilipita hapa kwamba, DAWASA mpya azaliwe, lakini wachangiaji wengi humu wanasema mara DAWASCO mara DAWASA, hapana. Tulishakubali *New DAWASA* ipatikane, tuwape nguvu suala hili litekelezwe kwa sababu lilihapita ndani ya Bunge. Kwa hiyo, nakuombeni sana Wizara wala msirudi nyuma, yale mliyokwishayafikia undeni taasisi ili watu wa Dar es Salaam wapate maji kwa urahisi na watu wa Mkoa wa Pwani. (*Makofi*)

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Dar es Salaam pale kuna shida moja, wakati wanaleta maji kutoka Ruvu Juu, Waziri ulishanijibu siku moja hapa ndani kuna watu wamekataa kutoka kwenye miundombinu ya maji pale, wameenda Mahakamani wameshindwa, lakini mpaka leo tunavyoongea hawataki kubomolewa, kunaingia siasa, ninyi ni Wizara, isaidieni *DAWASA*, wale watu wavunjiwe ili watu wa Chuo Kikuu wapate maji, kwa sasabu mtu ameshashindwa Mahakamani anatakiwa kutoka, mpaka leo hajatoka analindwa na nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, nani anamlinda tusaidieni tu? Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wakati unakuja kwenye majibu yako, hebu njoo na majibu tunafanyaje kuwasaidia hawa watu?

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hii inatengenezwa na watu kutoka nje, wameshalipwa akifika pale anasimama anaanza kutudai Serikali alipwe fidia kwa sababu mmemchelewesha kumaliza kazi. Naomba Wizara mkija hapa mtuambie, kama mnaruhusu kwa sababu alishashindwa Mahakamani kwa mujibu wa sheria abomolewe mtamke wazi, ikishatamkwa sasa kule waulizwe kwa nini wale watu hawajaondolewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme hili la jumla, ajenda ya maji kuna watu wanasema Tume na kadhalika, hebu mpeni Mheshimiwa Waziri huyu nafasi, amekuwa Waziri mwaka mmoja mnamuundiaje Tume? Alikuwa Naibu Waziri, ukiwa Naibu Waziri kama Mheshimiwa Aweso siyo mwenye Wizara. Huyu anao mwaka mmoja ndani ya Wizara leo unamuundia Tume, unaenda kufukua kaburi au unaenda kufanyaje.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Tumpe nafasi, afanye kama anavyofanya na umri wake anajitahidi ili tumuunge

mkono. Mpitishieni bajeti ili kipindi kijacho sasa kama liko jambo muweze kumuuliza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, dakika tano sina uwezo wa kuzipanga, acha niseme hayo machache, naomba kuunga mkono hoja tu. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Lathifah Chande atafuatiwa na Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, Mheshimiwa Amina Makilagi ajiandae.

**MHE. LATHIFAH H. CHANDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi hii ya kuweza kuchangia kwenye Wizara hii ya Maji.

Awali ya yote napenda kuzungumzia kuhusiana na suala zima la kutunza vyanzo vya maji. Tunatambua kwamba mabadiliko ya tabianchi na ongezeko la shughuli za kibinadamu linapelekea hali hatarishi kupelekea kwenda kukosa maji katika siku za usoni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikitumia mabilioni ya fedha kwenye miradi ya usambazaji wa maji, lakini imeacha kuijwekeza katika suala zima la kutunza vyanzo vyetu vya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naweza kusema kwamba Serikali imeshiriki katika kuhujumu vyanzo vya maji. Kwa nini nasema hivyo? Ni kwa sababu haijaweka kipaumbele kwenye suala hili hata katika hii bajeti ambayo inaenda kuitishwa hamna fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutunza vyanzo vya maji. Miradi hii ambayo ikitumia mabilioni ya fedha *sustainability* yake itakuwaje, maana yake itakuwa ni miradi isiyo endelevu kama vyanzo vyenyewe vya maji hakuna mkakati wowote wa kuvilinda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haijaweka mpango wa muda mfupi wala wa muda mrefu katika suala zima la kutunza vyanzo hivi vya maji. Nasema hivyo nikitambua kabisa nchi nzima hili tatizo limejitokeza. (*Makofi*)

## **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa mfano wa Lindi na Kilwa Kusini tangu enzi za wakoloni kuna mto mmoja unaitwa Mto Mavuje ulikuwa una uwezo wa kusambaza maji kwenye kata nne, Kata za Pande, Kilwa Masoko, Limalyao na Kivinje. Enzi za wakoloni walizua maji kwenye mto ule wakaweka na mageti lakini leo hii mageti yale yameanguka Serikali haijachukua hatua yoyote ya kuweza kwenda kuyarudishia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu, Serikali hii hii illichokifanya imeingia mkataba na mwekezaji wa nje *Bio Shape* kwa ajili ya kuja kulima mimea ya nishati. *Bio Shape* alikuja hapa kwa ajili ya mradi huo, cha kushangaza mradi huo ulihitaji awe anakata misitu, kwa hiyo akakata miti katika eneo hilo la mto na mradi huu umeota mabawa. Ameenda kukata miti kwenye mto huo, kumebaki jangwa na mto huo sasa unashindwa hata kuhudumia kata nne kama ilivyokuwa enzi za wakoloni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maji ni la kidunia siyo kitaifa tu, ndiyo maana unakuta nchi za wenzetu Serikali inachukua hatua katika kudhibiti vyanzo vya maji. Mfano naweza nikatoa Australia, wameweka udhibiti kwa kuhakikisha kwamba wale wanaoingia katika maeneo ya vyanzo vya maji wanatozwa, kwa hiyo inakuwa fundisho kwa watu wengine. Siyo huko tu, South Africa wameanzisha kampeni ya *Water Wise*, ambayo inahamasisha na kuelimisha wananchi juu ya utunzaji wa vyanzo vya maji, kwa nini sisi Tanzania tushindwe? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Wizara ya Maliasili na Utalii imeweza kushirikiana na *TANAPA* katika kudhibiti watu kuingia na kufanya shughuli hovyo katika hifadhi za misitu na maeneo ya mbuga za wanyama, kwa nini ishindikane kuja na mfumo/mpango madhubuti kwa ajili ya kuweza kudhibiti na kutunza vyanzo vyetu hivi vya maji huku tukitambua kabisa kwamba Serikali inatumia pesa na mabilioni ya pesa katika miradi mbalimbali ya maji ambayo haiwi endelevu. (*Makofi*)

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine ni *Stiglers Gorge* ambao hautokuja...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako tayari Mheshimiwa, ahsante sana. (*Makofi*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Makilagi, Mheshimiwa Rose Kamili ajiandae.

**MHE. BONVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiswaga kwa dakika kumi, Mheshimiwa Amina Makilagi kwa dakika kumi na Mheshimiwa Rose Kamil kwa dakika tano.

**MHE. BONVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niipongeze Serikali kwa kazi nzuri inayofanya kuhakikisha kwamba inatatua kero za wananchi wake japo kwa muda ambao imejiwekea. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wake na Makatibu Wakuu kwa namna ya pekee ambavyo wanajituma kwenda kuwaangalia wananchi huko vijijini wanavyotaabika na huduma hii ya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wote hapa kila linapoulizwa swali la maji wanasmama nusu ya Bunge. Maana yake ni kwamba hakuna hitaji muhimu tofauti na maji kwa wananchi. Wananchi hawa wanapata taabu sana hasa wakati wa kiangazi. Mimi nimekwisha kusema hapa kwamba sisi tunayo maeneo ambayo wananchi wanapata shida lakini maji yako karibu. Kwa mfano, kijiji changu cha mwisho kule Mahaha, Tarafa ya Ndagalu ni kilometra 58

kutoka Ziwa Victoria, lakini mpaka leo tunazungumza hapa hakijaweza kupatiwa maji. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu nimeshampelekea andiko mara nyngi, nimeshazungumza naye lakini bado sijaona njia sahihi ya kuweza kutatua kero ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma sana kwenye kitabu hiki nimeona Tarafa ya Ndagalu yenyeye wakazi takribani 80,000 imetengewa shilingi milioni 100. Shilingi milioni 100 ni visima vitano tu vya maji ambavyo ni vijiji vitano. Hii tarafa ina vijiji 21, ni kubwa kama ilivyo Wilaya na Jimbo la Mheshimiwa Waziri. Ni tofauti sana, tunapozungumza hapa kuna majimbo na vijimbo, sisi tunayo majimbo na wengine mna vijimbo, mtuelewe tunapozungumza jambo hili. Tarafa moja tu inameza jimbo lako, lakini haina maji, lazima mtuelewe vizuri Mheshimiwa Waziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi niombe sana tusiwe tunalalamika hapa tusaidieni kutatua kero za maji. Tukitatua kero za maji ndipo tutakapokuza uchumi wa Watanzania, uchumi wa wananchi wetu kwa sababu akina mama ndiyo wazalishaji wakuu, lakini wanapoteza muda mwingi sana kuchota maji na wala hawaendi tena kuchangia shughuli za kiuchumi. Kwa hiyo, niombe sana tatizo hili lishughulikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewahi kusema hapa kwamba asali ni tamu sana na kila mmoja anatamani kuinywa, lakini wako humu watu hawanywi asali lakini kila mmoja anakunywa maji.

Kwa hiyo, mimi niombe sasa pamoja na kwamba inaonekana katika makusanyo yetu hatuwezi kutosheleza miradi ya maji tuje na mpango. Kama tumekuwa na mpango wa kununua ndege, tumekuwa na mpango wa kujenga *standard gauge*, kwa nini tusije na mpango wa kumaliza tatizo la maji? Kama ni kukopa shilingi trilioni tatu tukaondokana na tatizo la maji kwa nini tusikope? Tuamue kama Taifa, tuamue kama nchi kwamba hivi tukimaliza tatizo la maji, tukasogeza huduma kwa wananchi tutakuwa

tumepunguza mambo mengi sana. Magonjwa yote yanayowasumbua Watanzania wetu yanatokana na maji. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe sana Serikali hata kama siyo leo ndani ya miaka mitatu au mitano tuje na mpango wa kukopa tumalize tatizo la maji ili Wabunge waendelee kusemea mambo mengine ambayo yanaweza kusaidia. Jambo hili likifanikiwa kama ambavyo tumefanikiwa kununua ndege, kama ambavyo tumefanikiwa kujenga *standard gauge*, litaleta matumaini mapya kwa Watanzania. Kwa hiyo, nikuombe hili liendelee kusisitizwa na Serikali na iweze kuweka mpango muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumza maji tunazungumzia uhai. Mji wa Kisesa wangu wa Kisesa, Jimbo la Magu ni mji mkubwa sana na nimesoma kwenye kitabu hiki nilitarajia kwamba nitaona mpango ndani ya miji ambayo inatekelezewa miradi ya maji lakini sijaona Mji huu wa Kisesa ukiwekewa maji. Kwa hiyo, niombe kama ambavyo tumeshaendelea kuzungumza na Waziri, kama ambavyo tumeshaendelea kuzungumza na Katibu Mkuu muone mipango ya miaka ijayo hasa mwaka kesho kuja na mpango madhubuti kuhakikisha kwamba maji katika Mji wa Kisesa yanapatiwa majibu. Kwa hiyo, niombe tu kwamba vijiji vyote hivi ni vizuri tukahakikisha kwamba tunaweka maji ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu skimu za umwagiliaji, ripoti inaonyesha tunazo skimu nyngi sana za umwagiliaji lakini ni skimu ambazo zinategemea hasa wakati huu wa masika ambazo zinakinga maji yale yanayotiririka kutokana na mvua nyngi, mvua zikikatika skimu hizi zinakauka. Ni vizuri tukaandaa skimu ambazo zitatumia mito isiyokauka, mabwawa yasiyokauka na ziwa ambalo haliwezi kukauka ili hizi skimu ziweze kuleta *impact*. Skimu zilizopo sasa hivi hazileti *impact* kwa sababu wananchi hawamwagiliajii wakati ambapo mvua haipo, zinasaidia tu wakati wa mvua. (*Makofî*)

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe na hili Serikali iwe na mipango madhubutu ya kuweza kusaidia ili tuweze kukuza uchumi hasa uchumi wa kilimo ambao kila mmoja wetu unamgusa na mwananchi wa kawaida unamgusa. Badala ya kupumzika muda mwingu aweze kuendelea kulima mazao ambayo atatumia skimu hizi za umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako maeneo hata tukizungumza leo tupeleke maji ya Ziwa Victoria hayatafiki, yanahitaji mabwawa. Mabwawa haya yakichimbwa maeneo hayo ambayo ni kame zaidi yanaweza kusaidia sana katika umwagiliaji, unyweshaji wa mifugo lakini pia katika matumizi ya binadamu. Kwa hiyo, tunapozungumza mabwawa mtuelewe vizuri wale ambao tuko maeneo ambayo yana shida na maji. Kwa mfano, Bariadi, Kwimba na Maswa yote haya yana shida na ukame mkubwa sana ni vizuri tunapojenga hoja mtuelewe kwamba hawa watu wanahitaji kupata maji yanayostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasikitika sana, kuna msemaji mmoja hapa amesema Serikali imefeli, juzi tu tarehe 1, yeye mwenyewe amempongeza Mheshimiwa Rais na Serikali yake kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi haina ubaguzi wa chama chochote inapeleka maendeleo kwa kila jimbo. Leo amejifanya tena kuwa mnafiki, hawa watu ni vuguvugu. Hayuko baridi, hayuko vuguvugu, huyu anapaswa kutapikwa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Amina Makilagi kwa dakika kumi, atafuatiwa na Mheshimiwa Rose Kamil kwa dakika tano na Mheshimiwa John Heche kwa dakika tano ajiandae.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Nishukuru pia Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi na fursa ya kuweza kuchangia katika hoja

hii muhimu kwani maji ni uhai, maji ni kilimo, maji ni uchumi, maji kwa kweli ni kila kitu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi naomba nianze kwa kuungana na wachangiaji wenzangu kuishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi njema inayoifanya ya kuhakikisha inapeleka maji mijini na vijijini kwa kiwango ambacho kimeripotiwa katika taarifa hii. Ni ukweli usiopingika kwamba kazi ya kupeleka huduma za maji hasa mijini imefanyika vizuri na ndiyo maana hata Mheshimiwa Msigwa mwaka 2010 nilikuwa naye Kamati ya Maji, mara baada ya kuona Serikali ya CCM imepeleka zaidi ya asilimia 99 katika mji wake wa Iringa alifikiria hata ajiondoe kwenye Kamati kwa sababu hali ilikuwa ni nzuri sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na mchangiaji aliyemaliza mwanangu Msigwa hebu usiwe na ndimi mbili, ulisema tununue ndege kwa ajili ya uchumi ulipokuwa Maliasili tumenunua, leo unasema tena ndege hazifai. Jana ulisema tujenge *standard gauge*, leo unasema tena tusijenge, kupanga ni kuchagua. Rais wetu ameamua kupeleka fedha na kujenga miundombinu ya kiuchumi ili kutengeneza fedha sasa za kwenda kujenga miradi ya maji kwa fedha zetu wenyewe bila kutegemea wafadhili. Ni kilio cha muda mrefu cha Wabunge, tulikuwa tunategemea fedha ziletwe na wafadhili, miradi inasimama tunategemea Benki ya Dunia...

## T A R I F A

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amina Makilagi kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Bungara.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumzia habari za maji siyo za Msigwa. Mimi nataka nimuulize tu, tuanze lipi ndege au maji? Ahsante sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa ajili ya muda wetu taarifa ya Mheshimiwa Bungara itakuwa ya mwisho. Mheshimiwa Amina Makilagi unaikubali taarifa hiyo?

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nafikiri anataka nisaidie tu kuendelea kutoa elimu kwamba huwezi kudai maji kama huna fedha. Kwa hiyo, miradi inayofanyika hii ya kujenga miundombinu ya kiuchumi lengo lake Tanzania iweze kujitosheleza kwa fedha na kuweza kupeleka maji vijijini, maji mijini na ndio maana nimesema kupanga ni kuchagua na nchi yoyote duniani huwezi ukafanya mambo yote kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana hapa Mzee Chenge ameeleza vizuri sana kwamba Serikali sasa imeamua kupeleka fedha za ndani kujenga miradi ya maji. Sasa kama huna fedha zako za ndani, hujalmarisha utalii ukununua ndege, hujajenga miundombinu ya kuleta uchumi, hizi fedha za kupeleka maji vijijini utapata wapi? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka kusema na Wabunge na kwa kweli na Watanzania wanaotusikiliza, mimi ni mama na ni mdau mkubwa wa maji, llani ya CCM tumedhamiria kuwatua wanawake ndoo kichwani. Nataka niwahakikishie ni kweli kama ambavyo amesema Waziri kwenye kitabu chake ukurasa wa saba kwamba ifikapo mwaka 2020 tutapeleka miundombinu ya maji kwa kiwango cha asilimia 85. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwahakikishie kwa sababu miradi mingi iko kwenye mchakato na miradi ya maji inajengwa kwa muda mrefu. Kama lipo tatizo la fedha kutumika vibaya, tumpe nafasi Waziri, naungana na Mheshimiwa Bulembo, hatuna haja ya kuunda Tume kwa sababu kuunda Tume unaongeza gharama. Waziri Mheshimiwa Kamwelwe ana nia njema, kwa muda mfupi tumemuona, yuko *smart* na ni mtu anayefuatilia, waende wakae chini wakokotoe na mimi kwenye mchangano wangu wa maandishi nimempa kabisa na njia za kukokotoa kwamba kuna miradi tuliyoofadhiliwa na Benki ya Dunia tupate

taarifa ni vijiji vingapi, fedha ngapi zilikwenda, vingapi vimekamilika na vingapi bado na hiyo pesa iko wapi na kama ilitumika vibaya waliohusika wako wapi, Waziri anaweza kazi hiyo. Vilevile miradi ambayo inaendelea fedha yake iko wapi, wallomaliza zile *certificate* walipwe ili ifikapo mwaka 2020 miradi iwe imefanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema kwamba tuendelee kuiamini Serikali yetu ambayo ina nia njema na imejiaandaa vizuri. Kama ambavyo Serikali imeweza kupeleka fedha za dawa na fedha za maji tutapeleka kwa sababu ndiyo kipaumbele pia cha Serikali ya CCM. Kama ambavyo tumeweza kujenga shule katika kila kata na siku moja suala la maji litabaki kuwa historia. Kama ambavyo tumeweza kupeleka madawati kila shule na mpaka yamebaki ya ziada tutafanya, kama ambavyo tunafanya miradi mikubwa ya kimkakati ya kuchimba gesi na mingine na mingine. Tuendelee kuwa na imani, imani huzaa imani na subira huvuta heri. Hakuna nchi yoyote duniani inaweza ikaendelea kwa kuwa na miradi minge na huu ushauri tumekuwa tukiutoa sisi Wabunge kwamba twende na miradi michache inayoteklezeka, lakini ya kimkakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa niendelee kuishauri Serikali, jamani kilio cha Wabunge wengi mmekisikia na mimi ninayezungumza ni mdau naongea na wanawake. Tunaomba katika mwaka huu wa fedha hii miradi ikamiliike na mwaka wa fedha ujao katika vipaumbele mtakavyovipanga maji, maji, maji, maji na bajeti ya maji iwe ni kubwa na fedha zote zipelekwe kama ambavyo zimepitishwa. Nina imani Serikali kwa kuwa ni sikivu wametusikia, kilio cha Wabunge ni kikubwa, kilio cha wanawake ni kikubwa na mimi hivi karibuni nilikuwa vijijini wamesema na mimi nahakikisha tutahakikisha maji yanapelekwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie mradi wa Mgango - Kiabakari - Butiama. Mheshimiwa Waziri nimefurahi kweli nimeona katika ukurasa wa 37 umezungumziwa. Hivi mnataka Mke wa Baba wa Taifa Mama Maria ndiyo aje

kuomba maji hapa? Huu mradi umeanza tangu mwaka 1978, umefanyiwa tathmini miaka 15 iliyopita kuititia wafadhili wa *BADEA* wametenga USD 32, leo hapa naona mmeandika 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi tangu nimekuwa Mbunge huu sasa ni mwaka wa kumi na kitu, tunazungumzia uendelezaji wa huu mradi hivi kuna shida gani na huu mradi? Hivi kweli Mama Maria aje kutuomba maji hapa Bungeni? Nataka nikuombe Mheshimiwa Kamwelwe utakapohitimisha leo uzungumze na wananchi wa Butiama na Mama Maria Nyerere akusikie. Hivi huu mradi wa *BADEA* unakuja lini? Kama mradi huu haupo, Serikali ina mkakati gani wa kutenga fedha zake za ndani kama ambavyo mmefanya katika miradi mingine, tupeleke maji kutoka Kiabakari - Butiama mpaka Mgango. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jamani Baba wa Taifa alikuwa ni kiongozi, alikuwa hajipendelei, aliangalia Watanzania wote na ndiyo maana mpaka leo hata barabara ya kwenda kwake hajajengwa ndiyo inajengwa sasa, tena mmeweka wakandarasi kumi, tumevumilia tunakubali. Mwalimu aliangalia watu wote, alipeleka maji mpaka Kilimanjaro yanatiririka yenyewe kuititia kwenye milima, hakujiangalia yeye. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali mpo hapa, hizi fedha za *BADEA* ni lini zinakuja na zipo kwa nani? Nakuomba jioni hii utakapo-*windup* hapa tuambie ili kama fedha hazipo tukawaambie wananchi wa Butiama, tukaongee na Mama Maria Nyerere kwamba huu mradi wa maji sahau mama hautakuwepo, tuendelee kuchimba maji na kutumia Mto Kialani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona nizungumze hili kwa uchungu kwa sababu nimekaa miaka kumi, huu mradi nimeupigania muda mrefu, Serikali iliniahidi kwamba *BADEA* ipo na hapa naiona, lakini leo nimesikitika kwamba eti sasa unaenda kufanyiwa tena upembuzi yakinifu, upi na wakati

upembuzi yakinifu ulishafanyika. Hebu leo Mheshimiwa Waziri toa kauli yako na sina mashaka na wewe utafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kujua huu mradi utahudumia wananchi wa Kata ya Mgango pale ambapo chanzo kipo, kwa sababu wale wananchi chanzo kinatoka pale lakini hawahudumiwi na mradi huu. Napenda kujua hizi fedha pia zitakazotengwa na *BADEA* watapeleka maji Kiliba na Tegeluka, Kata hiyo hiyo ya Musoma Vijijini au itaishia hapo peke yake na kupeleka Kiabakari hawa ambaa ndiyo wa chanzo cha maji watabaki kuwa watazamaji? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujua hii Wilaya ya Musoma Vijiji, Wilaya aliyozaliwa Baba wa Taifa, Wilaya ambayo imeasisiwa miaka mingi iliyopita kutokea Mrangi mpaka Busekela, kutokea Busekela mpaka Kukilango na Bugwema, hivi tatizo la maji ni la nini wakati Wilaya imezaungukwa na ziwa? Nimepekuapekua humu sikuona vizuri, hebu tuambie Wilaya hii ya Musoma Vijijini na Butiama Serikali ina mpango gani kuwafikishia wananchi maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuipongeza Serikali kwa kusikiliza killio cha muda mrefu cha Wabunge kupeleka huduma ya maji katika Mji wetu wa Musoma na miji mingine mingi hapa nchini, hali sasa hivi ni nzuri ikiwepo na Jiji la Dar es Salaam, napongeza sana. Dar es Salaam sasa miundombinu ya maji imejengwa, hata juzi nilipokuwa kwenye kampeni Kinondoni haikuwa tena hoja, naomba niipongeze Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu sasa naiomba Serikali pelekeni fedha *DAWASA* na *DAWASCO* kwa ajlili ya kujenga miundombinu ya maji maana iliyokuwepo imechakaa na mabomba yanapasuka kusababisha upotevu wa maji na kwenye taarifa ya Waziri umesema. Bila kujenga hii miundombinu na *pressure* ya maji haya yanayokuja kwa sababu ni mengi tutakuwa hatujafanya chochote na maji yatakuwa yanapotea bila sababu yoyote. Ukiwemo na Mji

wa Musoma, Bukoba na miji mingine yote ambayo miundombinu yake imechakaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilete ombi maalum huo mradi wa *BADEA* unachelewa, nawaomba tu...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. AMINA S. MAKILAGI:** Mara hii? Naunga mkono hoja, ahsante sana. Mengine nimeleta kwa maandishi myazingatie, ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Rose Kamil atafuatiwa na Mheshimiwa John Heche, hawa ni dakika tano/tano, Mheshimiwa Prosper Mbena ajiandae kwa dakika kumi.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa na mimi fursa ya kuweza kuchangia Wizara hii ya Maji. Na mimi pia niungane na wenzangu kusema kwamba maji ni uhai, maji ni uchumi wa viwanda na hasa kilimo pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninachosikitika ni kwamba ndugu zetu wanasifia, wanasifia halafu wanadai, wanalia. Mimi napenda kuwaeleza Mheshimiwa Waziri kazi yako unaifahamu kama Wizara, jukumu lako ni kutafuta fedha, kuandaa miongozo ya utekelezaji na kutoa ushauri wa kitaalam. Mikoa kazi yao ni kusimamia na kutoa ushauri wa kiufundi na Halmashauri zetu kazi zake ni kutekeleza miradi ya maji vijijini. Kinachoshindikana kwetu ni wewe Waziri kushindwa kutekeleza wajibu wako. Umeshindwa kututafutia fedha, kwa nini umeshindwa kutafuta fedha? Kila Mbunge anakulilia kuhusu maji. Angalia bajeti yetu tulioipitisha ni kwamba tulipitisha shilingi bilioni 623.6 lakini ukashindwa kutafuta hizo fedha umetupatia shilingi bilioni 135, asilimia 22; ni wajibu wako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ni wajibu wako kwa nini hukwenda kumilia mwenzio, Waziri wa Fedha yupo hapa, mko naye kila kila siku, mpo nao kwenye Baraza lenu la Mawaziri mmeshindwa kututafutia hizo fedha, kuna nini au kuna mtu mwingine ameshikilia hii hela kwa sababu wapitishaji na waidhinishaji ni Bunge na Bunge likipitisha maana yake ni fedha na kodi za wananchi, siyo hela ya mtu binafsi. Kwa nini hizi hela zimeshindikana kuja kwenye mradi wa maji, kosa lipo kwako, tutakulaumu. Watu wanasema wewe ni mgeni, wewe sio mgeni kwenye Baraza hili la Mawaziri, ulikuwa Naibu Waziri wa Maji, kwa hiyo, wewe sio mgeni na Wizara, hakuna ugeni kwenye Wizara, wewe sio mgeni unafahamu kila kitu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo muhimu ya kuzungumza ni kwamba, je, maji ndiyo kipaumbele au *bombardier* ndiyo kipaumbele au *standard gauge* ndiyo kipaumbele. Waziri alipokuwa anatoa hotuba hapa, *glass* ya maji iko karibu yake, ya nini? Maana yake anataka kutengeneza uhai wake. Alipokuwa kwenye *Tulia Marathon* nimewaona kabisa mmebeba maji, ya nini kama sio muhimu? Mimi nadhani maji ni muhimu na tuangalie suala la maji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napenda kuzungumzia suala la fedha zilivyotafutwa ambapo ameshindwa Waziri na tunakulaumu wewe Waziri kwa kweli kushindwa kutafuta hizi fedha. Kulikuwa na *BRN* ya kutekeleza miradi ya vijijini na hiyo *BRN* ilienda wapi? Zile shilingi trilioni 1.45 zipo wapi, za miaka mitatu iliyopita? Ina maana kwamba fedha zile zilipatikana, zilipokwenda vijijini hazikufanya kazi halafu wewe ukienda vijijini kule kutembelea miradi unapokelewa na Mkuu wa Mkoa/Mkuu wa Wilaya unaenda kupelekwa kwenye mradi mmoja tu kumbe miradi mingine yote ni mibovu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Kamati ya *LAAC*, *CAG* anatuelekeza kabisa kusema kwamba miradi ni mibovu na kweli tukienda kukagua miradi yote ni mibovu haijatekelezeka halafu kwenye kitabu chako huku

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

umeandika miradi yote imetekelvezeka, haikutekelezeka. Ndiyo maana tunaomba kuunda Tume ambayo itaenda kuangalia haya masuala na ni watumishi wako wanaofanya hiyo kazi na wewe hukwenda kuwasimamia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna miradi ya Same – Korogwe ambayo imetolewa taarifa yake. Tangu mwaka 2014 ilitolewa fedha dola milioni 41.36, ni kutengeneza mradi huo amba mmeuweka tena mwaka huu, sijui wa kuweka dawa, kutandika bomba, sijui wa kitu gani, haukutekelezeka. (*Makofi*)

*(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa John Heche atafuatiwa na Mheshimiwa Prosper Mbena, Mheshimiwa Kunti Majala ajiandae.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuitisha familia yangu katika kipindi hiki kigumu ambacho mdogo wetu Suguta alichomwa kisu na polisi kwenye Kituo cha Polisi akiwa amefungwa pingu na akafariki dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo moja linalonisikitisha, sijui ni kwa makusudi au ni kwa bahati mbaya, haijatoka *official statement*ya Serikali kwa maana ya Waziri anayehusika kukemea au kulaani kitendo kile kiovu kilichofanywa na polisi. Kwa hiyo, hilo namuachia Mungu na kwa sababu wao wanafikiri wako salama waache wajidanganye.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hii inashauriwa mara nyingi na mimi nasikitika mipango ya Serikali ya CCM ni mipango ya miaka miwili au mwaka mmoja na ndiyo maana mipango mingi ina-fail. Mngekuwa mnachukua mawazo hapa na mnayafanya kazi mmengekuwa hampati matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mnakumbuka wakati mnajenga kituo cha *DART* pale, Mheshimiwa Mnyika

aliwaambia kwamba hapa huwa panajaa maji na wakati ule Rais huyu wa sasa akiwa Waziri. Mmejenga pale kituo kwa mabilioni ya pesa za Watanzania, leo kinajaa maji. Hiyo ndiyo mipango yenu, miaka miwili haijapita kituo kinajaa maji pale mafuriko. Sasa nimeona gazeti la leo linasema mnataka mhamishe kituo pale mpeleke Ubungo, pesa mlishawekeza pale, nani analipa hizo pesa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala la maji na tuelewane vizuri, Mheshimiwa Kamwelwe wewe umeenda Tarime ukakimbia huktuambia sisi, ukaenda. Kuna miradi pale Waziri Mkuu amekuja ameionna, mradi kwa mfano wa Gibaso shilingi milioni 900 imepelekwa hautoi hata tone la maji. Leo watu wanasesma hapa tuunde Tume ya Kibunge ipitie miradi nchi nzima ilete taarifa Bungeni siyo kwa ajili yako, kuangalia hawa watu waliopelekewa pesa na wamekula pesa za walipa kodi wengine wanasmama hapa wanapinga, sasa mnappinga nini yaani hata hamueleweki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu miradi imepelekewa pesa, pesa zimeliwa leo mnakuja hapa Wabunge mnasema muweke tozo shilingi 50 kwa wananchi maskini ambao mmeweka kwenye REA, pesa za REA mmeweka shilingi 50 haziendi mpaka sasa, miradi ya *densification* na miradi ya REA imesimama. Pesa hizi muweke kwa mama anayesaga kwa mafuta ya dizeli, mama ambaye anapanda bodaboda kijijiini, mama ambaye ananunua mafuta ya taa mumuwekee ongezeko la shilingi 50, mumuumize wakati tunajua na tuna uhakika hamtapeleka maji wala hayo maji hayatapatikana. Sasa hii kitu haikubaliki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana tunasema *Engineer Kamwelwe* uliambie Bunge hili, mwaka jana ultuambia kuna dola milioni 500 kutoka Serikali ya India, zipo wapi hizo pesa? Kama umesahau sisi wengine tuna kumbukumbu, tunakukumbusha, zipo dola milioni 500 ambazo miltuambia kwamba zipo kwa ajili ya maji vijijini, zipo wapi? (*Makofii*)

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nimesoma kitabu hiki cha kwenu, mama Makilagi amesimama pale anachangia Mbunge aliyepita sasa hivi amezungumza hata kwa Mwalimu Nyerere hakuna maji. Mimi nimezaliwa Tarime maji yapo, miaka ya 1980 watu wanatumia maji ya bomba. Kadri tunavyoenda mbele tunarudi nyuma yaani leo mwaka 2018 hakuna maji ya bomba, mwaka 1980, 1985, 1986 kuna maji. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi tukiwaambia bora wakoloni kuliko ninyi Serikali ya CCM hivi mnapinga nini? Kama wakoloni waliacha mabomba, leo hata mabomba waliyoacha yamekuwa, yamewashinda, hivi ninyi mnapinga nini sasa hapo yaani mnapingana na nini kwa sababu Serikali yenu imeshindwa. (Makofi)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri muda wake wa kuchangia umekwisha, ahsante sana.

Tunaendelea na Mheshimiwa Prosper Mbena kwa dakika kumi atafuatiwa na Mheshimiwa Kunti Majala, Mheshimiwa Tunza Malapo kwa dakika tano ajiandae.

**MHE. PROSPER J. MBENA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru sana Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa jitihada kubwa anazofanya katika kutuletea maendeleo katika nchi yetu. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa jitihada kubwa anazofanya katika sekta hii ya maji. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kwa kweli kumshukuru kwa dhati, kulikuwa na tatizo la muda mrefu la

fidia ya watu wa Selembala katika Jimbo langu, fidia ambayo zaidi ya miaka minne tumekuwa tunahangaika nayo lakini kwake ye ye amelifanikisha na wananchi wamelipwa jumla ya shilingi bilioni 3.3. Siyo pesa ndogo, amejitahidi namshukuru sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo changamoto ndogo ndogo ambazo bado sekta hii tunaiomba itusaidie kuitia kwa Waziri. Moja, yapo maeneo katika Jimbo la Morogoro Kusini ambayo kwa kweli yanapewa maji ya visima, lakini hayastahili kunywa maji ya visima. Zipo sehemu za Sesenga na maeneo ya Kisaki, nashauri tuwe na mradi wa kupeleka maji ya bomba. Hili linawezekana kwa sababu tuna mito mikubwa tu ambayo ipo maeneo yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nitaliomba kwa Mheshimiwa Waziri ni kuangalia uwezekano wa kuwa na mradi ndani ya Jimbo lile wa kueneza mabomba ya maji, yachukue kutoka kwenye vyanzo vya mito ili wananchi wapate maji safi na ya uhakika, tuachane na visima. Yapo maeneo kweli yanastahili visima lakini sio katika jimbo lile ambalo limezungukwa na mito mikubwa, sehemu nyngi hizo na *details* zake nitampatia Mheshimiwa Waziri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu nitakaloomba kwa Waziri, atakapokuwa anangalia uwezekano wa kutengeneza miradi mikubwa ya namna hiyo, aone wataalam waliopo katika halmashauri zake. Halmashauri zetu wakati mwingine tunakosa kuwa na miradi mizuri kwa sababu ya kukosa watu wenye uwezo wa kubuni na hili ni suala la utaalam. Nitamuomba sana aliangalie kwa upande wa Morogoro Vijijini ili tuweze kuwa na wataalam wa kutosha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, langu mimi kubwa ilikuwa nimshukuru Waziri amefanya jitihada kubwa sana, ahsante sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Shukrani sana Mheshimiwa. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Kunti Majala atafuatiwa na

Mheshimiwa Tunza Malapo na muda wetu ukiruhusu Mheshimiwa Aisharose Matembe ajiandae.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia Wizara hii ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu niseme kwamba hakuna Mbunge hata mmoja ambaye anaamini kwamba maji siyo muhimu. Nisikitike tu watu wanaopinga suala zima la kuundwa kwa tume ya kwenda kuchunguza hali halisi ya miradi ya maji kwenye maeneo yetu. Leo kama Wabunge tungekosa maji hakuna Mbunge hata mmoja angekuja humu ndani, hayupo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uundwaji wa tume, Wabunge tunahitaji tume iundwe kwa sababu tumekuwa tukizungumza suala zima la ujisadi kwenye miradi ya maji, Serikali kwa maana ya Wizara mmekuwa hamtuelewi. Mwaka jana nilizungumza suala la Mradi wa Ntomoko, mwaka juzi hali kadhalika, mradi huu sikuwahi kupata majibu, uliendelea kupigwa danadana kwenye vitabu vya Waziri, safari hii hata kwenye kitabu cha Waziri Mradi wa Ntomoko haupo na matokeo ni mpaka Rais ndiyo amekwenda kutoa kauli ya kwamba waliotumia fedha za Mradi wa Maji Ntomoko wachukuliwe hatua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tuna kosa gani Wabunge tukisema Mawaziri hawako tayari kwenda kufanya kazi na kusimamia miradi hii ya maji kwa ukamilifu wake? Kwa nini tukisema kwamba Mawaziri mmeshindwa, amebaki mtu mmoja peke yake ndiye anayetoa kauli za miradi na shughuli mbalimbali za Serikali kutendeka.

Suala la Ntomoko tumelisema hapa miaka nenda, miaka rudi, hamkuwahi kusema chochote na hamjawahi kuchukua hata hatua yoyote mpaka Rais amekwenda kuchukua hatua. Sasa ninyi Mawaziri kazi yenu ni nini, si bora mtoke wote abaki Rais Magufuli peke yake afanye kila kitu, ninyi mnafanya nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la upatikanaji wa maji nchini ni changamoto kubwa sana. Vijijini kuna shida ya maji wote humu ndani sisi ni mashahidi. Taabu hii wanaoilpata ni wanawake wanaoishi vijijini. Mwanamke wa kijijini kulala kwake analala saa mbili, anaamka saa saba za usiku, saa tisa za usiku anatembea zaidi ya kilometra 20, 40 anakwenda kutafuta maji, anarudi mwanamke huyu amechoka bado anatakiwa kwenda kuihudumia familia yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini watoto wetu wa kike wanapata taabu kubwa sana. Leo watoto wa kike wanapata mimba za utotoni kwa sababu ya kutembea umbali mrefu kwa ajili ya kwenda kutafuta maji na Serikali mnawakatalia watoto wetu wa kike kurudi shule wanapopata mimba za utotoni eti kwa sababu amepata mimba, akienda shuleni atakuwa ni mzazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Chama cha Mapinduzi haina dhamira ya dhati ya kwenda kumtua mwanamke na mtoto wa kike ndoo kichwani. Serikali ya Chama cha Mapinduzi inaendelea kumdidimiza Mtanzania wa chini aendelee kudidimia kwenye shughuli za kiuchumi, elimu na hatimaye sisi Wabunge tulio wengi wa Chama cha Mapinduzi tunaopata maji safi na salama, elimu bora na familia zetu zinasoma vizuri ili watu hawa wanyonge wa huko chini watoto wao wasisome, wasipate maji safi na salama, wafe kwa maradhi, ili familia zenu viongozi wa Chama cha Mapinduzi waje waendelee kuliongoza Taifa hili. Dhambi hii Mwenyezi Mungu anawaona na hakuna malipo yanayokwenda kulipwa akhera, tutalipana hapahaha duniani na kila mmoja ataonja jasho lake. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee suala zima la madeni ya taasisi za maji. Mwaka jana nilisema taasisi za Serikali zinadaiwa na Mamlaka za Maji zikiwemo Ofisi ya Rais, Ofisi ya Makamu wa Rais, JKT, Polisi na Magereza. Taasisi zote hizi za Serikali zinadaiwa na Mamlaka za Maji. Kibaya zaidi unakuta taasisi hizi zinadaiwa hazikatiwi maji, Mtanzania/mwananchi wa kawaida anadaiwa mwezi mmoja tu hajalipa anakwenda kukatiwa maji, huu ni uonevu. (*Makof*)

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mbaya zaidi Jeshi la Polisi kwa hapa Dodoma ilifanyika operesheni, walivyokwenda kukatiwa maji Jeshi la Polisi likaamua kukamata magari yote ya *DUWASA* pamoja na pikipiki, vifaa vyote vikakamatwa vikaenda kujazwa pale kwenye kituo cha polisi. (*Makofi*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa Kunti. Mheshimiwa Tunza Malapo, atafuatiwa na Mheshimiwa Aisharose Matembe na Mheshimiwa Injinia Edwin Ngonyani ajiandae kama muda utaruhusu.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kuna kitu kimoja bado sijakielewa vizuri. Serikali hii wanatuambia kwamba wanakusanya makusanyo yanapita mpaka lengo kwa mwezi, lakini cha kushangaza kwenye bajeti ya maji inaenda asilimia 22, sasa hizo hela zinazokusanya zinakwenda wapi? Mtakapokuja kuhitimisha Waziri wa Fedha atueleze, wanatudanganya hawakusanyi ama wanakusanya lakini pesa zinatumika nje ya bajeti tunazopitisha hapa Bungeni? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka tupate ufanuzi huo, asilimia 22 kwenye utekelezaji wa mambo ya msingi, mambo ya maji ni jambo la aibu, la kusikitisha na linalokatisha tamaa wananchi wa Tanzania. Ukiangalia kwenye Ripoti ya CAG ya mwaka 2016/2017 ukurasa wa 99 hadi 100 inaonekana kuna pesa shilingi bilioni 410 zilikusanya na *TRA* ikiwepo pesa kwa ajili ya usambazaji wa maji, lakini kuna pesa haikutolewa kwenda kule inakotakiwa kwa ajili ya kusambaza maji katika maeneo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natokea Mkoa wa Mtwara, tuna tatizo kubwa la maji katika sehemu

mbalimbali. Ukienda maeneo ya Newala Mjini, Newala Vijijini, Nanyamba ukiingia huko ndani Mtwara Vijijini, Mtwara Mjini kwenye kata za pembezoni kuna tatizo kubwa la maji; wale watu wanafikia wanunua mpaka dumu moja la lita 20 shilingi 1,000, shilingi 800, shilingi 500; lakini wale watu wa Mtwara kila siku nasema wanachangia pato kubwa la nchi hii kupidia kilimo cha korosho ingawa nako pia kuwalipa hawalipwi kwa wakati lakini wanachangia. Kwa nini hatukai tukaangalia suala la maji likawa ni suala la kipaumbele? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nataka nipate ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri anapokuja kuhitimisha kuhusu ule mradi wa kutoa maji Mto Ruvuma kuja Mtwara Mjini ambao tunaamini ungefanyiwa utekelezaji wake ungesaidia kwa kiasi kikubwa pale bomba lilipotaka kupita. Mwaka jana tumeona pesa zimetengwa tunaambwa kuna *processes zinaendelea*, hizo *processes zitaisha lini?* Sisi tunachotamani tuone maji safi ya baridi yanapatikana ambayo hayo maji pia yangeenda kusaidia katika uwekezaji wa viwanda ambao mnausisitiza lakini tuna tatizo kubwa la maji katika mkoa wetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maji ni suala mtambuka. Tukikosa maji ya uhakika maana yake magonjwa yatakuwa mengi, hata kama Serikali itakuwa inatoa fedha nydingi kwa ajili ya dawa lakini tukumbuke bajeti ya dawa itakuwa kubwa kwa sababu ya matumizi ya maji ambayo siyo safi na salama. Nasema pia ni suala mtambuka kwa sababu mama anapoamka asubuhi kwenda kutafuta maji kule anakumbana na vikwazo vingi, anaweza akabakwa, akibakwa kesho mnamuita tupime *DNA*, mnapimaje *DNA* wakati ninyi ndio mlisosababisha hayo yote yanayotokea? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tusifanye vitu kwa ajili ya kutaka kujionesha, twendeni tutoe hela. Kama hela zinakusanywa kupita kiwango hizo hela zinakwenda wapi? Watu wakihoji hapa kwamba kuna hela shilingi *1.5 trillion* zimepotea watu mnakasirika, lakini mnasema mnakusanya,

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

kwenye maji haziendi, kuziona hatuzioni. Tunataka tupate majibu ya uhakika ili tujue mustakabali wa nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ungeniuliza mimi kipaumbele ningekwambia maji ni kipaumbele kwa sababu ni mtambuka. Kama huna maji kiwanda hakifanyi kazi, kama huna maji hata hiyo ndege hauwezi kupanda kwa sababu hautakuwa na afya nzuri, unaumwa na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sina mengi ya kuyasema lakini tunaomba tupate kueleweshwa, nakushukuru. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aisharose Matembe atafuatiwa na Mheshimiwa Edwin Ngonyani.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba hii muhimu kwa maendeleo ya Watanzania. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kuwapongeza sana Waziri wa Maji, Mheshimiwa *Engineer Kamwelwe*, Naibu wake, Mheshimiwa Aweso na timu nzima kwa kufanya kazi nzuri ya kuhakikisha Watanzania wanapata huduma muhimu ya maji. Nawapongeza sana na nawatia moyo waendelee kufanya kazi hiyo pamoja na changamoto zillizopo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na wenzangu kusema kwamba maji ni uhai, shughuli nyingi zinategemea uwepo wa maji. Viwanda, kilimo, mifugo na binadamu wote uhai wake ni maji. Waathirika wakubwa wa ukosefu wa maji ni wanawake, wanawake hawa wamekuwa wakitembea umbali mrefu kutafuta maji na hivyo kutokushiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji mali na wakati mwingine

kuhatarisha ndoa zao kwani hutoka usiku sana kutafuta maji hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Maji inamtaka mwananchi kutembea umbali wa mita 400 ili kuweza kuyapata maji. Kwa Mkoa wa Singida maeneo mengi ya vijiji ni imekuwa ni kinyume, wanatembea umbali mrefu hasa wanawake waishio maeneo ya vijiji kuyasaka maji. Kwa kuwa tunaelekea Tanzania ya viwanda, niombe sana maeneo haya ya vijiji niweze kupatiwa maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Singida ni mionganini mwa mikoa ambayo inakua kwa kasi, lakini inapata mvua kwa msimu mmoja kwa mwaka. Hivyo basi naiomba Serikali kuja na mkakati mahsusini wa kuchimba mabwawa ya kuweza kuhifadhi maji kwa mwaka mzima ili kuwawezesha wanawake ambao ni wakulima wazuri wa mazao ya biashara na chakula kuweza kulima kwa muda wa mwaka mzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Serikali kwa kutupatia fedha katika miradi ya maji ya vijiji kumi vya Mbwasa katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni. Niombe iongeze juhudini zaidi kupeleka fedha katika mpango wa pili wa ukamilishaji wa mradi huo.

Pia naishukuru sana Serikali kwa kutupelekeea fedha katika Mradi wa Maji wa Uliyampichi uliopo Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, lakini changamoto iliyopo katika mradi huo ni kwamba hakuna *pump* na fedha za kuweza kuunganishwa na umeme ili uweze kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida Vijiini kuna Mradi wa Maji wa Kijota, lakini mradi huo umekuwa ukitumia *pump* ya dizeli ambayo kwa sasa imeharibika. Niombe sana Serikali iweze kupeleka fedha kiasi cha shilingi milioni 94.6 ili basi waweze kutumia *pump* ambayo itatumia umeme na kwa kuwa kuna miundombinu ya umeme mradi huo uweze kuunganishwa na umeme. (*Makofi*)

## **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi kilichopita nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya LAAC na kazi kubwa tulyokuwa tukifanya ni kukagua miradi ya maendeleo na mingi ilikuwa ni ya maji, lakini changamoto kubwa tulizokuwa tukikutana nazo ni miradi mingi ya maji kutokukamilika kwa wakati au utakuta miradi mingine imekamilika lakini haifanyi kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninao mfano hai kwa Mkoa wangu wa Singida wa Mradi wa Unyanga na Mradi wa Mchama B, ni miradi ambayo imetumia mamillioni ya fedha za walipa kodi lakini haifanyi kazi. Namuomba Waziri wakati wa majumuisho atuambie ni kwa nini miradi ya maji ambayo imetumia fedha nyingi za walipa kodi haifanyi kazi? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Itigi unakua kwa kasi lakini hauna kabisa mtandao wa maji. Naiomba Serikali langalie vile visima ambavyo tayari vimechimbwa basi ipeleke fedha za kutosha ili kuweza kuunganisha miundombinu na mji huo uweze kupata maji ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache, nakushukuru sana, mengine nitachangia kwa maandishi, ahsante sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tumalizie na Mheshimiwa *Engineer Edwin Ngonyani*.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii, ingawa nikiangalia saa pale inanipa shida kidogo, lakini nitajitahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza moja kwa moja na suala la Jimbo langu la Namtumbo. Miradi iliyokuwa inaitwa ya *World Bank* ambayo ilianza mwaka 2005/2006 na kwa maana hiyo ni wakati ambapo Serikali ya Awamu ya Nne ilipokuwa inaingia madarakani, kwangu kwa kweli imepata msukumo mkubwa sana na Mheshimiwa *Engineer Kamwelwe* kama Waziri wa Wizara hii ya Maji na Umwagiliaji. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, umelipa *certificates* mbili za Mradi wa Mkongo - Gulioni na Nahimba na

nimeambiwa kwamba kutokana na ile *certificate* ulioilipa katika wiki zijazo maji yatakuwa yametolewa kutoka kwenye chanzo na kuingizwa kwenye matenki na baada ya hapo, hatua ya pili ya kuyatoa kwenye matenki na kusambaza kwa wananchi itafuatia, nakushukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri nikuombe mradi mwingine katika hii miradi ya *World Bank* wa Likuyu - Sekamaganga ambayo *advanced payment* au *certificate* ya awali inahitaji nayo ilipwe ili na huo mradi nao upate msukumo mkubwa kama ambavyo umeipa msukumo mkubwa huu Mradi wa Mkongo - Gulioni na Nahimba. Naomba na huu Mradi wa Likuyu - Sekamaganga nao upate msukumo mkubwa kama huu mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini vilevile Mradi wa Luhimbaillo na Naikesi ni kati ya miradi hiyohyo ya *World Bank*. Nikuombe nayo uipe msukumo mkubwa, kulikuwa na tatizo la ubadilishaji wa chanjo kwa sababu chanjo cha mwanzo ilionekana maji sasa yalikuwa hayatoshi kutokana na miaka hii kumi yote iliyopita na sasa chanzo kipyaa kimepatikana, kina maji mengi sana. Nikuombe na huo mradi tupate fursa ya kuutangaza ili nao utekelezwe. Pamoja na kwamba ultitakiwa utekelezwe miaka kumi iliyopita lakini kwa namna wewe Mhandisi ninavyokuona utanisaidia na huo mradi uanze kutekelezwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mradi mwingine mkubwa unao-cover vijiji karibu vitano, unajulikana kama Mradi wa Hanga – Mawa – Msindo. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, kwa kasi kubwa ulioianza ya kutusaidia miradi hiyo miwili ya mwanzo na huu nao uupe msukumo mkubwa ili hatimaye Wanamtumbo, ambao zaidi ya asilimia 95 ni watu wa vijijiini waweze nao kunufaika na sera au na kaulimbiu ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuwafikia wanyonge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuhakikishie katika miradi hii ambayo umeanza kuipa msukumo, hakika unatekeleza kauli mbiu hii ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano ya

kuwafikia wanyonge, watu wa chini na kwa kweli kwa upande wa Wilaya nzima ya Namtumbo tunaongelea zaidi ya asilimia 95. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *certificate* ya pili kwa Mradi wa Kumbara – Litola ambaa naamini Mheshimiwa Rais atakapofika kutembelea Wilaya ya Namtumbo pengine tutapata fursa ya ama kuwekea jiwe la msingi au pengine ukiwashisha kulipa fedha hizo atafika tayari maji nayo yatakuwa yametoka kwenye chanzo na kufika kwenye matenki kwa sababu ujenzi wa matenki tayari umeshakamilika. Nikuombe sana hii *certificate* ya pili ya kazi nayo ilipwe ili miradi hii ipate msukumo, imechelewa kwa muda wa miaka kumi lakini tunataka kuitekeleza katika miaka miwili, mitatu ya Serikali ya Awamu hii ya Tano. Nikuombe kwenye hilo unisaide sana iweze kukamilika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna miradi hii iliyokuwa imetwa ya *quick win*, ni kwa ajili ya vijiji vya Namabengo na Mchomoro. Tuliiweka katika Programu ya Miradi ya *Quick Win*, ilitengewa shilingi milioni 300 kwa mwaka huu unaokaribia kuisha, nadhani unafahamu kwamba tumeomba toka mwezi wa saba na baadae kukawa na mawasiliano ya kubadilisha makadirio na namna ya ku-*design* tukabadilisha, mwezi wa tisa tukawaletea. Tunaomba tupate kibali cha kutangaza kwa sababu huo ndiyo utaratibu, pamoja na kwamba fedha zimetengwa hizo milioni shilingi 300 katika hiyo miradi miwili na lengo lilikuwa ni *quick win* lakini mpaka sasa hatujapata kibali cha kutangaza. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, hebu ongeza msukumo kwa watendaji wako, miradi hii miwili ya *quick win* ipate ruhusa ya kutangazwa ili hatimaye tuitangaze na tuwahi kabla ya tarehe 30 Juni tuweze kutumia hizo shilingi milioni 300 tulizotengewa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu fedha hizi za shilingi milioni 300 kwa miradi hii miwili ya *quick win* kama hatutaweza kutangaza ina maana tutashindwa kuzitumia. Sasa mmetutengea shilingi milioni 80 kwa kila mradi, toka

shilingi milioni 300 tunashuka kwenye shilingi milioni 80, tusipoitumia ile shilingi milioni 300 hiyo shilingi milioni 80 haitafanya kazi kubwa na kwa kweli maana halisi ile ya *quick win* haitakamilika. Nikuombe sana utusaidie, tupe ruhusa ya kutangaza ili tuweze kutangaza na tuweze kuzitumia hizi shilingi milioni 300 ili hizi shilingi milioni 80 zinazofuata kwa mwaka 2018/2019 tuweze sasa kukamilisha kabisa na wananchi wale wa Mchomoro pamoja na Namabengo waweze kupata maji kama ambavyo Serikali ya Awamu ya Tano ilikusudia kufanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri nikuombe sana liangalie hilo. Kibali cha kutangaza ni barua tu na kwa maana ya kuutathmini huo mradi mlishefanya hiyo kazi kuanzia mwezi Julai mwaka jana. Nikuombe sana, hebu tupe hicho kibali ili hii miradi iweze kuanza kutekelezwa na maana ya *quick win* ikamilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri nikuombe sana unisaidie katika maeneo mengine sugu sana ya Mgombasi, Matepwende ya Msisima, Matempwende ya Ligera au Matepwende ya Milonji, Lometa pamoja na Mtakanini, ni vijiji ambavyo vina matatizo makubwa sana ya maji. Labda tu nikwambie pale Mtakanini...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ngonyani, sekunde mbili, malizia.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pale Mtakanini hilo ombi lilitolewa na Marehemu Mzee Kawawa na likakubalika na wakati huo Rais wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Mkapa lakini mpaka sasa hatujapaangalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuombe sana na hapo napo tupaweke vizuri ili wananchi wa Mtakanini na Lometa... (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer* Ngonyani, muda wako umekwisha.

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsanteni sana, Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu. Mchana tutaendelea na wachangiaji wachache, tutaanza na Mheshimiwa Vedasto Ngombale atafuatiwa na Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vulu na Mheshimiwa Sikudhani Chikambo.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo mawili; tangazo mojawapo ni la kuwakumbusha na nilikwishalitangaza asubuhi, mnakumbushwa kwamba leo kutakuwa na warsha itakayohusu uhamasishaji wa afya bora na jinsi ya kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza. Mnaombwa kufika Ukumbi wa Msekwa mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge.

Tangazo lingine, mnatangaziwa na Mheshimiwa Shally Josepha Raymond ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuia ya Mtakatifu Thomas Moore - Bunge, anawatangazia kwamba leo siku ya Jumatano tarehe 9 Mei, kutakuwa na Ibada ya Misa kwa Wakristo Wakatoliki mara baada ya kuahirisha Bunge saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Msekwa, ghorofa ya pili, nadhani anamaanisha Jengo la Msekwa ukumbi ambao ni ghorofa ya pili. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kushiriki misa hii.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni leo.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka Mheshimiwa Spika alikuwa ametoa maelekezo jana kwamba Serikali tutakapoanza Bunge mchana huu ituletee taarifa kuhusu

mafuta ya kula. Kwa hiyo, nitamuita Mheshimiwa kwa ajili ya taarifa hiyo. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, taarifa. (*Makof*)

### **Taarifa ya Serikali Kuhusu Upungufu wa Mafuta ya Kula**

#### **WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilipokea maelekezo ya Ofisi yako kwamba tutoe taarifa kuhusu tatizo la upungufu wa mafuta ya kula nchini ifikapo saa 11.00 jioni leo tarehe 9 Mei, 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya mafuta ya kula nchini yanakadiriwa kuwa kati ya tani 400,000 mpaka 450,000 kwa mwaka. Vyanzo vya mafuta hayo ni pamoja na mbegu za pamba, alizeti, ufuta, karanga kwa kutaja baadhi. Hata hivyo, vyanzo viliviyotajwa hapo juu vinatosheleza asilimia 30 ya mahitaji ya nchi huku asilimia 70 ikiagizwa kutoka nje ya nchi. Mafuta yanayoagizwa ili kuziba upungufu wa mahitaji ya soko ni mafuta safi (*refined*) na mafuta ambayo hayajasafishwa (*crude palm oil* au *crude sunflower*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2017 makampuni binafsi ambayo ndiyo huagiza mafuta kwa minajili ya kuyasafisha kwenye viwanda vilivyoko nchini waliagiza tani 344,369.9 hii ikiwa ni wastani wa tani 28,697 kwa mwezi. Kwa mwaka huu wa 2018 kwa miezi mitatu ya mwanzo Januari hadi Machi, 2018 wastani wa mafuta yaliyoagizwa kwa mwezi ni tani 30,210.71.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya kiasi cha mafuta kilichopo katika hifadhi kwa sasa ni tani 68,902 ambayo yameagizwa na Kampuni ya *East Coast, Murzah Oil, BIDCO, G and B* na *Mikoani Traders*.

Wakati huohuo, mafuta yaliyoko kwenye meli yakisubiri kushushwa kwa ajili ya makampuni hayo ni tani 46,000. Katika kiasi hicho cha mafuta yaliyoko baharini, taratibu za ushushaji zimeanza tokea juzi na kwa sasa tani 16,500 zimeshashushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nieleze kwa kifupi taratibu za uagizaji na ushushaji wa mafuta mpaka kwenye viwanda nya usafishaji. Mafuta yanapoagizwa na kufika bandarini, *TBS* kwa maelekezo ya *TRA* huchukua sampuli ili kuhakiki kama mafuta hayo ni ghafi au si ghafi. *TBS* hutumia vigezo vikuu viwili katika kubaini kama mafuta hayo ni ghafi au siyo ghafi. Kipimo cha kwanza ni *Free Fat Acid (FFA)* na kipimo cha pili ni rangi ya mafuta hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya vipimo nya *TBS* huwasilishwa kwa *TRA* ambaye ndiye mwenye mamlaka kwa mujibu wa sheria za kodi kuachia mafuta ili yaingie viwandani. *TRA* pamoja na matokeo ya *TBS* huwataka waagizaji kuwasilisha nyaraka zifuatazo:-

- (i) Nyaraka mbalimbali kutoka kwenye mamlaka inayotambuliwa kutoka kwenye nchi ambako mafuta yametoka; na
- (ii) Vielelezo vinavyoonesha malipo ya mizigo ilioagizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichotokea katika jambo tunalozungumzia leo ni kwamba kuna shehena ya tani 68,902 ambazo kutohana na vipimo nya *TBS* zimebainika kwamba sehemu ya shehena hiyo imekutwa kuwa na utata katika viwango. Kama nilivyoeleza awali, matakwa ya kiforodha kabla ya kuruhusu shehena mwagizaji pamoja na majibu ya *TBS* anapaswa kuwasilisha nyaraka nilizozitaja hapo juu. Waagizaji pamoja na kutakiwa na *TRA* kuwasilisha nyaraka hizo hawajafanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na wastani wa uagizaji wa mafuta kwa miezi mitatu ya mwazo ya mwaka 2018 kuonyesha kuwa uagizaji umekuwa juu ya wastani wa mwaka 2017 inashangaza kuona kuna uhaba wa mafuta nchini. Hii inatokana na ukweli kwamba mafuta yaliyoagizwa miezi mitatu ya mwanzo mwaka 2018 yalitegemewa mpaka sasa ndiyo yangkuwa yanaingia sokoni baada ya kusafishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Bunge lako tukufu lifahamu mambo yafuatayo:-

(i) Kuna mafuta ghafi ya kutosheleza mahitaji ya nchi kwa wastani wa miezi mitatu kwa takwimu nilizozieleza hapo juu;

(ii) Kufuatia kiasi cha mafuta ghafi yaliyoagizwa miezi mitatu iliyopita, tunapaswa kuwa na mafuta safi ya kutosheleza mahitaji ya wananchi kwa sasa;

(iii) Kulingana na utaratibu wa kiforodha, waagizaji wote wanatakiwa kwa mujibu wa sheria kuwasilisha nyaraka zinazohitajika na *TRA* jambo ambalo mpaka sasa hawajalifanya.

(iv) Kutokana na maelezo hapo juu, ni dhahiri kuwa wenye viwanda wamekataa kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulihakikisha Bunge lako Tukufu kuwa Serikali itahakikisha wananchi wanapata mafuta ya kula katika hali ya kawaida kama ilivyokuwa mwanzo. Aidha, tunapoingia katika kipindi cha mwezi Mtukufu wa Ramadhani, Serikali itatumia uwezo wake wote kuhakikisha kuwa hakuna mtu atakayechonganisha Serikali na wananchi wake kwa kusababisha upungufu wa mafuta na bidhaa yoyote nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.  
*(Makofii)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa wiki iliyopita siku ya Alhamisi wakati wa Maswali ya Papo kwa Papo, nimewahi kujibu swalii hili sambamba na swalii ambalo lilikuwa linataka maelezo juu ya sukari na nikaeleza kuwa nimeunda timu ambayo inafanya mapitio ya kero ambayo jana nimetoa maelekezo na leo Waziri ametoa maelezo yake pia ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikubaliane naye kwamba maelezo yake ni sahihi kwa sababu ni jana tu nilikuwa napokea taarifa hii ya mwenendo wa mafuta yaliyoingizwa nchini na upungufu wa mafuta uliopo na kwa nini upungufu huu upo lakini na kile ambacho kilikuwa kinazungumzwa kwamba kuna mgongano wa taasisi zinazohakiki ubora, *TBS*, Mkemia Mkuu wa Serikali na *TFDA* kwa *TRA* kwamba labda *TRA* anakataa takwimu zilizopimwa na taasisi zetu zinazohakiki ubora.

Mheshimiwa Naibu Spika ni kweli kwamba eneo hili *TBS*, *TFDA* pamoja na Mkemia Mkuu mzigo wote unapofika nchini huwa wanajiridhisha ubora wake baada ya kuwa wamepokea nyaraka za nchi mzigo huo unakotoka na ubora wake ndipo sasa *TRA* wanaendelea na taratibu za tozo kadri ya ubora na kuruhusu kuingia nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa takwimu ambazo tunazo sasa, nataka nirudie kuwashakikishia Watanzania kwamba kusingekuwa na sababu ya kukosekana kwa mafuta au kupanda bei kwa mafuta ya kula nchini sasa hivi kwa sababu ya zile sababu zilizoelezwa na Mheshimiwa Waziri kwamba wastani wa mafuta kila mwezi yanayotumika nchini ni lita zisizozidi tani 28.9 na sisi kila mwezi kwa mujibu takwimu tulizonazo, tunaingiza mafuta si chini ya tani 30,000. Kwa hiyo, mafuta tulioagiza Januari, Februari, Machi yayofikia zaidi ya tani 30,000 yalikuwa yanaweza kabisa ku-*cover* mwezi Aprili na mafuta mwezi Mei ambayo yamepokelewa jana na leo yanaendelea kupokelewa zaidi ya tani 46,500 kusingekuwa na sababu hiyo ya kupungua kwa mafuta. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili hatuwezi kukubaliana nalo tukaliacha hivihivi kama lilivyo kwa sababu uko mpango unaonekana wa kutaka tu kuyumbisha Watanzania na hasa kipindi hiki ambacho tunajua Waislamu wanaenda kufunga, kama ambavyo nilieleza wakati najibu swali la nyongeza la kwa nini sukari haipatikani, mafuta hayapatikani, kipindi hiki ambacho tunaelekea kwenye Ramadhani. Nataka nitoe wito pamoja na maelekezo kwa wafanyabiashara ambao wanahusika kwenye eneo hili la

mafuta lakini pia hata sukari. Tunahitaji kuwa na sukari ya kutosha, Serikali imeweeka utaratibu mzuri na mafuta yapo, lakini sukari pia ipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali tunatoa siku tatu kuanzia kesho Alhamisi, Ijumaa na Jumamosi mafuta yote yaliko bohari yaondolewe, yaendelee kupatikana nchini kote kwa sababu mafuta uhakika yapo ili Watanzania wasihangaike, wasilazimike kununua kwa bei ya juu. Mafuta yaliyoko bandarini yanaendelea na taratibu zake, wafanyabiashara wenye matatizo tutakuwa tunazungumza nao na kuondoa mafuta yao ili yaweze kusambaa ili nchini kote watu wapate mafuta. Kuanzia Jumapili tutalazimika kuingia viwandani na kwenye maghala ili kuhakiki kama mafuta hayapo au la kwa sababu kwa kufanya hilo Waheshimiwa Wabunge shida tunayoipata ni sisi na watu wetu bila sababu yoyote ile na kwa namna hiyo hatuwezi kuvumilia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa nataka nisheheneze hii taarifa ambayo ametoa Mheshimiwa Waziri ili Watanzania watambue kabisa jambo hili haliko kwa bahati mbaya, kwamba mafuta yapo yanatakiwa yaende mitaani, watu wapate kununua tena kwa bei ileile kwa sababu mafuta yapo.

Kwa hiyo, nilikuwa nataka nisheheneze hili ili Waheshimiwa Wabunge mtambue kwamba mafuta tunayo na taratibu za kawaida za kusambaza mafuta zipo, pale ambapo taratibu zinaendelea kwa sababu mafuta yapo tunatarajia kila eneo nchini litakuwa na upatikanaji wa mafuta kama kawaida na bei ni zilezile.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Upande wa Serikali umewasilisha taarifa na hawakusema taarifa hiyo imewasilishwa kwa mujibu wa

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Kanuni gani. Kwa hiyo, maana yake ni taarifa ya Serikali Bungeni ambayo imekuja kama hoja ambayo inastahili ijadiliwe na Wabunge. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimesimama kukuomba utoe nafasi kwa mujibu wa Kanuni kwamba taarifa hiyo ya Serikali ijadiliwe ndani ya Bunge hili tukufu. Tunasema hivyo kwa sababu... (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Umeshaeleweka Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naelezea kwa nini ni muhimu ijadiliwe.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika, umeshaeleweka kaa chini.

Waheshimiwa Wabunge, mwazoni kabisa nimetoa maelezo kwa nini Mheshimiwa Waziri anazungumza saa 11.00 hii. Mheshimiwa Spika alitoa maelekezo jana kwamba Mheshimiwa Waziri aje aeleze kinachoendelea kuhusu mafuta. (*Makof*)

Sasa Mheshimiwa Mnyika anasema taarifa ya Mheshimiwa Waziri Mwijage haijasema inaletwa kwa Kanuni ipi kwa sababu Waheshimiwa Wabunge mnafahamu wazi Kanuni ambayo inaleta taarifa ya namna hii iko Kanuni ya 49. Mheshimiwa Mnyika kwa kuwa Kanuni hii haijatajwa kwenye taarifa hii, anasema yeye kwa tafsiri yake anaona imeletwa kama hoja, kwa hiyo, anaomba Kiti kiruhusu jambo hili ijadiliwe kama hoja nyingine yoyote.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema tangu mwanzo ingekuwa Serikali ndio yenye inataku kuleta hiyo taarifa inatumia Kanuni ya 49, taarifa iliyoletwa leo hapa ndani ni kwa maelekezo ya Mheshimiwa Spika ambayo ameyatoa kwa mujibu wa Kanuni ya 5.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika alivyotoa maelekezo hayo hakusema taarifa hii iletwi kama hoja na kwa hiyo

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

alisema taarifa iletwe na Serikali na Serikali imekwishaleta jambo hilo na kwa maana hiyo maelekezo yake yamekwisha kukamilika. (*Makof*)

Tunaendelea, Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea, niliwataja Wabunge tutakaoanza nao mchana huu.

Mheshimiwa Mnyika naomba ukae.

Tutaanza na Mheshimiwa Vedasto Ngombale atafuatiwa na Mheshimiwa Zaynabu Matibu Vulu. Mheshimiwa Vedasto Ngombale atachangia kwa dakika kumi, Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu dakika tano, Mheshimiwa Sikudhani Chikambo dakika tano.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili basi na mimi nichangie katika Wizara hii ya Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 22 ya bajeti ya maendeleo ambayo imekwishatolewa mpaka sasa ni kielelezo tosha kwamba Serikali ya CCM maji siyo kipaumbele chao cha kwanza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya CCM ina kipaumbele cha mipango tu lakini siyo utekelezaji wa mipango hiyo na ndiyo maana mpaka sasa hivi sehemu kubwa ya Watanzania wameshindwa kupata huduma ya maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niseme kwamba bado Serikali hajafanikiwa kuondoa tatizo la maji kwa wananchi wake kwani wananchi wana shida kubwa ya maji. Sina shida na utendaji wa Waziri na Naibu wake wanajitahidi na kama wangkuwa wamewezeshwa basi mambo yangeweza kwenda sawasawa, lakini tatizo hilo lote kubwa linatokana na Wizara ya Fedha ambayo inashindwa kutoa pesa kwa wakati ili Waziri na Naibu Waziri waweze kutekeleza miradi ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya CCM imekuwa ikijigamba kwamba inakusanya pesa zaidi ya mipango yake, lakini cha kushangaza utekelezaji wa miradi ya maendeleo na maendeleo muhimu kama ya maji inashindwa kutekelezwa, tunashindwa kuelewa. Kama mnakusanya pesa za kutosha kwa nini miradi ya maji ikwame? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali bado haijaliona tatizo hili, sera inaelekeza kumtua mama ndoo kichwani, lakini bado akimama wa vijijini wanapata maji kwa kuyabeba kichwani. Serikali iliangularie hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala zima la Azimio la Bunge lako tukufu. Kamati yangu ya Kudumu ya Usimamizi wa Serikali za Mitaa tulipokuwa tunawasilisha taarifa tulitoa angalizo na Bunge likaazimia kuundwe Kamati Teule ya Bunge kwa ajili ya kuangalia utekelezaji wa miradi ya maji. Lile lilikuwa ni Azimio la Bunge na Bunge lilitaka Kiti kihakikishe kinaunda Kamati Teule ya Maji kuangalia utekelezaji wa miradi ya maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu imefanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo tumegundua kuna tatizo kubwa la utekelezaji wa miradi ya maji na ndiyo maana tukaja na pendekezo lile ambalo sasa limeshakuwa Azimio la Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi kukikumbusha Kiti, tunaomba Kamati Teule iundwe ili utekelezakji wa miradi ya maendeleo uweze kuangaliwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji wengi wamejaribu kueleza tatizo la utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya maji ni shamba la bibi. Naomba hiyo Kamati iundwe haraka ili Bunge liweze kuangalia tatizo hili na kutafuta suluhi yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye matumizi ya maji ya Mto Rufiji. Mito yote mikubwa tayari ina miradi mikubwa ya maji, lakini mpaka hivi leo Mto Rufiji maji yake yanamwagika bure tu baharini. Maji ya Mto Rufiji mamba na boko wanaogelea tu, hayajakuwa na faida za moja kwa moja kwa wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa za kijiolojia zinaelekeza kwamba ukanda wote wa Pwani ukichimba maji utapata maji ya chumvi. Kwa hiyo, ili basi kuwezesha kutoa huduma ya maji kwa wananchi wa Ukanda wa Pwani, maji ya Mto Rufiji yatumike. Tunaomba Serikali ianzishe mradi mkubwa wa maji ili basi wananchi wa Ikwiriri, Muhoro, Somanga, Njianne, Miteja, Kilwa Kipatimu, Kibata wapate maji, tunaomba sana katika hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna suala zima la miradi ya maji katika Jimbo langu la Kilwa Kaskazini. Mpaka hivi ninavyozungumza zipo kata ambazo bado hazijapata miradi ya maji. Kuna Kata za Namayuni, Chumo, Kibata, Kinjumbi, Somanga na vijiji vya Mkarango, Mtondo wa Kimwaga na Ndembu katika Kata ya Kipatimu havina mradi wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni wenzetu wa *DDCA* walikuja na wakafanya utafiti kwa baadhi ya vijiji lakini wakashindwa kufika katika Kijiji vya Nandembo na Kibata. Niwaombe wafike katika vijiji vile kwa sababu wananchi katika maeneo hayo bado wana matatizo makubwa ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala zima la huduma ya maji katika Hospitali ya Wilaya pale Kilwa Kivinje, bado kuna matatizo makubwa. Tuiombe Serikali ihakikishe hospitali ile inapatiwa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna suala zima la Wakala wa Maji Vijijini na Mijini, limezungumzwa na wachangiaji wengi na Serikali pia ilishaelekeza kwamba ina mpango huo, tunaomba hili jambo lianze kwa haraka. Angalizo ni kwamba, wakati jambo hili litakapoanza Madiwani katika halmashauri zetu wapewe elimu ya kutosha namna gani wakala hii itakavyokwenda kufanya kazi ili kuepusha mgongano ambao unaweza ukatokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala zima la umwagiliaji. Katika Jimbo langu la Kilwa Kaskazini ambalo lina utajiri wa mabonde hakuna mradi hata mmoja wa umwagiliaji ambao unatekelezwa. Kwa mfano, tuna Mabonde ya Ngamwana, Marendege, Nambacho, Nalulo, Liomanga, hayo ni mabonde ambayo yanatiririsha maji wakati wote lakini hakuna *project* ya umwagiliaji hata moja. Niilombe Serikali iangalie eneo hilo na sisi tupate miradi ya umwagiliaji ili basi wananchi wetu waweze kuijendeleza kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo mnafahamu eneo la Kilwa na Lindi kwa ujumla wake sisi tumekuwa wapokeaji wa wafugaji. Kuna maelfu ya mifugo yapo katika maeneo yetu lakini mpaka sasa Serikali hajafanikiwa kujenga mabwawa kwa ajili ya kunywesha mifugo hiyo. Kwa hiyo, kunakuwa na mgongano mkubwa kati ya wenyeji pamoja na wafugaji kugombea maji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuiombe Serikali ihakikishe maeneo yale yanajengwa mabwawa ya maji ili kuwezesha kunywesha ile mifugo ili tuondokane na migongano isiyokuwa na sababu kati yetu na wafugaji. Tunawapenda wafugaji lakini miundombinu haijaandalialiwa. Kinachotokea sasa hivi ni migongano ya kugombea maji. Naomba sana Serikali illiangalie hilo kwa sababu ni jambo muhimu sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mradi wa Mingumbi - Miteja ambao uligharimu karibu shilingi 4,750,000,000 umekamilika lakini mara tu baada ya kukamilika haufanyi kazi na haufanyi kazi kwa sababu vifaa vilivyotumika pale ni

kama vifaa *fake*, mabomba yanapasuka hovyo hovyo, ule mradi ni kama mfu ndani ya muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ni kwamba kuna hizi Mamlaka za Watumiaji wa Maji bado hazijapewa elimu ya kutosha kuona ni namna gani zinaweza kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma hii ya maji. Naomba suala hilo liangaliwe...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa, ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vulu kwa dakika tano, Mheshimiwa Sikudhani Chikambo kwa dakika tano watafuatiwa na Mheshimiwa Mama Salma Kikwete.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa dakika ulizonipa ni chache, lakini kwa kutumia taaluma yangu nitahakikisha nazitumia vizuri na naomba ridhaa yako nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingu wa rehma kwa kutuwezesha kuwa hapa leo na kupata nafasi hii ya kuchangia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kikubwa zaidi, naomba ridhaa yako niweze kuishukuru Serikali yangu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli akisimamiwa na Makamu wa Rais na Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo alichokifanya Waziri Mkuu leo humu ndani ni cha kihistoria cha kuhakikisha mafuta yanapatikana, sisi wengine ni wananchi tunaotokana na wazazi wenyewe kipato cha chini ambao tunatumia mafuta katika biashara ndogo ndogo na kutuwezesha kuishi katika nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu kila la kheri, Mawaziri wote kila la kheri pamoja na watendaji na Watanzania wote sasa

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

ambao tunakaribia kufunga mwezi wa Ramadhani na wale ambao hawatahitaji kuyatumia mwezi wa Ramadhani kwa kweli hii ndiyo nafasi yao.

### **KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zaynabu Vulu, naomba ukae, Kanuni Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 64(1).

Mheshimiwa Naibu Spika, mchangiaji anajadili jambo ambalo umekataa tusilijadili, sasa ye ye anaendelea kulijadili hapa. Naomba ajielekeze kwenye hoja illyoko Mezani kwa sababu tumeomba tujadili kwa pamoja sasa ye ye anajadili kwa mlango wa nyuma. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vulu, endelea.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba unilindie dakika zangu. La pili, nadhani Mchungaji hajui lugha ya Kiswahili vizuri amezoea lugha ya Kichungaji, nimesema naomba nipongeze, sijasema naomba nichangie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumzia bajeti ya Wizara ya Maji. Nchi yetu awamu hii tunakwenda kwenye awamu ya viwanda, lakini pamoja na hayo tunahitaji maji ya kutosha kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wetu. Naomba Serikali iangalie uwezekano wa kutuletea maji maeneo mengi, Wabunge wengi humu ndani wamesimama wakielezea tatizo la maji kwenye maeneo yetu. Kwanza naomba wataalam wafike hadi kwenye miradi ya vijiji vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, mradi wa Wilaya ya Kisarawe ambao umepata baraka za Mheshimiwa Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba maji kutoka Ruvu Juu yafanyiwe utaratibu yaweze kwenda hadi Kisarawe. Mradi huo tayari taratibu zote zimeshakamilika, ni nini na ni lini Serikali itaanza utekelezaji wa mradi huo na kitu gani ambacho kinakwamisha mradi huo mpaka leo usiweze kufanya kazi? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maji kwa Mkao wa Pwani kwa kweli tukisema kwamba kuna maeneo maji hayapatikani inasikitisha sana kwa sababu mkoaa wetu umezungukwa na mito mingi sana. Kwa mfano, Mto wa Rufiji maji yake yanamwagika hovyo, kwa nini usitengenezwe utaratibu wa kuutumia? Toka nimeingia ndani ya jengo hili nimekuwa nikiomba maji ya Rufiji yaweze kutumika maeneo mengine, hajjawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuna Mto Wami nao una maji mengi sana. Tatizo linakuja wakati wa mvua yale maji yanakuwa machafu kwa maana yanakuwa na tope nydingi. Je, ni lini Serikali itaona umuhimu au itatengeneza utaratibu wa kuhakikisha maji yale yanasaishwa na kuweza kutumika kwa maeneo yaliyo jirani? Hakuna sababu sasa hivi maji ya kwenda Chalinze yatoke Ruvu Juu wakati Mto Wami uko jirani na Chalinze. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kero ya maji ni kubwa sana kwenye shule zetu za msingi na maeneo ya huduma muhimu kama zahanati, vituo vya afya na hospitali. Kwa nini haya mashirika na idara za maji zilizopo zisipewe jukumu la kusimamia uvunaji wa maji ya mvua wakawezesha kuwapatia maji watoto wa shule, vituo vyetu vya afya na kwenye huduma muhimu? Maji ya mvua yakivunwa yanaweza kutumika kwa ajili ya wananchi na kuondoa kero ya maji na tumeahidi kumtua mwanamke ndoo ya maji kichwani japokuwa wanaume wakibeba maji wanauza, lakini shida ni ile ile. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye suala la maji taka, mfumo wa maji taka Dar es Salaam siyo mzuri. Tunajua maji taka, mniwie radhi kwa kutumia hili neno, ni maji ya

kinyesi au ya uchafu mwингine, lakini sasa hivi Dar es Salaam imefurika maji taka kweli. Machupa machafu yamo humo, mifuko ya rambo imo humo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa muda wako umekwisha, ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Sikudhani Chikambo kwa dakika tano atafuatiwa na Mheshimiwa Salma Kikwete kwa dakika tano, Mheshimiwa William Dua Nkurua kwa dakika tano.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijaalia leo kupata fursa hii ya kuchangia katika Wizara hii ya Maji, sote tunafahamu umuhimu wa Wizara hii kwamba maji ni uhai.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kumshukuru Mwenyezi Mungu, naomba nimshukuru sana Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanazozifanya. Ukiangalia kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 126 na 127, wameeleza miradi mbalimbali ambayo itatekelezwa katika Mkoa wetu wa Ruvuma. Naomba niipongeze sana Serikali wametutengea shilingi 15,393,653,000, ni mkoa wa kwanza katika kutengewa pesa. Naomba sana niishukuru Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba niseme kutenga pesa ni hatua moja lakini kupeleka pesa katika miradi ni hatua nyingine. Niombe wakati utakapofika tupeleke hizi pesa ili kuhakikisha miradi ambayo tumekusudia kutekelezwa inatekelezwa. Miradi ambayo imepangwa kutekelezwa katika Mkoa wangu wa Ruvuma ni katika Wilaya za *Madaba DC*, Mbinga, Mbinga Mji, Namtumbo, Nyasa, Songea, Songea Manispaa na Tunduru. Kwa hiyo, naishukuru Serikali na niombe sana kwamba wakati utakapofika Mheshimiwa Waziri kama vile ambavyo umetuweka namba moja katika kututengea pesa nyingi basi ni vizuri katika

utekelezaji vilevile tuwe namba moja katika kupeleka pesa.  
*(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spka, naomba pia nizungumzie Miradi ya Benki ya Dunia ambayo ilitakiwa itekelezwe katika Vijiji vya Mchoteka, Nakapanya, Majimaji na Muwesi. Naomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri anakumbuka hicho kitu kwamba mionganoni mwa vijiji ambavyo viliwekwa kwenye mpango wa utekelezaji wa Miradi ya Maji ya Benki ya Dunia ni pamoja na hivyo vijiji ambavyo nimevisema. Niliwahi kusimama katika Bunge hili kuvizungumzia vijiji hivyo na Waziri alitoa majibu kwamba vijiji vile vimekosa vyanzo. Niombe, tafadhali Mheshimiwa Waziri naomba niseme kwamba vyanzo kule bado viro. Ni vizuri sasa twende tukatekeleze katika kuona tunatafuta vile vyanzo vya maji kata hizi ambazo tunazifirkiria kupata maji zipatiwe maji. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie tena suala la fidia Bonde la Mto Luhila - Songea. Mheshimiwa Waziri ninapozungumzia Bonde la Mto Luhila - Songea naamini utakuwa unakumbuka kwamba wananchi walipisha pale mradi mkubwa wa maji na hivi ninavyozungumza kiasi cha pesa karibu shilingi bilioni 1.9 wananchi wale wanadai. Imekuwa kero kwa sababu wananchi wale walikuwa wasikivu, walipisha huu mradi mkubwa, lakini mpaka hivi navyozungumza wananchi karibu 803 hawajapatiwa pesa zao. Nikuombe Mheshimiwa Waziri wakati utakapofika uhakikishe tunalipa fidia kwa wananchi wale ambao walijitolea kupisha mradi huu mkubwa wa maji. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie upatikanaji wa maji katika Miji Midogo ukiweno Miji ya Namtumbo na Lusewa. Naomba nizungumzie sana Lusewa hata ukija katika Kata ile ya Lusewa kuna kituo cha afya ambacho hakina maji. Nikuombe Mheshimiwa Waziri, naamini bado mwanya upo, utufikirie katika kituo chetu cha Lusewa kutupatia maji. Tunapozungumza maji kama walivyosema Wabunge wenzangu sisi akina mama, watoto ndiyo hasa tunaathirika katika suala hili la maji. Tunapokuwa na kituo cha afya ambacho hakina huduma ya maji ni

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

mtihani mkubwa sana. Nikuombe tufikirie sisi wananchi wa Mkoa wa Ruvuma na hususani wale wananchi waliopo katika Kata ile ya Lusewa wakati utakapofika ili tupate mradi wa maji katika Kijiji kile cha Lusewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungmzie...

*(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimia Naibu Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Salma Kikwete atafuatiwa na Mheshimiwa William Dua Nkurua, wote dakika tano tano, atafuata Mheshimiwa Josephat Kandege.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, nikushukuru wewe kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia Wizara hii muhimu kwa ustawi na maendeleo ya wananchi wa Taifa letu la Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, naomba nitoe pongezi zangu za dhati kwa Wizara hii kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaifanya ya kutatua tatizo la maji hapa nchini. Natambua na sote tunatambua kwamba wakati tumepata uhuru na baadae, nchi yetu ilikuwa na watu wachache, sasa hivi watu ni wengi sana na kila mwananchi ana mahitaji makubwa ya maji. Kwa jinsi hiyo, bado maji ni tatizo kwa wananchi wengi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo Serikali imefanya juhudini kubwa na ya dhati kabisa kuweza kutatua matatizo ya maji katika maeneo kadhaa ya Taifa letu. Hakuna mtu ambaye anaweza kutatua tatizo hili kwa wakati mmoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, alianza Baba wa Taifa akafanya kazi yake, akaja Mzee Mwinyi akafanya kazi yake, akaja Mzee Mkapa akafanya kazi hiyo, akaja Mheshimiwa Mstaafu, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, mume wangu akafanya kazi yake na sasa hivi yuko Dkt. John Pombe Magufuli anafanya kazi yake na ataiacha hii na bado kazi itaendelea. Tunaamini Serikali ina dhamaira ya dhati kabisa kuondoa tatizo la maji hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo sasa naomba nielekee kwenye eneo langu ambalo nallifanya kazi kule Lindi. Naipongeza na kuishukuru sana Serikali kwa mradi mkubwa kwa mabilioni ya pesa ambaao walitupatia na hatimaye leo hii wananchi wa Wilaya ya Lindi Mjini wanapata maji. Tatizo kubwa lilitopo hapa pamoja na kupata yale maji, kuna tatizo dogo siyo kubwa sana, naamini wataalam wakikaa, aidha, Wizara ya Maji pamoja na Wizara ya Nishati wanaweza kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa la kukatikakatika kwa umeme ndiyo linasababisha *pump* zisiweze kupeleka maji kwenye matenki hatimaye maji yale yakapelekwa kwenye maeneo husika. Naomba Wizara hizi mbili zikae kwa pamoja ili waweze kutatua tatizo hili ambalo linawakabili wananchi wa Wilaya ya Lindi Mjini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishukuru Serikali kwa dhati kabisa kwa kutupa fedha kiasi cha shilingi bilioni 2.5 kwa ajili ya miradi mikubwa miwili; ujenzi wa miundombinu ya maji safi katika eneo la Ng'apa na Mitwero. Fedha hizi au miradi hii itasaidia kuondoa changamoto ya maji kwenye maeneo hayo niliyoyataja. Unaweza ukaangalia ukurasa wa 188 jinsi ambavyo Serikali imeweza kutuona. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka niende kwenye eneo la umwagiliaji. Tunajua na tunatambua kwamba kupanga ni kuchagua, na eneo hili ni muhimu sana kwa usalama wa chakula hapa nchini. Mwananchi yoyote pamoja na kuhitaji maji anahitaji kula. Tukiangalia eneo la umwagiliaji ni eneo ambalo lina uhakika wa kutupatia chakula hapa nchini. Kwa mfano takwimu zinaonesha kwamba hekta 475,520 sawa na asilimia 24. Asilimia 24 hii inachangia chakula kinachopatikana hapa nchini. Sasa kama tukiongeza mara mbili yake ina maana kwamba tutakuwa na asilimia 48 na asilimia hizi 48 zitatuongezea kiasi kikubwa cha upatikanaji wa chakula hapa nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Upotevu wa Maji. Tunaamini na tunajua kwamba maji mengi yanapotea. Sasa katika hili ni lazima Serikali ichukue hatua makini zaidi kuweza kuthibiti hayo maji. Lakini hasa kule majumbani, maji mengi yanapotea; tuwe makini kuwaambia vijana wetu maji haya yasipotee. Wakati mwingine kikombe moja kinatumia maji zaidi ya lita tatu au lita nne kusafishia. Hii haikubaliki na hili haliwezekani ni lazima tuwe makini katika udhibiti wa maji yetu haya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naona muda umenitupa mkono, lakini naomba kuunga hoja hii kwa asilimia 100, ahsante sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Shukurani sana, Mheshimiwa William Dua Nkurua dakika tano, Mheshimiwa Josephat Kandege dakika tano, Mheshimiwa Kakunda ajiandae dakika tano.

**MHE. WILLIAM D. NKURUA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, awali ya yote niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na watendaji wote wa Wizara, hakika wanatenda kazi, hatuna shaka nao katika utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa ya Wizara hii tunafahamu kwamba ni pesa, lakini mimi naiomba

sana Serikali, hapa naiambia moja kwa moja Serikali, hizi pesa ambazo tumezitenga kwa ajili ya Wizara hii naiomba Serikali ihakikishe kwamba inazipeleka kadri zinavyopatikana na ikiwezekana zipatikane kwa asilimia mia moja, kwa sababu kama wanavyosema watu maji ni uhai. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa sababu katika bajeti hii, kabla ya hapo nilikaa na Mheshimiwa Waziri nikamueleza tatizo kubwa la bwawa letu kule katika Kijiji cha Namasogo na tatizo la mfumo wa maji taka pale Mangaka mjini. Nashukuru katika bajeti hii nimetengewa shilingi milioni 400 katika Bwawa la Namasogo, lakini pia shilingi milioni 500 kwa ajili ya mfumo wa maji taka pale mjini Mangaka kwa kweli nawashukuru sana kwa hiki, kidogo ambacho tumeanza nacho. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Katika bajeti hii pia tumetengewa pesa zaidi ya shilingi milioni 1300 kwa ajili ya maji vijijini. Basi hizi pesa nalihakikishia Bunge lako tukufu tutakwenda kuzisimamia, mimi pamoja na Madiwani wenzangu kule tukiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri kuhakikisha kwamba lengo la Serikali linatimia. Kwa sababu kama Diwani nina jukumu la kusimamia pesa hizi ili zifanye kazi tarajiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mionganoni mwa Wilaya ambazo zinashida kubwa sana ya maji katika nchi hii ni pamoja na Nanyumbu. Kwa hiyo, ninaomba sana Serikali katika bajeti zingine iangalie wilaya gani zina tatizo kubwa katika mgawanyo wa hizi pesa ili tuweze kufanana katika kutatua tatizo kubwa la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye mradi mkubwa wa maji kutoka Mto Ruvuma mpaka Mjini Mangaka. Serikali ilikuwa imeshandaa utaratibu wa kuyatoa maji kutoka Mto Ruvuma na kufikisha katika makao makuu ya Wilaya pale mjini Mangaka. Hatua tuliyokuwa nayo ni ya usanifu wa kina na kuandaa makabrasha kwa ajili ya kutangaza zabuni. Sasa niiombe Serikali, kwanza *speed* ya upembuzi yakinifu iwe kubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, muda hautusubiri lakini wananchi wanatusubiri. Kwa hiyo nashauri sana hawa watu tuliowapa hili jukumu wafanye kazi kwa *speed* ili wananchi waone matokeo ya sisi kuwa viongozi wao katika awamu hii ya tano.

Kwa hiyo nashauri sana Wizara isituangushe katika utendaji wa kazi ili maji kutoka Mto Ruvuma yafike pale mjini Mangaka. Lakini nilishaomba na tena naomba yale maji upembuzi yakinifu uelekee hadi Lumesule kupitia Michiga na Likokona. Vilevile tufike pia Nagomba, Mikangaula, na Mpakani mwa Wilaya yetu na Masasi pale Namatumbusi. Tukifikisha maeneo hayo nia uhakika kwamba tumesaидia eneo kubwa la Wilaya ya Nanyumbu kupambana na shida kubwa ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya kwa sababu muda wangu ni mdogo sana, basi naunga mkono hoja, nashukuru, ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na kuniwezesha kuchangia Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni uhai wa binadamu, wanyama na kilimo na kila kilichoumbwa. Bajeti ya Wizara hii ni ndogo mno kwa sababu maji katika nchi hii ni tatizo kubwa na ndoa zinakatika kwa ajili ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wakati wa kampeni yake na baada ya kushika madaraka alisema atahakikisha kuwa anamtua mama ndoo kichwani, lakini bado tatizo liko pale pale, bado ndoo iko kichwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatenga fedha za miradi, lakini inachelewesha kuzifikisha fedha katika

Halmashauri na utakuta utekelezaji wa mradi unakwama na kuchukua muda mrefu. Vilevile wakandarasi ni lazima wasimamiwe kikamilifu kwa sababu wanununa mabomba yaliyokuwa hayana viwango. Utakuta muda mdogo yanapasuka na kusababisha maji kupotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile wako wakandarasi ambao hawana utalaam wa kutosha, wanachimba visima virefu lakini maji hayapatikani na baadae kufeli na kusababisha kuitia hasara Serikali na mradi kusimama, hili ni tatizo. Tunaomba watendaji waache kukaa ofisini, wafike kwenye miradi kuisimamia ili kufanikisha malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile fedha zitengwe kwa ajili ya kujengwa mabwawa ya kuhifadhi maji ya mvua ili kupunguzia wananchi tatizo la mifugo yao hasa wakati wa kiangazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wasomaji wa mita wana matatizo, hawasomi mita vizuri na wanawabambikia madeni makubwa wananchi ambao wanashindwa kulipa baadae wanawakatia maji na kupata usumbufu mkubwa.

Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha shule zote nchini zimepata maji ili kuwaondoshea usumbufu watoto wetu hawa wasichana pale wanapokuwa kwenye siku zao waendelee na masomo yao waondokane na kubakia nyumbani?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango wangu huu naomba kuwasilisha na kabla sijawasilisha, nauliza; ikiwa hatuna maji ya kutosha hivyo viwanda vitafanyakazi vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasiliaha.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Maji. Pia ninaomba mchango wangu huu wote uingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni uhai, suala la maji ni muhimu sana katika jamii. Miradi ya maji mingi inayotokana na *World Bank* ni miradi ambayo imetumia pesa nyingi sana na mingi haijakamilika. Ni kwa nini wahusika katika miradi hii ya maji ambayo hajatekelezeka hawachukuliwi hatua? Iko miradi zaidi ya minne ya fedha za *World Bank* ambayo haipo katika hali nzuri mkoani Ruvuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuainisha miradi ya maji iliyoko katika Mkoa wa Ruvuma ambayo haijakamilika na kimsingi fedha hizo hazijulikani ziliko kwa kuwa inaonesha fedha zimetumika na miradi haijakamilika kama ifuatavyo:-

- (1) Mradi wa Maji Mkako katika Wilaya ya Mbinga ambaao umetumia fedha zaidi ya shilingi 600,000,000;
- (2) Mradi wa Maji wa Litola Wilayani Namtumbo umetumia fedha zaidi ya shilingi million 700,000,000; na
- (3) Mradi wa Maji wa Matemanga Wilayani Tunduru (Tunduru Kaskazini) ambaao umetumia fedha zaidi ya 500,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubadhirifu huu unaofanywa katika Wizara hii kwenye miradi hii ya maji hauvumiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu iundwe Tume ya kufuatilia miradi hii ili tupate majibu sahihi juu ya miradi hii na ujisadi mkubwa uliopo kwenye miradi hiyo. Mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya *LAAC* ninajua vizuri juu ya miradi mbalimbali ya maji iliyoko katika nchi yetu katika mikoa ya Tanga, Mbeya, Iringa na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ZITTO R. Z. KABWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya CCM, zililongwa mbali, zilitendwa mbali. Katibu Mkuu Hazina na sekta binafsi kushiriki kwenye sekta ya maji kinyume na sera ya Serikali na kauli ya Wizara ya Maji. Kiburi anapewa nani?

"Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwepo kwa mahitaji makubwa ya kuboresha huduma za maji na umwagilaji, mchango wa sekta binafsi kwenye uwekezaji katika kutoka huduma hizo bado si wa kuridhisha. Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi, ikiwa ni pamoja na kutunga Sera ya Taifa ya Ubia baina ya Sekta ya Umma, Sekta Binafsi ya mwaka 2009 na Sheria ya Ubia ya mwaka 2010 na Kanuni zake ili kuweka mazingira mazuri ya kuwavutia wawekezaji. Vilevile Wizara imeendelea kuwapatia wataalam wake mafunzo yanayohusu uwekezaji ikiwa ni pamoja na ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi kwa lengo la kuwajengea uwezo wa namna ya kutekeleza miradi ya ubia." Waziri wa Maji Bungeni, Mei 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Waziri anaeleza hii kama changamoto, benki binafsi inanyang'anywa kazi ya mradi muhimu wa kupunguza gharama za uendeshaji wa miradi ya maji vijijini. Sekta binafsi itapata wapi matumaini ya kushiriki kwenye sekta ya maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Dunia inapanga majaribio ya kutumia umeme wa jua kuendesha miradi ya maji vijijini kwa kutoa mkopo nafuu kwa Jumuiya ya Watumilaji wa Maji (*COWSOs*) kwa kushirikiana na taasisi za fedha nchini. Baada ya Benki ya Dunia kukamilisha mchakato wa kupata benki ya kufanya kazi hiyo ya kukopesha *COWSOs*, Serikali imeilazimisha benki hiyo kutoa kazi kwa benki nyingine ambayo kwa sasa inaelekea kuanguka kutohana na kuwa na mikopo chechefu mingi na changamoto za uendeshaji. Serikali inapotaka sekta binafsi kushiriki kwenye sekta ya maji au sekta yoyote nyingine na wakati huo huo kuweka vikwazo, huu ushuriki wa namna gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Katibu Mkuu Hazina anataka benki iliyoshinda zabuni ya kutekeleza mradi huu muhimu iondolewe badala yake *TIB* wapewe kazi ambayo walishindwa na kuamua kujitoa na kwamba pia hawana uwezo wa kuifanya? Hii ni *pilot* tu kwa nini Hazina wasiache ifanyike ili ikiwa na mafanikio ndipo Benki ya Serikali

iingie kwa mradi mkubwa? Nina zabuni ya mradi huu wa majaribio, Bunge likihitaji litawasilisha. Bunge liitake Serikali iache kuingilia mchakato huu ili tuweze kuona majaribio haya yana faida gani kwa nchi kabla ya ku-scale upya hii project.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote. Nawatachia kila la heri katika kazi zenu muhimu na ngumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuomba kwa niaba ya wananchi wa Urambo mradi wa *Lake Victoria* ufike Urambo. Naomba *DDCA* ianzé kazi, Urambo tuna shida kubwa ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 272 wa kitabu cha Wizara, Kituo cha *VETA* cha Ulyankulu ambacho kipo Wilaya ya Kaliua imeandikwa kipo Urambo, naomba pasahihishwe. Kila la heri.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi kwa umahiri wa Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli pamoja na Waziri, Mheshimiwa *Engineer Kamwelwe* kwa umahiri wake katika kusimamia kazi za Wizara na miradi yake ili kumtua mama ndoo.

Pia pongezi kwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi wa Maji Vijijini na Mijijini na watendaji wote katika Wizara. Pia pongezi kwa Wizara kubadili utaratibu wa malipo kwa hati kutumwa Wizarani badala ya kupeleka pesa katika Halmashauri ambazo ziliweza kubadilishwa matumizi au miradi kuchelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mabonde ya maji; Mamlaka ya Mabonde bado yana changamoto za watumishi katika maeneo yanayotakiwa kusimamiwa ipasavyo. Hivyo nashauri Wizara ya Maji iangalie itahusisha vipi Halmashauri au Manispaa kusimamia kwa kutoa fedha za usimamizi ili kulinda vyanzo vya maji ambavyo vinavamiwa sana na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu banio katika Mto Katuma na Mto Mpanda Mkoa wa Katavi; Wilaya ya Mpanda, Kata za Itenka, Kakese na Mwanamkulu zinalima sana zao la mpunga hivyo kuna haja ya kupata skimu ya umwagilaji ili kilimo kifanyike mara mbili kwa mwaka. Pia kuwekea mabanio ya kusambaza maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu chanzo Ziwa Tanganyika, Mkoa wa Katavi bado unategemea vyanzo ambavyo si vya uhakika, mfano, Manispaa ya Mpanda wanapata maji kutoka Ikorongo chanzo ambacho hakikidhi mahitaji. Hivyo tunaomba Wizara ifanye upembuzi yakinifu kwa ajili ya kutoa maji Ziwa Tanganyika na kutumika Wilaya mbili yaani Tanganyika na Mpanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la madeni ya miradi ya maji katika Halmashauri, kampuni ya kizalendo ya Kahama ilikopesha wakandarasi katika Halmashauri takribani kumi ikiwemo ya Nkasi ambayo kuna utata wa mkatuba na vigezo ambapo kampuni mbili zinadaiwa takribani shilingi bilioni mbili. Naomba Serikali iingilie kati mgogoro huo ili kampuni hiyo iweze kulipwa madeni. Ahsante.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kufanikisha malipo ya wapiga kura wangu walio katika Chanzo cha Maji Champala, kwa kweli nakushukuru kwa hili, Mwenyezi Mungu akujalie afya, busara na hekima.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mheshimiwa Waziri naomba sana tatizo la maji katika Mji Mdogo wa Kilwa Kivinje ambapo ipo Hospitali ya Wilaya ambayo ina upungufu wa maji kwa muda mrefu. Nakuomba sana Mji Mdogo wa Kivinje uangaliwe kwa jicho la huruma sana, tena sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, napenda kukukumbusha Mradi wa Maji wa Mavuji ambao upembuzi yakinifu umekamilika lakini tatizo ni upatikanaji wa fedha kwa ajili ya mradi huo. Mradi wa Mavuji utakapopata

fedha na kukamilika hilo ndilo suluhisho la upatikanaji wa maji katika Mji Mdogo wa Kivinje/Masoko. Nakuomba sana usimamie mradi huu wa Mavuji ambao upembuzi yakinifu ulifanya na Wabelgiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba fedha zilizopangwa mwaka 2017/2018 zitolewe katika miradi ya maji na pia fedha zilizolengwa katika bajeti ya mwaka 2018/2019 zipatikane ili matatizo ya maji yapungue. Natanguliza shukrani, ahsante. Tunakuelewa na tunakukubali.

**MHE. JUSTIN J. MONKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa juhudini kubwa ya kuwaletaa wananchi miradi ya maji katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri bado tunalo jukumu kubwa mbele yetu katika kufikia malengo ya mwaka 2020 ya kutoa huduma ya maji vijiji kwa asilimia 85. Katika Jimbo langu la Singida Kaskazini tunalo tatizo kubwa la maji katika vijiji vyetu na kuwafanya wananchi kuhangaika kutafuta huduma ya maji. Hata katika baadhi ya maeneo yaliyo na vyanzo vya maji, maji hayo siyo safi na salama kwa matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru sana Serikali kwa kuliweka Jimbo la Singida Kaskazini katika mradi wa matumizi ya teknolojia ya nishati jadidifu ambao tayari umeshaanza katika vijiji vya Ghalunyangu na Mughunga. Pia kwa kutengenea fedha shilingi 1,644,481,000 kwa ajili ya miradi ya maji vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipo vijiji na vitongoji katika Kata ya Mughunga ambavyo ni kijiji cha Nduamughanga na vitongoji vya Mukulu ambavyo vipo umbali wa kilometra 25 kutoka makao makuu ya kijiji. Maeneo haya hayana huduma ya maji safi na salama. Pia vipo vijiji vya Lamba, Sughana, Misuna, Gairo na vingine vingi katika Jimbo la Singida Kaskazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali kuongeza fedha za miradi ya maji ili kupunguza tatizo hili na kufikia malengo tuliyonadi kwenye llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa kilimo cha umwagiliaji, ipo miradi mingi ambayo inafaa kwa umwagiliaji ambayo tayari Wizara imeainisha na niombe kupatikana fedha za kutekeleza miradi hii sasa ili iweze kuongeza tija. Miradi ipo maeneo ya Ikhanda, Itanika, Ngimu, Songambele, Songa, Ndang'onyo na Sagara. Lipo pia Bwawa la Msange ambalo utafiti ambao umeshafanyika na miradi bado hajaanza. Niuombe Mheshimiwa Waziri aweze kutembelea jimbo langu na kujionea miradi ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 144 kwenye ukarabati wa mabwawa, inaonesha kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Singida inatengewa fedha, Iakini bwawa hili na vijiji vilivyoainishwa vipo katika Wilaya ya Ikungi, Jimbo la Singida Mashariki. Niuombe Mheshimiwa Waziri wafanye marekebisho ili yaingizwe mabwawa na vijiji vya Jimbo la Singida Kaskazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii. Awali ya yote nashukuru sana kwa ziara za Mheshimiwa Rais, Waziri wa Maji, Naibu Waziri wa Maji na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji katika Jimbo letu la Mikumi. Natumaini mmezisikia changamoto za watu wa Mikumi kuhusu maji na ninashukuru sana baadhi ya changamoto hizo zimepata ufumbuzi. Baada ya kutoa shukrani hizo, naomba nichangie changamoto kadhaa za muhimu Jimboni Mikumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mradi wa Maji wa Madibira, huu ni mradi wa muda mrefu sana tangu mwaka 1974 hadi 1975 na miundombinu yake imechakaa sana. Nashukuru Serikali imetenga shilingi 300,000,000 ili kukarabati

na kutanua *intake* pamoja na upanuzi wa mitandao ya kuunganisha wateja. Ila nasikitika kuwa karibu mwaka mmoja sasa mzabuni amepatikana ila bado hajapewa kibali cha kuanza kazi kutoka Wizarani. Tunaomba sana apatiwe kibali ili aanze kazi hiyo ya kukarabati miundombinu mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Sigaleti (Kata ya Ruaha); chanzo hiki cha maji kilifanyiwa usanifu na wataalam wa maji wa Wilaya ya Kilosa baada ya kuagizwa na Mheshimiwa Waziri ambaye alifanya ziara Jimboni Mikumi mwaka 2017. Wataalam walijiridhisha kuwa chanzo hiki kina maji mengi na salama na uhakika na pia yanaweza kusaidia sana wananchi wa kata kubwa ya Ruaha yenyewe wakazi 35,000 pamoja na kata za jirani za Kidodi, Vidunda na Ruhembe. Pia wataalam walifanya tathmini kuwa kiasi cha shillingi billioni mbili kinatakiwa ili kufanya mradi huu uweze kuhudumia wananchi hawa wanaoteseka na tayari tathmini hiyo nilishaikabidhi kwa Waziri husika. Tunaomba sana mradi huu uweze kuingizwa katika bajeti ya mwaka huu ili kumtua mama wa Ruaha ndoo kichwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bwawa la Dachi (Kata ya Malolo); bwawa hili ni muhimu sana kwa umwagiliaji katika Kata ya Malolo, mradi huu ulifadhiliwa na JICA ya Japani kwa fedha shillingi 600,000,000 ili kujenga makingio ya mchanga unaotishia kuupoteza kabisa Mto Mwega unaotumiwa sana na kutegemewa sana na wananchi wa Kata ya Malolo kwa kilimo. Kumetokea ubadhirifu mkubwa sana wa fedha hizo na makingio yaliyojengwa yamejengwa chini ya kiwango na kusababisha mchanga kuendelea kumwagika kutoka milimani na kwenda kujaza Mto Mwega. Nilishawahi kuomba Serikali iingilie kati na Mheshimiwa Waziri aliahidi kulifuatilia jambo hili, lakini naona hakuna majibu mpaka sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujumuisha atuambie amefikia wapi na tunaomba sana Wizara iweze kuingilia kati na kusikia kilio hiki cha muda mrefu sana cha wananchi wa

Kata ya Malolo kwani tegemeo lao la kilimo linategemea sana Mto huu wa Mwega.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana tusaidiwe visima virefu katika Jimbo la Mikumi kwani tumekuwa tukisahauliwa sana katika uchimbaji wa visima virefu hasa katika kata za Ruhembe, Vidunda, Mhenda, Tindiga, Zombo, Malolo, Uleling'ombe, Kisanga, Mabwerebwere, Kilangali, Mikumi, Ruaha, Kidodi, Masanze na Ulaya. Tunaomba sana kata hizi za Jimbo la Mikumi zifikiriwe kwa jicho la huruma maana wananchi wetu inafika mahali wana-share kunywa maji kwenye mito na wanyama kitu ambacho kinahatarisha sana afya zao na magonjwa ya maambukizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikumi tumebarikiwa kuwa na vyanzo vingi sana vya maji. Mwisho kabisa niiombe sana Wizara itume wataalam wake kwenye Jimbo la Mikumi kwa kuwa pamoja na taabu na changamoto kubwa sana ya maji tunayokabiliana nayo lakini Jimbo la Mikumi limebarikiwa vyanzo vingi sana vya maji ambavyo vingeweza kumaliza kabisa kero ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Jimbo langu la Mikumi tunaomba sana wataalam waje kuviangalia vyanzo vifuatavyo; Mto Iyovi, Mto Simbalambende na Kisanga. Natumaini tukifanikiwa kuvitumia vyanzo hivi tutakuwa kwa kiasi kikubwa tumefanikiwa kumtua mama ndoo kichwani. Ahsante.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mungu kwa kuniwezesha kuendelea kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa. Pia nikushukuru wewe binafsi kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wangu, Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake wote kwa kazi nzuri zinazofanyika kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji kwa Watanzania, yaani kumtua mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni muhimu sana na ni ukweli usiopingika Serikali inafanya kazi kubwa sana ingawa ziko changamoto nyingi likwemo upungufu wa pesa pamoja na wataalam wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii pia kuishukuru Wizara ya Maji kwa pesa ambayo tumetengewa mwaka 2017/2018 shilingi bilioni 2.1 ambazo zimetusaidia kuboresha miradi mbalimbali kama mradi wa Mabila, Kaisho, Isiringiro, Rutunguru, Kagenyi na mengineyo midogo midogo. Lakini pia tumeweza kuanza mradi mpya wa vijiji 57 ambavyo utakuwa mkombozi kwa Wanakyerwa ambaao utaweza kuhudumia zaidi watu 200,000 utakapokuwa umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huo mkubwa tumefikia hatua ya kutangaza *tender*, namuomba sana Mheshimiwa Waziri na watendaji wake wa Wizara kutufuta machozi ya kilio cha muda mrefu cha kukosa maji kwa wana Kyerwa ambaao hali yao ya upatikanaji ni mbaya sana. Kwa kweli naomba sana Serikali imetuweka kwenye bajeti tumetengewa shilingi bilioni moja tu ambapo mradi unahitaji zaidi ya shilingi bilioni 140. Natambua sana hatua hii tuliyofikia ya usanifu na *design* Wizara imefanya kazi kubwa. Waziri, Mkurugenzi wa Maji Vijiiji kuhakikisha tunafikia hapa, bado imani yangu ni kubwa sana kwao mpaka mradi huo unakamlilika na Wanakyerwa wanapata maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji inafanya kazi nzuri na kubwa sana lakini miradi inayosimamiwa na Halmashauri ni kampuni za mifukoni na za kupeana kiurafiki, na hatimaye miradi ni ya hovyo. Mfano miradi ya Itera, Mradi wa Rutunguru, Kaisho na Isingiro mpaka sasa hakuna kinachoendelea. Kuna mradi kata ya Rukuraijo vifaa vimeibiwa kama *solar* na vingine, lakini hakuna hatua zilizochukuliwa na maradi wa Kigorogoro ambaao una zaidi ya miaka kumi lakini hakuna kinachoendelea. Niombe Wizara kufuatilia miradi kujua kinachoendelea, lakini pia kukagua kazi iliyofanyika, kwamba ni sawa na pesa iliyotolewa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Wabunge wengi walivyoshauri kuongezwa shilingi 50 kwenye mafuta ili mradi kama wetu ambaao ni mkubwa uongezewe pesa na hii itasaidia Wizara kuendelea angalu kuongeza bajeti yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na usimamizi usioridhisha wa baadhi ya Halmashauri kwenye sekta ya maji kama ilivyokuwa kwenye upande wa barabara zilizokuwa zinasimamiwa na Halmashauri na ikaundwa *TARURA*, tuombe sana Serikali kuunda chombo ambacho kitasimamia maji vijiji yaani Wakala wa Maji Vijiji hii itasaidia sana Wizara kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo niendelee kumshukuru Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wake wote wa Wizara kutusaidia kufika hapo tulipofika kuanzisha mradi wa vijiji 57 ushirikiano umekuwa mkubwa sana. Naunga mkono hoja.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa masikitiko makubwa sana kwa ukosefu wa maji katika majimbo ya pembezoni ya Mkoa wa Iringa. Wananchi wanapata adha kubwa sana. Katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 271 namba 63, 65 na 66 jinsi ambavyo Wizara na watendaji wake wamefanya kazi ya ku-*copy and paste* kwani wameonesha visima hivyo viro katika Mkoa wa Iringa wakati visima hivyo viro Mkoa wa Njombe na si Iringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya makosa yanasaababisha adha kubwa kwa wananchi wa Mkoa wa Iringa hasa Wilaya ya Iringa, Jimbo la Kalenga na Isimani ambapo kuna changamoto kubwa sana ya maji. Kuna shida kubwa ya fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa ya umwagliaji ya vijiji vya Ibumila na Mgama ambavyo viro kata ya Mgama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kalenga kumekuwa na uchakavu wa miundombinu ya maji yote, hivyo tunaiomba Serikali itoe pesa wananchi wapate maji. Vivyo hivyo kata

za Kihorogota na Kisinga vilivyopo Jimbo la Ismani vipatiwe maji.

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza Waziri wa Maji, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watenddji wote walioshiriki katika kutekeleza miradi ya maji hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kwa kueleza changamoto zilizoko katika sekta ya maji na umwagiliaji. Kumekuwa na matukio mengi ya maafa yanayosababishwa na mafuriko ya mvua nyingi hali ambayo husababisha uharibifu wa mali na hata vifo vingi kwa wananchi wetu viliviyotokana na mafuriko ya mvua hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara hii ya Umwagiliaji inakuwepo kipindi chote cha awamu zote na utawala na kumekuwa na matamko na ahadi mbalimbali kwa kuahidi kujenga mabwawa na miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji hapa nchini, lakini hakuna matokeo ya kuridhisha katika sekta hii ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua kwamba jiografia ya nchi yetu ya Tanzania imejaaliwa na Mwenyezi Mungu kuwa na mabonde mengi ya kuvuna maji, mito, maziwa, milima mingi na rasilimali ya mvua, vyote hivi vikitumika ipasavyo tunaweza kutatua changamoto kadhaa kama za kilimo cha umwagiliaji na kutenga maeneo ya malisho kwa ajili ya wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na upotevu mkubwa wa maji ya mvua ambayo hutiririka mabondeni kuelekea kwenye makazi na mashamba ya watu, hali hiyo husababisha maafa na uharibifu mkubwa wa mali na hata vifo vingi kutokana na mafuriko na mvua nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokanana maafa hayo mara nyingi Serikali hulazimika kutoa misaada mbalimbali kwa dharura kwa ajili ya wahanga hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ingewekeza kwenye kujenga miundombinu ya umwagiliaji kwa kujenga mabwawa kwa ajili ya kilimo cha kisasa cha umwagiliaji na kujenga miundombinu kwa ajili ya malisho ya wafugaji. Kwa kuwekeza katika sekta hii ya umwagiliaji kutatua tatiozo la ajira kwa vijana na akinamama. Vilevile kutasaidia kupunguza mafuriko ya mara kwa mara kwa kuwa maji mengi ya mvua yatavunwa kwa ajili ya umwagiliaji na malisho, hivyo ugomvi baina ya wakulima na wafugaji utakuwa umekwisha. Maana mapigano yanasa babishwa na ukosefu wa malisho kwa mifugo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ihamasishe wananchi jinsi ya kuvuna maji ya mvua na hasa katika taasisi za umma kama shule, taasisi za kiserikali na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali itenye fedha kwa ajili ya kuwekeza katika kujenga miradi mikubwa ya mabwawa kwa ajili ya malisho ya mifugo yote hapa nchini. Awamu ya Tano inasthili sifa kubwa kwa mageuzi makubwa katika sekta ya maji, kazi kubwa inaendelea na inaonekana.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe pongezi za dhati kwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara hii na watendaji wote. Jambo kubwa la pongezi ni namna ambayo tayari juhudini kubwa za makusudi ambazo zimeanza kuonekana katika suala zima la kutatua tatiozo la maji kwa wananchi wa Tanzania. Tumeona miradi mikubwa ikianzishwa. Hata hivyo nina ushauri kwamba hebu Serikali ichukue hatua za makusudi za kuunda tume maalum itakayochanganyika na Wabunge ili waende kwenye maeneo yote ambayo yalidumu kwa muda mrefu bila kukamilika ilhali Serikali inakuwa imetoa fedha za miradi hiyo ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni miaka zaidi ya kumi sasa niko ndani ya Bunge na kila mwaka nimeshuhudia tukipitisha bajeti ya maji hata kama ni kidogo. Je, fedha hizo ni kweli hadi sasa bado hazijatatuwa angalau kwa asilimia ndogo ya tatiozo la maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli inasikitisha kwani zaidi ya fedha za Serikali pia kuna fedha za wahisani zimekuwa zikiletwa nchini. Mimi nina mashaka huenda kuna chungio linapitisha fedha hizi. Hivyo nashauri tume iundwe na iangalie kuanzia miaka kumi iliyopita na fedha ambazo zimeshatoka na kama zilitumika ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni kwa nini Mkao wa Singida hauna mradi mkubwa wa maji? Naomba na sisi Singida tupate mradi mkubwa wa maji utakaotatua tatizo la maji kwenye mkoa wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa fursa ya kuchangia hoja ya Wizara hii muhimu na ya kipaumbele kwa mustakabali wa maendeleo, afya na ufanisi wa Taifa letu. Mengi yaliyochangiwa na Wabunge kuhusu utaratibu mzima na usimamizi wa Wabunge kuhusu utaratibu mzima na usimamizi wa miradi ya maji ni ya maana na ni lazima sasa hivi ufanywe uchunguzi wa kina kuhusu matumizi ya fedha nyingi sana za miradi ya maji ncjhi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuungana na Wabunge wenzangu waliopendekeza kuwa miradi ya maendeleo ya maji isimamiwe moja kwa moja na Wizara ya Maji yenye badala ya huu utaratibu wa sasa wa kuachiwa Halmashauri. Hii tunaiomba kwa sababu tumeona kule ambako Wizara imesimamia miradi imekuwa na ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali kwa mara nyingine tena kuwa Tanzania ina mikoa mingi inayopata mvua nyingi sana na inaishia ardhini au baharini. Serikali ituoneshe mpango mkakati iliojiwekea wa kuvuna maji nchi nzima kutumia njia mbalimbali, kuchimba mabwawa makubwa ili yatumike kumwagilia mazao, kufuga samaki na kutumiwa majumbani na taasisi, kuwekwa matanki ya kukinga maji kwenye taasisi za kijamii na kaya za watu maeneo yote. Tunaitaka Serikali ije na mpango madhubuti

ulioainisha maeneo ya kujenga mabwawa na kuweka matenki (mapipa).

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji ishirikiane kwa karibu sana na Wizara ya Mazingira na Wizara ya Ardhi na ya Kilimo kwa ajili ya kuweka mipango ya pamoja ya uvunaji maji, ulinzi wa vyanzo vya maji na umwagiliaji na kilimo na ufugaji. Hili ni muhimu, tunaomba tamko na mkakati wa Wizara katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna miradi mingi mipyta ya maji imeshapata kibali cha kuingwa mikataba kutoka Wizara ya Maji, lakini haipelekewi fedha, je, utaratibu ukoje? Vilevile Halmashauri nyingi zimewasilisha hati za madai Wizarani, lakini fedha hazijatolewa na tunajua kuchelewa kulipa husababisha *penalty* ambazo zinatuletea gharama nyingine, je, kuna utaratibu gani katika ulipaji wa *certificates*?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna haja sana ya bajeti ya kuhamasisha na kutoa mafunzo ya umuhimu wa kutunza vyanzo vya maji na kuweka adhabu kali kwa wote wanaovamia vyanzo vya maji kama ambavyo Maliasili wamesimamia maeneo yote ya hifadhi. Ninaomba Wizara ya Maji ijifunze kutoka nchi kama Israel, Afrika Kusini au Australia na hata nchi za Marekani Kusini juu ya jinsi ya kutunza maji yote yanayopatikana Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi wa fedha inayotolewa kwenye miradi ya maendeleo ya maji si ndogo kwa kiwango chochote kile. Kitu kinachohitajika sasa ni jinsi ya kufanya ufuutiliaji na tathmini ya karibu ya matumizi ya fedha hii ili kila senti ilete thamani stahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo unda kamati ya kufuatilia matumizi ya fedha yote iliyoingizwa kweye maji kwa miaka mitano iliyopita. Naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii

muhimu kwa uhai wa wananchi wetu. Nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na uzima hata tumefika jioni hii ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Wizara kwa kazi ya utekelezaji wa miradi ya maji katika jimbo langu na ziara ya Mheshimjiwa Waziri na Naibu wake kafika katika jimbo langu kuona changamoto ya upatikanaji wa maji safi na salama na miradi ya maji ya umwagiliaji. Naomba Serikali kutupatia fedha za ukarabati na upanuzi wa miradi ya maji ya vijiji vya Mkuyuni, Pangawe na Kizinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Mkuyuni ni mradi chakavu na wa muda mrefu, tangu mwaka 2000 wakati huo mahitaji ni madogo na watu wachache. Naomba Serikali kutenga fedha za ujenzi wa tenki kubwa, kubadilisha mabomba kutoka nchi nne na kuweka ya nchi sita na kujenga kidaka maji kipyaa juu zaidi ya chanzo, ili kuwe na msukumo mkubwa zaidi kuwezesha maji kufika katika vitongoji vyote na kijiji cha Kivuma ambacho kipo juu zaidi ya Mkuyuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba upanuzi wa Mradi wa Maji wa Pangawe na Kizinga na ukarabati mkubwa, kwa sababu mahitaji ya maji yameongezeka, uelewa wa watumia maji safi na salama umeongezeka, idadi ya watu imeongezeka na ujio wa viwanda katika kata hii ya Mkambarani kama vile cha Phillip Morris na Mahashree yanaongeza idadi ya watu na mahitaji kuongezeka. Naomba mahitaji ya vifaa kama vya mradi wa Mkuyuni na Kivuma ipatiwe fedha kwa mradi huu wa Pangawe pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu la pili ni kukipatia maji kijiji cha Mfumbwe kwa sababu wana chanzo cha maji ya msereko karibu, pia vijiji vyote vilivyozunguka vina maji kasoro kijiji hicho kimoja kilicho katika kata Mkuyuni.

Pia naomba Serikali itupatие fedha katika mradi wa umwagiliaji katika shamba la kijiji cha Kibwaya katika Bonde la Mto Kibwaya, Kisemu mpaka Mfumbwe ili kuwawezesha wakulima kulima zaidi ya mara moja kwa mwaka na

kuongeza kipato cha wakulima na uhakika wa chakula katika kijiji hiki, Kata na Tarafa nzima ya Mkuyuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba Serikali kufanya ukaguzi maalum katika mradi wa umwagiliaji wa kijiji cha Kwika sababu umechukua muda mrefu tangu mwaka 2005 mpaka sasa. Pamoja na kutuma kiasi kikubwa cha fedha, lakini bado mradi haujamalizika na kujengwa chini ya kiwango na kupoteza fedha za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja na mchango wangu uzingatiwe pamoja na ule wa mdomo.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi kwa Wizara, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakuu wa Taasisi chini ya Wizara, wataalam, Wenyeviti wa Bodi na kikosi kizima cha Wizara. Majukumu ya Wizara hii ni mengi, makubwa na magumu, tunafahamu, lakini jitihada zenu zinaonekana. Hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shukrani. Nimrona miradi michache ambayo jimbo langu limebahatika kutengewa fedha, baadhi ni ile inaendelea, hususan ule wa huduma ya maji, Tunduru Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mradi wa Maji Tunduru Mjini, tunaomba kasi ya utekelezaji iongezeke ili mradi huu ukamilike haraka iwezekanavyo. Tunaomba ukamilifu wa mradi kwa viwango vya kitaalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Miradi ya Maji Vijijini, hali sio nzuri kwa upatikanaji wa huduma za maji vijijini katika Jimbo langu la Tunduru Kaskazini. Kwa kuanzia, naomba vijiji vifuatavyo vipewe kipaumbele; Nakapanya, Muhunesi, Majmaji, Sisi Kwa Sisi, Cheleweni, Huria, Namwinyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wahandisi, mafundi sanifu na mafundi sadifu; kuna uhaba mkubwa sana wa wataalam

katika Wilaya ya Tunduru. Katika hali hii ni vigumu kupata ushauri sahihi kusimamia miradi kwa uhakika na kutekeleza majukumu ya kitaalam. Ushauri huu ni kwa Taifa zima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikiano kati ya wataalam wa Halmashauri ya Wilaya na wale wa Mamlaka ya Mkoa au Mhandisi wa Maji wa Mkoa ni vema kanuni na taratibu zilizopo zikaangaliwa upya. Iwapo kuna kasoro za kisera, kisheria, kanuni na taratibu zirekebishwe na iwapo tatizo ni utekelezaji tu basi wahusika wapewe miongozo kwa msisitizo na wale wanaokaidi bila kujali ni mara ngapi wameshauriwa wachukuliwe hatua stahiki.

**MHE. ZAINABU M. AMIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwapa afya njema Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa *Engineer Isack Aloyce Kamwelwe* (Mbunge), pamoja na Naibu Mheshimiwa Jumaa Aweso (Mbunge). Pia nawapongeza kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii.

Kutokana na upatikanaji wa visima virefu maeneo ya Kimbiji, Dar es Salaam hivyo naishauri Serikali katika bajeti hii ya mwaka 2018/2019 itenye fedha kwa ajili ya kusambaza maji hayo katika maeneo mbalimbali ya mkoa wa Dar es Salaam. Wakulima wengi wa mboga mboga Mkoani Dar es Salaam wanatumia maji ambayo si safi na si salama kwa umwagiliaji. Hivyo naishauri Serikali iwawezeshe wakulima hao wachimbe visima virefu kwa ajili ya kupata maji safi na salama ya kumwagilia mboga zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali isimamie vya kutosha malalamiko ya wananchi wanaobambikiwiwa bili hewa za maji ili haki iweze kutendeka. Naishauri Serikali iboreshe miundombinu katika Mkoa wa Dar es Salaam katika maji taka. Kwa kuwa wakati wa mvua *septic tanks* zinafumuka na kumwaga maji machafu yenye vinyesi ambayo ni hatari kwa afya ya binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali itoe elimu ya kutosha kwa wananchi kuhusu utunzaji wa vyanzo vya

maji, mfano katika Milima ya Uluguru, Morogoro. Naishauri Serikali itoe elimu ya kutosha kwa wananchi kuhusu jinsi ya kuvuna maji ya mvua na jinsi ya kuyahifadhi kwa sababu wananchi wengi hawana uelewa wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iweke chujio la maji madhubuti katika Bwawa la Mindu liliopo Mkoani Morogoro kwa kuwa wakati mwingine maji huwa na uchafu wa rangi ya kijani. Pia yawekewe dawa ya kusafisha maji kwa sababu wakati mwingine yanakuwa na harufu ya samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya miradi ya maji zipelekwe kwa wakati katika eneo husika ili kuweza kuondoa matatizo ya upatikanaji wa maji katika nchi yetu. Naishauri Serikali wakandarasi ambao wameonesha kiwango cha chini cha utekelezaji wa miradi ya maji wachukuliwe hatua za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nawatachia afya njema na umri mrefu ili kuyatekeleza majukumu yenu ya kila siku.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie machache juu ya Wizara hii ya Maji na Umwagiliaji.

Kwanza nitoe pole kwa Wizara hii nyeti sana kwa kuwa wanapewa fedha kidogo sana kwa ajili ya kusambaza maji. Kwa sababu hiyo, naomba kupendekeza kuwa Serikali ichukue hatua madhubuti ya kutenga fedha angalau si chini ya asilimia 60 ili kuondoa tatizo kubwa linalowakabili wananchi wengi hapa Tanzania. Nchi haiwezi kuwa ya uchumi wa kati wa viwanda kama hata maji nchi imeshindwa kupelekea wananchi wake. Ni wazi kwamba ukosefu wa maji unasababisha magonjwa ya milipuko na hivyo kuongeza matatizo ya wagonjwa kujazana hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili naishauri Wizara ya Maji na Umwagiliaji ianze kuweka takwimu sahihi za vyanzo vya

maji ili ianze kuyatumia kikamilifu kabla ya kuchimba visima ambavyo baada ya muda mfupi vinakauka. Jimbo la Same Mashariki lina maji mengi ya mito, lakini maji yote yanaelekea baharini badala ya kupelekwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kuchukua nafasi hii kuishukuru Serikali kwa kuona umuhimu wa kufanya uamuzi mzuri wa kutenga fedha za upembizi yakinifu na usanifu wa Bwawa la Yongoma. Mradi huu wa Bwawa la Yongoma utaweza kuinua uchumi kwa kiwango kikubwa katika vijiji vikubwa vya Ndungu, Misufini, Kalemawe na Makokane. Naamini baada ya upembizi huu na usanifu mradi utatengewa fedha ili tupunguze matatizo ya maji kwenye Jimbo la Same Mashariki. Ahsante.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naunga hoja mkono na ninakupongeza Waziri, Mheshimiwa *Engineer* Kamwelwe, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, na timu yote ya Wizarani kwa kazi nzuri ya kuwapatia wananchi wa Tanzania maji safi na salama. Changamoto ni kuwa Tanzania imezungukwa na maziwa (*lakes*) kadhaa, lakini hatujaweza kunufaika nayo. Nini kifanyike ili vyanzo hivyo vya maji vinufaishe wengi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uvunaji wa maji ya mvua, msimu wa mvua maji yanatiririka hovyo kila mahali na mvua zikiisha shida iko pale pale. Kwenye kitabu imesemwa kidogo sana, swali, ni lini sasa Serikali italeta Muswada hapa Bungeni wa kutunga sheria ya kuokoa kila tone la maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, haingii akilini kwamba Serikali inaingia gharama kubwa sana kutibu maji machafu hadi yawe safi na salama wakati ambapo yale ya mvua yaliyo safi *naturaly* yanapotea ardhini. Maji ya mvua yanayotiririka barabarani na kuharibu miundombinu yajengewe mabwawa. Mfano, maji yanayotiririka Kibaigwa, njia ya Dodoma – Dar es Salaam ni lini sasa maji hayo yatakingwa kama ilivyo Morogoro (*Mindu Dam*)?

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza sana mamlaka zote za maji nchini, ombi, Wizara izisaidie kudai madeni ili zifanikiwe kuendesha shughuli zake kwa amani na utilivu. Taasisi za Serikali zinadaiwa hela nyngi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi mabovu ya maji safi na salama viwandani, shambani/bustani, *car wash* na kwingineko; ombi, Serikali itujulishe mkakati wake wa kukomesha jambo hilo kwani maji safi na salama ni ghali sana; vifaa/*taps* za maji zinamwaga maji hovskyo, Serikali itoe tamko kuhusu jambo hili. Kwenye taasisi, mashulenii na majumbani zitumike zile bomba za kuhisi (*sensor*).

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi wa uchimbaji visima vijijini unaposimamiwa na wataalam Wizarani si mzuri kwani gharama zinakuwa mara mbili. Wengi wanaona ni vyema Halmashauri zikasimamia. Wizara Isilingillie maji yanayosimamiwa na wafadhili, mfano Hai - Himo - Njia Panda; mradi unaosimamiwa na *Kilema Kusini Water Users Association* uwe huru kuijendesha kama ulivyo Mradi wa Uroki. Nashukuru kwa Mradi wa Mwanga/Same – Korogwe kutengewa hela. Naomba kuwasilisha.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na uchakavu miundombinu. Kulingana na miradi mingi ya umwagiliaji kutekelezwa ikiwa chini ya kiwango na kuleta usumbufu mkubwa kwa wananchi na kuwa chanzo cha upotevu wa pesa za wananchi wanaolipa kodi halafu zinaliwa na watu wachache ambao Serikali iwachukulie hatua za kinidhamu wale wote waliochukua na kutumia pesa za walipa kodi wa nchi hii.

Miundombinu ya maji imekuwa changamoto kubwa na kusababisha upotevu mkubwa wa maji pale ambapo inatokea mabomba kupasuka na kusababisha upotevu mkubwa wa maji katika maeneo mbalimbali nchini. Serikali inapaswa kulitafutia ufumbuzi ili kumaliza suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi nyngi kuendelea kudaiwa na kusababisha maumivu makali kwa Watanzania

ambapo wanaotakiwa kulipa ni Serikali. Inapochelewa kulipa madeni hayo kwani kunakuwa na ubaguzi kwani wananchi wa kawaida wasipolipa bili japo ya mwezi mmoja wanakatiwa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kutumia Ziwa Tanganyika hususan kusambaza maji katika mikoa inayozunguka Ziwa Tanganyika, suala hili likikamilika litasaidia kumaliza changamoto zinazokabili mikoa ya Rukwa, Kigoma, Katavi kwani wananchi wakitumia ziwa hilo ambalo litakuwa la uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bili hewa, kumekuwa na utaratibu mbovu sana wa bili za maji kuja wakati maji hayatoki. Hizi mita zinakuwa na shida au watu wote walipe madeni ambayo ni halali.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kuchangia na kuzungumzia yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi kujengwa chini ya kiwango; miradi mingi nchini inajengwa chini ya kiwango hivyo kutumia fedha nyingi za Serikali na kuleta hasara kwa Serikali, huku ikiachwa miradi hiyo itakuwa haitoi maji kama ilivyotegemewa. Mfano, Mradi wa Maji wa Vikawe wenye gharama ya shilingi milioni 531 ambaao hautoi maji baada ya wananchi kuukataa kutokana na mabomba kuvuja na kuongeza gharama za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu umwagikaji maji hovyo (upotevu wa maji), nashauri Serikali kuliangalia suala hili la maji kwa wananchi imekuwa kawaida kwa mamlaka kurudisha hasara kwa wananchi. Mamlaka zimekuwa zikifanya uzembe wa kufanya matengenezo ya mara kwa mara ili kudhibiti upotevu wa maji unaondelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhaba wa wahandisi wa maji, maeneo mengi hapa nchini hakuna wahandisi wa maji, wanatumiwa wale ambaao hawana ujuzi na hivyo kusababisha miradi mingi kujengwa chini ya kiwango. Mfano,

Mhandisi wa Halmashauri ya Kibaha ambaye ni wa mazingira hivyo kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi. Naishauri Serikali kuendelea kuwaandaa wahandisi katika vyuo vyetu ili kupata wahandisi bora ili kulinda fedha za Serikali zinazopotea bila sababu.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza Wizara kuitia Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa ya kusimamia Wizara hii. Natambua Waziri alifika katika Jimbo langu la Iramba ya Mashariki na kuona tatizo la maji na jinsi watu wanavyohangaika, hii ni tofauti na mifugo. Ninashauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi kwa mradi wa uchimbaji visima katika vijiji kumi pesa ambazo zilitolewa na Serikali lakini baadhi ya visima havina maji ya kutosha na pesa zimelipwa. Serikali ione namna ya kujenga na kutoa fedha kwa ajili ya mradi huo wa visima kumi. Pia Serikali ione namna ya kusaidia Wilaya kame kupata malambo na mabwawa ikiwemo Mkalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makao Makuu ya Wilaya ya Mkalama ni Nduguti, mji ambao hauna maji. Naomba Wizara ione namna ya kuanzisha mradi maalum katika Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetoa shilingi milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya Kinyambuli, ni muhimu mradi wa maji ukapelekwa kwenye kituo hiki cha afya.

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia katika bajeti hii ya Maji na Umwagiliaji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, akinamama na watoto ndio wanaoumia zaidi na tatizo la kukosekana maji nchini Tanzania. Kama inavyojulikana akinamama ndio wapishi katika familia zetu za Kiafrika pamoja na watoto kwa maana ya kuwafundisha kazi kwa ajili ya maisha ya baadae. Mfano, katika Jimbo la Ngorongoro Kijiji cha Naiyobi, Mkoani Arusha

kuna kero kubwa sana ya ukosefu wa maji kwa muda mrefu sasa, akinamama na watoto wanakesha hadi siku tatu kwenye bomba la kijiji kwa ajili ya kusubiria maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana tatizo la maji lishughulikiwe na kupewa kipaumbele kwa ajili ya kuwasaidia akinamama hawa ambao wamekuwa wanateseka na tatizo la maji kwa muda wa miaka 20 sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Ngorongoro ni Jimbo la kitalii kuititia *Crater* ya Ngorongoro ambayo pia ni kati ya maajabu ya dunia. Kama inavyojuilikana sekta ya utalii ni sekta inayoongoza kuliingizia Taifa letu fedha za kitalii na pia kuongoza kwa kuongeza pato la Taifa baada ya madini ya dhahabu kushuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Wilaya hili ipate ufumbuzi wa tatizo hili la maji ambalo limedumu kwa muda wa miaka 20 sasa.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natanguliza kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri, pia pongezi kwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji kwa utekelezaji mzuri wa llani.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Bagamoyo wanaishukuru Serikali kwa kujengewa tenki kubwa la maji Mjini Bagamoyo, huu ni ukombozi wa huduma bora za maji safi na salama kwa wananchi wa Mji wa Bagamoyo na maeneo ya jirani. Kwa vile tenki sasa limekaribia kukamilika je, mradi wa usambazaji wa mabomba lini utaanza? Pia mradi wa usambazaji mabomba ya maji utahusu kata zipi za Jimbo la Bagamoyo? Tunaomba Mheshimiwa Waziri atupe majibu ya maswali haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa *CHALIWASA* unahudumia vijiji vya Mwavi, Fukayosi na Makurunge katika Jimbo la Bagamoyo ila huduma ya maji kwa vijiji hivi imekuwa hairidhishi tangu mradi umeanza. Mabomba ya *CHALIWASA* hayatoi maji. Napendekeza Wizara ibuni mradi wa maji

kutoka Mto Ruvu katika eneo la Mtoni ili kuhudumia vijiji vya Kata za Makurunge na Fukayosi kwa upande wa Jimbo la Bagamoyo. Huduma ya maji katika kata hizi ni duni sana. Mheshimiwa Waziri atujulishé mpango wa Serikali juu ya kuwapatia maji wananchi wa Makurunge na Fukayosi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa jitihada zake za makusudi inazochukua katika kuhakikisha wananchi wa Tanzania wanapata maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa kuhangaika kuhakikisha wananchi wanapata maji safi na salama na kushughulikia miradi ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuunganisha *DAWASCO* na *DAWASA*, ni jambo jema kwa watumiaji wa maji, ufanyike uchunguzi kwa *DAWASCO* na *DAWASA* kuhusiana na madeni, hasara na changamoto zote zilizopo katika taasisi hizo. Katika chombo hicho kipyä kitakachoundwa watendaji watakaopewa kukiendesha wateuliwe wale ambao wana maadili na waaminifu ili kuepusha matatizo hasara na madeni ya lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali na Wizara iendelee na juhudzi zake za kutafuta fedha kwa madhumuni ya kuongeza miradi ya maji nchini ili Watanzania wapate huduma hiyo muhimu ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, ahsante sana.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara ikiongozwa na Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kazi wanayofanya na kuweza kutekeleza zaidi ya asilimia 50. Lini mradi wa maji toka Ruvu Juu kwenda Kisarawe utaanza ukizingatia kazi zote

muhimu za uzalishaji mradi huo umeanza, wananchi wanahitaji maji na viwanda pia vinahitaji maji. Mradi wa Kimbiji na Mpera lini utaanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mto Wami una maji mengi sana lakini wakati wa mvua maji hayo huwa machafu, nini mpango wa Serikali wa kuweza kuyasafisha yatumike wakati wote na kuweza kuondoa kero za wananchi Mkoo wa Pwani. Nini mkakati wa Serikali kwenye matumizi ya maji ya Mto Rufiji? *DAWASA* wapewe jukumu la kuvuna maji ya mvua maeneo ya shule na hospitali. Naunga mkono hoja.

**MHE. ESTER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ninapenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara ya Maji chini ya uongozi wa Katibu Mkuu Profesa Kitila Mkumbo, kazi wanayofanya ni kubwa sana, hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo naomba nieleze changamoto kadhaa wanazopitia wakazi wa Mkoo wa Manyara hasa wanawake kwa kuwa wao ndiyo wanaopata adha kubwa ya utafutaji wa maji kwa ajili ya familia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua juhudii kubwa zilizofanywa na Wizara ya Madini ya kujenga ukuta katika eneo la Simanjiro Kata ya Mererani kwa nia njema ya kuhifadhi madini yetu. Wananchi wa kata nne zinazozunguka ukuta huo ambazo ni Marerani, Naisanyai, Endiamtu na kadhalika walikuwa wanapata maji kutoka *Tanzanite One* lakini hivi sasa hayo maji yapo ndani ya ukuta ambako *movement* za kuingia ndani ya ukuta ziko *monitored* sana, hivyo ningeomba Wizara ya Maji kwa kushirikiana na Halmashauri ili mabomba yatolewe nje ya ukuta na wananchi waweze kuendelea kupata maji kama ilivyokuwa mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikzungumzia suala hili hali ni tete zaidi kwa vijiji vya Emishiye na maeneo ya jirani na vijiji hivyo kwani ukuta wa Mererani una kilometra za mraba 24.5 ili akinamama wa Emishiye wapate maji hayo yaliyoko ndani

ya ukuta wanatembelea kilometa zaidi ya 30. Akinamama ndio gumzo ya uchumi wa familia yoyote, sasa kama mama anatumia saa 12 kutafuta maji? Maji yenyewe haya ninayozungumzia si kwamba ni maji mazuri kwa kiwango hicho, maji haya *yana floride*, mifugo na wanyama wanaotumia maji haya wamepinda miguu na kung'oka meno kabla ya umri wao.

Naiomba Serikali yangu sikivu iwaonee huruma wakazi hawa wa Simanjiro ili waweze kupatiwa maji kutoka *West Kilimanjaro* ili wapate ahueni ya maradhi yanayosababishwa na madini haya ya *floride*. Kwa sasa wakazi hawa wanenanuua ndoo moja ya lita 20 kwa shilingi 500 gharama hii ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya ukosefu wa maji ni kubwa Mkoani Manyara, Wilaya ya Kiteto ni moja ya Wilaya zinazoongoza kwa ukame zifanyike juhudzi za makusudi ili kutega maji haya ya mvua yanayopotea ili kupata mabwawa yatakayosaidia watu na mifugo wakati wa kiangazi. Wilaya ya Babati, Kata ya Singu tuna shida kubwa ya maji tunaomba msaada wa Wizara yako kama tunaweza kupata maji kutoka *BAWASA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naomba kuunga hoja mkono.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni uhai na ni rasilimali muhimu sana kwa maendeleo ya binadamu katika kila sekta, kilimo kinahitaji maji, viwanda, binadamu, wanyama na viumbe vyote hai bila maji haviwezi kuishi, hivyo maji ni kitu muhimu sana kwa uhai hata mwisho wa uhai wa mwanadamu bado hawezizikwa lazima atumie maji kusafishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji safi na salama bado ni tatizo katika Mikoa mingi mfano hapa Dodoma bado maji siyo salama kupelekeea wananchi wengi kupata magonjwa ya mlipuko na pia kuwepo na *typhoid*. Kwa kuwa Dodoma ni Makao Makuu na ni mji tunategemea kuwepo na

ongezeko kubwa sana la watu. Je, Serikali ina mkakati gani ya kuboresha mfumo wa maji taka kuwa mkubwa zaidi ili uweze kubeba maji yote na kuwepo na dampo la kutupa taka? Hii ikiwa ni sambamba na kupata maji safi na salama ya kunywa. Kwa mfano, Manispaa ya Moshi mbona ina maji safi na salama kama iliwerekana kule, hata hapa itawerekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mradi wa maji uliopo Jimbo la Moshi Vijijiini, Kata ya Mbokomu mradi uliofadiliwa na *ADB*, mradi huu umejengwa chini ya kiwango na chanzo cha maji kilivyojengwa hakina uwezo wa kudhibiti uchafuzi wa maji isitoshe maji yameelekezwa kwenye *chamber* ya bomba kwa kutumia mfumo ya sandarusi (*sulphate*) ilijoazwa udongo na *chamber* ya kutolea maji ilifunika bati yenye kutoa kutu hivyo maji kupita kwenye bomba bila kuchujwa, hii ni hatari sana kwa afya za wananchi wa kule. Nashauri Serikali ije itembelee mradi ule uliojaa ufisadi, isitoshe hata maji ya uhakika hayatoki na ichunguze waliodhinisha kwa kutia saini kwamba mradi huu wa maji umekamilika na kuidanganya Serikali ili wawajibishwe na mradi ule ule ukarabatiwe upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la kutua mama kubeba maji kichwani hasa vijiji bado ni tatizo kubwa sana la maji, Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya maji vijijiini na miundombinu yake lakini panakuwepo na changamoto nyingi mfano kufikia mwaka 2018 Serikali kwa kushirikiana na wadau ilijenga vituo mbalimbali 125,068; vituo hivi vilikuwa vihudumie watu milioni 30.9 sawa na asilimia 85.2 ya wananchi milioni 36.3 wanaoishi vijijiini, cha kusikitisha ni vituo 86,877 pekee vinavyotoa huduma kwa watu milioni 21.7 sawa na asilimia 59.8 ya wananchi waishio vijijiini. Hivyo vituo 38,209 vilivyojengwa havifanyi kazi sawa na asimilia 30.5 ya vituo vyote. Je, kwa mtindo huu Serikali ina mikakati ya ukweli ya kumtua mama kubeba maji kichwani?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, mpaka sasa Mfuko wa Maji una kiasi gani, Serikali ina mpango gani? Bado naendelea kutoa pendekezo la kutoza shilingi 50 kwenye

mafuta ili zirudi kwenye Mfuko wa Maji. Ni lini mradi wa maji uliopo Kata ya *Old Moshi Magharibi*, Jimbo la Moshi Vijijini, Kijiji cha Manda utakamilika?

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa *Engineer Isack A. Kamwelwe* (Mbunge), Waziri wa Maji na Umwagiliaji na Mheshimiwa Jumaa Aweso (Mbunge), Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Profesa Kitila Mkumbo, Katibu Mkuu pamoja na wataalam wote wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa kazi nzuri waliofanya katika kipindi cha mwaka 2017/2018. Mpaka Machi, 2018 utekelezaji wa Wizara ni zaidi ya asilimia 56 ambayo ni zaidi ya mara mbili ukilinganisha na asilimia 25 ya mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa ziara wanazozifanya nchi nzima, zimeleta tija kubwa katika utekelezaji wa miradi. Katika ziara ya Naibu Waziri Mheshimiwa Aweso, alibaini mapungufu makubwa ya mradi ya maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya. Mheshimiwa Aweso alipokagua mradi wa maji wa vijiji vya Horongo, Itimu na Mwampalala alijiona udanganyifu mkubwa wa mradi kutekelezwa chini ya kiwango na hata pale alipoambiwa mradi unatoa maji aligundua hata matenki hayakuwa na maji. Pia Mheshimiwa Kamwelwe alishuhudia utekelezaji wa asilimia mbili tu ya bajeti ya mwaka 2016/2017 huku taarifa zikipotosha kuwa miradi imekamilika na kulikuwepo madai ya wakandarasi wakati siyo kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ziara ya Waziri wa Maji aliagiza miradi yote iliyokuwa imekwama kwa zaidi ya miaka saba isimamiwe na Wizara ya Maji kupitia kwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Mbeya, uamuzi huo umeleta matunda na miradi ifuatayo iko katika hatua nzuri sana za utekelezaji, mradi wa kijiji cha Ganjembe umekamilika asilimia 90. Mradi wa vijiji vya Swaya na Lupeta umekamilika kwa zaidi ya asilimia 80. Mradi wa Mbawi na Jojo umekamilika kwa asilimia zaidi ya 90.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa vijiji vya Idimi na Haporoto umekamilika kwa zaidi ya asilimia 60. Mradi wa vijiji vya Mshewe, Muvwa, Njelenje, Mapogoro na Njele bado upo kwenye hatua za mwanzo. Mradi wa kijiji cha Ilota upo kwenye hatua za mwanzo na napenda kuwashukuru *Tulia Trust* kuahidi kuchangia shilingi milioni 250. Mamlaka ya Maji ya Mji Mdogo wa Mbalizi imekubalika kuunganishwa na Mamlaka ya Maji Mbeya ili kuboresha huduma ya maji kwa Mji wa Mbalizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa maji wa Izumbwe, Iwindi na Mwashiwala umekamilika kwa zaidi ya asilimia 50. Mradi wa skimu ya umwagiliaji kwa kijiji cha Mashewe umekamilka kwa zaidi ya asilimia 90.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hatua nzuri ya miradi hapo juu bado kuna mahitaji makubwa ya maji kwa maeneo mengi ya Wilaya ya Mbeya hasa kwenye miji midogo ya Ilembo, Inyala, Isuto, Santilya, Iwigi, Ikhoho, Mjele. Kunahitajika maji kwenye vituo vya afya, zahanati na mashule karibu yote hayana maji. Nashukuru kuwepo kwa mradi wa maji kutoka Mto Kiwira na Truu ni mkombozi pia kwa Mbeya Vijiji na hata Mji Mdogo wa Mbalizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na upungufu mkubwa wa maji kwenye mito kutokana na mabadiliko ya tabianchi na changamoto zingine napendekeza kujenga mabwawa makubwa kwenye maeneo ya vyanzo vya mito ambayo iwe pamoja na mabwawa makubwa kwenye vijiji vyenye uhaba wa mvua kama vile Mjele, Mshewe na Songwe. Rasilimali ya maji inaendelea kupungua kwa kasi kutokana na ongezeko la watu, uharibifu wa mazingira na pia mabadilko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wastani wa maji umepungua kutoka mita za ujazo 7,862 kwa mtu katika mwaka 1962 na kupungua hadi wastani wa mita za ujazo 1,800 kwa mtu kwa mwaka 2017. Inaelekea mwaka 2025 upungufu utafika mita za ujazo 1,500 kwa mtu ambayo ni chini ya wastani wa mita za ujazo 1,700 kwa mtu. Kwa mwaka

2025 tutakuwa tumeingia kwenye kundi hatarishi (*water stressed countries*). Kutokana na hali hiyo napendekeza Wizara ichukue hatua kubwa za kukabiliana na changamoto hizi ikishirikiana na Wizara ya Mazingira. Jitihada za kukabiliana na changamoto za upungufu wa maji zionakane kwenye bajeti ikiwemo kuongeza bajeti ya mabwawa na utunzaji wa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mahitaji makubwa ya bajeti ya maji na pia changamoto za upatikanaji wa fedha za nje napendekeza kuongeza tozo za mafuta kwa kila lita ya petroli na dizeli kutoka shilingi 50 hadi shilingi 100. Imedhihirika kwa mwaka 2017/2018 Mfuko wa Maji ulikusanya shilingi bilioni 158 na Wizara imetumia ipasavyo na imeleta mafanikio makubwa katika utekelezaji wa kwenye miradi ya maji vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na changamoto za utekelezaji wa miradi ya maji katika Halmashauri zetu napendekeza uanzishwaji wa Wakala wa Maji Vijijini. Wakala wa Maji Vijijini atawezesha kupunguza uhaba wa wataalam wa maji na pia ataongeza uwajibikaji katika utekelezaji kwa wakala wa maji vijijini kutawezesha utekelezaji wa miradi ya maji kwa ubora na ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara kwa kazi nzuri. Ninayo maeneo ambayo ningependa niyasemee.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukosefu wa maji safi na salama katika Wilaya ya Kigamboni, Wilaya hii hakuna utaratibu wa upatikanaji wa maji na mfumo wa utoaji wa maji taka. Eneo la Mbagala pamoja na jitihada za Serikali kuchimba visima virefu Mbagala na kusambaza maji lakini bado hatujafikia asilimia 100. Maeneo ya Chamazi, Mbande, Toangoma, Kibondemaji, Mchikichini na Mianzini hata visima vyenyewe ni vya shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu visima vya Kimbiji na Mpera, napongeza sana Serikali kwa kuchimba visima, vimekamilika kwa asilimia kubwa. Swali langu kama visima karibu saba vimekamilika kwa nini hakuna utaratibu wa kuanza sasa kusambaza maji angalau kwa kata zilizo jirani na visima hivyo? Kata ya Kisarawe II - Kibada, Pemba Mnazi na zile zilizo jirani tuanze kutumia maji ya visima hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mfumo wa maji taka, kwa kweli kuna tatizo la maji taka Kurasini, maeneo hayo yamekuwa ya mjini na mifumo imekuwa ya kizamani. Ni vema tukaangalia vizuri mfumo mzima wa maji taka Wilaya za Temeke, Kigamboni, Ubungo na Kinondoni. Ilala kuna nafuu kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bwawa la Kidunda; Serikali langalie na waweke fedha katika Bwawa la Kidunda kusaidla upatikanaji wa maji kwa uhakika katika Mto Ruvu. Wakazi wa Dar es Salaam tunategemea sana Bwawa la Kidunda kupata maji safi ya kunywa toka Mto Ruvu, lakini kipindi cha kiangazi maji yanapungua, kwa hiyo tunahitaji hilo bwawa lijengwe ili lisaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo vya maji katika nchi hii vinahitaji kuhifadhiwa kwa nguvu kubwa kwani kasi ya kuharibiwa ni kubwa mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa alipofanya ziara Bonde la Eyasi mwaka 2016 alitoa kauli za Serikali zifuatazo:-

(a)Chanzo cha Qangded kihifadhiwe kwa *radius* ya mita 500 pande zote.

(b)Mashine zote zilizoko mtoni ku-*pump* maji ziondolewe na ziwekwe nje kabisa ya chanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi leo miezi 17 tangu tamko litoke hakuna liliofanyika. Nimuombe Waziri wa Maji na Umwagiliaji afike Bonde la Eyasi ili kutekeleza maagizo hayo ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Kijiji cha Getamvua uliojengwa chini ya *WSPP* kwa zaidi ya shilingi milioni 600 haufanyi kazi kwa kujengwa chini ya kiwango. Wataalam wa Wizara walienda kufanya tathmini na hadi leo fedha za ukarabati bado hazijaletwa. Nimuombe Waziri awakumbuke wananchi wa Getamoa ili mradi ule wa maji ufufuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Karatu kwa kushirikiana na Shirika la Kidini la *CRS* wamefanya mradi wa maji katika kijiji cha Qaru kwa kutumia mfumo wa *prepaid water meters*. Mfumo huo una mafanikio makubwa sana kwani hata mapato yameongezeka mara tatu. Tunamuomba Waziri afike azindue mradi huo ili kutoa hamasa kwa wadau wengine.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya bajeti ya Wizara hii. Aidha, nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingi ya maji, baadhi ya watendaji walioko kwenye Halmashauri hawasimamii ipasavyo. Kumekuwepo na ubadhirifu ambao umepelekea kujengwa miradi iliyo chini ya viwango. Ninao mfano wa Halmashauri ya Igunga, mradi ulikamilika lakini wananchi hawapati maji na tenki kubwa likijazwa maji linavuja. Kamati ya *LAAC* imeagiza *CAG* akague mradi huo. Aidha, miradi mingi iliyotekelawa ya *World Bank* haipo sawa, ni vema Mkaguzi Mkuu (*CAG*) akaikagua miradi hii ili tuweze kujua zaidi hali halisi kwani fedha hiyo ni ya jasho la wananchi ambao watarejesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Korogwe Mjini tumeanzishiwa mradi wa maji kwa kupewa shilingi milioni

500. Mradi huu tenki limekamilika tatizo ni miundombinu ya kusambaza maji kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mradi ultengewa fedha wa viji kumi vya Lwengera Darajani, Relini na Msambiazi. Nashukuru Msambiazi mradi upo karibu kukamilika asilimia 80 mpaka 85, tenki limejengwa na virura vimeshajengwa, mkandarasi hajalipwa na ndiye aliyepewa mradi wa Lwengera Darajani/Relini. Naomba Wizara imlipe mkandarasi huyu kwani madai yake (*certificate*) zilishawasilishwa ili aweze kuendelea na kazi ya Lwengera Darajani, vinginevyo Wizara inafanya kazi vizuri anahitaji kupewa fedha ili kukamilisha miradi iliyopo.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Segerea linakabiliwa sana na uharibifu wa miundombinu ya barabara inayosababishwa na kupasuka mabomba ya maji mara kwa mara. Je, ni kwa nini Wizara haisimamii yakanunuliwa mabomba yenye viwango kuепusha hasara ya uharibifu wa miundombinu hiyo? Mfano, barabara ya Mnyamani, Kata ya Vingunguti, Kata ya Kisukuru, Kata ya Tabata barabara ya Mawenzi – Mwananchi, Kata ya Kimanga, barabara ya Twiga, barabara ya Kimanga Liwiti; kuititia mtaa wa Amani, barabara ya Bombom Kijiwe Samri Kata ya Minanzi Mirefu na Kiwalani.

Mheshimiwa Naibu Spika, usafishaji wa mabwawa ya Spenko yanayotumika kuhifadhi maji taka toka viwanda katika eneo la Mnyamani, Mtaa wa Mji Mpya na Kisiwani. Ni lini haya mabwawa yatakumbukwa kwa kuwa yanatoa harufu mbaya kwa wakazi wa eneo hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, kisima cha maji safi kimeendelea kukamilika katika Kata ya Kisukuru, ni ombi letu kwamba vifaa vya usambazaji maji vifike kwa wakati hasa mabomba ya mradi katika eneo hili la shule ya msingi Magoza ambapo pia Naibu Waziri alifika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kusisitiza umuhimu wa kuanzisha kilimo cha umwagiliaji hasa wa

mboga mboga katika maeneo ya Chanika ili kuondosha tatizo la wananchi kula mboga zenyenye sumu zinazolimwa Mto Msimbazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu Wizara ije na mpango wa namna gani itazidi kudhibiti upotetu wa maji yanayovuja mitaani ilhali maeneo mengine hayapati maji kama vile upotetu wa maji *BAWASA* wa thamani ya shilingi bilioni 1.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, *CAG* ameainisha kiasi kikubwa cha pesa kinakusanywa kupitia kwa Wakala wa *MAXCOM* kutowasilishwa kwa wakati licha ya kwamba inakuwa imekusanywa kiwango hicho kwa niaba ya *TANESCO*, mfano mpaka Juni, 2017 *MAXCOM* alikusanya shilingi milioni 756 na aliwasilisha shilingi milioni 400 tu. Hii inaathiri utendaji wa *DAWASCO* na kuendelea kukwamisha juhudzi za maji Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, *DAWASCO* imeelezwa kutumia isivyo fedha zilizotengwa kufanikisha uunganishaji wa maji kwa wateja wapya kwa mujibu wa *CAG page 84 report* ya ukaguzi wa mashirika ya umma kwa mwaka 2016/2017.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na Mradi wa Maji Mjini Nansio. Bado mradi huu haujaweza kuwa na tija kufikia malengo yaliyotarajiwu kuondoa tatizo la maji kwa wananchi zaidi ya 70,000 katika Mji wa Nansio. Hili linatokokana na matatizo ya mara kwa mara kwenye mfumo wa mradi huu. Mfano, kupasuka kwa mabomba na wakati mwingine kukatwa kwa umeme kwenye mtambo wa kusukuma maji, kutopanuliwa kwa mtandao wa mabomba na kadhalika. Hali hii imekuwa inachangia kuendelea kwa maradhi mengi yanayosababishwa na matumizi ya maji yasiyokuwa safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri/ombi, Mamlaka ya Maji Mwanza (*MWANAUSA*) iweze kusimamia na kufuatilia kwa karibu ili kuondoa tatizo la maji katika Mji wa Nansio.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa maji vijijiini (vijiji kumi) kutokamilika kwa haraka kwa mradi huu ni kikwazo kwa upatikanaji wa maji salama katika vijiji mbalimbali katika Wilaya ya Ukerewe. Hii inasababishwa pamoja na sababu nyingine kutokuwa na watumishi wa kutosha wenye wataalam katika fani ya maji mfano, wahandisi, mafundi mchundo na kadhalika. Ombi/ushauri wangu ni moja, Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe ipatiwe wataalam wa kutosha katika Idara ya Maji. Mbili, wakandarasi wanaohusika katika usambazaji maji wafuatiliwe kwa karibu kuititia Mhandisi wa Maji Wilayani kulipwa kwa wakati ili mradi huu ukamilike kwa wakati/haraka na kutoa huduma kwa wananchi wengi kadri iwezekanavyo.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia kwa maandishi. Napongeza hotuba nzuri ya Wizara ya Maji ikiongozwa na Mheshimiwa Kamwelwe na timu yake. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani kwa Mkoa wa Mtwara kutengewa kiasi cha shilingi bilioni 12.9 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji vijijiini (mwaka 2018/2019). Katika miradi ya kimkakati Wilaya ya Tandahimba imetengewa shilingi bilioni moja. Kutengewa ni jambo moja na kupewa ni hambo lingine. Nasema hivi kwa sababu mwaka 2017/2018 Serikali ilitenga shilingi bilioni 2.3 kwa ajili ya Mradi wa *Mkwiti Group Water Supply Scheme* ambao utahudumia wananchi zaidi ya 36,000 katika Wilaya ya Tandahimba. Cha kushangaza hakuna fedha ambayo imetolewa hadi sasa. Wilaya ya Tandahimba ina wakazi takribani 243,000 lakini upatikanaji wa maji ni asilimia 24 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi, mkandarasi ameshaandaa vifaa viko katika eneo la mradi kwa asilimia 80. Kwa zaidi ya mwezi mmoja sasa ameomba *advance* ya shilingi milioni 400 lakini hajapewa hadi sasa. Ameomba shilingi bilioni moja kwani amekidhi *certificate*, lakini hajapewa. Tafadhalii mkandarasi apewe fedha hii ili aweze

kufukia mabomba na kukamilisha *phase one* vinginevyo mabomba yataibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Halmashauri inaomba kibali cha kupata shilingi bilioni 8.5 zote ili watekeleze *phase* zote nne za Mradi wa Mkwiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Halmashauri ipate kibali cha kuanzisha Mamlaka ya Maji ya Tandahimba.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika majumuisho naomba majibu ya Serikali kuhusu masuala yafuatayo mahsusini ya Jimbo la Kibamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, Kata ya Goba kuna shida ya maji mitaa yote. *DAWASCO/DAWASA* waliahidi kwamba maji yatapatikana baada ya ujenzi wa matenki ya maji Sabasaba na Changanyikeni. Hata hivyo, ukweli ni kuwa maji hayajapatikana kwa wakati kwa kuwa mabomba ya maji hayajaanza kabisa kusambazwa. Wizara ieleze lini mabomba yataanza kusambazwa kwenye Kata nzima ya Goba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Msigani ina mitaa mitano; mitaa ya Msingwa, Malambamawili, Temboni, Msigani na kwa Yusuph yapo mabomba ambayo yalijengwa awamu ya kwanza (maarufu kama mabomba ya Mchina) na ya sasa (maarufu kama mabomba ya Kihindi) ambayo mpaka sasa hayatoi maji. Ni lini yataanza kutoa maji? Aidha, yapo maeneo katika mitaa hiyo ambayo hakuna kabisa mabomba. Ni lini maeneo hayo mabomba yatasambazwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Saranga, mitaa saba ina mabomba ya maji lakini si maeneo yote maji yanatoka. Hivyo, *DAWASCO* ifuatilie katika maeneo ambayo maji hayatoki. Hata hivyo katika kata hiyo kuna mitaa miwili ya Saranga na Ukombozi ambayo hayana kabisa mabomba ya maji. Wizara ieleze ni hatua gani ya haraka zinachukuliwa kuhakikisha kwamba mabomba ya maji yanasantazwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Kibamba miradi ya maji inasuasua, kuna maeneo mabomba yamerundikwa bila kuchimbiwa kwa muda mrefu na mitaro imeachwa wazi. Hivyo, hatua zichukuliwe kuhakikisha mabomba hayo yanachimbwa na pia maeneo ambayo hayana mabomba nayo mabomba yatandazwe kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Mbezi mitaa ya Msakwi na Msakwi Kusini hali ya maji ni mbaya. Yapo mabomba ambayo kwa muda mrefu hayatoi maji. Aidha, mitaa ya Mpiji Magohe na Msumi haina kabisa mabomba ya maji hivyo Wizara ieleze ni lini mabomba ya maji yatasambazwa katika maeneo hayo. Wizara ihakikishe fedha zilizopaswa kupelekwa kwa Manispaa ya Ubungo zinafikishwa kwa haraka kupunguza ukubwa wa tatizo. Lakini izingatie kuwa misaada hiyo hailingani na ukubwa wa mahitaji na kasi ya ukuaji wa maenezo ya wakazi katika mitaa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kunajitokeza tatizo katika eneo linalojengwa barabara ya lami kutoka Mbezi kwenda Goba ambapo *TANROADS* walijenga juu ya mabomba bila tahadhari hivyo mabomba yamepasuka wananchi kukosa maji na miundombinu kuharibika hasa karibu na Mazulu Kanisani na Njiapanda ya Goba na Makabe. Hali hiyo iko pia Mbezi mwisho *round about*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Kwembe ipo mitaa ambayo mabomba yamewekwa lakini mpaka sasa maji hayatoki, ni lini maeneo hayo yatatoka maji? Aidha, limejitokeza tatizo katika maeneo hayo la mkandarasi kutoshindilia vya kutosha na kuweka kifusi mwaka baada ya kuchimba mitaro na kuwekwa mabomba. Matokeo yake ni kuwa mvua zimenesha na udongo kuondoka na mabomba kubaki wazi na miundombinu ya barabara kuharibika. Kabla ya wakandarasi kumaliziwa malipo yao watakiwe kwenda kurekebisha miundombinu hiyo. Aidha, kuna mitaa kwenye kata hiyo ambayo haina kabisa mabomba, ni lini yatasambazwa? Kwa ujumla kuchukua hatua kamili *DAWASCO* ikutane.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dharura na madiwani na wenyeviti wa mitaa na watendaji wa Jimbo la Kibamba mapema mwezi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa maji katika eneo linalohudumiwa na Ruvu Chini si wa uhakika pamoja na uwekezaji mkubwa uliofanyika kwenye mitambo ya Ruvu Chini. Hali ni tete zaidi wakati wa ukame ikililinganisha na kipindi cha mvua. Hali itakuwa mbaya zaidi kutokana na mabadiliko ya tabianchi (*climate change*). Hivyo, ujenzi wa Bwawa la Kidunda unapaswa kuharakishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Waziri pamoja na taarifa ya Kamati zinajenga matumaini hewa kwamba ujenzi unakwenda kuanza. Hata hivyo, ukweli ni kuwa randama ya Wizara inaonesha kuwa ili mradi ukamilike kinahitajika kiasi cha dola za Marekani millioni 215. Taarifa nilizonazo ni kuwa mpaka sasa Serikali imeshindwa makubaliano na masharti ya kupata mkopo kuhusu mradi huo. Hivyo Wizara ieleze katika majumuisho ni namna gani fedha za mradi huo zitapatikana kwa kiasi cha kutosha katika mwaka huu wa fedha na ni lini mradi huo utakamilika? Wizara izingatie kuwa miaka nane iliyopita tumehoji kuhusu mradi huo na Wizara imekuwa ikitoa majibu ya kutoa matumaini bila utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, juu ya mchakato unaoendelea wa kuunganisha *DAWASA* na *DAWASCO*, naomba Wizara katika majumuisho itoe maelezo ya kina juu ya mchakato huo. Aidha, kama Mbunge wa Jiji la Dar es Salaam naomba kupatiwa nakala ya taarifa zilizombwa na Kamati kuhusu mchakato huo hasa kwa kuzingatia pia suala hilo linapaswa kuhusisha marekebisho ya sheria au kutungwa kwa sheria mpya ya kusimamia masuala ya maji katika Jiji la Dar es Salaam na maeneo ya jirani ya Mkoa wa Pwani yanayohudumiwa na mabomba ya Ruvu Juu na Chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bunge la Kumi kutokana na ukubwa wa matatizo ya maji nchini na haja ya Wabunge kupata majibu ya kina nilitoa hoja na Serikali

ikakubali kwamba kwenye kila Mkutano wa Bunge Serikali ilikuwa ikiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maji. Kwa hali ilivyo kwa sasa ya wastani wa upatikanaji wa maji vijijini wa asilimia 56 tu kwa vijiji na asilimia 69 kwa mijini pamoja na hoja ya nyongeza ya fedha, upo umuhimu wa Bunge hili la Kumi na Moja Serikali kuweka utaratibu wa Wizara ya Maji kutoa taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika kila Mkutano wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, fursa ya maswali ya Wabunge pekee haitoshi ndiyo maana kwenye Mkutano wa Bunge, Wabunge husimama kutaka maswali ya nyongeza bila kupata nafasi. Katika kujibu michango ya Wabunge, Serikali ielete itakavyotekela utaratibu huo.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe na nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama na kutoa mchango katika hoja hii muhimu ya maji na uhai.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa sekta hii ya maji na umwagiliaji kwa kazi nzuri walifanya kuandaa randama na hotuba hii na kuiwasilisha vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza Waziri na timu yake kwa jinsi wanavyojituma kufuatilia kero za maji na kuzipatia ufumbuzi. Hakika ninaungana na nukuu ya usemi wa Mzee Makamba kwamba; “ujana siyo sifa na uzee siyo sifa, sifa ni hapa kuna kazi nani anaiweza.” Hongera sana Waziri pamoja na umri wako kazi ya sekta hii unaiweza na umefanya vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kujenga miundombinu ya maji mijini na vijijini kwa kiasi kupunguza tatizo la maji hasa mijini ukiwemo na mradi mkubwa wa kupeleka maji katika Jiji la Dar es Salaam na miji mingine hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi, nashauri zitengwe fedha kwa ajili ya kujenga miundombinu ya maji katika Jiji la Dar es Salaam na katika miji mingine ili kuondoa tatizo la upotevu wa maji na mradi wa maji wa visima vya Mpera, Kimbiji na Ruvu ili uwanufaishe wananchi wa Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya Maji Vijijini iliyofadhiliwa na Benki ya Dunia pamoja na kuipongeza Serikali, Benki ya Dunia kwa kutafuta fedha na kujenga miundombinu ya miradi ya maji katika vijiji na katika kila Halmashauri za Wilaya na kuwezesha wananchi/wanawake kuondokana na kero ya maji. Pamoja na pongezi hizi, miradi ya maji ya vijiji kumi katika baadhi ya Halmashauri za Wilaya haikusimamiwa vizuri na baadhi ya miradi haikukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali, ningependa kujua:-

- (i) Ni vijiji vingapi miradi imekamilika na wananchi wanapata maji na katika Halmashauri zipi?
- (ii) Ni miradi mingapi imekamilika lakini maji hayatoki na njue tatizo ni nini na ufumbuzi wake ni nini?
- (iii) Miradi mingapi iko katika hatua za ujenzi na itakamilika lini na iko katika Halmashauri ya Wilaya gani na itakamilika lini?
- (iv) Je, Serikali imejipangaje katika kuhakikisha miradi ambayo ilikamilika na haitoi maji inatoa maji na miundombinu ya miradi ambayo haijakamilika. Nini mipango ya kukamilisha miradi hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji Mugango wa Kiabakari Butiama, mradi wa kujenga miundombinu Mugango - Kiabakari - Butiama ni mradi ambaao ulipangwa kutekelezwa miaka mingi zaidi wakati wa Waziri wa Maji Ndugu Mwandomsya, tangu wakati huo hadi sasa maelezo ni kwamba mradi huo utajengwa kwa fedha za wadau *BADEA* na kwamba zimekwishapatikana USD 32.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa miundombinu ya kupeleka maji mpaka Butiama kwenye kaburi la Baba wa Taifa kwa kweli limekuwa ni jambo linalotia simanzi kubwa sana kwa wananchi wa Wilaya ya Butiama kwa sababu mradi huu hautekelezwi kama ulivyopangwa. Swalii:-

(a) Ningependa kujua hivi tatizo hasa ni nini mbona ujenzi wa mradi huo hauanzii?

(b) Je, fedha hizo kutoka *BADEA* USD 32 zipo na ziko katika akaunti gani na zimeingia lini?

(c) Mkandarasi aliyeulewa kujenga miundombinu ya maji ya mradi huu wa Mgango - Kiabakari - Butiana ni nani na anaanza kazi lini?

(d) Ningependa kujua pia kama mradi huu utakamilika utawahudumia pia wananchi Kata ya Buruma, Butuguli na Mulyaza kwa sababu mradi huu miundombinu yake itapita katika baadhi ya vijiji vyta hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri, ningependa kujua kama mradi huu utawahudumia wananchi wa Kata ya Mgango, Kiriba na Tegeruka maeneo ambayo yako karibu sana na chanzo cha Mradi wa Maji cha Mgango.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa miundombinu ya maji katika maeneo yanayozungukwa na maziwa na mito; pamoja na kuipongeza Serikali kwa kujenga miundombinu ya maji katika vyanzo vyta maji ya maziwa na mito mfano, Ziwa Victoria linatoa maji mpaka Tabora na Wilaya zake. Ningependa tutumie fursa ya mito na maziwa kujenga miundombinu ya maji katika:-

(a) Mkoa wa Mara unazungukwa na Ziwa Victoria, Mto Mara na Mto Sisiti.

(b) Mkoa wa Mwanza tupeleke maji katika Wilaya zote kwa kutumia maji ya Ziwa Victoria na Mto Sibiti.

(c) Mkoa wa Geita - Ziwa Victoria.

- (d) Mkoa wa Simiyu – Ziwa Victoria na Mto Simiyu.
- (e) Mkoa wa Kagera – Ziwa Victoria, Mto Kagera na mito mingine.
- (f) Mkoa wa Ruvuma – Ziwa Nyasa Mkoa wa Ruvuma, Mbeya, Songwe na Ruvuma na Mkoa wa Katavi na Kigoma tutumie Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ijengwe miundombinu ya maji katika mikoa ya Pwani, Dar es Salaam, Lindi, Tanga, Mto Rufiji utosheleze maji katika Mkoa wa Pwani, Dar es Salaam na Lindi. Mikoa ya Morogoro na Mto Kilombero, Mkoa wa Dodoma Mto wa Mtera na Mto Zigi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha umwagiliaji, pamoja na kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri ya kujenga miundombinu ya umwagiliaji, naishauri Serikali yafuatayo:-

(a) Kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji ili kuongeza kiwango cha uzalishaji wa chakula na biashara hasa katika maeneo ambayo hayapati mvua za kutosha. Pia tuwe na uhakika wa chakula bila kutegemea mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa kilimo *Bugwema Irrigation* ningependa kujua:-

- (a) *Bugwema Irrigation* inamiliikiwa na nani?
- (b) Je, kuna mkakati gani kuhakikisha mradi huu unaufufiliwa na unaleta tija kwa wananchi wa Musoma Vijijini na Mkoa wa Mara na Taifa kwa ujumla na hasa Wilaya ya Musoma Vijijini, Butiama, Bunda na Wilaya ambazo zimekuwa zikikumbwa na ukame. Vilevile ardhi kuchoka na pia kuna ugonjwa wa mihogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji Manispaa ya Musoma pamoja na kuipongeza Serikali kwa kujenga miundombinu ya maji na kuwawezesha wananchi kuweza

kupata maji kwa kiwango kikubwa ijengwe miundombinu kwa ajili ya kufikisha maji katika vijiji vya Kata ya Nyakanga, Bukabwa Wilaya ya Butiama na Kata ambazo ziko karibu sana na chanzo cha maji Musoma Mjini na miundombinu iliyojengwa ikiboreshwia kidogo inaweza kufika huko. Pia nashauri mradi huu ufikishe maji katika vijiji vya Bukanga Kata ya Etalo, Kata ya Rifulifu, Nyegina na Nyakatende Wilaya ya Musoma Vijijiini kwa sababu wako karibu na chanzo cha maji yanayokwenda Musoma Mjini. Naunga mkono hoja.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu naomba kuhoji Serikali kimaandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa maji taka Mtwara Mjini upoje, Mtwara Mjini hakuna mfumo wa maji taka kabisa na bahari ipo karibu kabisa. Nataka kujua kwa nini Serikali haitaki kujenga mfumo wa maji taka Mtwara Mjini? Kuna uchafu mwangi sana majumbani ambao kungekuwa na mfumo wa maji taka magonjwa kama kipindupindu yasingeweza kutokea Mtwara Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukosefu wa maji taka Dodoma - Chaduru; Dodoma Jijini Mtaa wa Medeli Mashariki eneo la Chaduru hakuna mfumo wa maji taka. Wabunge wengi tunaishi huko, ni karibu na Bunge, ni mjini sana lakini hakuna mfumo wa maji taka. Je, ni lini mfumo huo utafika Dodoma Chaduru?

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya maji Mtwara Mjini kususua, naongea tena, miradi ya maji Mtwara Mjini inasusua sana. Mkandarasi wa mradi wa kutoa maji Lwelu kuja Mitengo, Mbae na Ufukoni anasusua kwa sababu hapati fedha kwa wakati. Naomba kujua kwa kuwa *pump test* tayari imefanyika lini ataanza kuchimba matenki na kusambaza maji kwenye kata husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za maji Mtwara Mjini haziji, ukurasa wa 224 wa hotuba ya Waziri wa Wizara ya Maji ametaja maeneo ya Mkoa wa Mtwara ambapo pesa

zimepelekwa kwa ajili ya miradi ya maji, cha kushangaza Mtwara Mjini (Manispaa) hakuna hata senti moja iliyopelekwa. Naomba kujua kwa nini wananchi wa Mtwara Mjini hatupewi pesa za Serikali kwa ajili ya maji?

**MHE. ESTHER L. MUDIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anazozifanya Mwenyezi Mungu ambariki sana. Pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa hotuba yao nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kutenga fedha shilingi bilioni 15 kwa ajili ya kuvuta maji toka Ziwa Victoria kuleta Simiyu, pamoja na Wilaya zake za Busega, Bariadi, Itilima, Meatu na Maswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nianze kuchangia, kuna Mradi wa Chujio Wilaya ya Maswa ni wa muda mrefu sana umeshindwa kabisa kukamilika. Mkandarasi kila akiongezewa muda ameshindwa kabisa kukamilisha, wananchi wa Wilaya ya Maswa wakiendelea kunywa maji siyo safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakigugumizi gani cha kuvunja mkataba na kumpa au kufunga mkataba na mkandarasi mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naunga mkono hoja hii na nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wote wa Wizara hii kwa namna wanavyojituma katika kutatua tatizo la maji nchini. Naomba yafuatayo yazingatiwe:-

(i) Uendelevu wa huduma ya kutoa maji lazima baadhi ya mifumo ya uendeshaji ifanyiwe utafiti.

(ii) Programu ya Maji (*WSDP*) inawatekelezaji wengi ambao wanatofautiana sana katika *approach* ya utendaji. Wizara imetengeneza sera lakini watekelezaji wake hawako chini ya Wizara kwa mfano Halmashauri za Wilaya na kadhalika. Nashauri katika suala la utekelezaji au ufungaji wa miradi wa maji vijiji na usimamiwe na Wizara.

(iii) Tuongeze juhudzi za uvunaji wa maji ya mvua, tujenge mabwawa mengi ili kuongeza rasilimali za maji na hili lisimamiwe na Wizara. Katika hili Jimbo langu la Wanging'ombe katika bajeti 2017/2018 Wizara ilipanga kufanya upembuzi na usanifu wa kujenga Bwawa la Ulembwe na Igwadianya, nataka kujua hatua ya utekelezaji na naomba mabwawa hayo yajengwe.

(iv) Mradi wa Mbukwa ulijengwa na *UNICEF* miaka ya 1976 ni chakavu ijapokuwa inahudumla zaidi ya vijiji 50. Najua toka Awamu ya Nne Serikali iliahidiwa na Serikali ya India kuwa mradi huu utaboreshwu. Nimeona kwenye hotuba zimelengwa dola za kimarekani milioni 48.99 kwa ajili ya kukarabati mradi huu. Naomba kwanza kuishukuru Serikali kwa kufuatilia utekelezaji wa mradi ili wananchi hasa wa kata za Wanging'ombe, Saja, Kijumbe, Ludinga, Illembula na Uhamhule wanashida sana ya maji na hasa kuanzia mwezi wa sita (wakati wa kiangazi).

(v) Mheshimiwa Waziri ulitembelea Jimbo langu na uliajidi visima viwili katika Kijiji cha Ihanjulwa na Itulahimba, wananchi wale walikuchezza ngoma kwa imani kuwa utawaondolea kero ya maji.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kuniwezesha kufika mahali hapa na mimi niweze kuchangia hoja hii muhimu iliyopo mbele yetu. Bajeti hii ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka 2018/2019 inakwenda kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi katika kutimiza yale yote iliyoyaanisha katika llani hasa kukamilisha miradi yote iliyopo katika sekta ya maji na umwagiliaji. Naipongeza Wizara kwa kuandaa bajeti nzuri inayokwenda kuleta

mapinduzi makubwa kwa kutatua kero zinazowakumba wananchi wetu hasa katika sekta ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya maji nchini imekuwa kubwa sana, Wabunge wote humu Bungeni tunakabiliana na changamoto hiyo nchi nzima ingawa Serikali imeendelea kuweka nguvu kubwa katika sekta ya maji, lakini bado suala la upatikanaji wa maji sehemu mbalimbali za nchi hasa vijijini imekuwa changamoto kubwa sana, kujenga na kupanua miradi mbalimbali ya maji vijijini itasaidia sana kukabiliana na changamoto hiyo, miradi 71 iliyokamilika bado ni idadi ndogo sana ukilinganisha na miradi inayoendelea kutekelezwa takribani miradi 366.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kuiweka sekta ya maji katika vipaumbele vyake kwani inawagusa watu wetu wa hali duni hasa vijijini ndiyo wanaohangaika kukesha kusaka maji usiku kucha na kuacha kufanya shughuli za kiuchumi na kimaendeleo. Naipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali inazoendelea nazo katika mipango yake ya kuhakikisha kwa mwaka huu 2018/2019 kukamilisha miradi yake ya maji ipatayo 387 kwenye Halmashauri mbalimbali nchini na pia kuanza miradi mipyä ya maji vijijini, ni jambo jema na lazima tulisemee kwa namna ya kupongeza na kuipa moyo Serikali kwa kuonyesha inatambua changamoto hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inajitahidi sana katika kuwaletea maendeleo wananchi wetu kwa kasi ya hali ya juu, lakini kumekuwa na changamoto mbalimbali katika safari hiyo ya maendeleo. Changamoto hizo zimenigusa mimi pamoja na wananchi wangu wa Kibaha Vijijini, kwa muda mrefu sasa tunaendelea kukabiliana na changamoto hiyo kwa muda mrefu sasa. Miradi ya maji ambayo ndiyo ingewakamua wananchi hawa kwa kupata maji safi nayo haikukamilika kwa wakati na ikizingatiwa chanzo cha maji kipo katika eneo lao na wao wamekuwa walinzi wazuri wa chanzo hicho ili kuepuka uharibifu wa aina yoyote unaoweza kutokea na kuleta athari kwa watumiaji wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wamekuwa wakishuhudia maji yakipita na kwenda maeneo ambayo yamekuwa sugu kwa changamoto ya maji ni Magindu, Gwata, Kipangege, Mwanabwito na Kisabi. Naomba katika bajeti hii kupewa kipaumbele katika sekta ya maji hasa katika miradi ya maji maeneo husika ili iweze kukamilika kwa wakati, na kwenye baadhi ya miradi ambayo ina changamoto ya kusimama kufanya kazi kutokana na kuharibika miundombinu yake basi nayo ipewe kipaumbele kwa kufanyiwa ukarabati wa haraka ili huduma iweze kurejea kwa wananchi, hii itasaidia kwa utekelezaji wa miradi ya maji ili wananchi waondokane na kadhia hiyo ya muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kuja na mkakati kabambe ikishirikiana na Wizara ya Kilimo ambao utakwenda kuanzisha utaratibu maalum wa kutoa elimu kwa wananchi hasa wakulima ili kuondokana na kilimo kilichopitwa na wakati na kuja na kilimo cha kisasa cha umwagiliaji ili kuwawezesha wananchi kuweza kufanya kilimo cha umwagiliaji nchini. Ushirikiano huo wa hizi Wizara mbili utaleta mabadiliko makubwa hasa katika sekta hizi husika. Naunga mkono hoja.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kazi kubwa wanayoifanya kwa ajili ya kumtua mama ndoo kichwani. Nampongeza Waziri wa Maji na Umwagiliaji kwa kazi kubwa anayoifanya akishirikiana na Naibu Waziri. Kwa kweli Mheshimiwa Kamwelwe (Waziri) na Mheshimiwa Aweso wamepewa Wizara stahiki na wanaitendea vema Wizara hii, ni imani yangu kuwa ifikapo mwaka 2020, vijiji vingine na mitaa mingi nchini itafikiwa na huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni uhai lakini pia maji ni maendeleo. Shughuli zote za kibinadamu na uhai wetu unategemea sana uwepo wa maji. Akinamama nchini wanatumia muda mwingi kutafuta maji kwa ajili ya kupika na matumizi mengine ya nyumbani. Wanafunzi mashulenii wamekuwa wakipoteza muda mwingi kutafuta maji na hii imekuwa ikiathiri taaluma. Kwa kuwa tulishakuwa na shilingi

50 kwenye kila lita ya mafuta na matokeo yake tumeyaona, bajeti ya maji imekuwa ikiongezeka na miradi ya maji mjini na vijiji ni ikiongezeka pia. Hivyo napendekeza tuongelee tozo toka shilingi 50 kwenda shilingi 100 ili bajeti iweze kuongezeka. Naamini tukiongeza shilingi 50 tena vijiji vingi na mitaa mingi itapata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni nchi yenye baraka au imebarikiwa sana, tunapata mvua nyngi sana ambazo zimekuwa zikisababisha mafuriko na uharibifu mkubwa wa miundombinu na majengo. Kuna baadhi ya nchi, mvua nyngi ni fursa za kimaendeleo. Nashauri maeneo yenye mvua nyngi ufanyike utaratibu wa kuvuna maji haya ili yatumike wakati wa kiangazi. Maeneo kama Mkoa wa Dodoma, Singida, Tabora, ungeanzishwa mradi wa uvunaji wa maji ya mvua na ujenzi wa mabwawa makubwa kwenye mabonde kama ya Fufu na mabonde mengine. Maji haya yakivunwa yanaweza kutumika kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji au matumizi ya nyumbani wakakti wa ukame.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Lupembe Halmashauri ya Wilaya ya Njombe imekuwa ikipata fedha kidogo sana kwa ajili ya miradi ya maji ukillinganisha na Halmashauri nyagine nchini. Vijiji vingi vya Halmashauri ya Wilaya ya Njombe Vijiji haina maji ya bomba pamoja kuwa na vyanzo vingi vya maji. Mfano Vijiji vya Matiganayoro, Myombo, Kichiwa, Upani, Ilengititu, Taganende, Kivitu, Lima, Isitu, Havaiga, Isohivaye, Kanikelele, Igombole, Ikang'asi, Welela, Sovi na Iyembela. Lakini naishukuru Serikali kwa kutenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, naamini fedha hizi zikitoka zitapunguza kero kubwa ya maji katika Jimbo la Lupembe na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa la usimamizi wa miradi ya maji. Wakandarasi wengi wamekuwa wakitengeneza miradi hii chini ya kiwango na kwa kutumia gharama kubwa. Ni muhimu Wizara hasa Waziri wa Maji na wataalam wa Wizara kuwa jirani na miradi hii,

kuwa na ufuatiliaji wa mara kwa mara ili kusitokee ubadhifuru unaofanywa na baadhi ya kandarasi wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kumpongeza Mheshimiwa Rais, Waziri wa Maji, Naibu Waziri na wataalam wa Wizara ya Maji kwa kusimamia na kufuatilia miradi ya maji. Hii itatusaidia kukua kwa uchumi wetu kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja iliyopo mezani.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mungu kwa kunipa uhai wa afya mpaka leo nipo humu Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitakuwa na uchoyo wa fadhili pasipo kuwapongeza watendaji wa Wizara ya Maji wakiongozwa na Mheshimiwa *Engineer Kamwelwe*, Naibu Waziri Juma Aweso, Katibu wa Wizara - Kitila Mkumbo na wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue fursa hii ya kuchangia kwa maandishi katika hotuba ya Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kuwa maji ni muhimu kwa binadamu, wanyama na mimea, lakini pia maji ni chanzo cha uchumi kwa nchi yetu kwani bila maji umeme haupatikani, bila maji barabara hazitengenezwi, bila maji mitambo haifanyi kazi, bila maji vyakula havipikwi, bila maji *operation* hazifanyiki katika hospitali. Hivyo naomba maji yapewe kipaumbele cha hali ya juu na kupelekewa fedha zinazotosheleza na zifike kwa wakati kwani ripoti ya Wizara na ya Kamati zinaonesha ni asilimia 22 tu ya fedha zinazoidhinishwa ndiyo zinakwenda kwenye maji. Naomba sana pesa zinazoidhinishwa ziwe zinakwenda kama zilivyoombwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi wa miradi ya maji; Mkoa wa Tabora umebahatika kuwemo kwenye mikoa

itakayopata maji toka Ziwa Victoria, lakini mradi huu utachukua muda mrefu mpaka kukamilika, hivyo tunaiomba Serikali ituwezeshe wananchi wa Tabora tupate vyanzo mbadala vya maji hususani Manispaa ya Tabora ambayo kwa kiasi kikubwa imekuwa ikipata vyanzo vya maji toka Bwawa la Igombe na Kazima ambapo mabwawa hayo kwa mujibu wa taarifa ya *engineer* wa maji ni kwamba yame-expire hivyo inapofika wakati wa kiangazi hukauka na kufikia kutoa tope badala ya maji na kuwasababishia adha kubwa wakazi wa Tabora Manispaa kukosa maji kwa muda mrefu na pia kulipuka kwa magonjwa ya mlipuko kutokana na watumiaji wengi kutumia maji yasiyo safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Manispaa ya Tabora wamekuwa wakikumbwa na adha kubwa ya bili ya maji ambapo inawapasa walipe bili kubwa kinyume na matumizi ya maji wanayotumia. Hivyo tunalomba Serikali kuwa na mita nzuri na wasoma mita wenye weledi kwani wamekuwa wakiwabambikia bili kubwa tofauti na maji wanayotumia. Lakini pia tunaiomba Serikali iwatolee wateja wa maji *service charge* kwani wanalipa bili kama kawaida, kufanya hivyo kutawasaidia wananchi hususani kina mama kuingiza maji kwenye majumba yao na hivyo kuiongezea Serikali mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utunzaji wa vyanzo vya maji, kumekuwa na tabia ya wakazi wanaoishi karibu na vyanzo vya maji kufanya shughuli mbalimbali za uchumi kama vile kilimo cha bustani hali inayosababisha vyanzo hivyo kuwa katika hatari ya kukauka. Hivyo niombe Serikali iweke sheria kali na kuwachukulia hatua za kinidhamu na kisheria wale wote watakobainika kuharibu vyanzo vya maji ili viweze kutumika kwa muda mrefu. Pia naomba vyanzo hivyo vitunzwe kwani pasipofanyika hivyo, kampeni ya kumtua mama ndoo kichwani haitafainikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la upoteaji hovyo wa maji, maji yamekuwa yakipotea hovyo hivyo kwenye vyanzo vya maji au kwenye mabomba baada ya kukatika na hivyo maji kupotea au kusambaa njiani kabla ya kuwafikia

watumiaji wa mwisho na hivyo kuwafanya wakose maji mara kwa mara.

Hivyo naomba Serikali iweke mikakati ya kuzuia upoteaji wa maji na pia kuwawajibisha wale wote wanaokata mabomba makusudi ili wajinufaishe au wapate maji bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naomba kuwasilisha.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hoja na kabla ya kuzungumza lolote napongeza jitihada ya Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na baadhi ya wataalamu kwa kazi nzuri waifanyayo kwa wananchi wa Tanzania na jinsi wanavyomuunga mkono Rais mpendwa kwa jitihada zake za kumtua ndoo mwanamke kichwani na kwa kuhakikisha maji yanapatikana ndani ya mita 400. Mola awape wepesi na nguvu ya kufikia azma ya Rais wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Rukwa ni kati ya mikoa ambayo inakumbwa na magonjwa ya mlipuko kila mara kutokana na kutokuwa na visima virefu vya maji safi na salama hasa vijijini. Wananchi hutumia maji ya visima vifupi, madimbwii, mito na Ziwa Rukwa ambayo ni maeneo yasiyo salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia ukurasa wa 267 hadi 279 kuna orodha ya visima 225 lakini hakuna kisima hata kimoja kwa Mkoa wa Rukwa. Tunaomba hawa Mawakala wa Uchimbaji wa Visima na Ujenzi wa Mabwawa (*DDCA*) wafike na Mkoa wa Rukwa kwa zoezi hili la uchimbaji wa visima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na upungufu wa maji nchi nzima na kuwa na miradi kadhaa ya maji ambayo bado haijakamilika na iliyokamilika hakuna maji na wakati pesa ya Serikali inakuwa imetolewa na huku haitoshelezi mahitaji, tunaomba miradi ambayo haijakamilika itambulike

na kuandaliwa mpango mkakati maalum wa kuikamilisha. Kwa ile miradi iliyokamilika na haina maji na pesa ya Serikali imetolewa ni vema wahusika wachukuliwe hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali kuona namna ya kuvuna maji ya mvua kwani mafuriko yamekithiri hapa nchini. Tutafute namna ya kuyavuna kuliko kupotea bure na kuyatumia kwa matumizi ya majumbani, mabwawa ya mifugo na hata umwagiliaji. Kwa matumizi ya maji safi na salama, kwa matumizi ya majumbani kwa wananchi wetu, ni vema Serikali kukubaliana na mapendekezo ya kuongeza shilingi 50 kwenye mafuta ya dizeli na petroli ili Mfuko wa Maji uwe na fedha za kutosha. Fedha za Mfuko wa Maji kwa Mkoa wa Rukwa shilingi 4,101,400,911 hazitoshelezi mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri tufanye ukaguzi wa miradi kabla ya kuiendeleza. Aidha, uwepo ukaguzi wa kila hatua ya miradi kabla ya malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali kuwa tete ya upatikanaji wa maji kutolingana na thamani ya fedha zinazotolewa na Serikali na mahitaji halisi ya wananchi wetu, nashauri wataalam walipo ni vema wakatathminiwa kwa maslahi ya wananchi na Taifa kwa dhamira ya Rais kuwatua akina mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya njema na kuniwezesha kuwa hapa Bungeni leo. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anazozifanya. Nimpongeze Waziri na Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanazozifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali inafanya jitihada kubwa za kuhakikisha wananchi wanapata maji safi na salama lakini bado kunahitajika jitihada za ziada katika suala hili la maji. Naishauri Serikali ili suala hili la maji liende

vizuri iweke ukomo kama ilivyoweka *TANESCO* kwamba ifikapo mwaka 2020 vijiji vyote vitapata umeme. Kwa hiyo, Wizara ya Maji nayo itamke muda rasmi wa kumaliza tatio la maji kwa vijiji vyote nchini, hii itasaidia miradi kukamilika kwa wakati.

Kuna mradi wa maji katika Wilaya ya Nyang'hwale leo ni mwaka wa sita tangu uanzishwe, wananchi wanateseka na haijulikani lini watapata maji. Niiombe sana Serikali iweze kumaliza mradi huu wa maji ili wananchi wa Nyang'hwale wapate maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya maji katika Mji wa Geita na vitongoji vyake ni makubwa sana ukilinganisha na maji tunayoyapata, mahitaji halisi ni lita 15,000,000 kwa siku lakini tunayopata ni lita 4,000,000. Kwa hiyo, kuna upungufu wa lita 11,000,000 kwa siku sawa na asilimia 29 ya maji tunayopata. Niiombe sana Serikali iongeze uwezo wa Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria ili tuweze kupata maji ya kutosha kulingana na mahitaji yetu ya maji kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mradi wa uchimbaji visima virefu 16 katika Halmashauri ya Mji katika vijiji 16 tofauti tofauti ambapo mpaka sasa mkandarasi amechimba visima vyote 16 na visima saba tu ndiyo vimefanikiwa kupata maji. Pamoja na vyanzo hivyo kuchangia kiwango hicho cha maji lakini bado huduma ya maji ni changamoto. Hivyo tunaiomba Wizara kuchukua hatua za makusudi katika kuhakikisha upanuzi wa Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria unafanyaika ili kukidhi mahitaji ya maji kwa siku katika Mji wa Geita na vitongoji vyake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna changamoto kubwa katika Idara ya Maji Geita nayo ni kukosa usafiri kwa ajili ya kufuatilia miradi ya maji iliyopo pembezoni mwa halmashauri. Tunaomba tupatiwe gari kwa ajili ya watendaji wetu ili wawewe kumudu vizuri shughuli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa malipo wa maji wa *pre-paid* ukisimamiwa vizuri utaleta tija kubwa na uendelevu wa Mamlaka na Bodimbalimbali za Maji hapa nchini. Wilaya ya Karatu ni miongoni mwa Wilaya za kwanza kuwa na mfumo huu na mafanikio yameonekana. Je, ni kwa nini Serikali isihakikishe Mamlaka za Maji kwenye miji mikubwa zinaanzisha mifumo hii ambayo itasaidia kufanya mamlaka hizi kuwa endelevu? Nawasilisha.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuanza mchango wangu kwenye Wizara hii kwa kuangalia Tume ya Umwagiliaji kwani ufanisi wa Tume hii ni wa kutiliwa mashaka. Miradi mingi ya umwagiliaji inayosimamiwa na Tume hii ukamilifu wake si wa kuridhisha na miradi mingi imehujumiwa sana kutokana na usanifu wa miradi hiyo kutokuwa wa kuridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mradi wa Ngongowele, Wilayani Liwale uliosanifiwa na Tume hiyo Kanda ya Kusini, mradi huu umehujumiwa sana hadi leo mradi huu umekwama sana. Hata hivyo, watu wa Japan wameonesha nia ya kuleta fedha ili kufufua mradi huu lakini tayari watu hao wa Kanda wameanza kutia mikono yao ili kuendelea kuhujumu mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maji mijini, pamoja na takwimu kuonesha hali ya upatikanaji wa maji mijini ni ya kuridhisha, je, Wizara ina uhakika maji haya yanawafikia wananchi kwani kiwango cha maji kinachopotea njiani ni kikubwa sana. Mfano katika Jiji la Dar es Salaam maji mengi hipotea barabarani kabla ya kuwafikia wananchi kutokana na ubovu wa miundombinu ya maji hasa kupasuka kwa mabomba kunakosababishwa na ukarabati wa barabara na ujenzi holela wa miundombinu ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kumtua mama ndoo, pamoja na nia nzuri ya sera hii lakini utekelezwaji wake si mzuri kwani miradi mingi inashindwa kukamilika kutokana na ukosefu wa fedha na utendaji usioridhisha kutokana na watendaji wengi kwenye Halmashauri zetu kushindwa

kuelewa miongozo ya Wizara hii. Mfano pale Waziri anaposema wahandisi watangaze kazi kabla ya kupewa fedha jambo ambalo halitekelezeki na linawachanganya wahandisi wengi wa Wilaya juu ya utekelezaji wake. Ni bora Serikali ikawa wazi juu ya jambo hili kwani miradi mingi vijijiini imekwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kushindwa kupeleka fedha za miradi ya maji ni kwenda kinyume na sera hii ya kumtua mama ndoo kichwani. Vilevile gharama za maji vijijiini ni ghali pengine kuzidi hata gharama za maji mijini, jambo hili limefanya miradi mingi iliyokamilika kushindwa kuijendesha kwa kukosa fedha za kununua dizeli za kuendeshea mitambo ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri ya Wilaya ya Liwale illkuwa na miradi ya kutafuta chanzo cha maji kwa ajili ya Mji wa Liwale baada ya chanzo chake cha mwanzo cha Mto Liwale kushindwa kukidhi mahitaji. Sasa ni miaka minne mradi huu umesimama huku fedha za mradi huu zikiendelea kuliwa bila chanzo hicho kupatikana. Mji wa Liwale unakua kwa kasi na unakabiliwa na uhaba mkubwa wa maji. Vilevile maji yanayopatikana hayana ubora kwani hayawekwi dawa kwa kuwa hawana dawa wala matanki ya kufanyiwa *treatment* ya maji, hivyo hulazimika kuyaleta kama yalivyotoka mtoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya takwimu tunazopewa na Mheshimiwa Waziri na uhalisia wake kwani hali ya upatikanaji wa maji nchini ni mbaya ukilinganisha na maeleo ya Mheshimiwa Waziri. Hakuna mji wala kijiji kilicho na utoshelevu wa maji. Hata pale yanapopatikana basi upatikanaji wake ni ghali sana hasa vijijiini. Ushauri wangu, ni vyema sasa watendaji walete takwimu sahihi ili sisi Wabunge tuweze kushauri vizuri Serikali ili kutatua tatizo hili sugu la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuongeza fedha kwenye Mfuko wa Maji ni bora sasa likatekelezwa ili kuiongezea fedha Wizara hii. Ongezeko kutoka shilingi 50

kufikia shilingi 100 kwani tatizo kubwa la Wizara ni fedha kwa ajili ya miradi yake

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nitoe shukrani kwa ujenzi wa miradi miwili iliyosimamiwa na *MUWASA* katika Jimbo la Moshi Vijijini, ule wa Mang'ana ulionufaisha vijiji vya kata ya Uru Kusini na Uru Kaskazini na ule wa Kaloleni unaonufanisha vijiji vya kata ya Mabogini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji aliahidi kupanua miradi ya *MUWASA* ili vijiji vilivyobaki katika kata ya Mabogini viweze kunufaika vyote yaani Mtakuja, Msarekia, Muungano na Remiti. Aidha, kata ya Kimochi sehemu kubwa ya miundombinu ya maji ni ya miaka mingi sana na imechakaa sana, inahitaji ukarabati na mahali pengi kujengwa upya. Tunahitaji Serikali kuja kufanya tathmini na kuchukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Mbokumu unaohudumia vijiji vya Tema, Kiwala na Korini Kusini na Kaskazini umekamilika lakini kuna malalamiko mengi sana juu ya kiwango cha ubora wa kujengwa kwake. Naomba Wizara ije ione ukweli huu na kuchukua hatua kwa kuwa mradi huu haufanyi kazi vizuri. Maji mengi bado yanapotea njiani na virura vingi havitoi maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho tunahitaji Wizara kuonesha kuunga mkono mifereji yetu ya asili katika vijiji vyetu vyote vya Moshi Vijijini kwani mingi inahitaji ukarabati mkubwa kidogo ambao wananchi wenyewe hawawezi.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Naibu Waziri na wasaidizi wake wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa miradi mikubwa inayotekelzwa jimboni kwangu. Nina mradi mkubwa wa kijiji cha Majalila na kijiji cha Igagala imetekelzwa na kutoa huduma kubwa sana kwa wananchi.

Naiomba Serikali kuptitia Wizara juu ya miradi ya Mwese, Ilangu, Kamjela na Kabungu ambayo bado hajitatekelezwa. Tunaomba Wizara isimamie kutekelezwa kwa miradi hiyo ambayo itawasaidia wananchi katika vijiji hivyo nilivyovitaja na ilitengewa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba ukarabati ufanyike katika visima katika vijiji vya Mishamo ambavyo vilichimbwa na Shirika la Wakimbizi la *UNHCR* mwaka 1978. Tunaomba vikarabatiwe ili viweze kutoa huduma ya maji kwenye vijij hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukamilika kwa ukarabati wa vijiji hivyo vya Ilangu, Bulamata, Kamjela, Ifumbula, Mazwe, Kapemba, Isenga Mazwe, Kusi Rugufu, Kabanga, Mgansa, Busongolala, Ipwaga na Mlibansi kunaweza kutatua tatizo la maji kwa gharama nafuu. Naomba sana vijiji hilvi mvipatie fedha za kukarabati visima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Kijiji cha Ngomalousambo uliibiwa fedha, tunaomba wahusika wa mradi huu wachukuliwe hatua kwani mradi huu umesababisha hasara zaidi ya shilingi 280,000,000 ambazo zimetumika bila kutoa maji. Wahusika wapo na hakuna hatua iliyochukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tatizo la ukosefu wa fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo ya maji. Hivyo tunaomba Serikali iongeze tengo la fedha ili tuweze kutekeleza miradi na mahitaji ni makubwa sana kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali katika utekelezaji wa miradi iwe na udhibiti mkubwa ili iwe na tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpungeze Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu Kitila na watendaji wake. Mnyonge

nyongeni lakini haki yake mpeni, Mheshimiwa Waziri na timu yake inafanya kazi kubwa sana kuhakikisha wanamtua mwanamke ndoo kichwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa walilokumbana nalo Wizara hii ni ukosefu wa fedha za kutekeleza bajeti za Wizara tunazopitisha. Natambua kuna fedha tulitakiwa kupokea mkopo wa dola za Kimarekani bilioni 500 toka *Exim Bank* ya India ili kutekeleza miradi mbalimbali ya maji nchini. Tatizo kubwa ni Wizara ya Fedha kuwataka walipie VAT mkopo huo. Tuombe sheria iletwe ili kumpa mamlaka Waziri wa Fedha kutoa msamaha wa kodi ili tupokee mkopo huo kutatua changamoto ya upatikanaji wa maji. Sambamba na hili tuongeze tozo ya shilingi 50 ili ifike shilingi 100 kuwezesha miradi mbalimbali ya maji kutekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie upande wa miradi ya maji Jimboni kwangu, moja ni Mradi wa Kalya. Naishukuru sana tena sana Serikali kwa kuwezesha mradi wa maji wa Kalya kukamilika kwa asilimia 95 na tayari maji yanatoka. Nimuombe Mheshimiwa Waziri kuongezewa pesa ili maji haya yanayotoka katika Vijiji nya Tambisho na Kalya yaende hadi Kijiji cha Kashaguru. Pia nimuombe Waziri yeye binafsi tuambatane hadi Kalya kuona jitihada kubwa sana za Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mradi wa Rukoma, nitoe masikitiko yangu kwenye mradi huu kwani tenki limejengwa lakini takribani miaka minne sasa hakuna chochote kinachoendelea. Tumeomba zaidi ya mara 20 mradi huu na wa Kandaga kuhamishiwa utekelezaji wake kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza, lakini hadi leo Halmashauri ya Kigoma Vijiji wamegoma kuileta miradi hii Halmashauri ya Uvinza. Tatizo kubwa ni Mhandisi wa Maji Mkoa kwani anatambua fika hii miradi iko kwenye Hamashauri ya Wilaya ya Uvinza. Pamoja na barua za Wizara kuelekeza miradi hii irudi Uvinza lakini yeye amekuwa ni sehemu ya kukwamisha Halmashauri ya Kigoma Vijiji kutoukabidhi Halmashauri ya Uvinza. Nimuombe Waziri

wakati akija Kalya tupite na kukagua miradi hii miwili ya Rukoma na Kandaga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Ilagala; kutokana na ukaribu wa kutoka Ilagala kwenda Mwakizega naomba Wizara itufikirie kuongeza mtandao wa maji kuelekea Vijiji vya Kabeba na Mwakizega.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Uvinza unaenda vizuri. Tunaiomba Serikali kuleta fedha kwa wakati ili mradi huu ukamilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Nguruka ulikuwa ukamilike tangu Desemba, 2017 lakini bado haujakamilika. Najua kuwa tuliomba Mheshimiwa Waziri utuongezee mtandao wa maji toka Nguruka hadi Miyabibi. Tunaishukuru Serikali kwa kukubali ombi letu la kupatiwa maji Kijiji cha Miyabibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nydingine ni vijiji vya Bweru na Itabula. Nimuombe Mheshimiwa Waziri aangalie uwezekano wa vijiji hivi viwili vya Bweru na Itabula vipate maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe Mheshimiwa Waziri atuangalie kwenye visima hali ni mbaya sana Halmashauri yetu ya Uvinza. Sambamba na hili tuombe suala la bomba la Maragalasi kuwa ni kitovu cha kilimo cha umwagiliaji. Nataka kujua kwa nini huu Mradi wa Kitaifa wa Ziwa Tanganyika usiwanufaishe na wananchi wa Vijiji vya Kalilani, Lufubu, Mgambo, Katumbi, Sigunga, Herembe, Igulula, Kaparamsenga, Kanawena, Kahama, Mkonkwa, Lyabusanda, Msiezi, Sunuka, Karago na kadhalika ili wananchi wanaoishi kando ya Ziwa Tanganyika wanufaikie na mradi huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya haya niendelee kuwapa pongezi Wizara hii kwa utendaji wao mzuri. Ili utendaji huu mzuri uendelee lazima Serikali iwe inapeleka fedha za miradi ya maendeleo tunazopitisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, elimu shirikishi na endelevu ni muhimu kwa wananchi juu ya namna bora ya kuvuna, kutawala na kutumia maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naambatisha maombi ya mahitaji ya maji katika Jimbo la Vunjo yaliyofanyiwa uchambuzi wa kitalamu. Mahitaji haya ni vijiji vipatavyo 37.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, hongera sana kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jimbo langu miradi ya vijiji kumi kila Wilaya imekwama karibu yote. Kijiji cha Kidenge mtiririko umekwama, kila siku maelezo ni yale yale tu na Kijiji cha Makose na Njiapanda nao umekwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba visima katika Vijiji vya Munguwi, Chipogoro, Ilamba na Lutalawe. Naunga mkono hoja.

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa dhamira yake ya dhati kuhakikisha Serikali yake inamtua ndoo kichwani mama wa Kitanzania mijini na vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza pia Mheshimiwa Waziri wa Maji na Naibu wake, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kwenye Wizara hii ya Maji kama ifuatavyo; maji ni uhai, maji ni roho, maji ni utu, yaana zaidi ya 65% ya mwili wa binadamu na maisha ya wanyama, mimea na binadamu yanategemea maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya Jimbo langu la Busokelo kuna miradi ya maji ambayo inaitwa Mwakaleli I tangu mwaka 2009 hadi leo hii mradi huu bado haujakamilika na mkandarasi anasuasua kiasi kwamba hadi sasa chanzo cha maji hakijajengwa na wananchi wangu wanapata shida kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa kwenye Wizara hii ni ukosefu wa wataalam ngazi za Halmashauri na Mikoani inayosababisha miradi mingi kushindwa kuendelea na kusimama. Wataalam wa Halmashauri wapo chini ya Wizara ya TAMISEMI, lakini Wizara ya Maji ambao ndiyo wasimamiaji wakuu wa maji, hawana mamlaka juu ya wataalam hao Halmashauri na hivyo kupelekea kuwa vigumu kuwawajibisha wanapokuwa wamekosea. Ushauri wangu wataalam hawa wawe chini ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya kuanzishwa kwa Wakala wa Maji Vijiji ili waweze kusimamia kwa ukaribu na ufasaha kuliko hivi ilivyo kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la miradi ya umwagiliaji limekuwa ni tatizo kubwa sana kwa wananchi wa Jimbo la Busokelo. Kuna skimu za umwagiliaji kwenye Mto Mbaka, Kata ya Kambasegela imesahaulika na kuna kituo cha umwagiliaji ambacho kilijengwa tangu mwaka 2009 hadi sasa hakuna mwendelezo wa aina yoyote na hivyo kuisababishia hasara Serikali maana kuna majengo ambayo tayari yalijengwa kama nyumba ya mtumishi, madarasa, mabweni ila bado bwalo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya kuongeza shilingi 50 kwa lita moja ya mafuta aina ya dizeli ama petroli.

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalam wetu ngazi za Halmashauri ni muhimu wapewe/kuvezeshwa namna ya *ku-design* na *ku-survey* miradi ili zoezi hili lisitegemee wataalam toka Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na Bonde la Mto Ruhuhu; mwaka 2016/2017 kuliwekwa lengo la ujenzi wa bwawa la umwagiliaji katika Bonde la Mto Ruhuhu ambalo linalounganisha Wilaya za Ludewa na Nyasa. Cha kushangaza bajeti ya mwaka 2017/2018 na mwaka 2018/2019 hajawekwa kabisa. Sasa ningeomba Serikali inipe ufanuzi kuna tatizo gani lillotokea mpaka likaondolewa kwa mwaka 2017/2018 na 2018/2019 na hata kwa mwaka uliowekwa tengo hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bonde la Umwagiliaji Lifua, tunaishukuru Serikali kwa kutupatia fedha kwa ajili ya Skimu ya Umwagiliaji ya Lifua ambayo kilimo cha mpunga kinastawi sana. Skimu hiyo imekamilika kwa asilimia 75. Tungeomba sasa Serikali itupe asilimia 25 zilizobaki ili tukamilishe kwa kiasi cha asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa uchimbaji wa visima katika vijiji vya Tarafa ya Masasi, kufuatia uwekwaji wa umeme wa *REA* katika vijiji vya Tarafa ya Masasi yaani Iwela, Kimetembe, Nkomang'ombe, Luilo, Lifua, Kipangala, Kingole, Lihagule, Kiyogo, Manda, Igulu, Mbongo, Illela, Ngelenge, Kipingu na Kipangala, tukichimba visima hivyo walau vitatu kila kijiji nina imani kwa kushirikiana na wananchi, tutatatua tatizo la maji kwa asilimia kubwa katika tarafa hii. Nina imani tukiweka mpango kazi tatizo hili litaisha katika maeneo haya ambayo *water table* ipo jirani sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi ya maji katika Wilaya ya Ludewa; kumekuwa na tatizo kubwa kwa wakandarasi wengi wa maji kutolipwa mapema pindi wanapowasilisha *certificates* zao Wizarani kwa malipo ili kazi iendelee. Inachukua muda mrefu sana toka wawasilishe *certificates* na malipo jambo linalopelekea miradi mingi kuchelewa na kukwama. Hii inapelekea hata lengo la pesa ilio katika bajeti kubaki huku miradi ikiwa bado hajamiliika. Kuna haja ya kuangalia namna nzuri ya malipo na

ikiwezekana tutumie mfumo wa *force account* ambao umeleta ufanisi mkubwa katika miradi ya ujenzi hasa wa vituo vya afya.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa *Engineer*sack Kamwelwe ambaye kwa upendo mkubwa aliweza kufanya ziara ya kikazi Mkoani Geita na hatimaye alifika Wilayani Mbogwe ambako alitembelea Mradi wa Maji wa Mji wa Masumbwe na kutembelea Makao Makuu ya Wilaya ya Mbogwe eneo la Kasosobe ambako alielezwa juu ya uhaba wa maji ulivyo mkubwa kiasi kwamba kila mahali panapochimbwa visima virefu vya maji, maji yamekuwa hayapatikani na matokeo yake ni upotetu wa nguvu, pesa na muda mrefu bila kupata maji ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi letu la muda mrefu limekuwa ni kuiomba Wizara kutusaidia kupatikana kwa maji toka Ziwa Victoria, maji ambayo tayari yamefikishwa katika Wilaya jirani ya Kahama na Mheshimiwa Waziri kwa uungwana wake aliahidi kulifanyia kazi ombi hili muhimu. Sisi wananchi wa Wilaya ya Mbogwe tunayo matumaini makubwa na Waziri katika kuhakikisha kwamba tunapata maji ya uhakika toka katika *chanzo cha KASHWASA*. Wananchi wa Wilaya ya Mbogwe hatuna msaada mwingine isipokuwa kwa Waziri na Serikali yetu, tunaomba msaada.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mhandisi wa Maji wa Wilaya ya Mbogwe amewasilisha maombi ya fedha kwa ajili ya kuomba pesa kwa ajili ya kuunganisha umeme katika vyanzo vya maji vya visima virefu katika vijiji vya Bulugala, Lulembela, Shenda na Masumbwe. Imani yetu ni kwamba fedha zitatorewa kwa wakati ili Shirika la Umeme nchini liweze kufunga umeme katika vyanzo hivi vya maji ambavyo vinatumia mashine zinazotumia dizeli, matokeo yake ni gharama kubwa za uendeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingine ya uchimbaji wa visima katika maeneo ya Luhala, Kabanga, Ilolangula na Iponya iko mbioni kukamilishwa. Tunaiomba Serikali itoe fedha kwa wakati ili vyanzo hivi vya maji katika visima hivi vikamiliike na kupunguza kadhia ya uhaba wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba Wizara itusaidie wananchi wa Wilaya ya Mbogwe kupatiwa wataalam na vitendea kazi hasa gari.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. ABDALLAH HAJI ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu muweza wa mambo yote. Aidha, nakupongeza wewe binafsi kwa uongozi wako mzuri Bungeni na unaotumia busara.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni maisha ya kila kilicho hai duniani. Kutokana na umuhimu wa maji, takribani Wabunge wote wametoa malalamiko yao kuhusu matatizo ya maji katika majimbo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kushangaza ni kwamba miradi mingi ya maji inalalamikiwa kwamba wakandarasi hawafanyi vizuri kwenye miradi hii ambayo huwa inaigharimu sana Serikali. Miradi mingi kwa mujibu wa maelezo ya Wabunge hukabidhiwa kwa wananchi kwamba imekamilika lakini kwa masikitiko ni kwamba miradi hiyo haitoi maji. Hii ni hasara kubwa kwa Taifa hakuna Mbunge ye yeyote ambaye alipopata nafasi ya kuchangia asitoe malalamiko ya shida ya maji kwa wapiga kura wake hususani majimbo ya vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hapa ndipo Serikali inapaswa kujitathmini yenyewe kwamba fedha inatoka kwa utekelezaji wa miradi ya maji, lakini upatikanaji wa maji hayo ni wa kusuasua na thamani ya fedha itumikayo ya walipa kodi na zile za wahisani ukweli haionekani. Hivyo wananchi wanolipa kodi wana haki ya kuilalamikia Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa maelezo ya Wabunge walio wengi kwamba sababu kubwa ya ukosefu wa maji ni wakandarasi wasio waaminifu au wasio na weledi wa masuala ya upatikanaji wa maji. Naishauri Serikali kwamba suala la maji ni mtambuka na ndio kipaumbele cha maisha ya kila kiumbe kilicho hai, sasa ikiwa Serikali imekusudia kumtua mama ndoo kichwani yenye we ijiongeze na iweze kusimamia utekelezaji wa wakandarasi na ihakikishe unatoa tija ili kuondokana na shida hii. Aidha, kufanya upembuzi yakinifu kwa wakandarasi wenyewe uwezo wa weledi wa miradi ya maji ili kuepuka kupewa dhamana kwa wasio na uwezo. Hili likiwezekana angalau kwa asilimia 50 litaepusha malalamiko ya wananchi na kutoa thamani ya fedha ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo hii sio mara ya kwanza kulizungumzia ni upotevu wa maji ya mvua ambayo ni neema kubwa kutoka kwa Mungu. Kwa eneo hili bado naishauri Serikali kutenga bajeti maalum ya kutengeneza mabwawa maalum ya kuvuna maji ya mvua ambayo yakifanyika hayo tunaweza kupunguza kwa kiasi kikubwa shida ya maji. Mabwawa yataweza kusaidia kilimo cha umwagiliaji, kunyweshea mifugo, kufugia samaki na matumizi ya nyumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tumekuwa wamwagaji wakubwa wa maji baharini kwa maana kwamba maji ya mvua yote kwa muda mfupi yanakimbilia baharini na kuiacha nchi ikiwa kame. Jambo la uvunaji na uhifadhi wa maji ya mvua pamoja na kwamba una hasara yake lakini una faida kubwa. Mfano hapa Dodoma mvua yote iliyonyesha lakini ni muda mfupi tu sasa maji yote hayaonekani. Ahsante.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Bwawa la Maji Kasamwa ni tegemeo kubwa kwa wananchi wa Kasamwa kwa kuwa visima vyote huwa vinakauka wakati wa kiangazi. Hivi sasa Bwawa la Kasamwa limepasuka kutokana na mvua kubwa. Naomba Wizara

ifanye ukarabati mkubwa katika bwawa hili ambalo hivi sasa limepasuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hali ya maji Kasamwa, Mji wa Kasamwa una watu wanaokadiriwa kuwa 25,000 ambaao wanategemea visima. Naiomba Serikali kupeleka maji ya bomba kutoka Geita Mjini kwa kuwa umbali uliopo kutoka Geita Buhalahala kwenda Kasamwa ni kama kilometra 10 umbali ambaao ni mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya maji Ihanamilo, Nyanguku, Mgusu na Bulela. Hizi ni kata ambazo ni sehemu ya Geita Mjini lakini hazimo katika hotuba ya Waziri na hali ya maji katika kata hizi ni mbaya sana. Naomba Serikali badala ya kufikiria kuchimba visima ni vyema kuweka mkakati wa kupeleka maji ya ziwa ya bomba ambayo yapo ndani ya kilometra 30 tu kutoka makao makuu ya mji.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kazi kubwa wanayofanya Wizara hii. Hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, naomba kuelezea shida na adha kubwa ya ukosefu wa maji safi na salama katika Jimbo la Kwela.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na adha hiyo, tunaomba Serikali itupatие fedha za kutekeleza miradi ya maji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa *Maji Muze Group* kwa vijiji vifuatavyo ambavyo vinawenza kupata maji katika chanzo cha maji cha Mto Kalumbaleza ni Kalumbeleza, Mnazi (MUA), Mnazi Mmoja (ASILIA), Ilanga, Mbwi, Muze, Kalakala, Uzia, Isangwa na Kalumbale (B).

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna Mradi wa Maji wa Kifinga kwa vijiji vya Kifinga na Mkamba; na Mradi wa Maji wa Mtowisa ambaao unatakiwa kufanyiwa ukarabati na

kupanuliwa kwa kuhudumia vijiji vya Mwela, Mtowisa A, Mtowisa B, Lwanji, Ng'ongo na Sontaukia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia upo mradi wa maji wa kijiji cha Msia na Mradi wa llemba unaotakiwa kufanyiwa ukarabati kwa kupanuliwa na kufikia vijiji vyote vya llemba A, B, C na Kaswepa.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo Mradi wa Maji wa *Kaoze Group* utakaosaidia vijiji vya Kaoze, Kianda Igonda, Mazinge na Kitongoji cha Kikwale.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna Mradi wa *Kaesenga Group* kwa vijiji vya Kaengesa A, Kaengesa B, Mkunda, Itela, Kitete, Kazi na Kazi Katonto. Vilevile tunao Mradi wa Kijiji cha Lyapona.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo Jimbo langu lina mabonde makubwa na mito mingi inayofaa kwa miradi ya umwagiliaji. Nashangaa kuona Wizara haijatenga fedha za umwagiliaji katika Jimbo langu kwa miradi ifuatayo:-

- (1) Mradi wa Umwagiliaji wa Maleza hekta 7000;
- (2) Mradi wa Maji wa Umwagiliaji wa Nkwilo;
- (3) Mradi wa umwagiliaji wa Uzia;
- (4) Mradi wa Umwagiliaji wa Msia;
- (5) Mradi wa Umwagiliaji wa Milepa; na
- (6) Mradi wa Umwagiliaji wa llemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba kutoa ushauri kwa miradi ya maji inayojengwa nchini baada ya kumalizika, itengewe fedha za matengenezo (*service*) kuliko kutegemea michango kuliko kutegemea michango ya wananchi ya shilingi 50 kwa ndoo moja. Kiasi hicho ni kidogo sana, hakiwezi kutosha kutengeneza miradi mikubwa ya maji iliyotumia mabilioni ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani zangu kwako kwa kunipa fursa hii ya kutoa mchango wangu katika hotuba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa uongozi wao wa kuongoza Wizara hii nyeti katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia Wizara hii, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Wizara kwa kuendelea kujenga na kuimarisha vyanzo vya maji nchini, mijini na vijijini na pia kuimarishwa Mamlaka za Maji katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu katika suala la vyanzo vya maji ni kusimamia na kuchukua hadhari kubwa ya namna ya kuyatunza maji. Siyo sahihi kuona kwamba mahodhi ambayo yanahifadhi maji huwekwa wazi bila ya kufunikwa. Anaweza kutokeza adui akarusha kitu cha kudhuru (sumu) kwenye maji na akasababisha madhara makubwa kwa wananchi. Mfano wa suala hili ni katika Mamlaka ya Maji Mwanza (*MWAUWASA*). Katika Mamlaka hii hodhi la kuhifadhia maji liko wazi. Kwa hiyo, naomba Wizara ielekeze mamlaka husika ichukue hadhari/udhibiti wa suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake yote kwa kazi kubwa wanayoifanya kwa kuhakikisha wananchi wanapata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Lushoto hasa katika Kata za Kwai – Makanya, Kilole, Malibwi Kwekanga, Mbwei, Ngulwi, Ubiri Gare pamoja na Kwemashai. Maeneo yote haya yana shida kubwa mno ya maji. Hivyo basi, naomba Serikali yangu iangalie kwa jicho

la huruma kabisa kutupatia fedha kwa ajili ya kunusuru wananchi hawa hasa akina ama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali yangu tukufu kwa kunipatia pesa shilingi milioni 770 kwa ajili ya maji katika Mamlaka ya Maji Lushoto, lakini pesa hizi hazitoshii kwani zinajenga banio moja na kisima kimoja chenye ujazo wa lita 600,000. Kwa hiyo, naiomba Serikali iongeze pesa ili kazi hii inayoendelea kufanyika iende sambamba na usambazaji wa maji yaani tupatiwe fedha kwa ajili ya kununua bomba na kutoa mabomba ya zamani ambayo ni ya tangu mkoloni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, kuna Kata mbili za Ngulwi na Ubiri; kata hizi huwezi kuzitenganisha na Mradi wa Mamlaka ya Maji Lushoto, kwani kata hizi zipo chini ya mji wa Mamlaka ya Mji Lushoto na mradi huo unaelekeea maeneo hayo ya kata hizo mbili. Hivyo basi, naiomba Serikali ituongezee fedha ili mradi huu uunganishwe na kata hizo mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wangu hasa waishio katika Mamlaka ya Mji hubambikiwa bili. Hivyo basi, naiomba Serikali ilichukue suala hili na kutoa hatua kali za kisheria maana watu hawa wa Idara ya Maji wananyanya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Ngulu umefanyiwa hujuma na Mkurugenzi wa Halmashauri baada ya kumsimamisha mkandarasi wa kwanza bila kufuata utaratibu na akampa mkandarasi mwingine bila kutumia utaratibu kwa minajili ya kupewa asilimia 10. Hii imepelekea mpaka sasa hivi mradi ule kusimama na wananchi wamekosa huduma mpaka leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ni shahidi, alikuja na kutoa maelekezo na baadhi ya Madiwani na Mwenyekiti wa Kijiji walimpongeza Mkurugenzi yule lakini akawaambia msimpungeze bado ni muda mfupi aliokaa. Hili limekuwa kweli. Hivyo basi, naomba Mheshimiwa Waziri

atume timu yake ikatoe mwelekeo au yeye mwenyewe akamalize suala hili ili wananchi waweze kupata huduma hii muhimu ambayo wanaisubiri kwa hamu kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi naunga mkono kuanzishwa kwa Mamlaka ya Maji Vijijini kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mradi wa Mtumbi, huu mradi ni wa muda mrefu lakini mpaka sasa mradi ule bado hauna hata dalili ya kuanza na sasa ni takribani miaka sita imeisha. Naiomba Serikali ipeleke pesa ili mradi huu uweze kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali yangu tukufu itujengee mabwawa hasa katika maeneo ya Mazashai, Mbwei, Makanya Kwai, Kwemakame, Boheloi, Mshangai, Ubiri na Mazumba kwani katika Wilaya ya Lushoto kuna mito mingi sana inayopeleka maji sehemu za mabondeni na maji haya kuharibika tu wakati wananchi wana shida kubwa ya maji. Hivyo basi, kwa kujenga mabwawa, itasaidia wananchi kupata maji ya kunywa pamoja na kulima kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Lushoto wana hali mbaya sana hasa wananchi waishio Kwemakame, yaani mpaka sasa wanunua ndoo ya maji shilingi 1,000. Nakuomba eneo hili uliangalie kwa jicho la huruma kwani imekuwa ni kilio changu kila tunapokutana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa za uchangiaji wa bajeti ya Maji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Bwawa la Mindu nimeona katika kitabu cha Waziri anasema yupo kwenye majadiliano na Wafaransa ili kufanya ukarabati wa bwawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa *population* ya Morogoro sasa Bwawa la Mindu haliwezi kuwa ni suluhisho sahihi, lazima Serikali ifikirie kuwa na bwawa llingine ambalo litasaidiana na Bwawa la Mindu ili kutosheleza wananchi wa Manispaa ya Morogoro pamoja na viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bwawa la Kidunda, fidia zilizotolewa na Serikali kwa wananchi ni ndogo, hazikidhi na bado yapo malalamiko ya wananchi wa ndani kupunjwa. Ni vyema Wizara ikajiridisha na fidia hizo hata kama zimefanywa na *evaluator* wa Serikali lakini bado mradi huu ili ufanikiwa lazima Wizara ijenge mahusiano na wananchi ambaao watakuwa ndio wanufaika na walinzi wa mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu gharama za *ku-drill* visima, suala la kupeleka maji kwa wananchi ni jukumu la Serikali, lakini cha kushangaza sana, mtu anakosa huduma ya maji anaamua kukusanya pesa ili kuchimba kisima; gharama za kufanya *survey* na kupata kibali cha kuchimba maji ni shilingi 250,000. Pia kila mwaka wananchi waliochimba kisima wanalazimika kulipa shilingi 250,000 kila mwaka, hiyo siyo sawa. Kama mwananchi amechimba kisima, analipia umeme kusukuma maji, *automatically* kwenye umeme analipa kodi, kwenye jenereta na analipa kodi ya dizeli kusukuma maji. Hivi kwa nini Serikali inalipisha kodi nyingine tena shilingi 250,000? Hii haikubaliki. Watu wa bonde wanapaswa kuangalia upya malalamiko hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuendelea *ku-harass* vijana na akinamama ambaao wanaweka *pump* za maji ili kumwagilia mboga mboga katika mashamba ambapo Morogoro akina mama na vijana walinyanganywa *pump* zao za umwagiliaji tu wanatakiwa kulipa kodi maji ambayo ni ya mto yanayoenda kupotea baharini.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanaamua kuya-*utilize* maji hayo ambayo yangeweza kupotea badala yake wananyang'anywa *pump* za umwagiliaji, tena vikundi vya akina mama wenye mkopo benki. Hii siyo sawa. Pengine Serikali ingeweza kusubiri wavune mboga na walipe

ushuru sokoni badala ya kuvi-*harass* vikundi vyatyanawake na vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipaumbele cha Serikali bado siyo maji na ndiyo maana fedha zinazotengwa haziendi kwenye Wizara na hii imezua mashaka baada ya kubaini baadhi ya maeneo. Mfano, Mkao wa Katavi umepelekewa miradi mingi kuliko mikoa mingine, hii haikubaliki. Lazima miradi hii ya visima igawanywe kwa usawa kwa kuwa tatizo la maji ni la nchi nzima.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Mto Mgembazi unalenga kutoa maji kwenye vijiji zaidi ya 15 toka chanzo chenye uhakika cha mto huu. Mradi huu ulishafanyiwa upembuzi yakinifu miaka ya nyuma na kuonekana gharama yake ni shilingi bilioni 10. Hata hivyo, mradi huu umeshajengwa *intake* ya zaldi ya shilingi milioni 200. Hivyo bado kazi ya kutandika mabomba na ujenzi wa tanki la kuhifadhi maji. Mradi huu unaweza kufanyika kwa awamu mbili kama ifuatavyo:-

Awamu ya kwanza ni kutandika bomba hadi Kakonko Mjini na kujenga tenki kubwa kwa kuyasambaza Mjini Kakonko na awamu ya pili ni kuyasambaza kwa vijiji vyajirani vya Kata za Kanga, Kakonko, Kiziguzigu na Kasanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji ya *BTC* waliahidi kuweka miradi ya maji katika vijiji vya Wilaya ya Kakonko. Vijihi hivyo ni Kakonko, Mbizi, Itumbiko, Muganza, Kiziguzigu, Ruyewizi na Kabingo. Miradi hii imekwama hadi sasa haijaanza kutekelezwa. Serikali ielete ni lini miradi hii itaanza kutekelezwa ili wananchi waliopewa matumaini waanze kunufaika?

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo miradi mitano katika Wilaya ya Kakonko ambayo imekamilika lakini haitoi maji wakati miradi ilishakabidhiwa na kulipwa fedha zote hata za *retention*. Miradi hiyo ni Nyagwijima, Kiduduye, Katanga, Muhamange na Kiga (huu una nafuu). Miradi hii ilifanyiwa ujisadi wa hali ya juu na hivyo hakuna *value for money*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba waliohusika na ubadhifuru wachukuliwe hatua yaani wakandarasi na wasimamizi wa miradi hiyo, yaani wahandisi wa Kibondo na Kakonko, maana ilianza kabla ya kugawa Wilaya za Kakonko na Kibondo. Naomba miradi hii ifanyiwe tathmini ili kujua inahitaji nini ili iweze kuhudumia wananchi baada ya kufanyiwa marekebisho muhimu yanayohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipo visima Wilaya ya Kakonko katika vijiji mbalimbali ambavyo vina maji lakini vina miundombinu mibovu ya visima kama vile *pump, rubber* na kadhalika. Visima hivi vinashindikana kutengenezwa kwa nguvu za wananchi kutokana na gharama za vjipuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri zianzishwe Kamati za Maji za Vijiji vyote vyenye visima ili Kamati zikusanye fedha kwa watumiaji wa maji zitakazotumika kukarabati miundombinu ya visima. Pia nashauri Idara ya Maji, Wilaya ipewe uwezo kifedha ili wataalam wake wawe wanakagua visima hivyo mara kwa mara kwa kuvifanya *service*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya Umwajiliani ndio pekee inayoweza kulitoa Taifa hili katika uhaba wa chakula pindi ukame unapoathiri nchi hii na pia msimu wote wa mwaka yaani kiangazi na masika. Hivyo nashauri iwepo miradi mikubwa ya kitaifa kwa kanda. Kila kanda iwe na *Irrigation Schemekubwa* ya mazao yanayostawi kanda hiyo. Pia kila Wilaya iwe na *Irrigation Schemes* zenye uwezo wa kilimo cha mwaka mzima yaani kiangazi na masika (*sustainable irrigation schemes*).

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu kwa kazi nzuri wanayoifanya kwenye sekta ya maji. Nawapongeza kwa sababu upatikanaji wa maji umeongezeka pamoja na kuwa bado yapo maeneo ambayo hawajapata maji safi.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kuona kuwa Serikali inaweka mikakati mikubwa ya kuongeza upatikanaji

wa maji nchini, lakini maji mengi sana yanapotea sababu ya uchakavu wa miundombinu. Hili ni tatizo kubwa, inafifisha kazi nzuri inayofanywa kwenye sekta ya maji. Je, katika bajeti hii zimetengwa fedha za kutosha kuboresha au kukarabati miundombinu ya maji iliyo chakaa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko Taasisi na Idara za Serikali ambazo wanatumia maji, lakini hawalipi ankara za maji, inabidi kila mtumiaji wa maji alipe maji kama Mheshimiwa Rais alivyoagiza. Kama hawalipi wakatiwe huduma. Na mimi naona wakatiwe ili walipe kusudi kuzipa nguvu Mamlaka za Maji ziweze kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa mpango wao wa kuiweka Bukoba Mjini kwenye mpango wa kuandaa mfumo wa kuondoa maji taka. Tatizo hili limekuwa la muda mrefu. Taka hizi hutiririsha maji machafu kwenye mfereji hadi ziwani. Nawapongeza *French Development Agency- AFD*. Je, mradi huu utaanza lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia juu ya udhibiti wa vifaa vyta usambazaji wa maji (*water supply accessories*) na madawa ya kutibu maji (*water treatment*). Inabidi tujiulize, ni nani anadhibiti ubora na bei ya vifaa hivi na madawa ya kutibu maji? Je, Wizara inajua kinachoendelea? Je, kuna chombo chochote kinachoshughulikia hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, uharibifu wa miundomibinu huchangiwa na kukosekana kwa taarifa sahihi za ubora. Kwa kuwa soko ni huria na wakandarasi wanatafuta faida, hivyo ni wazi watakimbilia *cheap price* ili kupata faida kubwa *at the end*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuhusu madawa ya kutibu maji, je, Wizara ina *mechanism* gani ya kujiridhisha kuwa mamlaka zote zinazosambaza maji nchini zinawajibika kutibu maji ili kutunza afya na uhai wa Watanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni chombo gani ndani ya Wizara chenye jukumu la kuhakikisha udhibiti wa upatikanaji wa madawa ya kutibu, kusambaza na kupanga bei? Kuliacha soko liamue juu ya bei ya vifaa vya usambazaji maji na madawa ya kutibu maji bila udhibiti, kutaendelea kulitia hasara Taifa kwa kuwa na miundombinu isiyo na ubora.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kukosekana kwa uhakika kuhusu usalama wa Watanzania wote wanaotumia maji kwani hakuna uhakika kama nguvu ya soko inaweza kuratibu upatikanaji wa madawa yenye ubora na kwa bei sahihi ya soko. Hali hiyo pia husababisha kila mamlaka kujipangia bei yake ya huduma ili kufidia gharama zisizothibitika za madawa na vifaa. Kwa mfano, Wizara ya Afya inadhibiti usambazaji na bei kupitia *MSD*.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hotuba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na tatizo la tabianchi, maeneo mengi ya Jimbo la Tunduru Kusini yameathirika kwa kiasi kikubwa kwa kukauka kwa mito mingi, hivyo kufanya kuongezeka kwa kukosekana kwa maji katika vijiji vingi sana. Kuna uhitaji mkubwa wa visima vya maji vifupi na virefu ili kupunguza kero ya maji hasa katika vijiji vyenye mkusanyiko mkubwa wa watu. Vijihi hivyo ni Azimio, Seveni, Mgalias, Mwaji, Jiungeni, Mrusha, Lukala, Mahande, Mitwana, Kazamoyo, Imani, Nasya, Tuwemecho, Namesaku, Mdingula, Chemchemi, Namasakata, Ligoma, Makate, Chiwana, Mkadu, Mbesa, Chikomo, Chinunje, Umoja, Misyaje, Mchuba, Meladi, Wenji, Njenga, Likwaso, Mcheteko na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Kijiji cha Mtina ni wa muda mrefu sana, tangu mwaka 2012 katika Miradi ya *World Bank*. Halmashauri imesitisha mkataba na mkandarasi tangu Desemba, 2017 na mradi umesimama. Tunaomba mradi ule ukamilishwe haraka iwezekanavyo ili kuondoa kero za wananchi wa eneo la Mtina.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa maji katika Kijiji cha Mbesa bado unasuasua. Tunaomba Serikali kuweka mkazo mradi huo ukamilike kwa wakati ili kuondoa kero za maji katika Kijiji cha Mbesa ambacho kina idadi kubwa ya wakazi kutokana na uwepo wa Hospitali ya Mbesa ya *Mission*. Mradi wa Umwagiliaji wa Misyaje ni wa muda mrefu sana. Umetumia zaidi ya shilingi milioni 800, lakini mpaka leo mradi huo haufanyi kazi kabisa. Hivyo fedha zinakwenda bure na upo kwenye kiwango cha chini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa umwagiliaji Madaba nao umegharimu zaidi ya shilingi bilioni moja, lakini haupo katika kiwango kizuri kwa maana na hufanyi kazi ipasavyo. Hivyo unahitaji marekebisho makubwa sana ili uweze kufanya kazi vizuri. Vilevile kuna miradi mipyä miwili katika vijiji nya Wenje na Mkapunda. Tunaomba miradi hiyo ifanyiwe kazi ili kuongeza uzalishaji wa mpunga ambaao unaonekana kuwa na tija kwa wakulima wa Tunduru Kusini.

Mhesjhimiwa Naibu Spika, miradi ya maji Lukumbule na Nalasi wananchi wanashindwa kuiendesha kwa kwa kuwa na gharama kubwa sana kutokana na kutumia dizeli. Tunaomba miradi hii ya wananchi itumie umeme wa *solar* ili kupunguza gharama za dizeli ambapo zaidi ya lita 60 kwa siku zinatumika kuendesha mitambo ya kusukuma maji. Kuna miradi mitatu iliandika andiko la miradi, tulileta Ofisi ya Wizara ya Maji ili kututafutia pesa kwa ajili ya kuchimba visima na kusambaza maji katika vijiji nya Namasakata, Tuwemacho na Malumba/Molandi pamoja na Kijiji cha Mchoteka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba miradi hiyo ipewe umuhimu wa kuifanyia kazi ili wananchi wa maeneo hayo wapate maji kuondoa adha inayowakumba.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kumpongeza Waziri wa Maji, Mheshimiwa *Engineer Isack Kamwelwe*; Naibu Waziri, Mheshimiwa Aweso na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri ya kuwasilisha bajeti hapa Bungeni. Wizara hii ni muhimu sana, lakini bado Serikali haijaweza kuleta pesa ya kutosha katika miradi ya maji

nchini. Kuna mtiririko wa fedha za miradi ya maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge hazipelekwi kwa wakati katika miradi yake. Nikiwa mmoja wa Mjumbe wa Kamati hii, naomba Serikali izingatie sana maoni ya Kamati na ifanye kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Kamati ya Bunge na Wabunge wote waliopendekeza kuwa kuwepo na ongezeko la tozo ya shilingi 50 kwa lita ya mafuta ya petroli na dizeli ili kutunisha Mfuko wa Maji kama ilivyo kwa miradi ya barabara na umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema sasa Serikali ikaanzisha Wakala wa Maji Vijijini kama ilivyo Wakala wa Umeme na *TARURA*. Hii inasaidia kwa haraka miradi iliyopo vijijini, sababu ndiko kwenye matatizo makubwa sana ya maji kuliko mijini. Pia tumeona jinsi hizo Wakala nyingine zilivyoweza kutekeleza kwa haraka na eneo kubwa, toka kuanzishwa kwake, ndiyo maana tunapendekeza kiundwe chombo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya umwagiliaji ndiyo mkombozi wa maendeleo ya nchi nyingi duniani. Tunatambua kuwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inahimiza umuhimu wa kuendeleza eneo kubwa lillipo nchini linalofaa kwa umwagiliaji kwa kuweka miundombinu ya umwagiliaji kwa ajili ya kuongeza tija na uzalishaji katika sekta ya kilimo, kwenye maeneo ya chakula, biashara, malisho na kilimo cha majani. Halmashauri nyingi sana zikiwemo Halmashauri zilizopo katika Mkoa wa Iringa, zinajenga miradi ya umwagiliaji kwa kuanza na kutumia pesa za Halmashauri. Miradi mingi sana inachelewa kukamilika kutokana na ucheleweshwaji wa pesa za miradi hiyo toka Serikalini (Wizarani).

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na wingi wa miradi hiyo, nilikuwa napenda kujua, je, Serikali huwa inatumia vigezo gani kupeleka pesa hiyo katika miradi ya umwagiliaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Meneja wa *IRUWASA* katika Mkoa wetu wa Iringa, amekuwa akisimamia miradi vizuri sana na kusababisha upatikanaji wa maji katika Manispaa ni asilimia 96. Tatizo lililopo ni mji kupanuliwa kwa haraka sana na Mkoa unahitaji sasa kupata mabomba makubwa ya kusambaza maji katika maeneo yote kwa wakati, kwa sababu yaliyopo sasa hivi hayatoshelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niendelee kumpongeza Mheshimiwa Waziri alipotembelea katika Mkoa wetu, kwani alitoa semina ambayo alitujengea uwezo mzuri sana wa kufuatilia pesa za miradi ya umwagiliaji. Pia uamuzi wa *IRUWASA* kusimamia miradi ya Mkoa wa Iringa ni la busara sana. Pia naipongeze Serikali kwa kusaini pesa za mradi mdogo wa maji llula, Jimbo la Kilolo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa na changamoto kubwa sana ya usambazaji maji safi na salama na hasa kulikuwa na yale mabomba ya Mchima ambayo yalikuwa ni tatizo. Nawapongeza angalau kwa sasa wameweza kujitahidi kwa kiasi kikubwa sana kuweza kusambaza maji hatia maeneo mengi. Pia nampongeza sana Meneja wa *DAWASCOL*akini naomba kasi iongezeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna changamoto kubwa sana katika shule zetu za msingi na sekondari hasa kuhusiana na elimu bure. Hakuna michango yoyote inayotolewa shulenii kwa ajili ya tozo za maji na umeme. Hivyo kufanya shule nydingi kukatiwa maji na kusababisha mlipuko wa magonjwa na watoto wetu kusoma katika mazingira magumu sana. Hivyo, naionomba Serikali jambo hili ilipime na ichukue maamuzi kama ilivyo kutoa elimu bure na tozo za maji ziondolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali itatoa elimu kwa wananchi juu ya uvunaji wa maji? Kwa sababu kumekuwa na kipindi kirefu cha mvua na kusababisha mafuriko na uharibifu wa mazingira; ni kwa nini Serikali isitumie

mvua, hivyo kutoa elimu ili wananchi wavune maji na yatumike wakati wa kiangazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. OMAR A. KIGODA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayofanya pamoja na Serikali yake. Pili, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Naibu wake kwa mapambano makubwa ya kuhakikisha ufumbuzi wa maji unapatikana. Vilevile nampongeza Katibu Mkuu na Naibu wake kwa kuongoza Wizara vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ushauri kidogo kwa Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Lazima sasa tubadilike na kuhakikisha watendaji wote wa Wizara na Idara za Maji hawafanyi kazi kwa mazoea. Mfano, kwenye Jimbo langu kuna watu wana zaidi ya miaka 30 wako eneo moja; kwa vyovypote mtu kama huyu hawezi kuwa na *performance* nzuri. Lazima sasa hivi watu wote walioajiriwa wapimwe utendaji wao (*performance*) ikiwezekana kwa kila mwaka kwamba wamefanya *engineer* katika Wilaya, unakaa miaka kumi hakuna chochote ulichofanya, lazima wapewe *performance time*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaelewa kuna tatizo la upatikanaji wa fedha, ila hata hiyo hela ndogo inayopatikana kama tunapata watendaji wabunifu, inaweza kupunguza shida ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwaambia Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwamba haya malalamiko wanayopata leo ni kwa sababu ya utendaji wa mazoea uliopita. Mfano, ni juzi Mheshimiwa Rais alivyompigia Katibu Mkuu wa Wizara mpaka leo tumeambiwa wataalam wameshakwenda na kazi imeanza. Hii inaonekana kabisa watendaji wa kwenye eneo husika hawakuwa makini (ufanyaji kazi kwa mazoea).

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nawapongeza sana kwa kupata hela ya fidia. Hakika kuna miradi mingi itanyanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ALFREDINA A. KAHIGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Maji, Naibu wake pamoja na watendaji wote wa Wizara. Mungu awabariki sana katika kazi ngumu wanayoifanya. Tunaona wanajitahidi, lakini nina machache ya kushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wajitahidi sana pale wanapoona Waheshimiwa Wabunge wanapiga kelele. Ni kweli shida ya maji ni kubwa sana hasa wakati wa kiangazi, ni janga kubwa. Katika Mkoa wangu wa Kagera, Wilaya ya Karagwe ina mradi uliopata ufadhili toka India. Ni Mradi wa Maji ya Rwakajunju wenye zaidi ya miaka kama 20 na zaidi. Je, Serikali ina kauli gani kuhusu mradi huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu aliusemea Mheshimiwa Marehemu Sir George Kahama, Mheshimiwa Gosbert Blandes na mpaka sasa Mheshimiwa Innocent Bashungwa, na mimi nausemea. Tunaomba jibu. Wananchi wa Karagwe wana shida sana ya maji, waonewe huruma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia na baadhi ya Kata za Bukoba Vijijini wana shida ya maji waokolewe na adha hii ya maji.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ile kaulimbiu ya kumtua mwanamke ndoo bado hajiatekelezwa kutokana na jitihada za Serikali zinazoonesha kwenda kidogo kidogo katika kuwapatia wananchi wengi maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Pangani Mkoani Tanga kuna baadhi ya vijiji bado havina maji, kuna mabomba lakini hayatoi maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kata ya Madanga Wilaya ya Pangani kuna vitongoji ambavyo havina maji. Vitongoji hivyo ni Zimbiri, Jaira, Barabarani, Nunda na vinginevyo wananchi wana saidiwa na maji ambayo taasisi za dini wamechimba visima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ije na majibu ya lini Kata ya Madanga, Wilaya ya Pangani watapata maji safi na salama?

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika Kata ya Mwalijembe Wilaya ya Mkinga wananchi wana tatizo la maji, wanashirikiana maji yao na wanyama. Maji ya kwenye mabwawa siyo safi na salama. Serikali iwahurumie wananchi hawa ili kuwaepusha na magojwa ya mlipuko.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Josephat Kandege, atafuatiwa na Mheshimiwa Kakunda, Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangala ajiandae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na mimi kupata fursa ili niweze kuchangia machache. Kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja na nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayofanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze katika maeneo mawili matatu ambayo yalipata kuchangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi ni vizuri likatolewa ufanuzi. Iliafikia hatua wengine wakasema kwamba Serikali hii haina mipango ndiyo maana Msimbazi maji yanaingia na hawaelewi nini ambacho kinaendelea, ni vizuri sana nikachukua fursa hii kuweza kutoa taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba Dar es Salaam ya miaka hiyo wakati tunapata uhuru na leo kuna tofauti kubwa sana, ongezeko la watu ni kubwa. Lakini Serikali inayoongezwa na Dkt. John Joseph Pombe Magufuli ina azma ya kuhakikisha kwamba, Jiji la Dar es Salaam linakuwa mahali salama kwa kuishi na hasa naomba niongelee Bonde la Msimbazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *DFID* kwa kushirikiana na Benki ya Dunia hivi sasa ninavyoongea kimetengwa kiasi cha dola milioni 20 na tayari wameshapatikana watalaam waelekezi, kampuni kubwa mbili za kimataifa ambalo moja kazi yake ni kuweza kufanya tathmini kujua athari za mafuriko ndani ya Bonde la Msimbazi hasa Msimbazi ya Chini, na kushauri nini kifanyike, ujenzi upi ufanyike ili athari hii ambayo tunaipata; sisi sote ni mashuhuda inayptokana na mabadiliko ya tabianchi. Kwa hiyo katika dola milioni 20 ni *package* kutoka katika paundi milioni 49 ambayo ina kazi nzima ya kuhakikisha kwamba kwa kupitia utaratibu wa *Tanzania Urban Resilience Programme* tutakabiliana na tatizo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari mshauri huyu anaitwa *COWI Tanzania Limited* ameshamaliza kazi yake na sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI tuko kwenye hatua za mwisho kwa kuweza kupata mshauri mwelekezi ili *feasibility study* ifanyike na ujenzi uweze kuanza kufanyika. Pia katika lile Bonde la Msimbazi kuna awamu ya pili ambapo tayari *package* nayo imeshatolewa ambayo tunataka kuanzia Bonde la Msimbazi mto unakoanzia kule juu kabisa, kutakuwa na kazi ya kuhakikisha kwamba kuna wale watu ambao wanatakiwa wahamishwe. Vilevile ujenzi ufanyike ili eneo lile ambalo tukipata leo unaona ni sehemu isiyofaa patengenezwe namna nzuri ni ile ambayo itakuwa ni *recreation areas* kwa ajili ya kuvutia. Pia kuwe na shughuli za kila siku ambazo zitafanyika tukiwa tunahakikisha pia hatuvi na tatizo la mafuriko kama ambavyo tumekuwa tukikubwa na hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama hiyo haitoshi, kuna mradi wa ujenzi wa barabara za mabasi yaendayo kasi

awamu ya pili, jumla ya kilometra 20.3 kuanzia Kariakoo kwenda mpaka Mbagala. Mpaka sasa hivi kandarasi imeshatangazwa na itafunguliwa tarehe 20 Mei, 2018. Kwa hiyo, akipita Mbunge anasema kwamba Serikali hii haina mipango, inawezekana labda mtu hana taarifa nini ambacho kinaendelea. Ni vizuri tukaelezana ili mkajua, kwamba tuko makini tumejipanga na tutahakikisha tunakonga nyoyo za Watanzania waliochagua Chama cha Mapinduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya haya machache naomba nimpishe mwenzangu naye achangie katika yaliyojitokeza. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango ajiandae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. GEORGE J. KAKUNDA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana kwanza naomba kwa kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wa Maji; na kwa faida ya Bunge lako tukufu niseme tu kwamba sisi Watanzania ni ndugu. Maana yake ni kwamba Kamwelwe ni Kandege, Kakunda ni Kandege na Kandege ni Kandege kwa hiyo, tuko vizuri tunatumia jina moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitoe ufanuzi kwa maeneo machache; kuna Waheshimiwa Wabunge ambao wamezungumza kwamba shule zote na taasisi zote za huduma za jamii zipatiwe huduma ya maji. Nitoe taarifa kwamba tumeshaziagiza Halmashauri zote kuweka kipaumbele cha kupeleka huduma za maji kwenye taasisi zote ikiwemo shule, zahanati, vituo vya afya na hospitali na tunalifuatilia sana kwa karibu agizo hilo kuhusu utekelezaji wake na tumewaambia Wakurugenzi wa Halmashauri tunawapima kwa kutekeleza vipaumbele hivi. Aidha, tumeagiza majengo yote ya shule na majengo ya taasisi yawekeewe mifumo ya kuvuna maji mvua ili kusudi kupata maji ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili; wako Wabunge ambao wamezungumzia umuhimu wa kuhamisha watumishi wetu mara kwa mara ili kuongeza ufanisi. Hilo ni wazo zuri, tumeshaanza kulifanya kazi. Katika kipindi cha miezi miwili iliyopita tu tumeshahamisha watumishi 26 na zoezi hili linaendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wetu, sisi katika serikali za mitaa, tunatekeleza kazi zetu kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 145 na Ibara ya 146 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Sheria Na. 7 kwa Halmashauri za Wilaya; Sheria Na. 8 kwa Halmashauri za Miji. Villevile tunafuatilia sana utekelezaji wa Sheria ya Huduma za Maji Na.12 ya mwaka 2009. Katika sheria zote hizo, kazi za Halmashauri na Serikali za Mitaa kwa ujumla ni utekelezaji wa miradi ikiwemo miradi ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za Serikali Kuu kwa ngazi za Mikoa na Wilaya ni ufuatiliaji na usimamizi. Kazi ya Wizara ya Maji ni kubwa mno, kutunga sera, mikakati, sheria, kanuni, miongozo ya kitaalam, ufuatiliaji na tathimini. Miradi mikubwa inayohudumia wilaya zaidi ya moja, vilevile miradi mikubwa mikubwa ambayo inahudumia Mikoa zaidi ya mmoja. Lakini kubwa zaidi wanafanya kazi kubwa sana ya kutafuta fedha za kutekelezea miradi hiyo yote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ushirikiano wetu ni mkubwa sana sana. Na changamoto katika kazi hizi kubwa huwa hazikosi. Kwa hiyo tunaendelea kutatua changamoto kwa ushirikiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningesema mengi lakini mengi namuachia mwenyewe Mheshimiwa kaka yangu atayazungumza yanayohusu mambo yote ya kitaalamu kuhusu miradi ya maji atazungumza. Naomba sana kuunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Mheshimiwa Jumaa Aweso ajiandae.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kushukuru kwa kunipa nafasi, lakini pia nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu na watendaji wote wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa kazi nzuri wanaoendelea kufanya. Pamoja na pongezi hizo niliona na mimi nisimame nitoe mchango wangu kidogo kwenye Wizara hii hususani pale ambapo mchango ya baadhi ya Wabunge wenzangu ilipojielekeza kwenye kujaribu kuangalia kipi ni kipaumbele muhimu zaidi kati ya kuwekeza kwenye kununua *bombardier*, ama kuwekeza kwenye kutoa huduma za maji kwa wananchi. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia sana katika muktadha wa maendeleo, unaweza ukapata changamoto kwamba kipi kianze na unaweza ukaingia kwenye mtego wa hadithi ya kuku na yai kwamba kipi kinaanza? Kuku ama yai ama yai ama kuku na matokeo yako unaweza kujikuta unashindwa kufanya uamuzi. Lakini kwa wale tulio pata bahati ya kusoma masomo ya kuweka vipaumbele (*priority setting*) na masomo ya usawa tunakubaliana kwamba cha msingi zaidi ni namna tu ya kuweka utaratibu wa kuweza kufikia malengo unayoyakusudia, na wale usiingie kwenye mtego wa kuamua kipi kianze kuku ama yai na vitu kama hivyo. Kwa hivyo, kweli hili la kwamba tunanunua *bombadier* ama tunawekeza kwenye maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwanza napenda nilihakikishie Bunge lako tukufu kwamba sekta ya maji ni katika sekta zinazopewa kipaumbele cha hali ya juu katika nchi yetu na kuna uwekezaji mkubwa unafanyika kwenye sekta hii na hata hili linadhibitika kwenye bajeti ya mwaka huu kuna zaidi ya bilioni mia sita tisini na saba zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maji hapa nchini. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ukisoma ukurasa wa saba wa kitabu cha Mheshimiwa Waziri utaona anaeleza kwamba malengo kwenye sera ni pamoja na kuwa asilimia 85 ya vijiji vya Tanzania vinapata maji safi na salama

kufikia mwaka 2020; na kwamba mpaka leo hii utekelezaji umeshavuka lengo la asilimia 85 ambapo utekelezaji umefikia asilimia 85.2. Japokuwa kuna mapungufu madogo madogo kwenye hiyo miradi, na kwamba katì ya utekelezaji huu wa kiwango hiki cha asilimia 85 ni asilimia 58.7 tu ndio ambao wanaweza kupata maji kutokana na miradi mbalimbali iliyotekelzeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachokiona hapa ni kwamba, zifanyike jithada za makusudi za kuongeza tija na ufanisi kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji, lakini si kwamba hakuna uwekezaji unaofanywa kwenye sekta ya maji na hivyo hatuwezi kufananisha uwekezaji kwenye ununuzi wa *bombardier against* ule wa kuwekeza kwenye huduma za maji hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo napenda kusema kwamba hakuna makosa yaliyofanyika kwenye kuwekeza kununua ndege za *bombardierna* ninampongeza Mheshimiwa Rais, kwa uamuzi huu mahususi wa kuamua kuifufua sekta ya Utalii kwa kuwekeza kwenye ununuzi wa *bombardier*. (*Makofii*)

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Taarifa Mheshimiwa Naibu Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther muda wetu umetutupa mkono sitaruhusu taarifa isipokuwa kuhusu utaratibu. Mheshimiwa Kigwangalla.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, anachangia huyo, hajibu hoja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa msiwe mnazungumza kitì kikishatoa maelekezo. Unasema anachangia hata asubuhi nilikataza taarifa wakati watu wanachangia. Kwa hiyo, ni jambo la kawaida, jambo ambalo kanuni hairuhusu mtu

kuendelea kuzungumza ni kuhusu utaratibu na si taarifa. Mheshimiwa Esther wewe ni Mbunge wa siku nyingi lazima ujue kanuni vizuri kuliko watu wengi humu ndani. Mheshimiwa Kigwangalla.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ninachopenda kumalizia kwenye mchango wangu ni kwamba Mheshimiwa Rais anapaswa apongezwe..

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Kuhusu Utaratibu Mheshimiwa Naibu Spika.

### **KUHUSU UTARATIBU**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kigwangalla; Mheshimiwa Esther, Kanuni!

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Kanuni ya 61(a) mchangiaji, anaongea taarifa Bungeni ambazo hazina ukweli. Wakati Waziri Mheshimiwa Hamisi Kigwangalla akichangia anajaribu kusema kwamba fedha kwenye maji zinazotengwa bilioni 690 amesema kwamba zote zinaenda kwenye utekelezaji wa miradi. Tulipokuwa tunaongea hapa kwenye *comparison* tume sema *bombardier* wamenunua kwa *cash in hand*, bila kutoa kipaumbele kwenye maji ambayo tumetenga *billions of money* lakini haziendi. Kwa hiyo taarifa anazotoa ni za uongo. asilipotoshe Bunge na Watanzania. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Esther Matiko anatujulisha kwamba Mheshimiwa Kigwangalla anavunja Kanuni ya 64(1)(a) kwamba anazungumza uongozo Bungeni. Waheshimiwa Wabunge Kanuni ya 63 inazungumzia kutokusema uongo Bungeni; na mtu anayepaswa kuonesha namna gani uongo unasemwa Bungeni ni yule anayeanzisha taarifa hiyo. Kwenye mazingira yetu haya, Mheshimiwa Esther Matiko naomba ushike Kanuni zako, Kanuni ya 63 inataka wewe ulithibitishie Bunge hili uongo wa Mheshimiwa Kigwangalla. Kanuni ya 63 inakutaka Mheshimiwa Esther

Matiko ulithibitishé Bunge hili uongo wa Mheshimiwa Kigwangalla.

Waheshimiwa Wabunge, nitamruhusu Mheshimiwa Kigwangala amalizie mchango wake. Jambo hili kwa kuwa uthibitisho wake unahitaji nyaraka, nahitaji nyaraka kwa sababu mimi hapa ukiniambia wewe ndio uthibitishé, Mheshimiwa Esther Matiko nitahitaji nyaraka zinazoonesha Mheshimiwa Kigwangalla alichokisema ni cha uongo kwa hiyo utaniletéa. Mheshimiwa Kigwangalla endelea na mimi nitatoa *rulling* kwa mujibu wa Kanuni ya 63. (*Makofii*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ninachojaribu kusema ni kwamba napenda kutumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuamua kwa dhati kabisa na kwa pesa zetu wenyewe kulifufua Shirika la Ndege Tanzania (*ATCL*) kwa kuwekeza kwenye ununuzi wa ndege za *bombardier* na *dreamliner* na pengine na *airbus* ziko njani zinakuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyozungumza hapa, wenzetu wa Ethiopia wamenunuwa ndege kumi, wameweka *order* za *bombardier* kumi kwa ajili ya kuendelea kujitanua na kuboresha sekta yao ya utalii na sisi hatuwezi kubaki nyuma. Tanzania inaongoza kwa kushika nafsi ya pili kwa vivutio vyá maliasili duniani lakini bado hatujavitumia ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapungufu tuliyo nayo ni pamoja na kuwa na miundombinu mibovu, ni pamoja na kukosa *national career* ambayo ingeweza kusafirisha watalii kutoka kwenye nchi zao kuja hapa ndani, lakini pia kuwatoa hapa ndani kutoka kwenye kituo kimoja kwenda kituo kingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo jitihada za kufufua Shirika la Ndege la Taifa zinapaswa kuungwa mkono na sisi Wabunge ambaó ni wawakilishi wa wananchi. Hivyo nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa jitihada hizo, na sisi wa sekta ya utalii tunafurahia sana lakini tuna kereká sana

watu wanavyoitupia mawe idea hii ya Mheshimiwa Rais ya kuwekeza kwenye manunuzi ya *bombardier*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tunafarijika sana na jitihada zinazofanywa na wenzetu kwenye sekta nyengine kama sekta ya ujenzi, kwa kufungua barabara shirika la reli pamoja na kujenga viwanja vya ndege. Zote hizi zinaenda kutia chachu ya kukua kwa sekta ya utalii ambapo katika nchi hii...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** ...ipo katika sekta ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, kabla hatujaendela Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji nimepewa taarifa hapa kwamba taarifa iliyosomwa haijagawiwa kwa Wabunge. Kwa hiyo, kwa mujibu wa Kanuni zetu naomba taarifa hiyo igawiwe wakati tunaendelea hapa kabla ya Kikao cha Bunge hakijaahirishwa. Upande wa Serikali Mheshimiwa *Chief Whip* simuoni Waziri hapa lakini nadhani unaweza kutusaidia kufatilia hilo.

Waheshimiwa Wabunge tutaendelea Dkt Philip Mpango atafuatiwa na Mheshimiwa Jumaa Aweso.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Na mimi nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yote ya wataalam kwa kazi nzuri wanayoendelea kulifanyia Taifa hili. Nianze kwa kusema naunga mkono hoja. Napenda kuchangia kwa kujibu hoja chache, moja ikiwa ni ile ambayo ilikuwa ina sema ziko wapi fedha za India, ule

mkopo nafuu wa dola milioni 500 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji katika miji 17.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi zilichelewa kupatikana kwa kuwa Serikali ya India iliendelea kusisitiza kwamba matumizi ya fedha hizi lazima zisamehewe kodi zote, za aina zote wala tozo zinazohusika. Na sisi kwa upande wetu kuititia Mamlaka ya Mapato Tanzania tulisisitiza kwamba kodi stahiki zilipwe kwa mujibu wa sheria na hususan Kodi ya Mapato. Mtakumbuka mwezi Septemba, 2017 Bunge hili lilitanya marekebisho ya Sheria ya VAT ambapo liliimpa mamlaka Waziri wa Fedha kusamehe VAT kwa miradi ambayo inagharamiwa kwa mikopo nafuu na ile ambayo inagharamiwa na wafadhiri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hili tukalimaliza, nillishauriwa ipasavyo na nikasamehe VAT, lakini zikabaki kodi za mapato, kwa mujibu ya Sheria ya Mapato iliyofanyiwa marekebisho mwaka jana ninaweza tu kusamehe pale tu ambapo nitakuwa nimepata ridhaa ya Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tumefanya hivi na tarehe 15 Aprili Serikali iliridhia kusamehe kodi za mapato. Kwa kifupi kuna *withholding tax on interest* kwa *Exim Bank* kwa kiwango cha asilimia 10 ambazo ni takribani shilingi bilioni 24.9. Pia kulikuwa na kodi ya mapato kwa makampuni na wafanyakazi. Kodi ya Mapato peke yake ni takribani dola milioni 30 na kwa wafanyakazi dola milioni 15. Lakini pia kulikuwa na *withholding tax on commitment fees* kwa *Exim Bank* ambazo imebidi tusamehe, takriban dola 375,000 na tano elfu. Pia zipo kodi zingine *SDL* na ushuru wa forodha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema tarehe 15 Aprili Serikali iliridhia kusamehe pia hizi kodi za mapato, na naomba kulialifu Bunge lako tukufu saa 11 na dakika 27 nimeletewa taarifa na naomba niisome inasema hivi; “*Kindly Lebam formed that we have successfully concluded the negotiations with Exim Bank of India, we will sign the agreement tomorrow morning In Shaa Allah.*” (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni taarifa ambayo nimeletewa na kiongozi wa *Government Negotiations Team* ambayo iko India kwa ajili ya kumaliza zoezi hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulisemea kidogo ni lile ambalo limesemwa kwa hisia sana na lilishatolewa azimio na Bunge lako tukufu kwamba Serikali iongeze tozo ya mafuta kutoka shilingi 50 mpaka shilingi 100 kwa lita na hizo zilizokusanywa zipelekwe kutunisha mfuko wa maji na hususani miradi ya maji vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu niseme kwamba Serikali kupitia kikosi kazi cha maboresho ya kodi, inakamilisha uchambuzi wa faida na hasara ya utekelezaji wa agizo hili na tutalitolea taarifa kwa umma na kwa Bunge hili kupitia hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali na uchambuzi ambaao tunafanya unahusu mambo mengi.

Kwanza ni pamoja na faida za hatua inayopendekezwa. Lakini pia tunatazama *risks* zake na ukubwa wake kwa uchumi wa taifa na hili ni muhimu lakini pia kungalia madhara yake na hasa kwa Watu wanyonge wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo linafanyika katika uchambuzi huu ni kuangalia vyanzo vingine vya ku-*finance* maji. Kwa hiyo, ukiaccha huu mkopo wa india ambaao nimeshausema, lakini tunaangalia pia mikopo mingine nafuu, na hususani mkopo wa dola milioni 300 ambaao tunautaraji kutoka Benki ya Dunia. (*Makof*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpango muda wako umeisha sekunde 30 malizia habari ya mpango wa kukopa milioni 300.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana naunga mkono hoja. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jumaa Aweso dakika 15.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nafasi ya kutoa hoja wakati mjadala ukiendelea.

**NAIBU SPIKA:** Kanuni gani Mheshimiwa Mnyika?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika nimesimama kwa kwa mujibu ya Kanuni ya 69(1) inayosema kwamba Mbunge anayependa mjadala unaoendelea juu ya hoja yoyote uahirishwe hadi wakati wa baadae anaweza kutoa hoja hiyo kwamba mjadala sasa uahirishwe na atataja mjadala huo hadi wakati gani na pia atalazimika kutoa sababu kwa nini anataka mjadala uailishwe.

Kwa hiyo, naomba nipewe nafasi sasa yakuweza kutoa hiyo hoja, nipewe nafasi ya kueleza hizo sababu kwa nini nataka mjadala usiendelee katika hatua inayofuata na niweze kutoa vilevile sababu mjadala endelee mpaka...

**NAIBU SPIKA:** Umeshamaliza kifungu kinachokuhusu.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Sijatoa hoja bado.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, ngoja kaa kwanza, nikusomee vizuri kanuni.

Mheshimiwa Mnyika naomba ukae nimesimama.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 69(1) inasema alichokisema Mheshimiwa Mnyika na fasili ya pili, kwa ajili yetu sote nitaisoma, inasema hivi; "kama Spika atakuwa na maoni kwamba kuwasilishwa hoja hiyo ni kinyume na uendeshaji bora wa shughuli za Bunge atakataa kuitoa ili iamuliwa. Vinginevyo papo hapo atawahoji Wabunge juu ya hoja hiyo kadri atakavyoona inafaa." (*Makofi*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

Waheshimiwa Wabunge tusikilizane, Mheshimiwa Mnyika nimesimama huwezi kusimama nikiwa mimi nimesimama tafadhalii! Huwezi kusimama mimi nikiwa nimesimama, tafadhalii! Tafadhalii!

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 69(1) inamruhusu Mbunge kufanya kama alichofanya Mheshimiwa Mnyika kabla sijasimama. Lakini mimi ndiye ninayeruhusiwa kikanuni kumruhusu Mnyika atoe hoja yake ama asitoe. Sasa...

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ni tafsiri mbaya ya kanuni nataka kwanza kueleza sababu, kueleza tarehe na wewe ndiyo ufanye maamuzi.

**NAIBU SPIKA:** Sasa Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mnyika kaa chini.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kwa hiyo kwanza unipe nafasi ya kueleza sababu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika kaa chini, Mheshimiwa Mnyika kaa chini, Mheshimiwa Mnyika kaa chini nimesimama.

Haya basi kwa sababu Waheshimiwa Wabunge hamtaki kusikiliza ninachokisema, kwa hivyo, kwa sababu mimi ndiye ninaendesha kikao hiki tutaendelea. Mheshimiwa Aweso.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aweso endelea.

**MGE. PAULINE P. GEKUL:** Ingesemwa hoja tungeisikia kwanza hiyo hoja yake.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kusimama hapa mbele. Nitumie nafasi hii

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Dawa zimeisha huyo, dawa zimeisha.

**NAIBU SPIKA.** Waheshimiwa Wabunge, muwe na adabu kwa Kiti kidogo, kwa sababu mimi nimesimama ili niwape utaratibu hamtaki kuusikia. Mheshimiwa Aweso endelea.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii lakini la pili nimshukuru sana Rais wangu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuniamini. Kwa kuniamini mimi maana yake ametuamini sisi vijana tuweze kumsaidia. Nataka nimuhakikishie Rais wangu Dkt. John Pombe Magufuli...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika naomba utoke nje, Mheshimiwa Mnyika naomba utoke nje.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Dawa zimeisha huyo! Dawa zimeisha!

*(Hapa baadhi Wabunge walizungumza bila kufuata  
utaratibu)*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Dawa zimeisha hiso, dawa zimeisha.

*(Hapa Mhe. John J. Mnyika alitoka ndani ya Ukumbi wa  
Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aweso endelea.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie nikushukuru sana kunipa nafasi hii kusimama hapa mbele...

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Tajiri hakosi baunsa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aweso naomba uendelee.

Waheshimiwa Wabunge, nina masikio mawili tu sina masikio zaidi ya mawili. Mheshimiwa Aweso naomba uendelee.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, lakini nitumie nafasi hii kumshukuru sana Rais wangu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuniamini kwamba kama kijana naweza kumsaidia katika Wizara hii Maji. (*Makof!*)

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko naomba ukae chini Mheshimiwa Aweso amesimama na wewe unazijua Kanuni. Mheshimiwa Aweso amesimama. Mheshimiwa Aweso naomba uendelee.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Rais wangu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuniamini kama kijana niweze kumsaidia katika Wizara hii ya Maji. Nataka nimuakinishe Rais wangu Dkt. John Pombe Magufuli kama kijana na kwa niaba ya vijana wengine wote na Waheshimiwa Wabunge sitokuwa kikwazo... (*Makof!*)

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, siruhusu mtu yejote kusimama Mheshimiwa Gekul naomba ukae chini Naibu Waziri amesimama hapa. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** ...nataka nimuhakikishie Rais wangu Dkt. John Pombe Magufuli kwa niaba ya vijana wenzangu na Waheshimiwa Wabunge sitokuwa kikwazo katika kuhakikisha Watanzania wanapata maji safi, salama na yenye kuwatoshaleza. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii pia kumshukuru sana Makamu wa Rais na Waziri Mkuu kwa ushirikiano wanaoutupa Wizara yetu ya Maji. Kwa namna ya kipekee nimshukuru mzee wangu Isack Kamwelwe kwa ushirikiano anaotupa sisi vijana katika wizara ile, nataka nimwambie waziri wangu ni Waziri jembe, na mimi kama kijana nitahakikisha namsaidia Waziri wangu katika kuhakikisha mipango mizuri inatekelezeka ili Watanzania wapate maji safi na salama na yenye kuwatoshaleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Katibu wangu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Maji. Tumejjipanga na tuna nia ya dhati katika kuhakikisha tunaenda kumtua mwana mama ndoo kichwani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sikumshukuru mama yangu mzazi, leo nipo naye kwa mafundisho aliyonifundisha mimi pamoja na mzee wangu kufariki na shughuli zake ndogo ndogo za biashara ya mama ntilie, lakini kwa kuamua kunisomesha leo nimesimama hapa kama Naibu Waziri wa Maji na Mkemia. Mama yangu ahsante sana na Mwenyezi Mungu anasema unapaswa kushukuru kwa kila jambo, ahsanteni sana mwenyezi mungu awabariki sana. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mchache niliokuwa nao naomba sasa nifafanue baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge kwa michango mizuri waliowasilisha katika Wizara yetu, ni michango yenye afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia maji ni rasilimali muhimu na maji hayana itikadi, hayana rangi, hayana dini na wala maji hayana mbadala, si kama wali ukikosa wali utakula ugali au utakula makande. Ukikosa maji tunaingia kwenye matatizo makubwa, hasa katika maradhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii sasa kujielekeza kujibu maswali na hoja za Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ilielekezwa katika Wizara yetu ni kuhusu miradi 17 ya Serikali ya India. Nilivyoingia katika Bunge hili ziliikuwa zinakuja hoja za miradi 17 mwili ulinisisimka, mwili ulinitetemeka, kwamba naenda kujibu nini; lakini Mheshimiwa Mpango leo nisimame kwa ujasiri umetuvisa nguo sisi Wizara ya Maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi kumshukuru Rais wangu Dkt. John Pombe Magufuli kwa jitihada kubwa sana alizozifanya. Sisi kama Wizara ya Maji tunachokisema fedha zile zitakazotoka kwa miradi 17 ya India tutazifatilia shilingi kwa shilingi kuhalikisha kwamba Watanzania wanapata maji safi, salama na yenye kuwatoshaleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili hatutamuonea haya mtu kwa sababu wakati mwingine fedha za Serikali zinaliwa kwa sababu ya kuoneana haya au kupeana kazi kiujomba ujomba au kiushemeji shemeji. Kwenye hili hatutakuwa na haya na mkandarasi ambaye atapewa, hata awe mtoto wa kigogo. Kama ye ye atakuwa mtoto wa kigogo anatekeleza mradi lakini hana uwezo tunamcharanga ili aweze kuwa kuni akawaahida, wananchi waweze kupata maji safi, salama na yenye kuwatoshaleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyiningine imezungumzwa na Mama yangu Anna Lupembe kuhusu mradi wa *Ikolongo One* pamoja na *Ikolongo Two* kwamba maji hayatoshelezi kwa kuwa miundombinu ni mibovu, hivyo maji hayawafikii wananchi kwa makanyagio na majengo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafanya jitihada kubwa kuhakikisha Mji wa Mpanda unapata huduma ya uhakika ya maji kwa kutekeleza miradi mbalimbali. Kwanza kuna mradi wa Kanonge uliopangwa kujengwa kwa awamu mbili; awamu ya kwanza imekalimika na utekelezaji awamu ya pili unaendelea. Mradi huu ukikamilika utazalisha maji lita za ujazo 1,200,000 kwa siku. Aidha, ujenzi wa maji kutoka *Ikolongo Two* utaanza mwezi Julai, 2018. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumepokea hoja kutoka kwa dada yangu Esther Bulaya kuhusu *DAWASCO* kwamba ilishauliwa kununua kifaa cha kupunguza upotevu wa maji agizo hili halijatekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumjibu dada yangu Esther Bulaya kuwa vifaa vya kutambua uvujaji chini ya ardhi yaani *liquid detector* viro. Vifaa hivyo vilinunuliwa wakati wa mradi wa kupunguza upotevu wa maji Jijini Dar es Salam.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine napenda kujibu hoja ya Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota kuhusu mradi wa Maji Makonde kwamba umechakaa na hivyo kuhitaji ukarabati mkubwa. Nataka nimwambie Mheshimiwa ndugu yangu Chikota ukiona giza linatanda ujue kunakucha. Pamoja na changamoto ambazo wamezipata wananchi wake lakini Mheshimiwa Mpango sasa ameshatupangia mambo yetu yapo vizuri, tunaenda kutekeleza mradi ule ili wananchi waweze kupata maji safi, salama na yenye kuwatoshaleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine inahusu Mheshimiwa Mbunge Maftaha Abdallah Nachuma, amezungumzia mradi wa maji kutoka Mto Ruvuma hadi Mtwara Mjini unaopita vijiji 26 vya Mtwara Vijijini kwamba haujatekelezwa kwa miaka mitatu sasa na wananchi wameshachukuliwa maeneo yao lakini fidia haijalipwa. Nataka nimjibu Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliandaa mradi wa maji kutoka Mto Ruvuma hadi Mtwara Mjini na kuititia vijiji 26 vilivyopo Mtwara Vijijini. Tayari usanifu wa mradi umekamilika na taratibu za kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi zinaendelea ikiwemo kufanya majadiliano na *Exim Bank* ya China. Tathmini ya maeneo ya mradi yalishafanyika kwa ajili ya kulipa fidia, lakini wananchi bado hawajaondolewa katika maeneo yao. Kabla ya utekelezaji wa mradi huo kwanza waanchi watalipwa fidia zao. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge sisi kama Wizara hatutakuwa kikwazo katika

kuhakikisha wananchi wako wanalipwa fidia na mradi ule uweze kutekelezeka kwa wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni ya dada yangu Lucy Owenya, kuhusu ujenzi wa mradi wa maji katika Jimbo la Moshi Vijijini Kata ya Mbokomu kwamba umejengwa chini ya kiwango na kusababisha mradi huu usifanye kazi. Mradi huu ulikuwa chini ya Halmashauri ya Moshi Vijijini ambaao uko chini ya TAMISEMI. Baada ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kupata malalamiko haya, imemuagiza Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Moshi Mjini kwa kushirikiana na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Moshi Vijijini kwenda kuangalia tatizo na kuandaa gharama za ukarabati wa chanzo hicho ambacho kitawezesha wananchi wa Kata ya Mbokomu kupata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine imetolewa na kaka yangu Mheshimiwa Ahmed Shabiby kuhusu mradi wa maji kwa mji wa Gairo kwamba ni muda mrefu ambapo mkandarasi amelipwa asilimia 80 lakini mradi huo hautoi maji. Ni kwei mradi wa maji Gairo umechukua muda mrefu kukamilika. Mradi ulianza kutekelezwa tangu tarehe 22 Agosti, 2010 na umetekelezwa kwa asilimia 87 ambapo hadi sasa mkandarasi amelipwa kiasi cha shilingi bilioni 3.844; dola za Kimarekani 1,071,525 ambazo kwa ujumla ni sawa na asilimia 64 ya gharama za mradi mzima ambazo ni shilingi 5,315,612,551 na dola za Kimarekani 1,919,763.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi haujaanza kutoa maji kwa kuwa unahitaji kufungw amtambo wa kuchuja chumvi yaani *reverse osmosis plant* kwa kuwa visima vilivyochimbwa maji yake yalioneckana kuwa na chumvi zaidi ya viwango vilivyokubalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuonekana mkandarasi ameshindwa kuagiza na kufunga mtambo huo kwa wakati, Serikali iliama kumnyang'anya kipengele cha uagizaji na ufungaji wa mtambo wa kuchuja chumvi pamoja na *pump*. Tangazo la kumpata mzabuni kwa ajili ya kazi hizo lilitangazwa tarehe 3 Mei, 2018 ambapo ufunguzi wa zabuni

unatarajiwa kufanyika tarehe 5 Juni, 2018. Mradi huu unategemewa kukamilika na kuanza kufanya kazi mwishoni mwa mwezi Novembba, 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kujibu hoja ya Mheshimiwa Zainab Mndolwa Amir kuhusu kwamba Serikali itoe elimu ya kutosha kwa wananchi kuhusu utunzaji wa vyanzo vya maji mfano katika Milima uya Uluguru Morogoro. Ushauri wake umezingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia napenda kujibu hoja ya Mheshimiwa Mbunge wa Songea kuhusu suala la wananchi wake kuweza kulipwa fidia. Nataka nimhakikishie Mzee wangu Ndumbaro akae sasa mkao wa kula. Katika bajeti hii ya mwaka 2018/2019 tutawalipa wananchi wale fidia kiasi cha shilingi bilioni sita. Kwa hiyo, jukumu sasa la Mheshimiwa Mbunge kuwasimamia wananchi wale badala ya fedha zile kwenda kuoa, sasa wazitumie katika mipango ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu hoja ya Mheshimiwa Elibariki Emmanuel Kingu kwamba Bwawa la Kidunda lijengwe. Wizara ipo katika hatua za mwisho za mazungumzo na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) ili kupata fedha za utekelezaji wa mradi huu muhimu. Matarajio ni kufikia makubaliano haya ya mwezi Juni, 2018 ili zabuni za kumtafuta mkandarasi wa ujenzi ziweze kutangazwa mwezi Julai, 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu hoja ya Mbunge wa Kasulu Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko kuhusu dola za Kimarekani milioni 500, kuna *phase one, logic* yake ni nini, kwa nini isiwe sambamba kwamba miradi yote ifanyike kwa wakati mmoja. Napenda kujibu hoja hii kwamba mradi wa miji 17 wa dola za Kimarekani kwa maana ya milioni 15 utekelezwa kwa awamu mbili yaani *phase one* na *phase two*. Awamu ya kwanza itahusisha usanifu wa miradi katika miji yote 17 na awamu ya pili itahusisha ujenzi wa miradi husika hivyo mradi yote inategemewa kukamilika bada ya miaka minne.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu hoja ya Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Mrisho Kikwete kuhusu usimamizi wa mradi wa Chalinze uangaliwe kwa makini. Serikali imekuwa ikisimamia mradi wa Chalinze kwa makini kwa kuweka wahandisi maalum kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wa kila siku. Hatua mbalimbali za kimkataba zimekuwa zikichukuliwa kwa mkandarasi kila aliposhindwa kutekeleza matakwa ya mkataba ikiwa ni pamoja na kutoa onyo na kumkata fedha. Hata hivyo, ilipofika tarehe 22 Februari, 2018 Serikali ililazimika kumsimamisha kazi mkandarasi kwa mujibu wa mkataba baada ya kusindwa kutekeleza makubaliano yaliyopo ndani ya mradi. Hivi sasa Serikali inashauriana na mfadhibili wa Benki ya Exim ya India jinsi ya kumaliza kazi zilizobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu hoja ya Mheshimiwa Mary Pius Chatanda wa Korogwe, kwanza anatoa shukrani kwa kupelekewa na Wizara kiasi cha shilingi milioni 500. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba shukrani zake tumezipokea na sisi kama Wizara tutaendelea kumpa ushirikiano ili wananchi wake wa Korogwe waweze kupata maji safi na itakapofika mwaka 2020 waende kumchagua kwa mara nyiningine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu hoja ya Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali, Mbunge wa Mchinga kuhusu kuchanganya kwa takwimu za maji. Mfano Dar es Salaam takwimu zinaonesha wakazi wengi wanapata maji lakini maji hayajafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zilizotolewa ni za ujumla, wananchi wanapata maji ya uhakika ni wale walioko katika maeneo yanayopata maji kutoka Ruvu Juu na Ruvu Chini. Ni kweli kuna maeneo ambayo hayapati maji ya bomba kwa sababu yako mbali na mfumo wa Ruvu Juu na Ruvu Chini au mtandao wa bomba haupo. Maeneo haya ni pamoja na Mbagala, Kongowe, Kigamboni, Chamazi, Chanika, Msongola, Kitunda, Yombo Vituka, Pugu, Gongolamboto na Kinyerezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya 2018/2019 Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuongeza mtandao wa mabomba ili kufikisha maji kwa wananchi wengi zaidi. Pamoja na changamoto katika Wizara yetu ya Maji, Mwenyezi Mungu anasema; "Waama bii neemati rabikka fahadith" (zielezeeni neema za Mwenyezi Mungu kwa kushukuru). Nataka nimwambie kaka yangu Mnyika, moja ya hoja yake alikuwa akilalamika kuhusu eneo lake la Kibamba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimwambie Mheshimiwa Mnyika, kazi kubwa sana imefanywa na Wizara hii ya Maji. Kulikuwa na kilio kikubwa sana Dar es Salaam lakini kumekuwa na utekelezaji wa kupanua Ruvu Juu na Ruvu Chini katika kuhakikisha wanaongeza lita kutoka lita 300 mpaka lita 504, Mwenyezi Mungu atupe nini? Atupe donda tufukuze nzii? Zipo changamoto lakini tunachotaka tunaomba ushirikiano ili zile kata zake sita sasa ambazo hazina maji twende kuwapatia maji na hii ni kazi nzuri yote inayofanywa na Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukizaa mtoto anafanya vizuri, jukumu lako ni kumuombea dua. Rais wetu anafanya vizuri Waheshimiwa Wabunge, jukumu letu ni kuhakikisha tunampa ushirikiano wa dhati na sisi wasaidizi wake tutafanya kila linalowezekana ili wananchi tuweze kuwapatia maji safi, salama na yenye kuwatoshaleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu hoja ya Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, kaka yangu kuhusu upungufu wa wataalam katika sekta ya maji na hatua zinazochukuliwa na Wizara kukabiliana na upungufu huo. Ni kweli kuna upungufu wa wataalam katika sekta ya maji hapa nchini, hali ambayo imesababisha baadhi ya mamlaka za Serikali za Mitaa kushindwa kusimamia miradi yake. Wizara imechukua hatua zifuatazo:-

Moja katika mwaka 2017/2018 Wizara ilipata kibali cha kuajiri watumishi 154 wa sekta ya maji ambapo hadi mwezi Mei, 2018 wataalam 106 walipangwi vituo vyaya kazi.

Kati ya wataalam hao 37 walipangiwa ofisi za mikoa na Halmashauri za Wilaya na 76 walipangiwa katika Bodi za Maji za Mabonde, Miradi ya Kitaifa na Mamlaka za Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa iliyopo kwenye eneo hili ni kwamba sekta inaendelea kukua, lakini pia kuna upungufu wa wataalam unaotokana na vifo, kustaafu, kuacha kazi na kufukuzwa kazi kutokana na sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu hoja ya kaka yangu Mheshimiwa Dunstan Kitandula kuhusu Makao ya Wilaya ya Mkinga kwamba hakuna maji. Serikali inaendelea kuhakikisha kuwa wananchi wote wanapata huduma bora ya majisafi na salama ikiwa ni pamoja na wananchi waishio katika Makao Makuu ya Wilaya...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aweso, muda wako umekwisha. Dakika mbili malizia.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie tena kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, sisi kama Wizara ya Maji na nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wangu wa Maji nilivyoteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Maji aliniambia nипите maeneo mbalimbali kuangalia hali na utekelezaji wa miradi ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na ninyi, hali ilikuwa hairidhishi. Ipo miradi ambayo imekamilika lakini haitoi maji, hakuna sababu ya kulalamika. Mheshimiwa Waziri amechukua hatua sasa ya kuunda RUWA ili twende kuisimamia ili wananchi waweze kupata maji safi, salama na yenye kuwatoshleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina maneno mengi sana. kikubwa tunachoomba Waheshimiwa Wabunge ni

ushirikiano, na sisi kama viongozi wa Wizara, tutafanya kazi kwa moyo na michango yenu leo mliyoitoa imetupa ari na moyo katika kuhakikisha tunafanya kazi hizi ili wananchi wetu waweze kupata maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, mtua hoja.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia siku zote tatu tangu tarehe 7 hadi leo tarehe 9 Mei, 2018 ametujalia afya njema na kuendelea kujadili bajeti yetu ya maji na umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kulishukuru Bunge lako tukufu kwa kujadili hoja ya hotuba ya Wizara yangu niliyoiwasilisha hapa Bungeni tarehe 7 mwezi Mei, 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hizi zimechangiwa na Wabunge 145, ninawashukuru sana. Napenda kiliarifu Bunge lako kuwa Wizara yangu imechukua na itafanya kazi ushauri na mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge pamoja na Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ili kuleta matokeo yanayotarajiwa kwa wananchi wote wa nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo kutokana na muda mfupi nilionao ninaahidi hoja zote tutazijibu kwa wananchi na kuwasilisha kwenu kupitia kwenye *Hansard*, na ninawaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba kabla hatujamaliza Bunge tarehe 29 Juni, 2018 Mwenyezi Mungu akitujaalia salama, basi majibu ya hoja zote mtakuwa mmeshayapata. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Wakati na mimi naanza

ubunge, naingia kwenye Bunge lako tukufu nilikutana na hoja ya dola milioni mia tano kutoka Serikali ya India lakini namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwamba nikiwa sasa kama Waziri wa Maji na Umwagiliaji hoja hii sasa imekamilika. Taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kama ulivyoona wewe mwenyewe Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wote watakaoguswa na mradi huu wamefurahi. Kwa maana ya fedha hizi kwenda kugusa kwenye hii miji 17, basi zile fedha ambazo ilikuwa tuzipeleke tumege kwenye fungu hili tulilotenga kwa fedha za ndani kupeleka maeneo yale zitakuwa zimeokolewa na zinaweza zikapelekwa maeneo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisome tu maeneo yatakayofaidika na hizi dola milioni 500 ambazo mkataba wetu wa kifedha utasainiwa kesho, ni pamoja na Muheza, Wanging'ombe, Makambako, Kayanga, Songea, Zanzibar, Korogwe, Njombe, Mugumu, Kilwa Masoko, Geita, Chunya, Makonde, Manyoni, Sikonge, Kasulu na Rujewa. Kwa hiyo, utaona fedha hizi itakapokuwa tumeanza kazi zitanufaisha wananchi wengi sana wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe taarifa tu kwamba hiyo Kamati iliyoko India, pia illichukua watumishi watatu wa Wizara yangu ya Maji na Umwagiliaji. Wakitoka huko watakuwa wameshakamilisha na mpango wote wa manunuvi. Kama unavyofahamu Wizara yangu na jinsi ninavyoipeleka, wakishasaini mkataba huo basi mimi mara moja kazi inaanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya majibu ya hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji; Serikali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo, inatekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ambayo ilianza mwaka wa fedha 2006/2007 na itakamilika ifikapo mwaka 2025. Utekelezaji wa programu hii unahuishisha programu

ndogo tano ambazo ni usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji, huduma ya maji vijijini, huduma ya maji mijini, usafi wa mazingira mijini, kampeni ya kitaifa ya usafi wa mazingira na kujenga uwezo wa kitaasisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya kwanza ya programu hii ililenga kujenga miradi 1,810 na hadi sasa tumeshatekeleza miradi 1,469 ambayo imekamilika. Miundombinu ya maji iliyojengwa ina vituo vya kuchotea maji 102,586 ambavyo vina uwezo wa kuhudumia jumla ya wananchi 30,972,000 sawa na asilimia 85.2 iwapo kama vituo vyote vilivyojengwa vingekuwa vinatoa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vituo 86,877 tu ndivyo vinatoa maji, vituo vilivyobaki havitoi maji. Hivi ndivyo ambavyo vimeshusha asilimia ambayo tungetarajia kipata sasa hivi. Tungetarajia kuwa na asilimia 85.2; lakini tuna asilimia 58 hadi 59.76. Sababu mbalimbali zipo ambazo zimefanya hivi vituo ambavyo vimeshajengwa kwa fedha hizi ambazo tulichangiwa na wahisani mbalimbai pamoja na fedha za ndani zimekuwa hazitoi maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa michango yenu Waheshimiwa Wabunge nimewasikiliza kwa umakini sana, ni kweli kwa Mheshimiwa Mbunge ambaye tumeenda kutekeleza mradi kwenye eneo lake na aliwaambia wananchi sasa mmeona nimeleta fedha, halafu leo hii yale maji hayatoki, kuna uwezekano mkubwa lile Jimbo ukaanza kulikimbia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewasikiliza kwa makini sana Waheshimiwa Wabunge, na hasa kwa kuzingatia na mimi kwa sababu nasafiri kila eneo, sababu zote ambazo mmezitoa, mmetoa sababu nyngi kwamba hela inaliwa, uadilifu hakuna, hela inagawanywa, inapelekwa kule kwenye Halmashauri halafu inarudishwa Wizarani, siwezi kuwakatalia hilo kwa sababu hapa ushahidi upo kwamba tumetekeleza miradi, lakini kuna miradi mingine ambayo haitoi maji. Waheshimiwa Wabunge, niwape taarifa tu kwamba suala hili nilishaanza kulifanyia kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Rais huyu mimi huwa nawaambia watumishi kwamba ukitaka kutekeleza kazi vizuri tekeleza kwa Rais huyu, kwa sababu Mheshimiwa Rais yeye anapenda kazi, hana majungu, hana maneno na mimi kwa sababu ninamfahamu nilikuwa nimeshajiandaa. Mheshimiwa Naibu Waziri Kakunda amezungumza kwamba utaratibu wa utekelezaji wa miradi ya maji, Wizara yangu kazi yake ni kupanga bajeti, kutoa miongozo na maelekezo lakini utekelezaji unafanyw ana Wizara kutoa miongozo na maelekezo, lakini utekelezaji unafanywa na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nimeshaifanyia kazi Ntomoko muda wote, kwa hiyo, pale Mheshimiwa Rais alivyosema Mheshimiwa Waziri najua unanisikia hawa watu wa watomokoe, saa 24 nilikuwa nimeshawatomokoa tayari kwa sababu nilielekezwa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu alienda Mara katika ziara yake akaniagiza kwamba fanya uchunguzi miradi yote ya Mkoa wa Mara na hata katika michango hii Waheshimiwa Wabunge wamelalamikia miradi iliyotekelizwa Mara. Natarajia ripoti ile imerudi na Mheshimiwa Waziri Mkuu nitamkabidhi ripoti hii Ijumaa. Waheshimiwa Wabunge lakini niseme tu kwamba yale maeneo yote tuliyotarajiwa kwamba tume pigwa wakandarasi wame-surrender wao wenyewe kwa barua kwamba, miradi hii wanaachana nayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana nasema jamani tuna kiongozi mzuri, Mheshimiwa Rais kwa sababu anatenda haki. Hata yule ambaye alizowea tabia fulani sasa anaanza kukimbia mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema kwa ufanyakazi wangu a ndani ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji nasema hili ni somo, kama yule ambaye ulikuwa unashirikiananae yeye mwenyewe ameanza kushtuka hivi wewe bado unabaki kuwa na akili hiyo? Itakuwa ni kitu cha ajabu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge tumekwenda mpaka kwenye Mradi wa Mugumu tumeufanya kazi. Tumegundua matatizo yote yaliyojitekeza, lakini ule hatuwezi kuusimamisha, tunatoa kibali mkandarasi aendelee na kazi ili mradi ule ukamilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo sababu mbalimbali ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge, lakini pia, na Wizara yangu kuna sababu mbalimbali ambazo wameniambia. Hivi vituo vilivyojengwa vikatumia hela nyngi vimeshindwa kutoa maji, moja ya sababu ni kukauka kwa vyanzo vya maji. Hata hivyo kama Wizara tunajiandaa kuhakikisha tunatunza rasilimali zote za maji, tunazuwia kuvamiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nikushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri katika hotuba yako umezungumza kwamba, hata pale Songea sasa tunakwenda kulipa fidia. Tumeshajandaa na tumetenga bajeti, Waheshimiwa Wabunge tunahitaji shilingi bilioni 18 ili tuweze kulipa yale maeneo yote makubwa, maeneo oevu ili yasiweze kuingiliwa na shughuli za kibinadamu. Tunayawekea sheria na tutawekea utaratibu na wale watakaokuwa wanayalinda, ili tuhakikishe kwamba, tunatunza rasilimali za maji, maana vinginevyo kila wakati tutakuwa tunatekeleza miradi halafu miradi ile inakuwa haileti tija inakauka, kwa hiyo itakuwa tumetumia fedha miradi inakuwa haitoi maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, uchaguzi wa teknolojia. Umetekeleza mradi kijiji bila kupima uchumi wa eneo lile, unapeleka *generator* ya kutumia dizeli, wananchi wanafika mahali hawawezi. Vyombo vya watumiaji maji tunavyoviunda hivi bado hatujaviimarisha, lakini tunaendelea kuwafundisha ili wawe na uwezo wa kusimamia hii miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru sana TAMISEMI wanaendelea kuvisajili na kuvifundisha, na mimi kazi yangu ni kutoa fedha ili waendelee kutoa elimu kwa hivi vyombo vya watumiaji maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakiri, kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge, miradi mingi haikusanifiwa vizuri na ndio maana imetupeleka huko ilikotupeleka; tumepoteza fedha. Hata hivyo tayari mwaka huu nimeshaunda timu ya wahandisi ndani ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji na wanaanza kufanya kazi. Wahandisi hao watapitia usanifu wote wa kwenye halmashauri hata wataalam washauri watakaonunuliwa na Serikali kwa ajili ya miradi ya maji, wakishakamilisha wataalam hawa waandisi tutahakikisha kwamba, wanapitia zile nyaraka, ili tuweze kuokoa fedha, *value for money* lazima ipatikane.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kumekuwa na muingiliano ambao unatusumbua kama Serikali. Hapa panasimamiwa na taasisi hii, pengine TAMISEMI, huku wanasi mamia Wizara, huku anasimamia Mhandisi Mshauri ambaye ameajirisha na analipwa pesa, hawa watu wanatuchanganya, tunataka kutengeneza mfumo ambao utasimamiwa na mtu mmoja ili kama tunamlaumu tunamlaumu mtu mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupata hoja nyingi za ubadhirifu wa fedha kwenye miradi ya maji, katika huu muda wa siku tatu ilikuwa tukitoka hapa tunakwenda kukaa na Katibu Mkuu Profesa Kitila Mkumbo, namshukuru sana na tarehe saba tulivyomaliza hotuba hapa nilikwenda kukaa na wafadhili, kumbe na wafadhili nao lilikuwa linawauma, wameafiki kwamba kuna haja ya kuunda timu ya wataalam watakaopitia miradi yote iliyotekelizwa, kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge mnapendekeza. Mlipendekeza kwamba iingie Kamati ya Bunge, lakini kabla hamjafika hapo sisi tayari tumeshaunda kamati na kamati hii itasimiwa na Profesa Mbwete wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaendelea kujaza wataalam ili tuhakikishe kwamba miradi yote iliyotekelizwa katika programu hii iliyoanza mwaka 2006/2007 inapitiwa, na Waheshimiwa Wabunge tutatumia sheria, tutatumia nyenzo zote ambazo zimebekwa na Serikali. Mheshimiwa Rais

amesema jamani hela ya maji awamu hii ni sumu, kama kuna mtu alihujumu basi wakati wake umefika.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi ndugu zangu na kwa umri nilio nao kwa kweli sina huruma na mtu ambaye ni mwizi na niko hivyo hata huko nilikotoka. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yetu kwamba Kamati hii itafanya kazi kwa uadilifu, na nitaisimamia, na tunaendelea kuchagua watu ninawajua, waadilifu ninawajua wako wengi tu ambao tutawaweka pale. Kwa hiyo, ninachowaomba Waheshimiwa Wabunge, naomba sana watakapokuja kwenye Halmashauri zenu, kwenye maeneo yenu muwape *support* kubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakinia pia ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, sisi ni Madiwani. Baada ya bajeti hii kupita wanapokwenda kutenegeneza mipango kazi kwenye halmashauri na sisi tuwepo, ni muhimu sana hili. Kwa sababu, wakati mwingine napata shida nakwenda kwenye halmashauri nakwenda na Mheshimiwa Mbunge, tunafika kule wakati wanapanga mpango kazi kumbe hata sisi madiwani hatukuwepo, wote tunakuwa wageni, naomba tushirikiane.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nikija kwenye jimbo lako nataka nipate taarifa kutoka kwa wewe Mbunge, kwamba hapa kuna hili, ili niweze kufanya kazi kwa sababu na mimi ni mtaalam. Naomba sana Waheshimiwa Wabunge ushirikiano wenu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka kwenye bajeti ya mwaka jana niliwaambia Waheshimiwa Wabunge, ndiyo maana tunawapa hivi vitabu vyaa bajeti. Tukishakamilisha hii bajeti Waheshimiwa Wabunge na ninawaomba sana, muipitishe, ili tutekeleze miradi ya maji baada ya hapo mwambie Mkurugenzi wako wa Halmashauri una shilingi kambi katika mwaka ujao wa fedha ili aanze kujipanga. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi wameonesha kwamba, fedha hazijatengwa, akiwemo mama yangu Mheshimiwa Magdalena Sakaya, nitakuonesha hela yako iko wapi kwenye kitabu bila wasiwasi wowote. Una fedha ya kutosha imetengwa, hatuwezi kuacha Halmashauri ya Kaliua. Nchi hii Rais ni Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, ndio Rais wa Watanzania. Ni Rais ambaye ametokana na chama tawala, Chama cha Mapinduzi, kwa hiyo, wananchi wote hawana mtu mwingine atakayewahudumia ni Chama cha Mapinduzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge katika Bunge la mwaka jana walimuelekeza Waziri wa Maji na Umwagiliaji aangalie uwezekano wa kuunda Wakala wa Maji Vijiji. Ninaomba kutoa taarifa kwamba tumefanya kazi hiyo miliyotuelekeza, tumeshirikiana kati ya Wizara yangu, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Ofisi ya Rais, Utumishi na Wizara ya Fedha na Mipango, tayari tuliunda kamati imeanza kuangalia uwezekano wa kuunda taasisi hii muhimu sana ya Wakala wa Maji Vijiji. Tumesrafika hatua ya mbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, *strategic plan* tayari, *business plan* tayari imeshaandaliwa, *framework document* tayari imeshaandaliwa, *establishment order* nayo imeshaandaliwa tayari. Kwa hiyo, taratibu za kisheria zinaendelea, lakini pia sasa tunaingia kupata maoni ya wadau kwa mujibu wa taratibu na tunatumia sheria ya uanzishwaji wa wakala *Executive Agency Act, Cap. 245*. Tufafika *stage* ambayo tutaomba ridhaa ya mamlaka husika, ili uweze kuanzisha huu wakala. Kwa hiyo, yale milioelekeza Waheshimiwa Wabunge tayari tumeshaanza kuyafanyia kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Waheshimiwa Wabunge walipochangia sana hotuba hii, na nishukuru kwa kweli Waheshimiwa Wabunge wamechangia na mimi nimefuatilia sana. Kulikuwa na tofauti kubwa za kitakwimu kati ya kitabu kilichoandikwa na Wizara ya Maji, lakini pia na kitabu kilichotolewa na Hoja za Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna tofauti ya kitakwimu kuhusu fedha za maendeleo zilizopokelewa na Wizara kati ya Taarifa ya kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji na Taarifa iliyopo katika Hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019. Tofauti hiyo imetokana na muda wa kuwasilisha Taarifa hizo. Nirudie tena, tofauti hiyo imetokana na muda wa kuwasilisha taarifa hizo, hadi tunakutana na Kamati mwezi Machi, fedha zilizopokelewa kwa Fungu 49 zilikuwa sawa na asilimia 22 kama Taarifa ya Kamati ambavyo ilikuwa imeeekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunakamilisha maandalizi ya hotuba ya bajeti hadi tunakutana na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti mwezi Mei, 2018 Wizara ilishapokea fedha zaidi, hivyo tuliona ni muhimu kutoa taarifa hadi kipindi hicho kwa sababu Hazina tayari walishatuletea fedha nyingine. Taarifa illyowasillishwa katika Kamati mwezi Machi ilijumuisha fedha za nje zilizopokelewa kutoka hazina kwa njia ya *exchequer* pekee. Aidha, kuna fedha za wafadhili ambazo hupelekwa moja kwa moja katika miradi ya maendeleo kabla ya kuingizwa kwenye *exchequer*.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi zinapelekwa kwenye miradi mbalimbali baada ya utekelezaji ambapo badaye baada ya mwaka Hazina huwa wanaziingiza kwenye *exchequer*. Lakini kwa sababu tulikuwa tunaendelea kukusanya taarifa baada ya kupata taarifa hizo tulilazimika kuingiza hizo fedha na baadae kuwasilisha kwenye Kamati ya Bajeti. Baada ya kuziingiza sasa tukawa tumepata, sasa fedha ambazo tulikuwa tumezipata hadi mwezi Mei ni shilingi bilioni 359.9 ambayo inafanya sasa fedha ambazo zimetolewa na Serikali hadi kufikia mwezi Mei ni asilimia 56. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge hiyo ndio tofauti ambayo tumeiona kati ya Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge na taarifa ambayo tumeitoa mwishoni kwa sababu ilibidi tukiri fedha ambazo tayari tumeshapewa na Waziri wa Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuishukuru sana Kamati yangu ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji. Tumefanya ushirikiano kwa muda mfupi, lakini tumefanya mengi. Tangu Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji iundwe au iteuliwe mwezi Machi, 2018 Wizara yangu imeshakutanayanayo mara tatu, tarehe na ajenda tulizojadili tulipokutana ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika tarehe 26 na tarehe 27 Machi, tulikutana na Kamati ili kupokea na kujadili na kupitisha bajeti ya Wizara ya Maji ya mwaka 2018/2019; tarehe 7 Aprili tulikutana na Kamati kupokea taarifa kuhusu utendaji wa Tume ya Umwagiliaji, lakini tarehe 20 Aprili, 2018 tulikutana na Kamati kwa ajili ya kupokea Taarifa Kuhusu Utendaji wa *DAWASA* na *DAWASCO* na mchakato wa kuunganishwa kwa taasisi hizi mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kikao cha kujadili taarifa ya utendaji wa *DAWASA* na *DAWASCO* Wizara iliwasilisha kwa kina taarifa ya uamuzi wa Serikali wa kuunganisha taasisi za *DAWASA* na *DAWASCO* na hatua iliyofikiwa katika mchakato huu. Ilielezwa kuwa kuanzia tarehe 01 Julai, mwaka 2018 Shirika la *DAWASCO* litakoma na kutabaki na Shirika moja la *DAWASA* liliofanyiwa maboresho ya kimundo na majukumu. Hatua iliyofikiwa hadi sasa ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, kuandaliwa kwa kuundo na majukumu mapya ya *DAWASA*; mbili kuandaliwa kwa muundo na utumishi wa *DAWASA*; lakini tatu ni kuandaliwa kwa muundo na mishahara ya *DAWASA* na nne ni kuandaliwa kwa orodha ya kazi, maelezo ya kazi na kanuni za utumishi za *DAWASA*. Pia namba moja hadi nne tayari zimeshawasilishwa kwa Msajili wa Hazina na Utumishi kwa ajili ya idhini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kufanya tathmini ya madeni na mali za *DAWASA* na *DAWASCO*; Kamati maalum iliundwa kufanya kazi hii na imemaliza kazi yake na imewasilisha taarifa yake jana kwa Katibu Mkuu, jana tarehe

8 Mei, 2018. Kwa sababu hizi taasisi mbili zinaungana kwa hiyo, lazima kubainisha madeni ambayo taasisi zinadaiwa na madeni ambayo taasisi zinadaiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zinazoendelea kuchukuliwa katika kukamilisha mchakato wa kuunganisha DAWASA na DAWASCO ni pamoja na; kuandaa *De-Establishment Order* ya DAWASCO kwa sababu tarehe 01 DAWASCO itakoma; kuunda Bodi ya DAWASA, kufanya marekebisho ya Sheria ya DAWASA ya mwaka 2001 na ile ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2009 kwa sababu hatuwezi kuwa na sheria mbili wakati taasisi hizi zinafanya kazi moja. Hatua zote hizi zinakwenda vizuri kwa mujibu wa ratiba iliyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika mchakato wote huu wafanyakazi wa DAWASA na DAWASCO kuititia vyama vyao vya wafanyakazi pamoja na wafanyakazi wote kwa ujumla wao wameshirikishwa kikamilifu. Hakuna tataruki yoyote inayotokana na mchakato huu katika Bodi, Menejimenti na wafanyakazi wa taasisi hizi mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo taarifa ya Kamati imekiri kwa kuishukuru Wizara katika taarifa yake ukurasa wa 52 kwa ushirikiano mkubwa ambao imekuwa ikiupatia Kamati yangu tangu Kamati ilipoteuliwa mwezi Machi, 2018. Wizara yangu itaendelea kuipa Kamati ushirikiano mkubwa katika utekelezaji wa majukumu yake ya kibunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na changamoto pia ambazo ziliikuwa zimeainishwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, lakini hoja hizi ambazo ziliibuliwa wakati tunapitia kutafuta majibu tumekuja kukuta kwamba ni hoja ambazo pia ziliikuwa zimeibuliwa na CAG. Sasa kwa sababu zimeshaibuliwa na CAG, na kwa mujibu wa taratibu hoja zimeibuliwa na CAG na zikaletwa katika Bunge, ninamuagiza Katibu Mkuu na nifurahi tu kwamba, majibu tayari wameshajibu sasa wanasubiri taratibu za kiserikali kwa ajili ya kuitwa na kupeleka PAC.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimuagize Katibu Mkuu ahakikishe kwamba hoja hizi zipelekwe, ili kwa mujibu wa sheria iliyopo hoja zikisha buliwa upo utaratibu maalum ambao unatumiwa, ili kuweza kuzififikasiwa kwenye Kamati ya PAC na baadae sasa ndio zitatolewa majibu kwa mujibu wa sheria na taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji pia ina tume ya umwagiliaji, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la Maendeleo la JICA imekamilisha kuandaa upya mpango kabambe wa umwagiliaji. Mpango huu umeweka dira, malengo na mikakati ya kuendeleza sekta ya umwagiliaji kati ya mwaka 2018 hadi mwaka 2035. Mpango huu umeandaliwa kwa kuzingatia hali ya upatikanaji wa rasilimali maji katika mabonde tisa na umeainisha kwa karibu na malengo ya Programu ya Pili ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo. Tunaamini utekelezaji wa mpango huo utahusisha na kuinua sekta ya umwagiliaji hapa nchini. Tukishakuwa na umwagiliaji maana yake ni kwamba kilimo chetu kitakua, kilimo kitakuwa na uhakika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti uliofanywa na timu hii ya Wajapan imebainisha mambo mengi sana. Tumekuwa na *scheme* za umwagiliaji ambazo zinafanya kazi mara moja kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamesema ni kweli, zinafanya kazi mara moja kwa sababu zilijengwa bila kujengewa chanzo cha maji. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge nina imani taarifa hii inakabidhiwa mwezi Mei na baada ya hapo sasa tutatoa taarifa rasmi kwa Kamati yetu ili pengine kwa jinsi itakavyoamua Kamati tunaweza kuja kutoa taarifa katika Bunge. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia miradi ya maji mijini tunaendelea kutekeleza. Mfano Jiji la Dar es Salaam na nishukuru sana na Mheshimiwa Naibu Waziri wangu amezungumzia. Jiji la Dar es Salaam tumetengeneza miradi mikubwa kwenye vyanzo vya maji vya Ruvu Juu na Ruvu Chini na maji sasa yanapatikana yapo kwa wingi. Kitu kilichobaki ni kuhakikisha kwamba tunaweka miundombinu ya kutosha ili tuweze

kuyasambaza maji kwenda kwa wananchi na tayari tumeshaanza. Serikali imefanya utafiti, imefanya utafiti/*study* na kuona kwamba tunahitaji dola milioni 100 ili tuweze kukamilisha kusambaza maji katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa kwanza wa dola milioni 32 umeanza na unakaribia kukamilika. Baada ya muda mfupi tumpata tena dola milioni 45 ambayo tunakaribia kutangaza *tender* ili tuendeleze kusambaza mabomba kwenye maeneo mengine ambayo bado hayajapata huduma ya maji safi na salama katika jiji la Dar es Salaam. Kwa kufanya hivyo Waheshimiwa Wabunge ni kwamba pia tutapunguza na upotevu wa maji na tunaendelea kutafuta teknolojia nzuri na tunafanya *trial* mbalimbali kama Mji wa Tanga kwa sasa, bomba likivuja ule mtandao wa bomba umeainishwa kwenye simu yako ya mkononi, kwa hiyo itakuwa ni rahisi ku-*detect* sasa kama maji yanavuja ni rahisi kutuma wataalam waende wakaone hapo kuna nini, kuna wizi na kuziba ili tuendelee kupunguza upotevu wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru tena sana Waheshimiwa Wabunge sipendi tena nipigiwe kengele kwa sababu kengele ya kwanza imeshapiga, lakini niwashukuru sana Wabunge kwa michango yao na niseme nitaendelea kama nilivyo tabia yangu napenda kuongea na Mbunge ye yeyote aniambie hoja moja kwa moja na nilivyo ukiniambia naifuatilia na lazima nitakuja hata kwenye jimbo lako ili tuizungumze ili niweze kuifikisha katika Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba sana Wabunge, Wizara yangu kwa kweli kama mlivyosema ninyi wenyewe ina mapenzi mazuri kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maji safi na salama.

Ninaomba mtupitishie bajeti hii ili tuweze kuendelea kupambana kwa kushirikiana na ninyi na taasisi mlizonazo kwenye majimbo ili tuweze kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Kwa hivyo tutaendelea na utaratibu wetu. Katibu.

### **KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa anayepewa utaratibu hapa ni yupi, ndiyo maana kwa ajili ya kulinda heshima yako naomba tuendelee, kwa sababu lazima awepo mtu unayempa kuhusu utaratibu, soma vizuri Kanuni. Katibu!

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

### **KAMATI YA MATUMIZI**

**NAIBU SPIKA:** Kamati ya Matumizi.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kuhusu utaratibu, acha kutoa tafsiri za uwongo za kanuni bwana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Katibu!

**NDG. LINA KITOSI – KATIBU MEZANI:**

### **KITABU CHA PILI**

### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 49 – Wizara ya Maji na Umwagiliaji**

Kif. 1001 - *Administration and HRM*.....Sh. 4,459,710,442/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, fungu hili ndilo lenye mshahara wa Waziri.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Ester Bulaya na Mheshimiwa Halima Mdee tuko kwenye Kamati ya Matumizi naomba tuendelee na mjadala uliopo mbele yetu sasa.

Mheshimiwa Halima Mdee tafadhali, tafadhali sana, sana tafadhali, tuko kwenye Kamati ya Matumizi.

Waheshimiwa Wabunge fungu lilirosomwa ndiyo lenye mshahara wa Waziri kwa hivyo kwa utaratibu wetu nimeletewa majina hapa kwa uwiano wa vyama, kwa hivyo nitaanza na Mheshimiwa Mattar Ali Salum.

**MHE. MATTAR ALI SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba maelezo ya kutosha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya, tafadhali hii ni mara ya mwisho. Mheshimiwa Ester Bulaya naomba utoke nje, naomba utoke nje, naomba utoke nje, naomba utoke nje Mheshimiwa Ester Bulaya naomba utoke nje!

*(Hapa Mhe. Ester A. Bulaya alitoka ndani ya Ukumbi wa Bunge)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mattar.

**MHE. MATTAR ALI SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba maelezo ya kina kama sikupata maelezo ya kina nitazuia shilingi ya Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tuna tatizo sugu sana la maji nchini na ukiangalia bajeti bado haitoshi. Wabunge wengi wamechangia ongezeko la shilingi 50 kwenda shilingi 100 kwenye Mfuko wa Maji ili kuweza kukidhi mahitaji ya maji kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Mheshimiwa Waziri sijapata majibu mazuri naomba kuna mkakati gani wa kuhakikisha shilingi 50 hii inaongezwa kwenye Mfuko wa Maji ili kuweza kutatua kero za maji katika nchi yetu? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa hoja ya Mheshimiwa Mbunge Mattar na yeye mwenyewe ni Mjumbe wa Kamati yangu ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wabunge tumeanza Programu ya Maendeleo ya Maji mwaka 2006/2007. Tangu mwaka huo hadi leo Serikali imeendelea kutenga bajeti na inatekeleza miradi. Nilijaribu kutafuta hii data na nikakuta hadi leo tumeshatekeleza miradi ya Shilingi 2,593,501,773,404 ni fedha nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Bunge lako katika mjadala wa bajeti yangu imelalamika sana kwamba *value for money* ina shida. Sasa nakubaliana kabisa na hoja ya Mheshimiwa Mbunge, lakini hebu ngoja kwanza ndiyo maana tumeunda tume ili iweze kuangalia kuna kasoro gani ambayo tumetekeliza miradi mingi lakini Waheshimiwa Wabunge wanalalamika kwamba ile miradi haitoi maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui kama ni busara tuendelee kutenga fedha wakati bado hatujaimarisha taasisi zetu ambazo sasa tutahakikisha kwamba tukipeleka fedha kwenye utekelezaji *value for money* inaonekana kama ambavyo tunaona kwenye Wakala wa Barabara (*TANROADS*), hakuna Mbunge anayelalamika. Hela inatengwa inakwenda kule na inatumika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Wizara yangu kwa sasa ndiyo maana inaendelea kuimarisha muundo wa taasisi ndani. Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mattar nakuomba tu rudisha shilingi na wewe mwenyewe ni mjumbe ili suala la Wakala wa Maji Vijiji tuko na wewe na unatupa ushauri ili tuweze kuunda, baada ya kuunda na tuka-*test* tukaona tunakwenda vizuri, kutakuwa na haja ya kutoa hela na kuipeleka ili iweze ikatumike. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mattar.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Afahamu Mheshimiwa Waziri hili ni Azimio la Bunge kwenye Kamati yetu. Natoa hoja Wabunge wanisaidie kujadili ili tujue hili suala linafika, natoa hoja.

**MWENYEKITI:** Hoja haijaungwa mkono. (*Makofii*)

Tutaendelea Mheshimiwa Martha Mlata.

Mheshimiwa Antony Komu Kanuni ya 56 inataka Wabunge kumi wawe wamesimama ndiyo kuungwa mkono. Mheshimiwa Martha Mlata.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nilikuwa naomba ufanuzi kwa Mheshimiwa Waziri kwenye suala la kutofautiana na Kamati yetu ya Mifugo, Kilimo na Maji zile *figure*. Pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri ametoa ufanuzi lakini katika maelezo yake wakati anatoa ufanuzi kwa kweli sikuridhika na ufanuzi ule kwa sababu Kamati ya Bunge ya Mifugo, Kilimo na Maji ndiyo inayoisimamia Wizara yake, lakini wakati anatoa ufanuzi ameeleza kwamba alienda kwenye Kamati ya Bajeti wakaingiza zile *figure* baada ya fedha zile kuja baada ya wao kuwa wameshaongea na ile Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba ufanuzi ni kitu gani kilichosababisha kutokushirikisha Kamati yako ambayo ndiyo hiyo inayosimamia Wizara yako, kwa sababu Kamati ile ni inafanya kazi kwa niaba ya Bunge hili. Inapoingia na *figure* ambayo inatofautiana kuna mtu mwagine anaweza akaondoka na *figure* ile akaenda akatafsiri anavyotaka na asiwe amepata hiki ulichokisema leo. Kwa hiyo, nilikuwa naomba ufanuzi na kama sijaridhika na ufanuzi huo nitatoa shilingi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru na kumpongeza sana Mama

yangu Martha Mlata, ni mfuatiliaji mzuri sana wa miradi ya maji. Kama nilivyoeleza katika hoja yangu ya msingi mara nyingi taarifa hizi tunazifunga mwezi Machi wakati ambapo tunakuwa tumeleshapokea fedha kutoka Wizara ya Fedha hadi kufikia mwezi Machi. Wizara yangu ilichukua *initiative* ilishaanza kufanya kazi hiyo kwa kushirikiana na Hazina kuangalia zile fedha ambazo zinalipwa moja kwa moja kwenye *earmarked project*. Kama ule mradi wako uliokuwa wa Iramba kule Singida, tukakuta kwamba kuna fedha ya kutosha na tukakubaliana na Hazina kwamba hii hatuwezi kuiacha kwa sababu tunaingia katika Bunge. Sasa kwa sababu Kamati pia tunakutana nazo kwa taratibu na Kanuni za Kibunge. Kwa hiyo, tusingeweza tukakurupuka tu kwamba leo unaona hiki unakipeleka, ni lazima tutoe taarifa kwa Mheshimiwa Spika ndio tuweze kukaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa muda ambao ulikuwa umebaki mdogo hilo halikuwezekana na ndiyo maana tumelitolea ufanuzi katika Bunge lako tukufu. Niseme tu kwamba Kamati yangu ya Kilimo, Mifugo na Maji tunashirikiana nayo vizuri sana sana na tutaendeleza ushirikiano huo kwa sababu sisi sote tunajenga nyumba moja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Martha Mlata.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufanuzi ambao ameendelea kuutoa Mheshimiwa Waziri nataka nimwambie kwamba hivi ni lazima ushirikishwaji huo uendelee na hili kwa kweli lilitotokea, maana unaambiwa uwe tayari kwa wakati unaofaa na wakati usiofaa ili kuleta taarifa ilio sahihi kuliko kuifanya kamati ijjikwae ndani ya Bunge, ni kitu ambacho kwa kweli si kizuri. Sasa kwa maelezo hayo na kwa sababu ametaja na mradi wa Iramba mimi namrudishia shilingi yake, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Saed Kubenea.

**MHE. SAED A. KUBNEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nakushukuru, katika michango ya Wabunge na katika

maelezo ya Kamati imeelezwa kwamba Serikali hajawahi kupeleka fedha zote za miradi ya maji katika muda wote ambao bajeti hizi zinapita. Kwa mfano mwaka 2015/2016 ziliombwa shilingi bilioni 485 lakini zilitolewa shilingi bilioni 136 sawa na asilimia 28 ya bajeti yote. Katika mwaka huu Serikali iliombwa shilingi bilioni 623 zimetoka bilioni 135 sawa na asilimia 22.

Kwa hiyo nilikuwa naomba kauli ya Serikali kwamba katika mwaka huu wa fedha uliyoisha ambao unaisha mwaka huu Julai zile asilimia zilizobaki za fedha zitatoka? Na kama sikupata maelezo ya kuridhisha natoa hoja ya kutoa shilingi mapema. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji. Mheshimiwa Waziri naomba uzime *microphone*. Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba niseme hivi, kwanza pana tofauti kubwa kati ya bajeti inayotengwa na fedha halisi zinazopatikana. Tunachogawa ni fedha halisi zilizopatikana na sababu ya fedha zinazopatikana kutolingana na fedha ambazo zilitengwa ziko nydingi kwa mfano, kuna ukwepaji mkubwa sana wa kodi tena wengine wako humu ndani tena wanajidai kwamba wao walikuwa ni majambazi wa kukwepa kodi. Hiyo ni moja tu ya sababu, lakini ziko nydingi ambazo zinasababisha *collections* zitofautiane na kile ambacho tulibajeti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ukweli ni kwamba wigo wetu wa kukusanya mapato bado ni mdogo ndiyo maana tunafanya jitihada ya kujenga uchumi wa viwanda ili tupanue wigo wa kulipa kodi. (*Makofii*)

Kwa hiyo, kwanza niliweke sawasawa kwa Fungu 49 mpaka kufikia Aprili fedha za ndani tulizotoa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni 185. 8 hizo ni za ndani ambazo ni sawa na asilimia..., samahani naomba nirudie hizo ni za mwaka jana.

Kwa mwaka 2017/2018 fedha ambazo zimetolewa na Serikali kwenda kwenye miradi ya maji fedha za maji ni shilingi bilioni 156.1 ambayo ni sawa na asilimia 38 sio asilimia 22 ambayo imekuwa inarejewa rejewa, hilo la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, villevile ni muhimu kuzingatia, tusiangularie tu *percentages*, shilingi bilioni 156 ni fedha nyingi sio fedha kidogo. Kwa hiyo, ni muhimu sana kuangalia pia hizo shilingi bilioni 156 zimetumikaje, *efficiency of expenditure*. Tusipoangalia *efficiency of expenditure* ndugu zangu hata uongeze fedha kiasi gani kama tunapelekea mchwa fedha za walalahoi/maskini hatutakuwa tunafanya sawa sawa. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kubenea.

**MHE. SAED A.KUBNEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe hoja ya kutoa shilingi ili Wabunge wapate nafasi ya kujadili jambo hili kwa sababu sioni *seriousness* ya Serikali kwenye jambo zito kama hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe hoja.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, sasa wabaki wamesimama wale wanaotaka kuchangia ili niweze kuchangia. Mheshimiwa Bobali, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Kanyasu, Mheshimiwa Lwenge, Mheshimiwa Kakunda, Mheshimiwa Kangi Lugola, Mheshimiwa Kingu na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha - Dkt. Kijaji. Tuanze na Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mbunge wa Ubungo na kinachonifanya niunge mkono hoja hii ni sababu kuu mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati anajibu hoja Mheshimiwa Waziri wa Fedha alisema kwamba bado ukusanyaji wa mapato sio mzuri. Takwimu ambazo tunazioata kila uchwao kutoka kwa TRA zinaonyesha kwamba Serikali ya Awamu ya Tano inakusanya kodi vizuri kuliko Serikali zozote zilizopita, hizi ndiyo takwimu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti tulioipanga na kuipitisha mwaka jana ya Wizara ya Maji na bajeti tulizopita na kuzipitisha kwenye Wizara zingine, hoja hapa ni kwamba kwa nini fedha kwenye Wizara ya Ujenzi zimepatikana zimenunua ndege tena kwa *cash*, fedha kwenye bajeti ya Wizara ya Maji hakuna. Kwa hiyo, tunahitaji kodi ya kiasi gani ili tupate fedha za kupeleka kwenye Wizara ya Maji lakini pia tupate fedha kupeleka Wizara nyngine? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono hoja kwamba kunaonekana hakuna *seriousness* ya Serikali hasa Hazina ya kutoa fedha kwenye Wizara ya Maji na sababu alizoisema hazitoshelezi. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, heshimiwa Halima Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mosi nashukuru Waziri wa Fedha amekiri Serikali yake ni mufilisi haina pesa. Haiwezekani mnatuambia mnakusanya zaidi ya shilingi triliuni 1.3 kwa mwezi, mmevunja rekodi za Serikali zilizopita bajeti yetu sisi tumepanga kutokana na vyanzo vyetu halafu utatuambia leo kumbe uwezo wenu ni kutekeleza asilimia 22 tu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Fedha anatuambia hapa kwamba Serikali haina uwezo wa kutoa pesa, kati ya Wizara ambayo imepewa bajeti *more than 70%* ya utekelezaji ni Wizara ya Ujenzi. Sasa hapa tunajiuliza hivi uhai wa binadamu wa kupata maji na hizo barabara zenu kipi ni muhimu. Unasema huna pesa imetoa pendekezo tutoe shilingi hamsini tuongeze tuweke kwenye mfuko mnakataa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama mnakiri, naomba unisikilize vizuri, kama mnakiri mnashindwa kutumia pesa vizuri, kwa nini mnakuja kutuomba shilingi bilioni 673. Sasa Bunge tuwapitishie shilingi bilioni 673 za maji ukijua bajeti hewa, ukijua unashindwa kwenda kuisimamia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo ya Serikali inakosa majibu halafu inajibu eti kuna watu majambazi wakwepa kodi, kama kuna majambazi na wakwepa kodi humu washughulikieni. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Kubenea na ndiyo ilikuwa *spirit* ya Mheshimiwa Mnyika kwamba jamani sekta hii muhimu imepewa asilimia 22, sekta nyingine ambazo sio muhimu sana zimepewa nyingi, tujipe *break*, tuongeze kidogo *at least* ifike hata 40, 50 ili akina mama muwatue ndoo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema, ni aibu sana kwa Serikali inayojifanya ya wanyonge, Serikali ambayo miaka yote mmekuwa mkiwadanganya wanawake kwamba mnawajali wanawapigia kura, lakini Serikali hii utekelezaji wa kumtua mama ndoo na utekelezaji wao wa utendaji kazi ni asilimia 22 halafu mnapita mtaani mnasema kwamba hapa kazi tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja tuongeze fedha ili bajeti i...

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** ...isaidie Taifa hili. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza naunga mkono hoja ya Serikali na sababu ninazo nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapaswa kufahamu kwamba matatizo ya nchi hii sio maji peke yake, hata kama tunafikiri suala la barabara zinazojengwa sio suala muhimu lakini kule ambako hakuna barabara leo, wanataka barabara kuliko unavyofikiria wewe. Suala la msingi hapa linajibu hoja ya aliyesema mtu mwingine mmoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha amesema tumetekeleza bajeti kwa asilimia 38 na zaidi ya shilingi bilioni 150 zimekwenda kwenye maji. Mimi juzi nilisema yapo maeneo pesa zimekwenda miradi imekamilika maji hakuna na Waziri amesema tatizo lipo kwenye utekelezaji wa miradi. Hapa tunapozungumza huwezi kuendelea kupeleka pesa na ninao mfano nimesema mimi kwangu nimepelekewa shilingi bilioni 6.6 leo mradi una miaka minne maji hakuna, tatizo sio pesa. Inawezekana tukatenga pesa nydingi, tatizo la usimamizi likabaki pale pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwamba pesa tulizonazo ziendelee kusimamiwa vizuri na kwa sababu Bunge na Serikali viro tutaendelea ku-solve matatizo haya taratibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Serikali. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lwenge.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana kwa hii nafasi. Kwanza naomba niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na pia naomba niseme tu kwamba kwa kweli waziri huyu anajitahidi kufanya kazi vizuri na kwa sababu nimemsikia sana Waziri wa Fedha, ni kweli fedha zinahitajika lakini ili tuweze kuzitumia fedha hizi vizuri lazima tubadilishe mfumo wa ufanyaji kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya programu ya maji tumekuwa na watekelezaji wengi ambao sasa tunalalamika kwamba maji hayatoki, sasa wamekuja na mpango wa

kuanzisha *Rural Water Agency* ambayo Wabunge tulisema kwa muda mrefu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili *Rural Water Agency* iweze kuleta matunda lazima uanze mahali. Sasa tunaanza na ile fedha shilingi hamsini ya mwanzo ya Mfuko wa Maji inahitaji usimamizi endelevu. Sasa mimi naamini kabisa Mheshimiwa Kubenea tukubaliane na hoja ya Serikali tumrudishie shilingi Mheshimiwa Waziri wa Maji ili kusudi aende na mfumo huu ambao nina hakika utaleta matunda na ikifika mwaka 2020 tuwe na asilimia 85 ya maji vijijini na asilimia 95 ya maji Mijini, ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kingu.

**MHE. ELIBARIKI E. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naungana kabisa na Mheshimiwa Mbunge aliyetangulia kusema kuunga mkono hoja ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikuhakikishie pamoja na changamoto tulizonazo katika sekta maji, tukubaliane kabisa ya kwamba tunaposema kwamba Serikali haijapeleka bajeti ya kutosha katika Wizara ya Maji, haimaanishi kwamba Serikali yetu haikusanyi kodi na kodi haziwafikii wanyonge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya kwa mwaka 2014/2015 bajeti ya Wizara ya Afya ilikuwa ni shilingi bilioni 38, leo tunazungumza tuna bajeti ya shilingi bilioni 400 za afya kwenye sekta ya dawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunapozungumza, miji mikubwa kama Arusha *ADB* wanatekeleza miradi ya maji yenye thamani ya shilingi bilioni 500 fedha kutoka *African Development Bank*. Nafikiri Waziri wakati mwingine hebu njooni mtoe hizi takwimu inawezekana hata hao Wabunge miradi inatekelezwa kwenye maeneo yao hawajui. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo alilolizungumza Mbunge mwenzangu Mheshimiwa Kanyasu, ninaungana na

Mheshimiwa Kanyasu changamoto tuliyonayo Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu uko humu ndani, simamieni utekelezaji wa miradi ya Serikali ili iweze kuleta tija. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoa mfano kwa mara ya kwanza toka uhuru, nimezaliwa mimi kwenye Kata inaitwa Sepuka, Wilaya ya Ikungi, mahali nilipozaliwa kwa mara ya kwanza toka uhuru nimechimbiwa visima 12 vyenye thamani ya shilingi bilioni 1.4; kwa mara kwanza. Mheshimiwa Waziri umekuja kwangu umezindua mradi mkubwa wa maji...

**MWENYEKITI:** Muda wako umeisha Mheshimiwa

**MHE. ELIBARIKI E. KINGU:** ...karibu 25 hatukuwa na maji. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa

**MHE. ELIBARIKI E. KINGU:** Serikali yetu tunakwenda vizuri, tuendelee kufanya kazi na Mheshimiwa Waziri wa Fedha endelea kukusanya fedha... (*Makofi*)

*(Hapa kengele illia kuashiria kuisha muda wa  
Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kingu. Mheshimiwa Kakunda.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. GEORGE J. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba na mimi kuunga mkono hoja ya Serikali hasa pale ambapo Mheshimiwa Waziri ameliarifu Bunge lako tukufu kwamba tangu tuanze kutenengeneza program hadi sasa tumetumia zaidi ya shilingi trillioni mbili kwa ajili ya miradi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zipo na miongoni mwa changamoto hizo ndio zimefanya utaratibu ubadilike kidogo katika miaka ya hivi karibuni kwamba ili

kusudi mradi upate fedha ni lazima utekelezaji ufanyike kwa kiwango fulani na mkandarasi pamoja na mshauri wake wadai fedha kwa utaratibu wa *certificate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imesababisha utekelezaji ambao unafuatiwa vizuri zaidi na hiyo ni mojawapo ya sababu kwa nini fedha imekuwa wakati mwingine inachelewa kupelekwa kwa sababu wakati mwingine wanachelewa kuleta *certificate*. Kwa hiyo, huo ni utaratibu mzuri na utaratibu huu utasaidia sana kuhakikisha kwamba miradi yetu imetekelezwa kwa viwango vinavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ambayo inapitishiwa na Bunge lako tukufu sio ile tu ya Wizara ya Maji nyininge inapita inakwenda moja kwa moja kwenye Halmashauri. Kwa mfano, mwaka huu wa fedha Halmashauri tulitengewa shilingi billioni 267. Kwa hiyo, Bunge lisifiki kwamba fedha zinazokwenda kwenye miradi ya maji tu ni ile ambayo inapangwa kwenye *vote 49*, hapana. Na *vote* nyininge kama TAMISEMI kuna fedha ambazo zinakuja kupitia kwetu na vilevile kuna fedha nyininge zinapitia Wizara ya Elimu kwa ajili ya miradi ya usafi wa mazingira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Mbunge arudishe shilingi ili kusudi tuendelee kuboresha miradi ya maji, ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaendelea, kwa mujibu wa Kanuni ya 104 naongeza nusu saa na kanuni hii hainihitaji kuwahoji, kwa hiyo, naongeza nusu saa. Mheshimiwa Dkt. Kijaji.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na nimuombe sana Mheshimiwa Kubenea aachie shilingi ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa Mheshimiwa Waziri wa Fedha amesema hapa na akasoma na *message*

iliyotoka India na kumfikia hapa kwamba milioni 500 kesho asubuhi zinasainiwa. Inamaanisha nini hii? Hii inamaanisha kwamba mpaka tunapofika tarehe 30 Juni, 2018 bajeti ya Wizara ya Maji itakuwa imetekelvezwa zaidi ya asilimia 80 kwa sababu ya fedha ambazo zinatiwa saini kesho, hicho ndicho ninachowenza kusema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwaambia ndugu zangu wanaohoji makusanyo *vis-a-vis* matumizi. Ni sahihi Serikali yetu inakusanya na tunakusanya na kubwa ambalo lipo tunapokusanya tunalipa kiasi gani kwenda kulipa Deni la Taifa ambalo liliapatikana kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ambayo leo utekelezaji wa miradi hiyo ya maendeleo, utekelezaji wa miradi ya maendeleo umelifungua Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *prediction* iliyotolewa na *Harvard University* juzi Tanzania itakuwa ni nchi ya nne kwenye ukuaji wa uchumi ni kwa sababu ya miradi ya maendeleo iliyotekelvezwa na ndicho hiki tunachokifanya, tunakusanya zaidi ya asilimia 100 kila mwezi na tunalipa madeni ambayo yamelifungua Taifa letu, uchumi wa nchi unakua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana Waheshimiwa tuweze kuelewa na ameshasema Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba tayari Serikali inakuja na *Rural Water Agency*, tunashughulikia na mfumo ambao tunapiga kelele hapa. Tunakuja sasa kuisimamia miradi ya maji kama ambavyo *TANROADS* imefungua barabara za taifa letu, kama ambavyo sasa *TARURA* inafungua barabara zetu na miradi ya maji kuhakikisha pesa zinazokwenda zinatumika ipasavyo na wananchi wapate maji na tunaenda kumtua mama ndoo ya maji kichwani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe na niwaombe pia twende kiuchumi zaidi, tupitie *budget execution* za nchi hata zilizoendelea, ni nchi gani ambayo imeweza kutekeleza bajeti kwa asilimia 100, ni nchi gani? Twende kwenye *Budget Execution Report*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Kubenea twende tusome uchumi kidogo halafu tuje ndani ya Bunge tuweze kuchangia hapa, nakushukuru sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, nataka kumrudisha mtoa hoja kwa hiyo shilingi yako.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwashukuru sana hoja za Waheshimiwa Wabunge, lakini pia nimshukuru Mheshimiwa Kubenea kwa kuona hiyo hoja. Lakini kama ambavyo nimejibu kwenye majibu yaliyopita, tumeanza utekelezaji wa miradi tangu mwaka 2006/2007 na kawaida ya binadamu kila unavyoishi unajifunza na ukijifunza unabadijika, ndio namna ya kuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwenda na mfumo fulani tukabaini kwamba lazima tuufanyie marekebisho, hili tumeliona na liliekezwa na ninyi wenyewe Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Kubenea usisahau kwenye michango mmenigonga kweli kweli kwamba *value for money* hamuioni, niendelee kupokea hela ikapotee tena? Mwisho mtanifunga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kubenea nikuombe tu ndugu yangu rudisha shilingi ili twende tukatekeleze miradi. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kubenea, mtoa hoja.

**MHE. SAED A. KUBNEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza maelezo yote ya Mawaziri wote waliozungumza, lakini nimejiridhisha pasipo na shaka kwamba Serikali hii haina sababu ya kuja Bungeni kuomba fedha, hawana uwezo wa kusimamia fedha za wananchi. Waziri wa Fedha amesema asilimia 38, Kamati imesema asilimia 22, Waziri wa Maji amesema asilimia 56, Naibu Waziri amesema asilimia 80 ya fedha tutapata na

anazungumzia fedha za India ambazo tokea wakati wa Mheshimiwa Jakaya Kikwete na zimo kwenye bajeti hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba ulihoji Bunge, kwamba je, ile asilimia 78 ya bajeti iliyobaki iende kwa wananchi au isiende ili hawa Wabunge wa CCM hawa wakubali kwamba hiyo hela isiende kwa wananchi halafu wananchi wawasikilize. Kwa sababu hoja hapa ni kwamba Serikali itoe fedha zilizobaki zote kama ilivyoomba kwenye bajeti au fedha zisitoke. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge hili lihojiwe kwa sababu hata fedha ya Deni la Taifa ambalo Naibu Waziri analizungumza limo kwenye bajeti, kwenye shilingi trillioni 15 tunalipa shilingi trillioni kumi. Sasa Naibu Waziri anakuja kubadilika kabisa na Waziri wake, yaani Naibu Waziri anakwenda mashariki Waziri anakwenda magharibi, sasa hii Serikali ipi? Isiyosimama katika mlango mmoja? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuhoji kwamba wangapi wanasema fedha ya Serikali iliyotengwa na Bunge hili tukufu asilimia 78 iliyobaki iende kwa wananchi na wangapi wanasema isiende, tohoji hivyo. Hiyo ndiyo hoja yangu, naomba uamuzi wa kura uwahoji hawa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kubenea nitafanya hivyo, lakini Waheshimiwa Wajumbe kabla sijawahoji lazima mjue mnahojiwa kuhusu nini, hoja hii anayotoa hapa mwisho ameibadilisha hoja yake ya mwanzo. (*Kicheko*)

*(Hapa baaadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe, hoja ambayo Mheshimiwa Kubenea alitaka kuitolea shilingi aliyotoa tangu mwanzo ninawahoji. (*Makof*)

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)  
(Hoja Iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tuendelee. Waheshimiwa Wabunge hoja ya Mheshimiwa Kubenea haijashinda. Kwa hiyo, tunaendelea na Mheshimiwa Hamidu Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Hoja yangu ni ndogo tu na kama sijapata majibu ya kuridhisha nakusudia kutoa shilingi ili Kamati ijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikipeleka fedha hizo hizo kidogo zinazopatikana zimekuwa zikipelekwa kwenye maeneo na kwenye miradi mbalimbali. Lakini wakati wa mjadala wa kuchangia bajeti Wabunge wengi na tunaweza tukawataja kwa majina wamelalamikia juu ya ufisadi na miradi mingi kuendeshwa kwa ubadhirifu. Mheshimiwa Keissy alikwenda mbali jana akapewa dakika 15 na akasema siyo wizi tu, kuna ujambazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba *commitment* ya Serikali kwamba miradi yote ambayo imeendeshwa na ndani yake kuna harufu ya ufisadi na Wabunge wameitaja na kwenye *record*, *Hansard* za Bunge zipo zimetajwa, na ipo mingine tutaongezea wakati wa kujadili. Naomba *commitment* ya Serikali kwamba je, hawa watu waliofanya ubadhirifu na kuisababishia nchi hasara kubwa ya kiwango hicho ni lini watachukuliwa hatua ama Bunge litaunda Tume ya kwenda kuchunguza juu ya suala hilo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba *commitment* ya Serikali juu ya jambo hili na vinginevyo nitaomba Kamati tujadili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji. Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa wa

Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu hoja ya ndugu yangu, Mbunge wa Mchingga, jirani yangu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka niungane naye kwamba ni jambo bayaa sana Serikali kupeleka fedha mahali zikatatue tatizo la maji zikatumika vibaya na ametaka *commitment* ya Serikali juu ya ubadhifru unaoweza kutokea katika utekelezaji wa miradi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa kumhakikishia kwamba vyombo nya Serikali, vyombo nya dola, sasa hivi vipo kazini vinafanya uchunguzi juu ya ubadhifru na hapa kwako tunachunguza, Ntomoko tunachunguza, Bunda tunachunguza, kutaja tu michache. Na ninataka nikuhakikishie tutakapokamilisha TAKUKURU itawafikisha mahakamani watakaobainika wamefuja. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza mzee wangu, Mheshimiwa Waziri wa Utumishi, lakini maelezo yake hayakuniridhisha, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono Waheshimiwa Wajumbe, wale wengine ambao hawahitaji kuchangia wakae. Mheshimiwa Ngombale, Mheshimiwa Ally Saleh, Mheshimiwa Bulembo, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Kangi Lugola, Mheshimiwa Martha Mlata nimekufuta, Mheshimiwa Musukuma, Mheshimiwa Kubenea si umetoka kwenye hoja, kwa hiyo kaa ili wenzio wapate nafasi tafadhalii. Mheshimiwa Ryoba Chacha.

Tuanze na Mheshimiwa Ngombale.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili basi na mimi nichangie katika hoja ya ndugu yangu, Mheshimiwa Bobali, kuhusiana na tatizo hili la utekelezaji wa miradi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeelezwa mara nydingi na mara zote, na ni siku nydingi na hata leo Serikali inavyosema ndiyo kwanza sasa hivi wametuma vyombo vyake vya dola kufuatilia ni kama tunashangaa kwa sababu tatizo hili ni la siku nydingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Usimamizi wa Hesabu za Serikali za Mitaa katika taarifa yake iliyotolewa mwanzoni mwa mwaka huu ilitoa pendelezo la kwamba Bunge lako tukufu liunde Kamati Teule ya Kibunge kuangalia utekelezaji wa mradi huu. Kuna tatizo kubwa ambalo tunashangaa kwamba mpaka sasa Serikali ndiyo inasema inaanza. Nafikiri suala hilo wamelefanya kwa kuchelewa na wamechelewa kwa sababu hawako makini katika kuhakikisha kwamba miradi ya utekelezaji wa maendeleo ya maji inatekelezwa ipasavyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niungane na ndugu yangu, Mheshimiwa Bobali, kwamba Kamati Teule ya Bunge iundwe ili basi kufuatilia nini sasa kinatakiwa kufanyika kwa maslahi ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Ally Saleh.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Bobali kwa sababu Serikali hii iliyopo madarakani hivi sasa inasema kwamba inapambana na rushwa na ujisadi. Sasa mimi nashangaa wakati Waziri ana-wind up ripoti yake hata hakugusa matakwa yaliyokuwa

yameenea humu ndani kwamba kuna haja ya kuunda tume na kuna haja ya kufanya uchunguzi. Kasubiri mpaka wakati hoja hii imenyanyuliwa na Mbunge, Mheshimiwa Bobali, Mheshimiwa Waziri mwingine anasema kwamba Serikali itaunda tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kweli hii hairidhishi, na kwamba kama Serikali inakubali kwa ushahidi wa wazi uliotolewa na Wabunge mbalimbali mpaka wa CCM kwamba kuna ujisadi mkubwa, lakini Serikali imenyamaza kimya, kusema kweli hairidhishi. Kwa hiyo, hoja hii isimame na kwamba lazima wananchi wa nchi hii wapate *value for money* na siyo *value for money* tu, wajue kwamba pesa zao zinatumika vipi, zinatumika namna gani na kwa kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali ilivyo hivi sasa inatisha, kwamba kiasi hicho cha pesa Waziri amefika mpaka amepandishwa kwenye tenki, ameona kwamba kuna popo badala ya maji na amekiria, halafu akanyamaza kimya hapa, kusema kweli hairidhishi na inaonesha jinsi gani Serikali ya CCM isivyowajali wananchi, isivyokuwa tayari kuwasaidia wananchi na inaendelea kuwadanganya kwamba inawafanyia haki lakini haiwatendei maendeleo wanayotaka na kwa maana hiyo basi, hoja hii iamuliwe kwa njia nyingine ili wananchi wapate salamu kwamba CCM haiwajali kama inavyosema. Ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri ametuonyesha Bunge zima mashaka kwamba anaogopa kupokea pesa nyingi kwa sababu kuna ujisadi mwiningi kule chini, na kwamba akipewa fedha zote za bajeti zitamshinda kusimamia kwa sababu kuna ujisadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nishauri, sisi ni Bunge, hatuwezi kusubiri TAKUKURU ifanye kazi yake kule na Bunge lina uwezo wa kuunda tume ikafanya kazi yake kwa muda mfupi ikaleta majibu na kazi ikaendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe tumsaidie Waziri sisi kama Bunge, tuisaidie Serikali, tuunde tume ya uchunguzi izunguke kwenye miradi yote ambayo hata Waziri, kila mtu hapa anasema ni kweli kuna ujisadi. Hata kwangu pale kuna ujisadi kweli kweli na ndiyo maana siku ile umekuja Mkuu wa Wilaya sjui na nani wanakukwepesha kweipesha ili usiende kwenye ile miradi ya kifisadi. Iko wazi, fedha zimeliwa, maji hayapo. Kama Bunge tuunde tume ambayo itakuwa ni kwa muda mfupi iende ikasimamie jambo hili. Ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ujisadi huu mkubwa unaofanya kwenye miradi ya maji binafsi naamini na Wabunge wengi ni wahusika. Kwa sababu sisi Wabunge humu ndani ni sehemu ya ukaguzi wa miradi, inawezekanaje mtu anakuibia mabilioni yote hayo ya hela unashiriki mpaka kuja kupiga kelele kwenye Bunge? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ni Mbunge wa Geita na ushahidi ninao nataka niwape mfano kwa sababu ni Mbunge makini kuliko hawa wanaopiga kelele humu ndani. Tulikuwa na mradi uliochakachuliwa zaidi ya shilingi bilioni 2.5, mimi mwenyewe nimeilipa Kamati yangu ya Fedha kufanya ziara ya kukagua huo mradi tukagundua ubadhirifu huo. Na nimefuata Mawaziri wote, kila anayekuja asipoenda... (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma, muda wako umekwisha.

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niongeze kidogo, ni kengele ya mtu aliyetangulia, yule aliye maliza.

**MBUNGE FULANI:** Kaa chini.

**MWENYEKITI:** Ni muda wako Mheshimiwa Musukuma.

Mheshimiwa Abdallah Bulembo.

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwamba naungana na Serikali. Lakini hoja yangu ni moja, kuna Wajumbe wanasesma tuunde tume, tukiunda tume tukamaliza itaenda wapi, si itarudi Polisi na TAKUKURU? Ndiyo, kwa sababu kama kuna kitu tumegundua hakifai itawarudisha huko huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Utumishi ameshajibu TAKUKURU iko kazini, tunaunda tume ya nini? Kwa hiyo kwa sababu TAKUKURU wako kazini, tuwape nafasi ili watuletee ujisadi. Waziri anachosema hajasema kushindwa kutumia pesa, anasema penye mashaka hawezi kupeleka tena pesa, kwanza ajiridhishe. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mwenye hoja akubali, Serikali imeshaweka mazingira ya kupata wale wezi, wakishapatikana si tutarudi hapa hapa Bungeni? Mrudishie mzee shilingi tupate maji. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja ya Serikali kwamba mpaka sasa vyombo vya Serikali vya kiuchunguzi viko kazini vinaendelea kuchunguza ujisadi ambao umefanyika kwenye miradi ya maji na ushahidi ni kuanzia mwezi Januari Mheshimiwa Waziri Mkuu akiwa Bunda kwenye Mradi wa Bunda aliagiza TAKUKURU na wakawakamata wale wakandarasi mbele ya wananchi, kule Nkasi Mkurugenzi alishasimamishwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba Wabunge waamini kwamba TAKUKURU wanafanya kazi vizuri

na tumeanza muda mrefu. Ndugu yangu Mheshimiwa Ryoba kusema kwamba tuachie Bunge likachunguze, haya mambo ni ya kitaalam, ni ya *profession*. Tungekuwa tunaenda kuchunguza mambo mengine ambayo hayahusu wizi kwenye fedha tungeweza kusema hivyo, lakini kama alivyosema Mheshimiwa Bulembo, tutakuja hapa bado tutasema waliohusika wapelekwe TAKUKURU na itafanya kazi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi naunga mkono kwamba Serikali na vyombo vyake watuache tufanye kazi, jambo hili halijatuhinda na matokeo watayaona na wale wote waliohusika hata kama kuna Wabunge humu ndani wametia mkono wao, Serikali itawashughulikia. (*Makof!*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha muda wa  
Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha. Mheshimiwa Mwigulu Nchemba.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niunge mkono hoja ya Serikali na niombi kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge kutofautisha mambo makubwa matatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, pana tofauti kubwa saba ya hatua za kisheria na hatua za kiutumishi. Hivi tunavyoongea kwenye miradi ambayo ilifujwa kuna hatua nyingi sana za kinidhamu ambazo zilishachukuliwa ambazo kuna wahandisi wamepoteza kazi zao, kuna wakurugenzi wamepoteza kazi zao na mmeshuhudia mpaka wakandarasi wengine tukashikilia mpaka *passports* zao ili waweze kuajibika. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya mengine ambayo taratibu zaidi za kiuchunguzi zinafanyika ni yale ambayo yanahitaji *evidence* ya kimahakama. Kwa hiyo, sasa kama mambo yameshafanyiwa uchunguzi hata yanesubiri kwenda mahakamani sisi tukianza kuunda tume leo hii

tutakuwa tuko nyuma sana, tumeachwa na matukio kwa mwendo wambali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bobali huwa ni mtu mwema namjua sana hakuna haja ya kuunda tume wala hakuna haja ya kushika shilingi. *With all the Government's query kuhusu ujisadi unashubiri mpaka ushike shilingi kwenye Serikali ya JPM kuhusu ujisadi? You guys are not serious. (Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe kuna hoja ambazo tunakubaliana wote na kuna hoja ambazo ziko *clear* na hatua zinachukuliwa na zinachukuliwa hadharani, mojawapo ni hii ya kushughulika na ujisadi. Tumuache Waziri akafanye kazi na hatua za wale ambao wamefanya ufujaji wa aina hiyo ziko kwenye hatua za mwisho na zitachukuliwa. Na hakuna ambaye atafanya ujisadi akabaki salama kwa sababu hiyo ni moja ya vitu ambavyo Mheshimiwa Rais amejipambanua, *he has zero tolerance on corruption* ya aina yoyote. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, kwa maana hiyo kama kuna mtu ana taarifa ya jambo la aina hiyo katika eneo lake ni jambo la kuleta taarifa tu kwa Mheshimiwa Waziri na nyingine leteni hata kwangu ambazo zinahusu ufujaji wa aina hiyo. Siku ileile watakamatwa watu wanaofanya ufujaji wa aina hiyo. *(Makof)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Maji.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru Wajumbe hasa waliounga mkono Serikali, wamechangia vizuri sana. Huu ni utawala wa kisheria kwa hiyo jambo linapotokea lazima lifanyiwe uchunguzi ili isije ikaonekana tena siku nyingine tumemuonea mtu, Mheshimiwa Bobali, hebu achia hiyo shilingi tukafanye kazi, nakuomba sana. *(Makof)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bobali mtoa hoja.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba niseme mambo machache sana, kwanza tangu nachangia juzi nilisema sina mashaka na utendaji kazi wa Mheshimiwa Waziri wala Naibu Waziri, hili lazima liwe *clear*, lakini nina mashaka kwamba inawezekana ndani ya Bunge humu kuna Wabunge hata hawajui jukumu la Bunge ni nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, anapotokea Mbunge akasema kwamba kuna vyombo vya Serikali vinafanya kazi, kuna haja gani ya Bunge kuingilia kat, inawezekana kwamba hajui jukumu la Bunge ni nini? Jukumu la Bunge ni kuisimamia na kuishauri Serikali. Wabunge wamelalamika ndani ya Bunge kwamba kuna ujisadi na ujisadi umefanyika wakati Serikali ipo. Kwa hiyo, sasa Bunge tuchukue *role* yetu ya kuisimamia Serikali, mojawapo ni hili la kuunda tume ya kwenda kuchunguza hiko kinachoelezwa kwamba ujisadi ili taarifa hizo za kifisadi zije kujadiliwa na Bunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili chini Spika Mheshimiwa Job Yustino Ndugai amewahi kuunda tume kadhaa hapa na zingine ziko kwenye hatua za mwisho zinafanya kazi, kuchukuza mambo ambayo siku zote Serikali hawakuja kuyaeleza hapa. Tumepata manufaa tumeelezwa kuna manufaa makubwa tumeyapata kwenye makinikia, ni matokeo ya tume ya Bunge iliyoundwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya yote yaliyoelezwa yako Mbunge amejenga hoja kwamba inawezekana mafisadi Wabunge ndiyi hiyo kazi ya tume pia mojawapo itakuwa kuwataja hao Wabunge amba wanakwamisha Serikali na miradi ya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba sina mashaka na Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini naomba tuweke *record* naomba jambo hili lifanyiwe maamuzi ili liingie kwenye *record* za Kibunge kwamba sasa Bunge ulihoji, hoji Bunge ili baadae *record* hii itakuja kutusaidia baadae. Nakushukuru. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Mheshimiwa Bobali. (*Makofii*)

*(Hoja lilitolewa lamuliwe)  
(Hoja lliamuliwa na Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo hoja ya Mheshimiwa Bobali imekufa.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliimba CCMjuu, CCMjuu)*

**MWENYEKITI:** Kweli hoja ya Mheshimiwa Bobali kiboko mpaka watu wanaisifia CCM hatari kabisa, Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga. (*Makofii*)

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Wabunge wengi walikuwa wanachangia hapa wameelezea sana matatizo ya maji katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Na Waziri wakati anafanya majumuisho hapa ameleezea kwamba kuna chombo ambacho wanatarajia kukiunda. Na kwa sababu huko nyuma kulikuwa na utaratibu mbovu na ndiyo maana Wabunge wamezungumzia sana tatizo la maji katika maeneo mbalimbali.

Sasa nataka nipate kauli ya Serikali ni lini chombo hiki kitaundwa cha kusimamia suala la maji na kama chombo hiki (Wakala wa Maji) sitadhirika na majibu ya Serikali basi nitatoa shilingi. Lakini wakati Mheshimiwa Waziri anafanya majumuisho tena amezungumzia kwamba kuna Kamati ya Wizara ambayo ameunda kwenda kuangalia miradi mbalimbali...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sanga hilo linauhusiano na ulilosema mwanzo au ni la pili liko tofauti?

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, linahuksiana, ninaboresha...

**MWENYEKITI:** Kama linahusiana malizia muda wako, lakini kama halihusiani jambo unasisima moja tu mahususi.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lile la mwanzo...

**MWENYEKITI:** Tubaki na hilo la mwanzo, Mheshimiwa.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi nabaki na lile la mwanzo, nipate kauli ya Serikali ni lini Wakala wa Maji itaundwa na kama sitapata jibu basi nitatoa shilingi. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Sanga na ninaimani leo anafuraha kwa sababu fedha aliyokuwa anaisubiri ya dola milioni 500 kutoka Serikali ya India. Kesho mkatuba wa fedha unasainiwa ili Waziri huyuhuyu unayemshikia shilingi ndio ataketekeleza. Nikuombe sana lakini ngoja nikupe majibu ya hoja ambayo Mheshimiwa Sanga umeilizilia, nimetoa tarifa kwamba baada ya Bunge kuazimia kwamba Wizara ya Maji iangalie uwezekano wa kuunda mamlaka ya kuhudumia maji vijijini. Wizara ya Maji ilipokea taarifa hiyo na imefanya kazi na hatua zilizofikiwa ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Ofisi ya Rais, Utumishi pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango imekamilisha kazi ya kuandaa nyaraka muhimu ambazo ni *strategic plan, business plan, framework document* na *establishment order*. Na kwamba tunaunda kwa mujibu wa uwanzishwaji wa wakala *The Executive Agency Act Cap. 245*. Kwa sababu huu ni wakala unaundwa kwa hii *Executive Agency* ambayo inataratibu zake huwezi ukaanza leo ukasema kesho unaunda. Ziko hatua mbalimbali zinazopitiwa, lakini nimekuonyesha Mheshimiwa Mbunge

kwamba tulipofika tumeshafika mbali siwezi ku-*estimate* hapa kwamba tarehe ngapi tutakuwa tumemaliza, lakini nikuhakikishie kwamba tulishaanza na hatua tuliko fika ni mbali sasa hivi tayari tuko tunapata maoni ya wadau. Baada ya kukamilisha maoni ya wadau basi tunapeleka kwenye mamlaka husika ikatoe idhini ili tuwe kuunda hiyo *Executive Agency*.

Mheshimiwa Mbunge nakuomba sana rudisha shilingi li tufanye kazi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni ya 104(2) sasa mtahoja kwa mafungu, Katibu.

#### **Fungu 49 - Wizara ya Maji na Umwagiliaji**

Kif. 1001 -Administration <i>HRM</i> .....	Sh. 4,459,710,442/=
Kif.1002 - <i>Finance and Accounts</i> .....	Sh.1,175,000,000/=
Kif.1003 - <i>Policy and Planning</i> .....	Sh. 732,279,000/=
Kif.1004 - <i>Government Comm. Unit</i> .....	Sh. 222,807,000/=
Kif.1005 - <i>Legal Service Unit</i> .....	Sh. 235,842,000/=
Kif.1006 - <i>Procurement Management Unit</i> ....	Sh.609,816,000/=
Kif.1007 - <i>Management Information System</i> ..	Sh. 245,499,000/=
Kif.1008 - <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh. 290,560,000/=
Kif.2001- <i>Water Resources</i> .....	Sh. 5,982,000,000/=
Kif.2002- <i>Central Stores</i> .....	Sh.151,673,000/=
Kif.2003 - <i>Water Laboratory</i> .....	Sh.1,888,000,000/=
Kif.3001- <i>Urban Water Supply And Sanitation</i> .....	Sh. 2,758,000,000/=
Kif.4001 - <i>Rural Water Supply</i> .....	Sh.1,496,408,000/=
Kif.4002 - <i>Water Sector Program Coordination Unit</i> .....	Sh.120,000,000/=
Kif.5001 - <i>Water Development And Management Institute</i> .....	Sh. 2,861,274,558/=
Kif.6001- <i>Drilling and Dam Construction Agency</i> .....	Sh. 2,861,274,558/=

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

### **Fungu 5 - Tume ya Taifa ya Umwagiliaji**

Kif.1001- *Administrationand HRM*.....Sh. 938,594,000/=  
Kif.1002 - *Financeand Accounts*.....Sh. 201,361,000/=  
Kif.1003 - *Planning, Monitoring and  
Evaluation*.....Sh.158,192,000/=  
Kif.1004 - *Government Communication Unit*..Sh. 21,890,000/=  
Kif.1005 - *ProcurementManagement Unit*....Sh. 138,596,000/=  
Kif.1006 - *Internal Audit Unit*.....Sh. 49,964,000/=  
Kif.1007 - *IC Technology*.....Sh. 74,600,000/=  
Kif.1008 - *LegalService Unit*.....Sh. 62,744,000/=  
Kif.1009 - *EnvironmentalandSocial Mgt*.....Sh. 74,886,000/=  
Kif. 2001- *Irrigation, Planning Design  
and Private*.....Sh. 771,580,000/=  
Kif. 2002 - *Irrigation Infrastructure Dev.* .....Sh. 477,154,000/=  
Kif. 2003 - *Irrigation Research &  
Tech. Promotion*.....Sh. 373,560,000/=  
Kif. 2004 - *Irrigation Operations  
Support Service*.....Sh. 409,136,000/=  
Kif. 2005 - *Irrigation Compliance  
Quality Assurance*.....Sh. 95,151,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **KITABU CHA NNE**

#### **MATUMIZI YA MAENDELEO**

### **Fungu 49 - Wizara ya Maji na Umwagiliaji**

Kif. 1001 *Administration and HRM*.....Sh. 21,037,584,677/=  
Kif. 1003 *Policy and Planning*.....Sh.19,276,450,000/=  
Kif. 2001 *Water Resources*.....Sh.41,000,000,000/=  
Kif. 2003 *Water Laboratory*.....Sh. 7,700,000,000/=  
Kif. 3001 *Urban Water and Sanitation*....Sh. 322,199,999,000/=  
Kif. 4001 *Rural Water Supply*.....Sh. 262,000,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## **Fungu 5 - Tume ya Taifa ya Umwagiliaji**

Kif.1003 - *Planning, Monitoring and Evaluation*.Sh.300,000,000/=  
=  
Kif.1009 - *Environmental&Social Mgt*.....Sh.200,000,000/=  
Kif. 2001- *Irrigation,Planning and Private*.....Sh.8,773,037.303/=  
Kif. 2002 - *Irrigation Infrastructure Dev*.....Sh.16,013,486,097/=  
Kif. 2003 - *Irrigation Research &  
Tech. Promotion*.....Sh. 200,000,000/=  
Kif. 2004 - *Irrigation Operation &  
Support Services*.....Sh. 233,934,600/=  
Kif.2005 - *Irrigation Compliance &  
Quality Assurance* .....Sh.100,000,000/=

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. LINA KITOSI - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekalisha kazi yake.

*(Bunge Lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae, mtoa hoja, taarifa.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo ya Januari mwaka 2016 Kanuni ya 104(3)(a) na (b) kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha zimekamilisha kazi zake. Naomba kutoa taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge. Naomba kutoa hoja. *(Makof)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, kwa hiyo tutaendelea na taratibu zetu, sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2018/2019.

*(Hoja Ilitolewa na lamulie)  
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa Fedha  
2018/2019 -Wizara ya Maji na Umwagiliaji yalipitishwa na  
Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji na Naibu Waziri wake kwa kazi nzuri walioifanya ya kutuleta Makadirio ya Mapato na Matumizi ambayo Bunge limepata fursa ya kuyapitia kwenye ngazi ya Kamati. Lakini pia kama Bunge Zima kwa siku tatu. Lakini pia wakati nikiwapongeza wao niwapongeze wataalam wao ambao wamefanyanao kazi Katibu Mkuu na vyombo vyote vilivyo chini ya Wizara hii. (*Makofi*)

Nichukue fursa hii kuwatakia kila la kheri katika utekelezaji wa hii bajeti ambayo imepitishwa na Bunge na ninaamini kwamba yale ambayo mmeyatolea ufanuzi hapa basi Waheshimiwa Wabunge watapa fursa ya kuyaona matunda ya hayo kwenye bajeti ijayo.

Waheshimiwa Wabunge, leo asubuhi niliombwa mwongozo na Mheshimiwa Gimbi Masaba kuhusu kutojibiwa kwa ufasaha swali lake la msingi namba 215.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Gimbi Masaba kwanza aliomba mwongozo kuhusu kutokujibiwa kwa ufasaha kwa swali lake la msingi. Lakini pia Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba aliomba mwongozo akitaka kujua ni kwa nini katika kujibu swali lake Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi alimtaja Mbunge wa Jimbo la Itilima, Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga.

Mimi nilitoa maelezo kwamba nitajibu mwongozo wa Mheshimiwa Gimbi Masaba baada ya kuzipitia Taarifa Rasmi za Bunge. Waheshimiwa Wabunge kuhusu kutojibiwa kwa swali lake la msingi namba 215 Mheshimiwa Gimbi Masaba alieleza kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya

Nchi amelidanganya Bunge kwamba kuna kituo kule Wilaya ya Itilima kinachojengwa. Katika kupitia Taarifa Rasmi za Bunge ambazo nikonazo hapa mbele majibu kuhusu ujenzi wa kituo cha polisi yalitolewa na Naibu Waziri wakati akiijibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Gimbi Masaba na si katika swali lake la msingi kama alivyoeleza wakati akiomba mwongozo.

Hata hivyo majibu ya Serikali ni kwamba kuna kituo cha poilisi kinajengwa huko Itilima. Ambapo Mbunge wa Itilima naye alitajwa kama mdau anayeshiriki katika ujenzi huo. Kama majibu hayo hakumridhisha Mheshimiwa Mbunge kuna mwongozo wa kiti ambaa ulishawahi kutolewa huko nyuma kwamba hatuwezi kujikita kuitaka Serikali itoe majibu ya kuridhisha katika maswali ya nyongeza. Hivyo Mheshimiwa Gimbi Masaba kama hakuridhika na majibu yaliyotolewa ya maswali hayo anatakiwa sasa kuyaleta maswali ya msingi ili Serikali iweze kuleta majibu mahususi kuhusu mambo hayo.

Waheshimiwa Wabunge kuhusu sehemu ya pili ya mwongozo wake kwamba ni kwanini Mheshimiwa Naibu Waziri alimtaja Mheshimiwa Mbunge wa Itilima katika jibu lake kiti kimeridhika kuwa kimsingi hakuna kanuni iliyovunjwa, Mbunge wa Itilima Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga alitajwa na Mheshimiwa Naibu Waziri kama mmoja wa wadau wanaoshiriki katika jitihada za ujenzi wa kituo cha polisi huko Itilima. (*Makofii*)

Kwa hiyo hakuna tatizo katika hilo kwani ni jambo jema la kimaendeleo, tunategenea kuwa masuala ya maendeleo ya wananchi, Wabunge wanaotoka sehemu husika na hata wanaotoka mbali watashirkiana bila kujali itikadi za vyama vyao na bila kujali kama mmoja ni Mbunge wa Jimbo na mwingine ni Mbunge wa Viti Maalum kwa sababu wote wana hadhi sawa, nyumba tunayojenga ni moja. Kwa hiyo, hakuna haja ya kugombania fito. (*Makofii*)

Kwa hiyo, kiti hakioni tatizo lolote katika majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na huo ndiyo mwongozo wangu.

Waheshimiwa Wabunge, wakati kabla hatujaingia kwenye Kamati ya matumizi nimeletewa taarifa hapa kwa maandishi kwamba kulikuwa na matumizi ya lugha ambazo zinakatazwa na Kanuni ya 64(1)(f) na (g).

Waheshimiwa Wabunge, niwasihii tena tuzingatii kanuni zetu, kanuni zinakataza lugha ya matusi, kusema vibaya, lugha ya kuudhi, lugha inayodhalilisha watu wengine, na sisi wote humu ndani tunaitwa Waheshimiwa Wabunge tukitarajiwa kwamba sisi wenyewe tunajjheshimu ipasavyo, tusitumie lugha ambazo Kanuni yetu ya 64 inatukataza.

Kwa hiyo, nimeona niseme hayo kwa sababu nimeletewa tarifa ya maandishi kwamba kulikuwa na matumizi ya lugha isiyofaa wakati kikao kikiendelea.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge naahairisha shughuli za Bunge mpaka kesho siku ya Alhamisi tarehe 10 Mei, 2018 saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.15 Usiku Bunge lilihairishwa hadi siku ya Alhamisi,  
Tarehe 10 Mei, 2018 Saa Tatu Asubuhi)*